**30 APRILI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Ishirini - Tarehe 30 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. MGORE M. KIGERA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu jinsi ambavyo amekuwa anatatua changamoto nyingi za wananchi wetu kwa utulivu na kwa hekima kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, kumekuwa na changamoto kubwa sana hapa nchini kwa wananchi wetu kukamatiwa pikipiki zao kwa makosa ambayo wakati mwingine ni madogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta wananchi wetu, vijana ambao wanatoka vijijini wanakuja mjini kwa nia njema ya kujipatia huduma, wakati mwingine kununua mbolea, mwingine amekuja kufuata dawa ana mgonjwa, wengine wanafuata mahitaji yao ya kibiashara waweze kuendelea kiuchumi, lakini wanakamatwa kwa makosa madogo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengi ya vituo vya Polisi hapa nchini, unakuta pikipiki zimelundikana pale zinachakaa, zinaharibika. Je, Serikali ipo tayari sasa kuandaa utaratibu

maalumu wa kupitia upya faini hizi ili vijana hawa waweze kurudishiwa pikipiki zao, waweze kuendelea na shughuli zao za kiuchumi kwenda kuijenga nchi ya Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niruhusu nitumie fursa hii kuipongeza timu yangu ya kazini, Timu ya Simba kwa ushindi walioupata kwa mbinde jana baada kushindwa kufanya hivyo kwa takribani michezo nane mfululizo iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kulileta swali hilo na ameendelea kuwa mtetezi wa wananchi wake wa Ushetu pamoja na vijana wengine wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na baadhi ya maeneo kuwepo kwa milundikano ya vyombo vya moto vikiwepo pikipiki ambazo zimekamatwa kwa makosa mbalimbali. Tuna mafungu mawili katika jambo lile ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema.

Mheshimiwa Spika, vipo vyombo vya moto vikiwepo pikipiki ambavyo vimekamatwa kwa ajili ya makosa makubwa ambayo yanahusisha uhalifu wa kutumia silaha ama makosa mengine yanayohitaji chombo husika kushikiliwa kama sehemu ya ushahidi. Mfano, chombo kilichobeba madawa ya kulevya, chombo kilichobeba wahalifu waliofanya uhalifu wa kutumia silaha ama chombo ambacho kimeshiriki katika makosa mengine makubwa kama ya ubakaji ama mauaji.

Mheshimiwa Spika, kwenye makosa haya ya kundi hili la makosa makubwa tumeweka sheria ya kushikilia vyombo hivyo ili viweze kutumika katika taratibu za kiuchunguzi na za kiushahidi kwa kuzingatia sheria zetu za makosa hayo makubwa.

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge, kwenye upande wa makosa haya madogo madogo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge watakumbuka, nilipopita katika ziara maeneo yote, nilielekeza kwamba vyombo

vinavyotumika kwa kazi ya vijana wetu hawa wa Kitanzania kujiletea kipato ikiwemo bodaboda, bajaji, magari haya ya *carry,* na magari ya biashara, kama limefanya kosa na tumejiwekea taratibu za sheria za hayo makosa, na mhusika anatambulika, basi hivyo vyombo vitumike kushikiliwa, badala yake warudishiwe wahusika ili wakafanyie kazi na kupata fedha ambayo wanatakiwa walipe faini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Watanzania wengi wako na vitambulisho vyao vya Taifa, wanafahamika na vyombo vyao vimesajiliwa wamiliki wao, na wanaoviendesha wanafahamika. Hakuna ulazima wa kushikilia chombo hicho, badala ya kujikita kwenye utaratibu ambao tumejiwekea wa faini na tumeweka muda ambao aliyefanya kosa anapaswa kuwa amelipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuelekeza tena, mahali popote ambapo kuna vyombo vya moto bado vimeshikiliwa na havijafanya makosa yale ya kundi la kwanza nililosema la makosa makubwa ya uhalifu, mauaji, nyara za Serikali, ubakaji, madawa ya kulevya na makosa mengine yote ya faini, vyombo vya moto visishikiliwe, badala yake wahusika watakiwe kulipa faini wakiwa na vyombo hivyo ambavyo ni vitendea kazi vya kufanyia kazi, kila mmoja aendelee na kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Mheshimiwa Rais alielekeza Serikali kupitia upya sheria zile za masuala ya faini. Faini zilikuwa kubwa sana, Mheshimiwa Rais akasema faini siyo chanzo cha mapato, tunarekebishana na tunasahihishana. Wekeni faini ambayo itakuwa na sura halisi kwamba hii siyo chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka Bunge lako Tukufu lilipunguza faini zile ambazo zilikuwa zinatozwa kwa bodaboda, bajaji na maeneo mengine ili kuweza kuhakikisha kwamba zinakuwa faini zinazoweza kulipika.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai pia kwa vijana wetu wa Tanzania kutokutumia hii kama fursa ya kufanya makosa. Makosa mengine yanahatarisha uhai wa Watanzania wengine ikiwemo

wale wanaobebwa kama abiria. Kwa hiyo, tuendelee kuchukua tahadhari, tunapotumia vyombo hivyo vya moto, kwa sababu zinatugharimu maisha na sehemu nyingine. Maeneo mengine vinasababisha ulemavu kwa wananchi, tena wanaotegemewa katika familia zao, ulemavu ambao hautibiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu.

**MHE. DOTTO J. BAHEMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi anavyotatua kero za wananchi. Wananchi wengi wanaamini kwamba kero zao zikifika kwake zitaisha na hata kule Ngara wanamsubiri kwa hamu Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu ni kwamba, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu yanayoelekezwa kwa Jeshi la Polisi kuchelewa kufanya uchunguzi katika mashauri mbalimbali hali ambayo inapelekea mashauri yale kushindwa kufanyiwa maamuzi na vyombo kama Mahakama na vyombo vinginevyo lakini inasababisha pia wananchi wengine kuchelewa kupata haki zao.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za karibuni tumeshuhudia kuna baadhi ya mashauri yaliyokuwa yanasabishwa na watu waliokuwa wakizua taharuki katika mikoa mbalimbali, ndani ya wiki mbili, tatu, nne zimepita, lakini Jeshi la Polisi lilishuhudiwa jinsi ambavyo lilikuwa linawakamata wale watu na haraka sana walikuwa wanashitakiwa na hukumu ilikuwa inatoka mapema sana. Kwa hiyo, uchunguzi ulikuwa ni wa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali, ni kwa nini Jeshi la Polisi lisitumie mbinu ambazo limetumia katika haya mashtaka ya majuzi ambayo wamechukua muda mfupi sana kuyachunguza ili yale mengine ambayo yanachukua muda mrefu yaweze kupatiwa hukumu ya haraka? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Dotto, Mbunge wa Jimbo la Ngara, kwa swali lake zuri ambalo linalenga kuwasaidia Watanzania wanapokuwa na masuala yanayohusisha ya upelelezi na uchunguzi kuweza kukamilika haraka ili waweze kujua hatima yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na malalamiko kama hayo, na kama utakumbuka, Mheshimiwa Rais aliunda Tume ya Haki Jinai ambayo ilifanya kazi yake nchi nzima ikikutana na wadau mbalimbali ambao walielezea pia kuguswa kwao na masuala ya upelelezi kuchukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, tayari Tume ile iliwasilisha taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais na tayari utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ile umeanza ambapo katika baadhi mapendekezo hayo na utekelezaji wake unayagawa makosa katika baadhi ya makosa ambayo ni makosa madogo madogo yanayotakiwa upelelezi wake ufanyike kwanza kabla ya mtuhumiwa kukamatwa, na atakapokamatwa, basi kiwe kimeshajulikana kile ambacho kinamhusu.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna mapendekezo ambayo yamesemea kwa makosa makubwa makubwa, basi upelelezi usizidi siku 90, ufanyike ndani ya siku 90. Yapo baadhi ya maeneo ambayo tumeshafanya marekebisho ya sheria, na yapo maeneo mengine ambayo tunaendelea na taratibu za Kiserikali na za Kibunge za kuweza kubadilisha sheria, na bahati nzuri Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo. Kwa hiyo, yapo ambayo yameshafanyiwa marekebisho ya sheria, na yapo ambayo yako kwenye taratibu za kufanyiwa marekebisho ya sheria.

Mheshimiwa Spika, tofauti na jambo la hivi majuzi, ambalo Mheshimiwa Mbunge amenukuu lililokuwa linahusisha taharuki iliyokuwa inajitokeza, yenyewe ushahidi wake ilikuwa rahisi kwa sababu, ulikuwa unaona, alisema, unaona alisemwa, mkihakikisha; haichukui dakika mnajiridhisha kwamba kilichosemwa ni uongo na nikuzua taharuki, basi hatua zinachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kufuatana na kazi kubwa ya Tume ya Mheshimiwa Rais iliyotumwa na ikafanya kazi kubwa na ambayo imesema sheria nyingine zimesharekebishwa na nyingine zinaendelea kurekebishwa, ni dhahiri kwamba tunakokwenda tutaendelea kupunguza na pengine kuyamaliza kabisa malalamiko haya yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa vyombo vyetu ambavyo vinatengeneza tasnia ile ya haki jinai, kujikita kufanya majukumu yao kwa weledi kwa kuzingatia sheria ambazo zimetoa uelekeo huo wa kufanya kazi katika maeneo yao hayo ya kiupelelezi na kiuchunguzi na pengine na taratibu za kimahakama ili kuweza kuhakikisha kwamba jambo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema halijirudiirudii.

Mheshimiwa Spika, kama nchi tumeshapiga hatua mpaka sasa, kwa sababu tumeweza ku-*automate* Ofisi yetu ya Mwendesha Mashtaka kwa *DPP* na Mahakama na sasa tunaunganisha vituo vya Polisi pamoja na Magereza.

Mheshimiwa Spika, zamani mafaili yalikuwa yanatembea kwa mkono, kwa sasa faili likiwa kwa *DPP* linaweza likaonekana kwenye Mahakama zetu na *movement* nyingine za wadau wote wa haki jinai. Kwa hiyo, hiyo na yenyewe itapunguza ule muda ambao ulikuwa unapotea kwa kusubiria mafaili yatembee kwa mikono na vitu vingine vya aina hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Johnston Mutasingwa.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninapenda nikushukuru sana kwa kazi nzuri unazozifanya za kutatua changamoto za wananchi na Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuuliza swali langu moja. Kwa sasa Mheshimiwa vijana wengi sana wamejiajiri katika idara au katika kuendesha pikipiki katika nchi yetu. Wengi wanaendesha pikipiki au bodaboda au guta. Kama tunavyofahamu, kazi ya

Serikali ni kutengeneza mazingira rafiki kwa watu wote wanaojiajiri *especially* katika vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa ninapenda kuuliza, je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha sekta hii ya waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda ili iweze kuwa sekta rasmi itakayoweza kuchochea uchumi na kuwa ajira inayotambulika ili iweze kukuza uchumi wa nchi yetu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Nimpongeze Mheshimiwa *Engineer* Johnston Mutasingwa, Mbunge wetu kwa swali zuri aliloliuliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kwamba sekta ya bodaboda (waendesha wa pikipiki wetu) ni sekta rasmi inayotambulika na Serikali. Ukienda pale Ilala waendesha pikipiki na Mkuu wao wa Wilaya Mheshimiwa Mpogolo wanawaita hawa ni Maafisa Usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, hii ni sekta iliyo rasmi na ni rasmi kwa sababu hii ni sekta ambayo inaajiri vijana wengi wa Kitanzania. Ni sekta inayotoa huduma ambayo inatambulika na kila Mtanzania na inawanufaisha Watanzania wote wa mijini na vijijini. Hii ni sekta ambayo inatumika mpaka kwenye shughuli pia za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku hizi ukienda kwenye masuala ya kibiashara unakuta, Maafisa Usafirishaji hawa ndio wanabeba fedha nyingi, wanapeleka kwenye kununua bidhaa, ku-*deposit bank* na maeneo mengine. Kwa hiyo, hii ni sekta ambayo ni kiungo muhimu katika uchumi.

Mheshimiwa Spika, la pili, sekta hii inaandikishwa. Kuna usajili wa chombo kinachotumika, usajili wa mmiliki na usajili wa anayeendesha. Kuna leseni katika chombo chenyewe, leseni kwa anayeendesha, na pia, ni sekta ambayo imeunganishwa kwenye taratibu za mitaji, kwa maana ya vijana wetu hawa wanaweza wakapata mikopo kwa ajili ya kuongeza mitaji katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya Serikali kuitambua, inaitambua kwamba, hii ni sekta rasmi ambayo inachangia katika pato la Taifa na inachangia katika utengenezaji wa ajira. Zamani ilikuwa sekta ambayo wanaofanya kazi hizo wanachukuliwa kuwa ni vijana tu ambao walikuwepo mtaani, lakini siyo hivyo kwa sasa. Ni sekta inayofanywa na watu wote waliosoma na wasiosoma, wanaume kwa wanawake. Kwa hiyo, ni sekta rasmi ambayo inafanya kazi kubwa ya kutoa ajira kwa vijana wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika ahadi ya siku 100 za Mheshimiwa Rais ambapo alitoa takribani shilingi bilioni 200 kusaidia vijana, baadhi ya vijana ambao wamenufaika na fedha hizo ni pamoja na ambao wako katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, ninatoa rai kwa ofisi zetu zote za Serikali, ofisi zetu za udhibiti, wanapokutana na vijana hawa watambue kwamba, wanakutana na sekta muhimu, ambayo inachangia katika kutengeneza ajira, inachangia katika kutengeneza pato la Taifa na inachangia katika kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja katika familia zetu. Kwa hiyo, pale ambapo vijana wetu hawa wanahitaji uwezesho wawezeshwe na watambue kwamba, Serikali iko pamoja nao katika kuhakikisha shughuli yao hii inakuwa na ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kila eneo katika nchi hii kuna vijana ambao wanatoa huduma hizi, mijini na vijijini. Kwa hiyo, ni sekta muhimu. Sisi, kama Serikali, tunaitambua na tutaendelea kadiri tunavyopata pia ushauri wa Wabunge kuendelea kuboresha mazingira ya vijana wetu hawa wanaofanya kazi hizo ili waweze kufanya kwa ufanisi mkubwa zaidi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kumwuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Amani, kwanza na sisi tunakupa pongezi kwa kazi nzuri ambayo unaifanya kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenye kutatua kero za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, swali langu liko kama hivi ifuatavyo: Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayongozwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, inafanya juhudi kubwa kuhakikisha watalii wanaongezeka nchini ili kukuza pato la Taifa letu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha watalii wanaongezeka ili kuweza kukuza pato kupitia mashindano ya mpira ya *AFCON,* ambayo yatakuja nchini, Tanzania itakuwa ni mwenyeji wa mashindano hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri alilolileta. Ni kweli, Tanzania pamoja na nchi jirani za Kenya na Uganda wataandaa kwa pamoja Mashindano ya *AFCON* yanayotarajiwa kufanyika mwaka 2027.

Mheshimiwa Spika, Serikali, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, wamefanya hatua kubwa ya kuandaa miundombinu ili kuweza kuhakikisha kwamba, mashindano haya yanafanyika kwa ufanisi. Hata hivyo, kwa upande huu ambao Mheshimiwa Mbunge ameuliza, kuhusu ni namna gani tutaongeza watalii ili kuweza kunufaika na uenyeji huo wa mashindano hayo, jambo hilo halijabaki nyuma katika mikakati.

Mheshimiwa spika, baadhi ya mikakati ambayo inaendelea hadi sasa ni kuwa na Kamati ambayo inaandaa utaratibu mzima ndani ya Serikali, kwa namna ambavyo sekta zitajipanga kuweza kuhakikisha kwamba, tunanufaika na mashindano hayo. Timu za wataalamu za kisekta na timu ya wataalamu ya ndani ya Serikali wanaendelea kubainisha, kukamilisha mkakati wa kuweza kunufaika na mashindano hayo, ambayo yatafanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya mikakati ambayo tunaifanya, ni kwenye kila viwanja vitakavyotumika kwa mashindano, tumeandaa mazingira ya kuweka matoleo ya kibiashara na

uwezeshaji wa kibiashara ili vijana wetu wajasiriamali na wafanyabiashara waweze kunufaika na wale wageni ambao watakuwa wanashiriki katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, moja ya mazingira tunayoyaandaa katika viwanja vitakavyotumika kwa mashindano na katika viwanja vitakavyotumika kwa mazoezi ni kuandaa barabara na viwanja vya kuweza kuweka bidhaa. Barabara hizo zitakuwa na taa, ambapo biashara inaweza ikafanyika saa 24 bila kuwa na shida yoyote ya masuala ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo, tunaendelea kuhamasisha bidhaa zetu ambazo ni za asili na nyingine ambazo zinapatikana ndani ya nchi ziweze kuwa karibu na maeneo hayo, ambayo wageni wetu watavutiwa waweze kunufaika nazo.

Mheshimiwa Spika, kingine, tunaendelea kutangaza utalii. Kama unavyojua, tuna vivutio vingi, tunaendelea kuvitangaza. Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara na sekta nyingine wanaendelea kutengeneza *roadmap,* wanaendelea kutengeneza bango kititia la vitu vyote vinavyoweza kupatikana na kutumia mawasiliano ya kimtandao.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, wale wageni ambao hawajaja Tanzania waweze kupewa *package* ambayo inaonesha akiwa kwenye mechi Arusha anaweza akatumia dakika ngapi na gharama kiasi gani kufika Ngorongoro kwenye eneo ambalo ingemgharimu zaidi, kama angekuja kwa ajili ya Ngorongoro peke yake.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, sasa hivi ata-*combine,* amekuja kwenye mechi, mechi ikiisha tu anaweza akatumia dakika 20 mpaka 30 amefika *Arusha National Park,* anaweza akatumia dakika 40 mpaka dakika 45 ama saa moja kufika mpaka Ngorongoro.

Mheshimiwa Spika, *package* hiyo itaeleza pia, kwamba, wakati anasubiri mchezo unaofuata anaweza akaunganisha kuanzia *Arusha National Park*, akaenda Ngorongoro. Kutoka Ngorongoro akaenda mpaka Serengeti, jambo ambalo

lingemhitaji safari nzima ya kutoka katika nchi yake kuja kwenda kwenye mbuga hiyo. *Package* hiyo, itaeleza kwamba, siku hiyohiyo anaweza akaona wanyama wa Serengeti na Ngorongoro; siku hiyo hiyo jioni akaenda akapumzika katika *beach* zenye mchanga wa kuvutia kule Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara ya Maliasili na Utalii iko kwenye hatua za mwisho za kuandaa baadhi ya viwanja vya mazoezi ambavyo vitakuwa ndani ya hifadhi. Hifadhi ambazo ziko karibu kama kama ile ya Arusha, ambapo hakuna wanyama wakali wanaoweza kuhatarisha maisha ya wachezaji ni mbuga ambayo inaweza ikawa na viwanja vya mazoezi, kwamba, wanafanya mazoezi huku wanaona wanyama.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo, hifadhi kama ya Mikumi ambako kwa sasa kuna *SGR* inaenda mpaka maeneo hayo ya hifadhi na yenyewe itakuwa moja ya *package* ambayo unaweza ukasema kwamba utamaliza mechi wakati unasubiri mechi inayofuata unaenda kwenye hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii itaendelea kuwashawishi wale ambao walikuwa wanapanga kuja tu kwa ajili ya utalii waone kwamba, wanaweza wakatengeneza *package* hiyo ya pamoja, ashuhudie mashindano na wakati ule ule aweze kwenda kujionea vivutio vya tofauti kabisa, ambavyo hawezi akavipata nchi yoyote duniani *except* hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba, maeneo haya ni mengi, hatuwezi kuyasemea yote hapa, lakini nalihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali, kupitia *sectors* na Kamati ya pamoja ya Kitaifa, tunaendelea kuweka hiyo *package* na kuitangaza, kupitia balozi zetu na mitandao ya kijamii, ili wenzetu watalii kutoka katika maeneo tofauti tofauti waone umuhimu wa kuja. Watakuwa wamepunguza gharama kwa kuja kuona mashindano hayo na wakati ule ule waunganishe masuala ya utalii.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Huyo ndiye Mbunge wetu wa mwisho. Ninakushukuru sana kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa hapa ki-*note* kinasema: "Mheshimiwa Spika, salamu za Mheshimiwa Waziri Mkuu zilitoka moyoni?" *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali ya Kawaida. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Mheshimiwa Stella Ikupa.

Na. 233

**Utekelezaji wa Waraka wa TAMISEMI kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa Waraka wa TAMISEMI wa 10/7/2017, kuhusu kutenga maeneo ya biashara kwa Watu Wenye Ulemavu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa Waraka wa tarehe 10 Julai, 2017 unaozielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo ya biashara kwa watu wenye ulemavu, ambapo angalau 10% ya maeneo hayo hutengwa kwa kundi hilo. Halmashauri zote nchini zimeendelea kusimamia na kuhamasisha utengaji wa maeneo ya biashara kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kusimamia zoezi la utambuzi na usajili wa watu wenye ulemavu wanaojishughulisha na biashara katika Halmashauri zote nchini, pamoja na kuwapa kipaumbele katika upangaji wa maeneo ya biashara, ikiwemo vizimba katika masoko na maeneo maalum kwa wafanyabiashara wadogo. Kwa kuzingatia umuhimu wa waraka huu, Serikali imejenga na kuyaboresha takribani masoko 800 nchini, kuwa na miundombinu rafiki kwa wenye ulemavu. Katika Mkoa wa Dar es Salaam hadi sasa jumla ya masoko 16 yametenga vizimba kwa ajili ya wafanyabiashara wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutekeleza waraka huu, ili kuwezesha ustawi wa bishara kwa watu wenye ulemavu kote nchini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaishukuru na kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo inafanywa kwa kundi hili, lakini pia, kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, maeneo haya yamekuwa yakivamiwa mara kwa mara na watu wasio na ulemavu, mfano mzuri ni maeneo ya waendesha bajaji Mkoani Dar es Salaam. Uvamizi huu unasababisha watu wenye ulemavu kukosa riziki na marejesho kwa sababu, bajaji hizi zinakuwa za mikopo, nini mkakati wa Serikali kuyalinda maeneo haya na uvamizi huu?

Mheshimiwa Spika, pia, kwa uelewa na ufahamu, ninaomba orodha ya maeneo tajwa, kwenye jibu la msingi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Stella Ikupa Alex. Kwa kweli, amekuwa msemaji madhubuti sana kwa watu wenye ulemavu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia kwamba, Serikali inatambua baadhi ya maeneo haya ambayo yanatengwa maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu yamekuwa yanapata changamoto ya kuvamiwa. Sababu kubwa ziko mbili; kwanza, yako maeneo ya vizimba vya masoko ambayo yanatengwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, lakini mara nyingine watu wenye ulemavu hawajitokezi kuomba kutumia maeneo hayo kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira hayo, halmashauri zimekuwa zikiwapangisha watu wengine, lakini kwa *condition* kwamba, wakitokea watu wenye ulemavu wawapishe kuendelea na biashara zao. Maeneo yale ya bodaboda au bajaji, ambayo yametengwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu halmashauri zimeendelea kuyasimamia kuhakikisha kwamba yanatumiwa na watu wenye ulemavu, na pale wavamizi wanapoingia, wamekuwa wakiondolewa, ili kuwapa nafasi nzuri watu wenye ulemavu wafanye biashara kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kusimamia suala hilo kuhakikisha maeneo yaliyotengwa yanatambuliwa. Tunaweka vibao kwenye *parking* za bodaboda na daladala, ili watu wenye ulemavu wafanye biashara vizuri. Pili, tutampa Mheshimiwa Mbunge orodha ya vizimba katika masoko yetu na maeneo ya biashara yaliyotengwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni.

Na. 234

**Ujenzi wa Daraja la Mto Saise**

**MHE. EDIFONSI J. KANONI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mto Saise litakalounganisha Kata ya Mambwe, Nkoswe na Mambwe, Kenya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Edifonsi Joackim Kanoni, Mbunge wa Jimbo la Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Utengule – Madibila yenye urefu wa kilometa 25 inaziunganisha Kata za Mambwe Nkoswe na Mambwe Kenya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo. Barabara hiyo inapitiwa na Mto Saise ambapo, ili kurahisisha usafiri na usafirishaji eneo hilo linahitaji daraja lenye urefu wa mita 80.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhitaji na umuhimu wa daraja hili, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 70 katika bajeti ya mwaka 2026/2027, ili kufanya usanifu wa daraja hilo kwa lengo la kujua gharama halisi za kutekeleza ujenzi wake. Serikali itatafuta fedha za ujenzi wa daraja hilo katika bajeti zake zijazo mara baada ya kujua gharama halisi za kutekeleza ujenzi huo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kanoni.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali na Mheshimiwa Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Moja ni, hili eneo ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Kalambo, katika Kata hizi mbili, Mambwe Kenya na Mambwe Nkoswe

Mheshimiwa Spika, hili daraja lipo katikati ya kijiji cha Madibila pamoja na Utengule. Kutoka makao makuu ya kata kwenda kata nyingine ni kilometa 100, lakini hili daraja likijengwa, ni kilometa 20. Je, ni lini sasa Serikali itaweka fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba hili daraja linajengwa kwa wakati ambapo limekuwa linatoa sana ajali na mwaka huu, katika wiki hizi mbili, wamefariki watu wawili kwa ajili ya kujaa kwa maji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Ninaomba sasa kwa ridhaa yako, ikimpendeza Mheshimiwa Waziri, aje kule katika Jimbo langu la Kalambo ili ajionee hali halisi ya mazingira yaliyopo katika

kata hizi mbili ili wananchi sasa watoe kero zao na aangalie Serikali itatoa majibu gani kwa ajili ya hilo daraja? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge amefuatilia kwa karibu sana ujenzi wa daraja hili na kwa kweli Serikali inafahamu umuhimu wa daraja hili kwa sababu, linaunganisha kata kubwa takribani mbili na shughuli nyingi za uchumi za wananchi wa Kalambo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, ndiyo maana Serikali tayari imetenga fedha shilingi milioni 70 kwa ajili ya kufanya usanifu kujua gharama halisi za ujenzi wa daraja hilo. Mara baada ya kujua gharama hizo, Serikali itaanza kutenga fedha kwa ajili ya kujenga daraja hilo na kuondoa changamoto katika eneo hilo. Namhakikishia kwamba, tayari tumeanza kulifanyia kazi na tutaendelea kuhakikisha linajengwa.

Mheshimiwa Spika, pili, niko tayari kuambatana na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kalambo. Tutakaa mimi na yeye tupange baada ya shughuli za Bunge tuweze kwenda kufanya shughuli za Serikali katika Jimbo la Kalambo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Alan.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Katika Wilaya ya Kakonko kuna barabara inayotoka Wilaya ya Kakonko kwenda Kibondo kupitia Mto Kahambwe, ambapo baada ya mvua kali kunyesha daraja hilo limeharibika na halipitiki kabisa. Sasa kwa kuwa, tumewasilisha maombi ya fedha kwa matengenezo ya dharura, ni lini sasa Serikali itachukua hatua ili wananchi hao waweze kupata huduma tena? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na kufanya tathmini ya uharibifu wa madaraja na barabara zetu unaotokana na mvua nyingi ambazo zimeendelea kunyesha. Tathmini hiyo pia imefanyika katika Jimbo la Kakonko, kwa Mheshimiwa Mvano, na tumepata taarifa ya uharibifu wa daraja linalounganisha Halmashauri ya Kakonko na Kibondo na tayari tumepata ripoti, na tunajua gharama ya matengenezo ya daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natumia nafasi hii kumwelekeza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Kigoma, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, na Meneja wa Wilaya ya Kakonko kwenda katika eneo hilo kuona kama kuna uwezekano wa kufanya matengenezo ya muda mfupi ya dharura, ili daraja hilo liendelee kupitika wakati tunasubiri hali ya mvua itulie kwenda kujenga kwa uhakika daraja liwe la kudumu. Kwa hiyo, wafanye hivyo ikiwa kuna uwezekano, ili wananchi waendelee kupita.

Mheshimiwa Spika, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeliingiza kwenye orodha na tutahakikisha linapata fedha kwa ajili ya matengenezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Kaiza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Ni kwa muda mrefu sasa Serikali imeahidi kujenga daraja linalounganisha Kata ya Kipawa – Liwiti na Vingunguti na kuna wakati ambao Serikali ilitenga kiasi cha fedha. Swali langu, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga daraja hili ili kunusuru maisha ya wananchi ambao kwa kipindi hiki cha mvua wanashindwa kupita katika hilo eneo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Daraja la Kipawa – Liwiti – Vingunguti ni moja ya madaraja muhimu sana katika Jimbo la Segerea na Mheshimiwa Mbunge

Agnesta Lambert amelifuatilia mara kadhaa. Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imelichukua, tumeshanza kuandaa utaratibu wa fedha kwa ajili ya kwenda kujenga daraja hili kwa kiwango bora kabisa ili liweze kupitika na kuondoa changamoto ya wananchi wa kata hizi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali iko kazini na inakwenda kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi na mimi niulize swali. Wananchi wa Mtaa wa Nyakehenene na Nyasebe, waliopo Kata ya Nyandoto, hawana kabisa mawasiliano kwa sababu daraja la Mori ambalo linaitwa daraja la Nyasebe halipo kabisa, limeharibika, yaani hamna; walikuwa wameweka miti, lakini imeondoka, na tumekuwa tunapoteza wananchi. Hata juzi tu tumetoka kuzika, na jana pia kuna Mzee Wambura Nyamaka amepelekwa na maji.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kwamba kuna udharura wa kuhakikisha wanajenga lile daraja ili kurudisha mawasiliano kati ya Nyasebe na Nyakehenene kwa sababu wanapoenda kuchunga na kulima lazima wapite ile sehemu ya Mto Mori?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninawapa pole wananchi wa Jimbo la Tarime Mjini, na Mheshimiwa Mbunge Esther Matiko, kwa madhara hayo makubwa ya kupoteza maisha katika daraja hilo, lakini niwahakikishie tu kwamba Serikali inafahamu kwamba madaraja yetu mengi kote nchini yameathiriwa na mvua, likiwemo daraja la Mto Mori.

Mheshimiwa Spika, tayari tulishatoa maelekezo kwa Meneja wetu wa Wilaya na Mikoa kuleta taarifa rasmi ya tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya matengenezo. Pili, kufanya

matengenezo ya dharura pale panapowezekana ili angalau yale madaraja yaweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, niwaelekeze na kuwasisitiza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Mara na Tarime wafike katika eneo hilo na kuona njia nyepesi, rahisi ambayo inaweza kufanyika kwa sasa ili wananchi waendelee kupita kwa usalama wakati tunasubiri kwenda kulijenga daraja hilo kwa hatua ya kudumu. Kwa hiyo, tutalifuatilia hilo kuhakikisha kwamba tunaokoa maisha ya wananchi, na pia tunarahisisha usafiri wa wananchi katika eneo hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mariam Azan Mwinyi.

Na. 235

**Elimu ya Upandaji Miti kwa Biashara ya Carbon**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya upandaji miti ili wananchi wetu washiriki vizuri katika biashara ya *Carbon* hasa wale wa vijijini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS)*

imeendelea kufanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha elimu ya upandaji miti inatolewa kwa wananchi hususan wale wa vijijini ili waweze kushiriki vizuri katika biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Spika, jitihada hizo ni pamoja na kuendelea kutekeleza kampeni za upandaji miti katika Halmashauri zote nchini, kuratibu vipindi vya redio na televisheni, ikiwemo kipindi cha Mazingira yetu na Tanzania Tuitakayo kinachorushwa kila siku ya Jumatatu kupitia *TBC* ambapo elimu ya upandaji miti na biashara ya kaboni hutolewa na kuendelea kuwajengea uwezo Maafisa Mazingira katika ngazi ya Serikali za Mitaa kuhusu umuhimu wa upandaji miti na fursa ya biashara ya kaboni ili kuhakikisha wananchi wote wanashiriki katika biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeendelea kutoa elimu kwa makundi yenye ushawishi katika jamii ikiwemo kundi la Waheshimiwa Wabunge ili wawe chachu ya kuhamisisha wananchi katika upandaji miti na kushiriki kikamilifu katika biashara ya kaboni. Aidha, Serikali itaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa jamii ili waweze kunufaika ipasavyo na biashara ya kaboni, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Mwinyi.

**MHE. MARIAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza. Je, Serikali ina mkakati gani wa upatikanaji wa miche bora ya miti kwa gharama nafuu hasa kule vijijini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika programu inayotolewa huko vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, swali la pili sijalisikia vizuri.

**SPIKA:** Swali la pili rudia tena.

**MHE. MARIAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa programu hasa kule vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mariam Azan Mwinyi, amekuwa msemaji na mfuatiliaji mzuri sana wa masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mazingira ni kitu muhimu sana katika maendeleo ya nchi yetu, kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, lakini nimhakikishie tu kwamba kupitia Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)*, kila Mkoa na kila kanda wanavyo vitalu vya miche bora ya miti ambavyo miti ile inapatikana bure bila malipo yoyote kupitia Maafisa Misitu na Maliasili katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie nafasi hii niendelee kuwasisitiza Maafisa Maliasili, Maafisa Misitu katika Halmashauri zetu kutumia fursa ya miche ya miti inayopatikana katika ofisi za mikoa za *TFS*, ofisi za kanda za *TFS* kupeleka kwa wananchi vijijini, ili wananchi waweze kupata miche hiyo na kuipanda, lakini kubwa zaidi kuitunza, kuhakikisha kwamba tunalinda mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kutokana na changamoto ambazo zinajitokeza vijijini, Serikali imeendelea kuratibu kupitia Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, na watendaji wa vijiji kuhakikisha kwamba changamoto zinazojitokeza katika programu ya upandaji wa miti zinatatuliwa kwa wakati, ikiwemo kuweka vyanzo vya maji katika maeneo yanayopandwa miti, lakini pia kusimamia ile miti isiweze kuharibiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya hivyo kuhakikisha kwamba tunaendelea kuifanya nchi yetu ya Tanzania kuwa ya kijani.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu ya Tanzania ni moja ya nchi ambayo ina misitu mingi sana na tuna mapori ya kutosha kabisa, na hii biashara ya *carbon credits* imekuwa ni biashara kubwa sana duniani na mashirika makubwa duniani. Ni lini sasa Serikali itakuwa na mkakati maalumu wa kufanya hii biashara ili kupata manufaa kwa nchi yetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchi yetu ina utajiri mkubwa sana wa misitu, maji na mikoko ambayo ni rasilimali muhimu sana kwa biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu ilianzishwa sheria na kitengo maalum cha kuratibu kaboni kipo pale Morogoro - *National Carbon Monitoring Centre*, ambayo tayari ina Bodi ya Wakurugenzi, ina *CEO*, na tayari imeanza kutoa maelekezo na miongozo mbalimbali ili wananchi, Halmashauri, na watu binafsi waweze kunufaika na biashara ya kaboni kote nchini.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili, tunayo kaboni ya *blue* ambayo inatokana na masuala ya maji na mikoko, lakini pia tunayo kaboni inayotokana na misitu. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Getere kwamba hivi sasa *Carbon Monitoring Centre* imeanza kazi kwa ufanisi mkubwa na matarajio ya Serikali ni kwamba Halmashauri zote zenye fursa za misitu, watu binafsi, lakini pia na maeneo mengine yote tutakwenda kuyaorodhesha na kuhakikisha tunayasajili kupata biashara ya kaboni ili tuweze kuingiza mapato katika Halmashauri zetu, watu binafsi na katika nchi yetu kwa ujumla.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Thomas Maganga

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Serikali imekuwa ikihamasisha sana upandaji wa miti hasa shuleni na maeneo mengine, lakini zoezi hili limekuwa likikwama kwa sababu wanafunzi na wananchi wanakuwa hawaoni manufaa. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuhamasisha upandaji wa miti ya matunda shuleni ili wanafunzi waitunze miti ile kwa sababu baadaye itawapa manufaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhamasisha shule zetu, vyuo, mazingira yao yote kupandwa miti na kujenga utamaduni wa wanafunzi wetu kupanda miti, kwa sababu tunatambua wanafunzi wetu ndio wananchi watakaokuja baada ya miaka kadhaa. Tunataka kujenga utamaduni wa wananchi hao kuwa na tabia na utamaduni wa kupanda miti katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Serikali imeendelea kufanya hivyo, na zipo shule ambazo zimepanda miti mingi na ya kutosha, lakini zipo shule na taasisi mbalimbali ambazo tumeendelea kuhamasisha kuhakikisha kwamba wanapanda miti. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaendelea kufanya hivyo, kutoa elimu na hamasa, kuwezesha upatikanaji wa miche ya miti, na kusimamia kutunza miti hiyo ili ikue na kuwa na Tanzania ya kijani na kuboresha hali ya hewa na mazingira ya nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Neema Majule.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba biashara hii ya kaboni ni mpya katika nchi yetu na

kwamba ni makisio kule kujua kwamba ni kiasi gani cha kaboni kinakuwa *replaced* kwenye *biosphere* ya kwamba ni makisio, na imeshikwa na wawekezaji ambao ndio wanaoenda kufanya *estimate* kwa wananchi na kuweza kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imeweka viashiria gani, au *control measures* gani kuhakikisha kwamba wananchi wa chini kabisa vijijini hususan wanawake na vijana wanalipwa kulingana na makisio yaliyofanyika kwenye misitu au kwenye ardhi yao? ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumekuwa tukifanya biashara ya kaboni. Kwa mfano, Halmashauri ya Tanganyika katika Mkoa wa Katavi ni moja ya Halmashauri ambazo zimenufaika sana na biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na ukosefu wa uwazi wa uhalisia wa malipo yanayotokana na biashara hiyo ya kaboni, kwa maana ya vipimo ambavyo wananchi wananufaika na biashara hiyo ya kaboni kutoka kwa wadau mbalimbali ambao tunashirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, Serikali, ndiyo maana baada ya kuona pengo hilo, imeanzisha kituo maalum cha kuratibu biashara ya kaboni *(National Carbon Monitoring Centre)*, ambayo iko pale Morogoro na itakuja Makao Makuu hapa Dodoma, ambayo kama nilivyosema tayari ina watendaji, Bodi ya Wakurugenzi, *CEO* na Wataalam wote wa Serikali ambao tutashirikiana na wadau pamoja na Serikali yenyewe, kuhakikisha kwamba tuna-*quantify* kwa uhakika kiwango cha kaboni kinachopatikana katika msitu au eneo husika na wale wananchi au wanaonufaika wanapata fedha au malipo yanayoendana na kiwango cha kaboni ambacho kinazalishwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo, tunakwenda kuondoa hiyo *black market* katika eneo hilo, kuhakikisha kwamba wananchi wanapata haki yao kulingana na *volume* ya kaboni inayopatikana katika maeneo hayo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdul Yussuf.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali ina *program* tofauti za upandaji wa miti kwa kila mwaka. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kukadiria miti ile ambayo inapandwa kwa kila mwaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, moja ya mkakati ulioandaliwa wa kijanisha Tanzania ni pamoja na kuhakikisha kwamba miti inayopandwa inatunzwa na kukua, kwa sababu ni kweli kumekuwa na jitihada nzuri za kupanda miti, lakini mara nyingine baadhi ya maeneo miti ile imekuwa haisimamiwi na kutunzwa ipasavyo na kukua.

Mheshimiwa Spika, moja ya mkakati katika upandaji wa miti ni kuhakikisha kwamba ile miti inawekewa miundombinu ya uhakika na ufuatiliaji na usimamizi wa uhakika ili iweze kukua. Katika mpango huo wa kijanisha Tanzania, liko eneo mahususi ambalo lina njia mbalimbali za kuhakikisha kwamba hiyo miti itaendelea kutunzwa.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwasisitiza viongozi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini, kuhakikisha kila eneo ambalo tunapanda miti ambayo ni malengo ya kila Halmashauri kila mwaka, wasimamie miti ile ikue na kuhakikisha kwamba inafikia malengo ambayo yapo kwa mujibu wa taratibu za kimazingira.

**SPIKA:** Mheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Ninamwita sasa Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, kwa niaba Mheshimiwa Issaay.

Na. 236

**Ujenzi wa Barabara ya Haydom – Labay**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY K.n.y. MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa barabara ya lami kutoka Haydom hadi Labay?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Emanuel Qambaji Nuwas, Mbunge wa Mbulu Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Haydom – Labay yenye urefu wa kilometa 25 ni sehemu ya barabara ya Serengeti *Southern Bypass* yaani Karatu – Mbulu – Haydom – Sibiti – Lalago – Maswa yenye urefu wa kilometa 389.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami, wa sehemu ya Haydom – Labay urefu wa kilometa 25 ambapo kwa sasa utekelezaji wake umefikia 11%. Kazi zinazoendelea kufanyika ni kusafisha eneo la ujenzi *(clearing and grubbing)* na ujenzi wa kambi ya Mhandisi Mshauri, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbulu kuishukuru sana Serikali yetu kwa kuwa imemlipa mkandarasi wa Mbulu - Garbabi kwa kiwango kikubwa hadi sasa. Maswali yangu mawili ni kwamba, kwa kuwa, sasa wananchi waliopisha mradi huu kwa takribani miaka minne hawajapata fidia ya maeneo yao na rasilimali mbalimbali, je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa

wananchi hao fidia yao kwa mujibu wa tathmini iliyofanyika miaka minne?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Barabara hii ya Mbulu - Garbabi hadi Haydom - Labay, katika kipindi cha masika, inajifunga sana na wananchi wanapata adha nyingi sana. Kwa kuwa Mkandarasi huyu hawezi kufanya matengenezo yanayofanana na mahitaji ya barabara hiyo na barabara haipitiki hata wakati huu, je, Serikali ina mpango gani sasa kumsimamia huyu mkandarasi ili afanye matengenezo ya barabara ya kawaida ili wananchi waendelee kupata huduma iliyo bora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wananchi hawa walipisha ujenzi, na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Mbulu pamoja na Wananchi wa Mbulu ambao walipisha barabara hii, hivi tunavyoongea tayari tumeshapata fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ikiwezekana, kama taratibu zote zitakwenda, kwa sababu Kamati zimeshaundwa, kabla ya mwisho wa mwezi huu wa Tano haujaisha nina hakika wananchi hao watakuwa wamelipwa fidia ambayo haizidi zaidi ya shilingi milioni 571.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ambayo mkandarasi yupo *site*, kwa maana ya Mbulu - Garbabi, lakini mkandarasi huyo huyo ndio yuko Labay hadi Haydom, pamoja na kile kipande cha katikati cha kilometa 35, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshamwelekeza mkandarasi, hasa kipindi hiki ambacho mvua imekatika kuhakikisha kwamba barabara yote inapitika kuanzia Mbulu mpaka Haydom, ikiwa ni pamoja na kile kipande cha katikati ambacho hakina mkandarasi, tutahakikisha kinapitika. Tumeshatoa maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Manyara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula Magangila.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza kabisa, niipongeze Wizara ya Ujenzi kwa barabara ya Kahama - Kakola ya kilometa 73 ambayo inaendelea kujengwa mpaka sasa hivi, na imefikia kilometa 15. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kuziingiza kwenye mpango wa kujengwa kwa lami barabara za Miji ya Segese na Kakola kule inakoenda kuishia barabara hii? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara za Miji ya Segese na Kakola kama ni zile ambazo tunajenga barabara kulingana na *design*, kwa maana kama ni barabara ambazo tunasema labda mabasi yatakuwa yanapaki kwa maana ya Segese na Kakola, na zipo kwenye ushoroba wa *TANROAD*, nimhakikishie Mbunge kwamba tutazijenga.

Mheshimiwa Spika, pia nikukumbushe kwamba katika hiyo miji ambayo imeshakuwa mikubwa, Segese na Kakola, itakuwa ni pamoja na kilometa tano. Kama ziko nje ya ushoroba, ambazo labda zitakuwa zinahudumiwa na wenzetu wa *TARURA,* basi tutaangalia namna ya kufanya ili hiyo miji ambayo inaendelea kukua kwa kasi sana iweze kujengwa na kuboreshwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kuuliza swali kwamba, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Malinyi, Londo mpaka Songea?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, hii barabara ya Malinyi - Londo hadi Lumecha - Songea ni barabara ambayo, inaanzia Ifakara - Lupilo - Malinyi hadi Songea. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaanza kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami. Kwa sasa upo mpango ambao tayari tuna mkandarasi, kuanzia Ifakara hadi Mtimbira kilometa

112, tutaanza kwa awamu. Baada ya kukamilisha hiyo barabara tutaendelea Malinyi na Songea, kama fedha itapatikana. Mpango wa Serikali ni kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Athumin Mapalilo.

**MHE. ATHUMIN O. MAPALILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, barabara ya Ziwani kuelekea Msimbati ni barabara muhimu sana kwa ulinzi na usalama na pia barabara hii kuelekea kwenye visima vya gesi ambavyo ni nishati muhimu kwa Taifa letu, je, Serikali itaanza kujenga lini barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tunatambua hiyo barabara ni barabara ambayo tunasema zinaenda kwenye maeneo ya kimkakati kutoka Mtwara hadi Msimbati kwenye visima vya gesi. Pia hiyo barabara inakwenda kwenye daraja la Mto Kilambo mpakani na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo kwenye mpango, tulishaisanifu, tunasubiri fedha tuone katika hii bajeti inayokuja hiyo barabara itakuwa na mpango gani? Pia tunatambua, pamoja na daraja, na vile vile kwenda Msimbati kwenye vituo vya gesi, kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza, ninaipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kumteua mkandarasi wa ujenzi wa Barabara ya Bigwa - Kisaki. Maeneo ya Mkuyuni, Mngazi na Kisaki katika barabara hiyo sasa hivi hayapitiki kabisa na wananchi wanasafiri kwa siku nzima au kulala njiani. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa haraka kuweza kuinasua barabara hii kwa kipindi hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba kweli Mkoa wa Morogoro ni moja ya mkoa ambao una mvua nyingi, lakini pia inapokea mvua kutoka sehemu mbalimbali na imekuwa na changamoto kubwa sana ya miundombinu.

Mheshimiwa Spika, ninajua mvua inapungua, hivyo ninamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Morogoro baada ya mvua kupungua ahakikishe kwamba anakwenda kurejesha mawasiliano maeneo yote ambayo yana changamoto. Kama itakuwa nje ya bajeti ya mkoa, awasiliane na *TANROADS* Makao Makuu kuhakikisha kwamba hiyo barabara inarudi katika hali yake ya kawaida.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Magamba - Mlola - Makanya - Milingano - Mashewa ni barabara ya kimkakati inayounganisha majimbo manne ya Mlalo, Lushoto, Bumbuli na Korogwe Vijijini. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kukamilisha barabara hii? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii aliyoitaja kwanza tunaifanyia usanifu halafu tuweze kujua gharama za ujenzi kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakachokifanya ni kukamilisha usanifu, tujue gharama ili tuweze kuanza mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza, kwa sababu tayari Serikali imeleta shilingi bilioni nne kwa ajili ya barabara ya Bigwa - Kisaki, leo hii hali yetu ni mbaya, magari hayapiti, tukienda *TANROADS* Mkoa, wanasema kwamba barabara ina mkandarasi. Je, ni lini Serikali itamalizia fedha iliyobaki ili hii barabara ikamilike? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Taletale, maana swali hilo ndilo lililoulizwa na Mheshimiwa Mfaume, ni barabara hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, moja ni kwamba mkandarasi huyo alivyopewa *advance*, sehemu ya malipo yake ya awali, ilikuwa kwanza kujenga makambi. Sasa hivi tunaandaa malipo ili tuweze kumkamilisha na aweze sasa kuingia kujenga barabara, maana mvua imepungua, na kuhakikisha kwamba hiyo barabara inapitika ikiwa ni pamoja na zile barabara za *diversion,* yaani, barabara za mchepuko kuhakikisha kwamba wananchi hawakwami wakati wanafanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Manispaa ya *Old Shinyanga* - Iselamagazi ambapo ni Makao Makuu ya Halmashauri Jimbo la Solwa, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ambayo inakwenda Makao Makuu ya Halmashauri ya Shinyanga tunaijenga kwa awamu. Tunachofanya sasa hivi ni kuhakikisha kwanza yale maeneo yote ya miji yanajengwa kwa kiwango cha lami wakati tunatafuta fedha kuijenga barabara.

Mheshimiwa Spika, barabara hii imeshafanyiwa usanifu yote.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Festo Sanga, kwa niaba Mheshimiwa Dkt. Swalle.

Na. 237

**Ujenzi wa Barabara ya Kipengele – Lupila kwa Kiwango cha Changarawe**

**MHE. EDWIN E. SWALLE K.n.y. MHE. FESTO SANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha changarawe barabara ya Kipengele – Lupila ambayo inaunganisha Halmashauri ya Wanging'ombe na Wilaya ya Makete?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kazi ya kufanya ukarabati wa Barabara ya Kipengele - Lupila yenye urefu wa kilometa 49 kwa kiwango cha changarawe kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya kilometa 7.5 zimejengwa katika maeneo ya Lupombwe na Ludilu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya kilometa 5.4 zimepangwa kujengwa katika maeneo korofi ya Kata ya Mbalatse na eneo la Shamba la Malisho. Kazi hiyo inatarajia kukamilika Julai, 2026.

Mheshimiwa Spika, barabara hii itaendelea kufanyiwa matengenezo mbalimbali kila mwaka ikiwa ni pamoja na kujenga mifereji na tuta la barabara kwa kiwango cha changarawe kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mbalatse, Ipepo na Lupila wamekuwa na kilio cha muda mrefu cha hii barabara. Pamoja na kuishukuru Serikali kwamba imeanza ujenzi wa barabara hii kwa awamu, je, ni kwa nini Serikali wasijenge barabara yote ili kumaliza kero hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; iko barabara ya Kibena - Nyombo - Lupembe - Madeke ambayo ina ahadi ya muda mrefu ya Serikali ya kujenga kwa kiwango cha lami. Hivi sasa hii barabara, yapo baadhi ya maeneo kwa sababu ya ufinyu wa

madaraja kumekuwa na ajali nyingi sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hii ya Kibena - Lupembe kwa lami pamoja na madaraja yake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Kipengele - Lupila, Mheshimiwa Swalle atakubaliana nami ni zile barabara ambazo zinakuwa zimepandishwa hadhi. Zilikuwa za *TARURA,* zimekuja *TANROADS*. Kwa hiyo, kazi kubwa inayokuwepo ni kwanza kuibadilisha ile barabara na kutengeneza tuta kuwa kwenye muundo wa barabara za *TANROADS* halafu kuanza sasa kujenga mifereji na pia kuweka changarawe.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana barabara hiyo haijapandishwa muda mrefu. Tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kulingana na upatikanaji wa fedha, tutaendelea kujenga. Hata hivyo, lengo kama ilivyo utaratibu wa barabara zote za *TANROADS* ni za changarawe. Tutakapopata fedha, tuna mpango wa kuijenga yote. Kwa kuwa ndiyo kwanza imepanda, tutaanza kwa hatua hizo, lakini tutaitengeneza yote kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusu barabara ya *Kibena Junction* - Lupembe - Madeke - Mlimba - Ifakara, tumeanza kujenga pande zote mbili. Tumeanza Ifakara - Mlimba, na pia tuna mpango wa kuanza *Kibena Junction* - Lupembe - Kidegembye kilometa 40.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea sasa hivi tunasubiri tu kibali cha kusaini kwa sababu taratibu zote tumeshakamilika, ikiwa ni pamoja na hayo madaraja ambayo anayasema Mheshimiwa Mbunge. Hilo Daraja la Ikanga liko katika hizo kilometa 40 ambazo watakwenda kuzijenga. Kwa hiyo, tunaamini kwamba mkandarasi huyo mkubwa atakapoanza itakuwa ni pamoja na kurekebisha hayo madaraja ambayo yako katika hilo eneo.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge.

Na. 238

**Ujenzi wa Gati la Kontena Bandari ya Tanga**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga gati ya kontena katika Bandari ya Tanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* imefanya uwekezaji mkubwa wa takribani shilingi bilioni 429.1 katika kuboresha miundombinu ya bandari hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza kina kutoka mita tatu mpaka mita 13, ujenzi na uboreshaji wa gati lenye urefu wa zaidi ya mita 450. Matokeo ya uwekezaji huo yameongeza mapato kutoka takribani shilingi bilioni 56 hadi shilingi bilioni 75; meli 113 hadi kufikia meli 456, pamoja na ujazo wa shehena kutoka takribani tani 735,525 hadi tani 1,326,415.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maboresho hayo yaliyofanywa, nikiri kuwa bado ipo changamoto ya ufinyu wa eneo kutokana na kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha mizigo. Katika kukabiliana na hali hiyo, Serikali kupitia *TPA* ipo katika hatua za awali za kutekeleza mradi wa ujenzi wa gati jipya la kisasa la makasha lenye urefu wa meta 300 katika Bandari ya Tanga, ambapo tayari imekamilisha tafiti na usanifu wa awali.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huo unatarajiwa kuanza mwaka 2026/2027 ukiwa ni sehemu ya awamu ya tatu ya maboresho ya bandari hiyo kwa lengo la kuongeza uwezo wa kuhudumia shehena, kuboresha ufanisi wa huduma na kuimarisha ushindani katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa uwekezaji mkubwa ndani ya Bandari ya Tanga. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imetumia fedha nyingi sana kwa kuongeza kina Bandari ya Tanga, swali langu ni kwamba, je, Serikali imewekeza kiasi gani kufanya tafiti kujua sababu ya kwa nini Bandari ya Tanga kina chake kinapungua?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, njia inayotumika sasa ya kuongeza kina kwa maana ya kuchimba *(dredging)* ni ghali na siyo endelevu, kwa maana utafanya *capital dredging* na utakuja kufanya *maintenance dredging.* Je, mpaka sasa Serikali ishawekeza kiasi gani kutafuta njia mbadala ambayo ni *cost effective* na ambayo ni endelevu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge kwa jinsi anavyofuatilia maendeleo ya Bandari yetu ya Tanga ambayo ni bandari muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu pamoja na wananchi wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)* inatekeleza mpango kabambe wa utendaji wa bandari za Tanzania yaani *Ports Master Plan* ambayo ndani yake ndiyo inatupa fursa ya kufanya upembuzi yakinifu wa hali ya mradi husika kabla ya kuanza kuutekeleza. Hapo ndipo tunajua gharama zitakazotumika, tunajua kina husika, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tusipate uwezo wa kusema *specifically* ni gharama kiasi gani, lakini ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kazi hiyo inaendelea kufanyika hatua kwa hatua. Hata ujenzi wa mradi huu mkubwa wa shilingi bilioni 429.1 uliofanyika ulitokana na upembuzi yakinifu ambao matokeo yake sasa tumefanya kazi kubwa ya kuchimba kina, kuongeza pengine upana pamoja na eneo la kugeuzia meli na maboresho mengine kadri inavyohitajika.

Mheshimiwa Spika, ili kumhakikishia Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge, ninaielekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania kuendelea na kazi ya kuchukua hatua za mara kwa mara, ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa kina pale ambapo mchanga unakuwa umejaa, sambamba na kutafuta suluhu ya kudumu ili changamoto hii ya kupungua kwa kina katika Bandari ya Tanga pamoja na bandari nyingine sambamba na maziwa makuu yote ambayo nayo unakuta yanajaa iweze kutafutiwa ufumbuzi.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Mohammed Mussa Utaly. Kwa niaba Mheshimiwa Twaha Mwakioja.

Na. 239

**Ujenzi wa Nyumba za Askari Polisi Lindi Mjini**

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA K.n.y. MHE. MOHAMED M. UTALY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga upya nyumba za Askari Polisi Lindi Mjini ili kuboresha mazingira ya makazi na kuongeza ufanisi kwenye ulinzi na usalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Mussa Utaly, Mbunge wa Lindi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga nyumba za makazi ya Askari Polisi katika eneo la Mitwero kwenye kitalu namba saba lenye ukubwa wa mita za mraba 1,092,569. Kwa sasa kinachosubiriwa ni kupata hati ya kumiliki eneo hilo toka Halmashauri ya Manispaa ya Lindi, ili Serikali iweze kulipanga, kuandaa michoro na kutenga fedha kutoka kwenye bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha. Waheshimiwa wengine zimeni *mic* zenu. Mheshimiwa Asia zima *mic* yako.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Baada ya kulifuatilia kwa karibu suala hili imebainika kwamba mwaka 2024 halmashauri iliwasilisha nyaraka mbalimbali Wizara ya Mambo ya Ndani ili ziweze kusainiwa na kuweza kukamilisha mchakato wa hati. Je, Serikali kupitia Wizara hii ya Mambo ya Ndani, ipo tayari sasa kukamilisha mchakato huo kwa haraka ili hati iweze kupatikana na nyumba hizi ziweze kuanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Hali ya makazi ya sasa yana changamoto kubwa ya mifumo ya majitaka na yanahatarisha usalama wa kimazingira na afya zao. Je, pamoja na mradi huo mkubwa wa ujenzi wa nyumba hizo mpya, Serikali ipo tayari kuboresha hali hii ya sasa iliyopo ya mifumo ya majitaka ili kunusuru afya za Askari wetu hawa katika eneo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed kama ambavyo yameulizwa. Nikianza na swali la kwanza linalohusu upatikanaji wa hati, Mheshimiwa ameeleza kwamba toka mwaka 2024 wameshawasilisha nyaraka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, nimwahidi Mheshimiwa Twaha kwamba nitakwenda kuhakiki au kuthibitisha wasilisho hilo na ikiwa limefanyika kweli ninamuahidi kwamba ndani ya wiki ijayo tutakuwa tumesaini na kurejesha halmashauri ili hatua nyingine ziendelee.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pili wa kuhusu utayari wa Serikali kufanya ukarabati wa hali ya sasa ya makazi ya Askari wa Lindi, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea na hatua ya ukarabati wa majengo

mbalimbali nchi nzima. Hata hivyo, kwa upande wa eneo hilo na kwa mujibu wa ombi alilolitoa, ninamhakishia tu kwamba mwanzoni mwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 tutahakikisha kwamba tunafanya ukarabati katika makazi ya nyumba za Askari hapo Lindi.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Engineer* Fadhili.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Licha ya kazi nzuri inayofanywa na askari wa Jeshi la Polisi ndani ya Wilaya ya Tunduru, makazi ya askari wale ni mabaya sana: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba nyingine kwenye maeneo yale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Tunduru. Kama alivyouliza, Serikali inafanya tathmini ya mwisho ili kuandaa mpango kamili wa nchi nzima wa ujenzi kwa ujumla wa makazi ya askari polisi kama ambavyo imekamilisha kufanya kazi hiyo kwa upande wa vyombo vingine vya ulinzi na usalama, kama vile magereza na uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hatua za awali tumelenga kujenga angalau majengo mawili makubwa ya ghorofa katika kila mkoa kwa ajili ya makazi ya askari polisi ndani ya kambi zao.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Omar.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Hanang' ina nyumba 10 tu za askari polisi. Je, Serikali haioni haja sasa ya kujenga nyumba zingine ili kuongeza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Hanang'. Ninataka nimwahidi kwamba Serikali inaona haja ya kujenga nyumba za Askari Polisi katika wilaya hiyo. Tunamwahidi kwamba katika mpango ambao tunauelezea, basi tutahakikisha kwamba na eneo la wilaya hiyo tutalizingatia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Askari Polisi wa Taifa hili la Tanzania ni watu muhimu sana kwa kuwa wao wanalinda usalama na mali za wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali, nyumba za Askari Polisi kwenye Wilaya ya Rungwe, Mbeya Mjini, kota zao zina hali mbaya sana. Pamoja na hayo, Mbarali, Kyela, Chunya pamoja na mji mdogo wa Mbalizi hakuna nyumba za Askari Polisi kabisa. Je, ni lini majengo hayo yatafanyiwa ukarabati, hasa kwa sababu Askari wanawake wanapata shida sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake muhimu kuhusiana na ukarabati wa makazi ya Askari Polisi nchini.

Mheshimiwa Spika, tukiri kwamba hali ya makazi ya Askari Polisi kwa maeneo mengi haiko vizuri na ndiyo maana tukasema kwamba Serikali inaendelea kufanya tathmini ya hali ya makazi kwa maana ya ukarabati na ujenzi mpya kwa nchi nzima na kuweka mpango wa dharura na mpango wa muda mrefu wa kuweza kufanya ukarabati wa nyumba za makazi ya Askari.

Mheshimiwa Spika, pia, katika kuhakikisha hilo, katika Bajeti ya 2026/2027 tumefanya mazingatio hayo na tutaleta mbele ya

Bunge hili Tukufu mpango wa utekelezaji wa hayo ambayo Waheshimiwa Wabunge wanayauliza.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hija Hija.

**MHE. HIJA HASSAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ninaipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Kituo cha Polisi Jimbo la Kiwani, na hivi ninavyozungumza, kazi inaenda vizuri. Lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kukaa na viongozi wa jimbo kuandaa mpango kabambe wa ujenzi wa nyumba za Askari wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Hija kwa swali lake la msingi na ninampongeza kwa kujali jitihada za Serikali pamoja na sisi tunathamini mchango wao katika jitihada za ujenzi wa vituo. Pia kama ambavyo tunakwenda kwenye ujenzi wa vituo, basi tunamhakikishia tu kwamba tuko tayari vilevile kushirikiana na uongozi wa Jimbo la Kiwani kuhakikisha pia na makazi ya Askari yanajengwa kwenye eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nami nauliza swali dogo la nyongeza. Natambua kwenye Jimbo la Bunda Mjini kuna mpango wa kutujengea kituo kipya cha Askari Polisi kupitia bajeti hii. Serikali haioni kwamba sasa huo mpango uendane na nyumba za Askari Polisi ili waweze kufanya kazi kwenye mazingira mazuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana, pia ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini kwa swali lake la msingi na muhimu. Kwa kweli tumekuwa na ushirikiano wa

karibu na amekiri kwamba tuna mpango wa kujenga Kituo cha kisasa cha Polisi katika bajeti inayofuata.

Mheshimiwa Spika, ninataka kumthibitishia kwamba katika mpango tulionao wa Serikali wa kuhakikisha kuwa tunaweka makazi ya Askari, basi ujenzi huo wa kituo utaendana na mpango vilevile wa ujenzi wa makazi ya Askari.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shadya Omar.

**MHE. SHADYA HAJI OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri aliongozana nami kwenda kutembelea na kukagua makazi pamoja na Vituo vya Polisi, je, ni lini Serikali itaanza kujenga nyumba za Askari Polisi Mkokotoni na kukamilisha ujenzi wa nyumba za Askari katika Kisiwa cha Tumbatu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Shadya kwa swali lake la nyongeza la msingi na muhimu. Ninakiri kweli tulifanya ziara ya kutembelea Jimbo la Tumbatu na tukaenda kukagua ujenzi wa Kituo cha Polisi kule Tumbatu ambao umekamilika.

Mheshimiwa Spika, vilevile tukakagua ujenzi wa nyumba za makazi ya Polisi ambao hivi sasa unaendelea kule katika Kisiwa cha Tumbatu. Kuhusu lini ukarabati wa nyumba katika eneo la Mkokotoni, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatenga fedha kwenye mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za Mkokotoni.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo.

Na. 240

**Matokeo ya Utafiti wa Gesi Ziwa Tanganyika**

**MHE. BAKARI B. SHINGO K.n.y. MHE. BAZILIO K. MBWILO** aliuliza: -

Je, nini matokeo ya utafiti wa Mafuta na Gesi katika Ziwa Tanganyika upande wa Jimbo la Nkasi Kaskazini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Bazilio Kapunda Mbwilo, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika Ziwa Tanganyika ulianza kufanyika tangu mwaka 2010 hadi 2015 ambapo *TPDC* ilishirikiana na mwekezaji anayeitwa *Beach Petroleum* kutoka Australia. Shughuli mbalimbali za utafutaji zilifanyika ikiwemo uchukuaji wa *data* za mitetemo ndani ya Ziwa Tanganyika kuanzia maeneo ya Mahale hadi Kusini mwa Ziwa Tanganyika ikijumuisha maeneo ya Nkasi Kaskazini kwa upande wa Kilando na Kipili Ziwani.

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya *data* zilizochukuliwa ilibaini uwepo wa mashapo yanayoweza kuwa na mafuta au gesi asilia. Pamoja na matokeo hayo, Kampuni ya *Beach Petroleum* mwaka 2015 iliamua kurudisha kitalu Serikalini na kuacha eneo hilo likiwa wazi. Kuondoka kwao kulitokana na sera yao ya ndani ya kurudisha mali zao zote zilizokuwa nje ya Australia. Kuanzia kipindi hicho, utafutaji wa mafuta na gesi katika Ziwa Tanganyika ulisimama.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wakala wa Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli *(PURA)* inaendelea na maandalizi ya zabuni ya kutangaza vitalu kwa lengo la kutoa nafasi kwa wawekezaji kuendeleza shughuli za utafiti kwenye

maeneo yenye uwezekano wa uwepo wa mafuta na gesi yaliyo wazi ikiwemo Ziwa Tanganyika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Ukonga.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri, ninapenda kujua kwamba gesi inayotumika sasa katika makazi yetu kwa ajili ya kupikia na kwenye magari ni sehemu ya gesi ambayo inavunwa nchini?

Mheshimiwa Spika, kama ikiwa ni ndiyo, je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kupunguza bei ya vifaa vinavyotumika kama majiko ama mashine zinazotumika kwenye magari kwa ajili ya kutumia gesi kupunguza bei ili kuweza kupunguzia wananchi gharama za kuishi na kuachana na shida kubwa tuliyonayo sasa hivi ya mafuta?

**SPIKA:** Haliendani na swali la msingi lakini lijibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru kwa swali lake la msingi, lakini pili ninaomba kumwambia tu kwamba moja ya jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunapunguza gharama hususan kwenye hii Ajenda ya Mheshimiwa Rais ya nishati safi kwa wananchi wote. Ndiyo maana umeona katika kipindi cha hivi karibuni Mheshimiwa Rais alikuja na ajenda mpaka ya kutoa majiko ya gesi kwa wananchi kama kutoa motisha ili watu waweze kuingia katika mfumo wa nishati safi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo hilo ni sehemu ya mpango wa Serikali wa kupunguza hizo gharama ili kuhakikisha nishati safi inawafikia wananchi wote. Pia, kuna uwekezaji mkubwa ambao unafanywa na Wizara ya Nishati na Madini ili kuhakikisha kwamba uzalishaji wa gesi nchini unaongezeka na kufika mpaka katika maeneo ya vijijini ambapo sasa nishati safi itakuwa ni sehemu ya matumizi ya wananchi wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ninakushukuru, lakini mchukue jitihada za kutafuta mtafiti mwingine. Toka kisima hiki kimeachwa, sasa ni miaka 10. Mahitaji ya gesi na petroli ni

muhimu sana kwa Taifa. Fanyeni kazi haraka ili tujue nani sasa anakuja kuchukua nafasi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Arif.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Spika, swali lilikuwa linaenda kwenye Wizara ya Nishati, lakini umeshamruhusu sasa Mheshimiwa Waziri. Lilikuwa ni swali la nyongeza kwa Wizara ya Nishati.

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Arif, kaa chini. Wizara ya Madini, Mheshimiwa Mabula.

Na. 241

**Kutenga Maeneo ya Wachimbaji Wadogo – Msalala**

**MHE. MABULA J. MAGANGILA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatenga maeneo maalum ya wachimbaji wadogo katika Halmashauri ya Msalala?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango mkubwa wa wachimbaji wadogo katika Halmashauri ya Msalala na umuhimu wao katika kukuza sekta ya madini nchini. Katika kuwawezesha na kuwaendeleza, Serikali kupitia Tume ya Madini inaendelea kufanya mapitio ya kisheria ya leseni nane za utafiti ambazo hazijaendelezwa, kwa lengo la kuchukua hatua stahiki ikiwemo kuzifuta, na hatimaye kuyatenga maeneo husika kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya uchambuzi wa taarifa za *Geo Science* kwa leseni zitakazofutwa ili kubaini maeneo yenye tija kwa uchimbaji na kuyatenga rasmi kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Aidha, kwa maeneo yatakayobainika kukosa taarifa za kutosha, Serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* itafanya utafiti wa kina kabla ya kuyatenga rasmi, ili kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapatiwa maeneo yenye taarifa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji, na mchango wao katika uchumi wa Taifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Msalala wamekuwa wakisubiria taarifa hizi njema kwa muda mrefu na kwa kweli wapo tayari kufanya kazi katika maeneo haya ambayo yatatengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Je, ni lini Serikali itakamilisha mpango wake wa kuyatenga na kuyafanyia utafiti ili wananchi hawa sasa wakanufaike na maeneo haya maalum kwa ajili ya wachimbaji wadogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninachukua fursa hii kumpogeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akiwajali na kuwapigania wachimbaji wake wadogo katika eneo la Msalala. Zoezi la ufutaji wa leseni za utafiti limeshaanza. Nilishatoa maelekezo kwa *RMO's* wote nchi nzima kuzibaini leseni ambazo hazifanyiwi kazi na orodha ipo tayari. Wiki mbili zilizopita tumeanza na leseni 40, tutaendelea mpaka katika eneo la Msalala, tutazifuta na baadaye wachimbaji wadogo watapatiwa maeneo hayo.

**SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri.

Na. 242

**Kuweka Minara ya Simu katika Hifadhi ya Mkomazi**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza: -

Je, Serikali ina Mpango gani wa kuweka Minara ya Simu katika Hifadhi ya Mkomazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* imefanya zoezi la uainishaji wa maeneo yenye changamoto za mawasiliano katika Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi. Maeneo yaliyoainishwa ni Geti la Kamkota, Geti la Kimango, eneo la *Mkomazi View Camp* na Geti la Ndea. Maeneo haya yatatekelezwa kupitia mradi wa awamu ya 11 ambao utajikita katika kupeleka mawasiliano kwenye maeneo maalum ya kimkakati, ikiwemo vivutio vya utalii, hifadhi za Taifa, maeneo ya mipakani na kwenye njia za reli ya *MGR*, *SGR* na *TAZARA*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Nimeshauliza swali hili la mawasiliano katika Hifadhi ya Mkomazi zaidi ya mara tatu hapa Bungeni na majibu yanayoletwa ni haya haya. Wananchi wa Same wanataka kuisikia Serikali yao sikivu kwamba ni lini sasa Hifadhi hii itapelekewa mawasiliano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa ongezeko la watalii limeongezeka sana, mwaka 2022/2023 paliingiza watalii 3,500, mpaka sasa hivi 2026 wameingiza watalii 11,000. Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya haraka kupeleka mawasiliano haya katika hifadhi hiyo ili kuwapa tabasamu watalii katika hifadhi hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, tuna awamu ya 11 ambayo sasa hivi iko kwenye hatua za manunuzi. Awamu hii inajikita katika kupeleka mawasiliano katika maeneo yote ya kimkakati ikiwemo Hifadhi za Taifa kama nilivyoeleza, maeneo ya mipakani, maeneo ya njia za reli ya *MGR*, *SGR* na *TAZARA* na maeneo mengine yote ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tuko kwenye hatua ya manunuzi, namhakikishia Mheshimiwa Zuena kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha kabla haujamilika tutakuwa tumeanza zoezi la kujenga minara katika maeneo hayo aliyoyataja.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kuleta minara ya simu, bado Kata kubwa kama Makame, Partimbo, Sunya na Loolera zina changamoto ya mawasiliano. Nini kauli ya Serikali katika kutuletea minara angalau mitano hivi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, Serikali tumeandaa mkakati wa miaka mitano kuanzia mwaka 2025 – 2030 ambapo tutayafikia maeneo yote yenye changamoto yakiwemo maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, mkakati wetu huu tunalenga kwanza kuanza na maeneo yote yenye changamoto kubwa ya mawasiliano, tutafuata maeneo yenye nafuu kidogo na yenye nafuu zaidi. Kwa hiyo, maeneo yote ambayo ameyaeleza Mheshimiwa Mbunge kwamba yana changamoto kubwa, tutayapa umuhimu wa kwanza katika utekelezaji wa mkakati wetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuweza kuuliza swali la nyongeza. Kata ya Kulimi na Kata ya Mwabayanda Wilaya ya Maswa kuna shida sana ya mawasiliano. Je, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwamba Serikali ina mkakati wa miaka mitano kuhakikisha kwamba tunamaliza kabisa changamoto ya mawasiliano katika maeneo yote ya nchi hii. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika kipindi hiki cha miaka mitano, kufikia mwaka 2030 tutakuwa tumemfikia na changamoto aliyonayo ya mawasiliano tutakuwa tumeimaliza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Patali Patali.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbeya Vijijini lina jumla ya kata 28. Kati ya hizo, kata nane zikiwemo kata za Izyira, Iyunga Mapinduzi, Ikukwa, Mjele, Shizuvi, Ulenje na Ijombe hazina mawasiliano ya uhakika. Je, ni lini Serikali itapeleka minara ya simu ili kuimarisha mawasiliano kwenye kata hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Patali, amekuwa akifuatilia kwa karibu sana kuhusu minara katika Jimbo lake, ananikosesha pumzi, kama jana ambavyo Simba iliwakosesha pumzi Waheshimiwa wa Yanga wale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba suala lake hili kwa sababu ya kufuatilia kwa karibu, tunalifanyia kazi kama Wizara. Katika awamu ya 10 tunayoendelea na utekelezaji wake sasa hivi, Jimbo la Mbeya Vijijini litapata minara mitatu itakayojengwa na mtoa

huduma *Vodacom* ikiwemo Kata za Ijombe na Ulenje alizozitaja na kata nyingine ya Ilungu.

Mheshimiwa Spika, kata zinazobaki tutaziweka katika mkakati wetu wa miaka mitano tunaoutekeleza kufikia mwaka 2030, zitakuwa zote tumezikamilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kata ya Susuni, Mwema, Sirari, Mbogi, Nyansincha, Itiryo, Nyanungu, Gorong'a, ziko mpakani mwa Kenya ambapo wanasikiliza nyimbo za Kenya, wanasikiliza *Safaricom*, na wanapoteza mpaka uzalendo. Nimeuliza swali hili tangu mwaka 2020. Ni lini hizi kata zitapata mawasiliano ndani ya nchi ili tutunze na kulinda uzalendo wa Watanzania wetu kwa sababu kuna shida kubwa ya mawasiliano katika eneo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi kwamba tuna mradi wa awamu ya 11 ambao tunaanza kuutekeleza hivi karibuni, kwa sasa uko katika hatua ya manunuzi ambao umejikita kupeleka mawasiliano katika maeneo ya kimkakati ikiwemo maeneo ya mipakani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chacha anauliza kwamba ni lini? Ni karibuni, ninamhakikishia ndani ya mwaka huu wa fedha tutakuwa tumeanza kutekeleza maeneo hayo aliyoyataja na yatakayobaki, tutayaingiza katika mpango wetu wa miaka mitano wa utekelezaji wa ujenzi wa minara ya mawasiliano katika nchi hii yote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Mkomazi ni hifadhi mpya kwa maana ya hadhi na ingependa kuongezewa sana uwezo ili watalii waweze kwenda kutembelea, lakini maeneo mengi wanapata mtandao kutoka nje ya nchi kwa

maana ya nchi za mpakani. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inaimarisha mawasiliano katika hifadhi ile ili na yenyewe iweze kukua na kuwa kama hifadhi nyingine? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mwenyewe amesimama.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pia ninapenda kushukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nimshukuru Mheshimiwa Sekiboko kwa swali na hasa katika kuweka hakikisho la upatikanaji wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya mpakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Mheshimiwa Naibu ametangulia katika uwasilishaji wa majibu yetu, tayari tumeshafanya tathmini katika mikoa 11 katika maeneo ya kimkakati 124 na ikiwemo kwa upande wa Tanga, Wilaya ya Mkinga, inahusika na maeneo mengine yote ya mipakani ya Tanga, Mara, Kagera, Mbeya pamoja na mikoa mingine 11 kama nilivyotaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa tumeandaa mpango mkakati kupitia ruzuku yetu. Mfumo wa Ruzuku ambao ni *subsidy model* ambayo ni *competitive;* na tuna uhakika, kwa mfumo wa *framework agreement* mwezi Mei mwaka 2026, basi tutakuwa tumeshaanza taratibu, na tumpe uhakikisho tunatambua kama maeneo muhimu sana na mahsusi kwa suala zima la ulinzi na usalama, masuala ya kibiashara pamoja na huduma nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Sasa ni kipindi cha matangazo, na tunaanza na wageni. Kwanza ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambao ni Ndugu Mohamed Khamis Abdullah, Katibu Mkuu; Ndugu Nicholaus Mkapa, Naibu Katibu Mkuu; Mhandisi Dkt. Abubakar Makame Rajab, Mkurugenzi wa Idara ya Mawasiliano Zanzibar na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari ya Zanzibar; Balozi Adadi Rajabu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. *(Makofi)*

Ninaona Mheshimiwa Mwana FA na wewe unapiga makofi vilevile. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Jones Kilimbe, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Balozi Meja Jenerali (Mstaafu) Gaudence Milanzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Posta Tanzania; Mheshimiwa Balozi Valentino Mlowala, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Mawasilino kwa wote; Mheshimiwa Peter Mwasalyanda, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Ndugu Macrice Mbodo, Posta Masta Mkuu, Shirika la Posta Tanzania. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine ambao ni Mhandisi Albert Richard, Kaimu Mtendaji Mkuu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; Dkt. Nkundwe Mwasaga, Mtendaji Mkuu Tume ya Taifa TEHAMA; Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi; *CPA*. Moremi Marwa, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Mawasiliano Tanzania; Ndugu David Mwankenja, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Ndugu John Sicilima, Mkurugenzi Mtendaji wa MINARA; na Ndugu Aisha Dachi, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali.

Wengine ni Ndugu Pendo Mbele, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Utangazaji; Ndugu Yahya Mohamed, Afisa Mwendeshaji Mkuu wa Kampuni ya Azam *Media*; Ndugu Charlse

Kamoto, Mkurugenzi Mtendaji wa *AIRTEL Tanzania*; Ndugu Tran Thi Thuy Dung, Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya *VIETTEL;* Ndugu Jacqeline Kweka, Katibu Mtendaji wa Umoja wa Makapuni ya Huduma za Simu Tanzania; Ndugu Sylivia Balwire, Mkurugenzi wa Udhibiti, Kampuni ya *YAS*. *(Makofi)*

Wengine ni Ndugu Johnson Mshana, Mkuu wa Uhusiano Kampuni ya *DSTV Tanzania*; Ndugu Mashaka Ngole, Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki; Ndugu Albert Msando, Mkuu wa Wilaya ya Ubungo; Ndugu Ragati Mbowe, Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Ubungo; Ndugu Lawrence Mlaki, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Ubungo na Diwani wa Kata ya Goba; na Ndugu Ibrahimu Ally, Naibu Meya, Manispaa ya Ubungo. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Kairuki, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wakurugenzi Wakuu wa Vitengo kutoka Wizara na Taasisi zake. Viongozi na wataalamu kutoka Sekta Binafsi, Wenyeviti Wenezi Makatibu wa CCM kutoka Kata ya Jimbo la Kibamba Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Ubungo, Madiwani kutoka Jimbo la Kibamba. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Switbert Zacharia Mkama, Naibu Waziri, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Walimu Wakuu wa Shule za Msingi kutoka Ukerewe, Mkoani Mwanza. *(Makofi)*

Wapo wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Dotto Jasson Bahemu, huyu ni Ndg. Francis Mwaniwe, rafiki yake na mfanyabiasha kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah, ambaye ni Ndg. Seifu Ramadhani wa Kampuni *Executive Secretary Impact of Change Initiative* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Twaha Said Mwakioja kutoka Jijini Dar es Salaam.

Wengine ni wageni wanane wa Mheshimiwa Selina Henry Kingalame, ni Viongozi wa TAHILISO.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndg. Dorah Mweta, Mwanasheria Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Pia wapo Maafisa wanne kutoka Kampuni ya *NETIS Tanzania Limited* ya Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyoelezwa kwenye Kikao cha *Briefing*, kwa Wabunge wote na baadaye Katibu wa Bunge kutoa tangazo kwenye Gazeti la Serikali, mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe 4 Mei, 2026 saa nne na nusu asubuhi kutafanyika Uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, uchaguzi huu unafanyika ili kuziba nafasi wazi kufuatia Wabunge watatu ambao walikuwa ni miongoni mwa wa Bunge la Bunge hilo kuchaguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wabunge hao ni Mheshimiwa James Kinyasi Millya na Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Jumanne Maghembe kutoka kundi D na Wagombea wa Tanzania Bara na Mheshimiwa Angela Charlse Kizigha kutoka kundi A la wagombea wanawake.

Baada ya kukamilika kwa taratibu za kuwapata magombea wa nafasi hizo leo siku ya Alhamisi tarehe 30 Aprili ambayo ndiyo siku ya uteuzi. Katibu wa Bunge ambaye ndiye Msimamizi wa Uchaguzi huo, atatoa taarifa kukamilika kwa zoezi la uteuzi na hivyo kuwataja Wagombea wa nafasi hizo.

Waheshimiwa Wabunge, wote mnahimizwa kudhuria bila kukosa siku hii ya uchaguzi ili kufanikisha zoezi la kuwapata washiriki wetu katika Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Wabunge wote wa CCM, anawatangazia kwamba kutakuwa kikao leo Alhamisi

tarehe 30 Aprili, 2026 saa 7.00 mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa hapa Bungeni. Waheshimiwa Wabunge wote wa CCM mnaombwa kuhudhuria kikao hicho bila kukosa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mwenyekiti kuendelea na kazi zilizopangwa leo.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha wa2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetujalia sote afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Tatu. Aidha,

ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 ikiwa ni bajeti yangu ya kwanza tangu nilipoteuliwa kuongoza na kusimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua Mheshimiwa Dkt. Switbert Mkama, kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaahidi kwa Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi wote kwa ujumla kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote katika kuendeleza Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ili kuwezesha nchi kufikia adhma yake ya kuwa na uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa unyenyekevu mkubwa, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na wananchi zaidi ya milioni 31.9 katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 na kumwezesha kuongoza Taifa letu katika kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya kauli mbiu ya “Kazi na Utu, Tunasonga Mbele.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha siku 100 tumeweza kumshuhudia Mheshimiwa Rais tangu alipoapishwa amefanya jitihada mbalimbali ambazo zimeendelea kufanyika kuweka mazingira wezeshi yanayochochea ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano, kama vile minara 758, Uongezaji wa Nguvu wa Minara 304, Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano kwa kushirikiana na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano na Uunganishwaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika nchi ya Jamhuri ya

Kidemokrasia ya Kongo – DRC. Hii kwa dhahiri inaonesha imani kubwa iliyopo kati ya wawekezaji na Serikali yetu ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano itaendelea kutekeleza miradi nane ya maendeleo ikiwemo mkongo wa Taifa wa mawasiliano, Mawasiliano Vijijini, Mradi wa Tanzania ya Kidijiti, Mradi wa Anwani ya Makazi na *post code*, ujenzi wa Kituo Kikuu na vituo vidogo vya kuendeleza ubunifu katika TEHAMA, kujenga uwezo wa taasisi katika utekelezaji wa majukumu, kuendeleza ubunifu, utengenezaji wa vifaa vya TEHAMA, na uanzishwaji wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijiti itakayojengwa hapa Nala Dodoma ili kufikia matarajio makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha Huduma za Mawasiliano zinawafikia Watanzania wote kama ilivyofafanuliwa katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri sana aliyoiwasilisha hapa Bungeni, ambayo kwa kiasi kikubwa imeweza kutoa Dira na Mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika mwaka wa fedha wa 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeeleza kwa kina mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2025/2026, Mipango ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 na Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaahidi kwamba Wizara ninayoiongoza itayafanyia kazi masuala yote yanayohusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kama yalivyoainishwa katika Hotuba na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili hotuba hiyo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Kumi na Tatu, la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatambua mchango wa Mheshimiwa Spika kwa namna ambavyo amekuwa akiibua mijadala mbalimbali yenye lengo la kuboresha sekta ya TEHAMA. Sote ni mashuhuda wa mabadiliko ambayo yametokana na mchango wa Mheshimiwa Spika wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika uongozi wa Mheshimiwa Spika na Naibu Spika umelifanya Bunge letu kuendelea kuwa chombo imara cha kutunga sheria, kusimamia Serikali na vilevile kuwakilisha wananchi kiufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mheshimiwa Najma Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini; na wewe Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Aidha, ninawapongeza kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Spika kutekeleza majukumu ya kuongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara

mbalimbali wanazozisimamia. Ninaendelea kuwaahidi ushirikiano wangu wa dhati katika kutekeleza majukumu yetu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa, ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Tanganyika kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu pamoja na Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa uchambuzi wao makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 68, kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 na kupitisha Bajeti ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Wajumbe wa Kamati yamezingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2026/2027. Vilevile, ninapenda kumshukuru sana Ndugu Baraka Leonard, Katibu wetu wa Bunge pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa uratibu wa shughuli za kila siku za Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa ninaomba kutoa shukrani za dhati kwa Chama cha Mapinduzi kwa kunichagua na kuniteua kuwa Mgombea wa CCM katika Jimbo pendwa la Kibamba katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025. Kwa hakika hii ni heshima kubwa na dhamana ya kipekee ambayo nitailinda kwa uadilifu na uwajibikaji mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninapenda kuwashukuru kwa moyo wa dhati na moyo mkunjufu wananchi wote wa Jimbo la Kibamba kwa kunipa kura nyingi za kishindo na kuniamini kuwa mtumishi na mwakilishi wao. Imani yao kwangu, upendo wao, ushirikiano na mshikamano kwa mama yao mzungu umekuwa nguzo ya mafanikio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kipekee kuchukua nafasi hii kumshukuru mume wangu mpenzi, Mheshimiwa Balozi Mbelwa Kairuki, pamoja na watoto wetu wapendwa Precious Kemilembe, Esther Kokubelwa pamoja na Hubert Mwesigwa kwa upendo wao na faraja yao kwangu wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru kwa kunivumilia ninapokuwa mbali nao, wanavyoniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ya kusimamia sekta hii ya kipekee ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na ninapohudumu katika Jimbo langu la Kibamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa pole kwa Bunge Tukufu, familia, ndugu, jamaa, marafiki na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na Wapendwa Wetu; Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Isimani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu, lakini ambaye pia niliwahi kuhudumu kama Naibu Waziri wake alipokuwa Waziri wa Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninapenda kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho. Wizara yetu ya Mawasiliano inatambua mchango mkubwa uliofanywa na Waheshimiwa Viongozi waliotutangulia, hasa katika utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nitoe pole kwa kuondokewa na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum akiwakilisha Kundi la Wafanyakazi. Tunawaombea Marehemu wote, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuona umuhimu wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari na kuweka mazingira wezeshi yanayovutia uwekezaji ambayo yamewezesha upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kisekta ambayo utekelezaji wake unachochea ukuaji wa uchumi wa Kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha uongozi wa Mheshimiwa Rais, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepata mafanikio ikiwemo kukamilisha ujenzi wa minara 758, kuongeza nguvu minara 304 iliyokuwa ya *2G* kwenda *2G, 3G* na *4G* ambapo miradi hii imekamilika kwa 100% na ujenzi wa minara hiyo unawanufaisha wananchi takribani milioni 8.5 na kwa minara 304 tuliyoongezea nguvu inawanufaisha wananchi milioni 4.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatekeleza Mradi wa Mawasiliano Vijijini wa ujenzi wa minara 636 ambapo minara 456 sawa na 72% imekamilika. Aidha, kati ya minara 456 iliyokamilika, minara 342 tayari imewashwa na inatoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa minara 114 iliyobakiwa, inatarajiwa kuwashwa ifikapo Juni, mwaka 2026, baada ya kukamilisha kazi ya ufungaji wa vifaa. Aidha, minara 180 iliyobakia inatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba, mwaka 2026. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha wananchi takribani milioni 2.5 kufikiwa na huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Wilaya 86 nchini na kuunganisha nchi saba kati ya nane. Kwa sasa Serikali imeanza utaratibu wa kuiunganisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo – *DRC* katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wizara imeendelea kusimamia ufikishaji wa miundombinu ya *fiber* mlangoni ambapo ilikusudiwa kufanya maunganisho 279,795. Hata hivyo, hadi mwezi Machi mwaka huu, ujenzi wa njia za maunganisho 132,793 umekamilika na kuwezesha kutoa huduma kwa wateja 64,266 kati ya 126,740 sawa na 51% ya lengo lililokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina majukumu ya kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera zinazohusu Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Posta na Mawasiliano ya Simu; kufanya tafiti za maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA; kuendeleza Wataalamu wa TEHAMA; kuanzisha na kusimamia Mfumo Postikodi; kusimamia na kuendeshaji

Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; kusimamia ulinzi na usalama wa TEHAMA; kuboresha utendaji kazi na uendelezaji wa rasilimali watu ndani ya Wizara; na kusimamia Taasisi, Programu na Miradi ndani ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano pia inasimamia Taasisi sita na baraza moja, ikiwemo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)*, Shirika la Posta Tanzania *(TPC)*, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)*, Tume ya TEHAMA *(ICTC)*, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi *(PDPC)* na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano *(TCRA-CCC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinabainisha kwamba, sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari imeendelea kukua na kutoa mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na mwaka 2023. Aidha, kulingana na taarifa ya hali ya uchumi wa Taifa ya mwaka 2024 shughuli za habari na mawasiliano zilikua kwa 14.3% ikilinganishwa na ukuaji wa 7.6% kwa mwaka 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na miundombinu ya mawasiliano; matumizi ya simu za mkononi na mitandao ya kijamii; mikutano ya mitandaoni; na matumizi ya malipo kupitia mitandao ya simu. Aidha, ukuaji huu umewezesha mchango wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari katika pato la Taifa kuongezeka kutoka 1.5% kwa mwaka 2023 hadi 1.6% kwa mwaka 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari ni sekta wezeshi na sekta mtambuka inayowezesha utekelezaji wa majukumu ya sekta nyingine kwa kutumia TEHAMA. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaendelea na uandaaji wa akaunti maalumu ya kupima uchumi wa Kidijitali *(Digital Economy Satellite Account – DESA)* ili kuongeza wigo wa upimaji wa mchango wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari kwenye pato la Taifa ili kutambua kwa usahihi mchango halisi wa sekta ya mawasiliano katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026 Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)*, Benki Kuu ya Tanzania, Tume ya Taifa ya Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Mamlaka ya Serikali Mtandao *(e-GA)* na Tume ya TEHAMA wameanza kukusanya takwimu zitakazotumika katika uandaaji wa Akaunti ya Upimaji wa Uchumi wa Kidijitali *(DESA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari imeendelea kukua. Aidha, takwimu zinaendelea kuonesha kwamba laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka laini milioni 90.4 Machi, 2025 hadi kufikia laini milioni 111.9 Machi, 2026 sawa na ongezeko la 23.8%. Aidha, watumiaji wa *internet* pia wameongezeka kutoka milioni 49.3 kwa Machi, 2025 hadi milioni 58.9 Machi, 2026 sawa na ongezeko la 19.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoaji wa huduma za kutuma na kupokea fedha kwa njia ya mtandao wa simu, wameongezeka kutoka milioni 66.5 Machi, 2025 hadi milioni 81 Machi, 2026 sawa na ongezeko la 21.8%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, idadi ya watoa huduma wa miundombinu ya mawasiliano imefikia watoa huduma 52 kwa mwezi Machi, 2026 ikilinganishwa na watoa huduma 38 waliokuwepo Machi, 2025 sawa na ongezeko la 36.8%. Watoa huduma za ziada *(Application Services and Value-Added Services)* wamefikia 173 kwa Machi, 2026 ikilinganishwa na watoa huduma 136 waliokuwepo Machi, 2025 sawa na ongezeko la 27.2%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaendelea kuonesha kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano na teknolojia ya habari kutokana na uwepo wa mazingira wezeshi ambayo ni maono na Dira ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na ujenzi wa minara ya mawasiliano ambapo kata 688 nchini zimepelekewa huduma ya mawasiliano kwa kujenga minara ambayo imeweza kuwanufaisha wananchi milioni 8.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufikishaji wa huduma ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika wilaya 86 kumewezesha kurahisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wananchi pamoja na utambuzi wa makazi unaofanywa kupitia Mfumo wa Anwani za Makazi. Hatua hizi zote zimewezesha baadhi ya maeneo yaliyokuwa na changamoto za mawasiliano kufikiwa na huduma za mawasiliano na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za Posta hususani usafirishaji wa vifurushi na vipeto, zimeendelea kuimarika nchini ambapo hadi mwezi Machi, 2026 jumla ya vifurushi na vipeto 142,496 vilitumwa ndani ya nchi. Aidha, kwa upande mwingine, hadi kufikia mwezi Machi, 2026 vifurushi na vipeto 286,334 viliweza kupokelewa ndani ya nchi ikilinganishwa na vifurushi na vipeto 183,348 vilivyopokelewa mwezi Machi, 2025 sawa na ongezeko la 56.2%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka 10 mwaka 2024 - 2034 ambapo Wizara kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali umewezesha maboresho ya miundombinu na mifumo ya TEHAMA ambayo maboresho hayo ndiyo msingi wa utekelezaji wa mkakati huo wa miaka 10. Aidha, mkakati huu unatekelezwa na sekta ya umma na binafsi kulingana na majukumu ya taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali unatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeandaa Mfumo wa Kielektroniki kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkakati ili kuiwezesha Serikali na sekta binafsi kuweza kutoa taarifa ya hatua iliyofikiwa kwa kila kiashiria katika utekelezaji wa mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea pia kuratibu maboresho ya Mifumo mbalimbali nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali kwa kuwezesha wananchi wetu kuweza kupata huduma za mawasiliano na

huduma nyinginezo katika ubora kusudiwa. Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma imeweza kufanya pia maboresho katika mifumo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkakati huu unatekelezwa na sekta binafsi kulingana na majukumu ya taasisi husika na ni kwa muktadha na kwa umuhimu huo, Serikali imeandaa Mfumo wa Kielektroniki wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa mkakati ili kuiwezesha Serikali na sekta binafsi kutoa taarifa ya hatua iliyofikiwa kwa kila kiashiria katika utekelezaji wa mkakati huo, na kuwezesha nchi yetu kuwa na mwelekeo unaoshabihiana katika kuhakikisha TEHAMA inachangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliahidi kutoa shilingi bilioni 200 kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuwezesha biashara ndogo, za kati na uendeshaji wa kampuni changa *(Startups)*. Aidha, Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni tano ni kwa ajili ya kuwezesha mitaji kwa Kampuni Changa za TEHAMA ili kukuza bunifu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla, Mheshimiwa Rais ametekeleza ahadi hii kwa kuwezesha upatikanaji wa shilingi bilioni tano kwa ajili ya mitaji ya kuwezesha uendeshaji wa Kampuni Changa za TEHAMA nchini. Aidha, kwa sasa, Wizara ya imekamilisha uandaaji wa mwongozo utakaowezesha kuwapata wanufaika wa mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa mikopo hiyo utafanywa na Benki ya *NMB* na inatarajiwa tutaweza kutoa mikopo kwa kampuni zisizopungua 50 changa za TEHAMA ambazo zitakuwa zimekidhi vigezo katika maeneo yanayogusa masuala ya kidjitali katika afya, sheria bunifu za fedha, utalii, bima, elimu, pamoja na mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi rasmi yatapokelewa kupitia mfumo wa kidijitali ambao utaunganishwa moja kwa moja na *NMB* ili kuweza kurahisisha zoezi la uchambuzi wa kuwapata wanufaika. Aidha, mikopo hii inatarajiwa kuanza kutolewa mwezi

Mei, mwaka 2026 kwa wanufaika wote watakaokuwa wamekidhi vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano iliidhinishiwa shilingi 291,533,139,000. Kati ya fedha hizo shilingi 14,485,656,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 277,047,483,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 6.9 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 7.5 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kati ya fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 98.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 178.5 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 120.3 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Machi, mwaka 2026 Wizara imeweza kukusanya shilingi bilioni 160.6 sawa na 133.5% ya lengo lililokusudiwa. Ufanisi huu umetokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika miundombinu ya mawasiliano ikiwemo kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambao umeunganishwa katika wilaya 86 na kuongeza uwezo wa njia za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepokea na kutumia shilingi bilioni 147.7 sawa na 50.6% ya lengo lililokusudiwa. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 7.8 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 139.8 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 4.1 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 3.7 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Vilevile, kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 55.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 84.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Sekta ya Mawasiliano na teknolojia ya habari

imeweza kuandaa waraka wa mapendekezo ya kutunga Sera mpya ya Taifa ya TEHAMA na kuhuisha Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi ndani ya Serikali kwa ajili ya kuridhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza pia kuanza taratibu za utungwaji wa Sheria ya Anwani ya Makazi pamoja na Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidjitali ya Mwaka 2026. Tumeweza kusimamia ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara zilizopo Mtumba, tumekamilisha ujenzi wa minara 758 nchini sawa na 100% la lengo lililokusudiwa, na tumeweza kuongeza nguvu katika kata minara 304 katika kata 231.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tumekamilisha ujenzi wa minara 456 kati ya 636 sawa na 72% ya lengo lililokusudiwa. Tumeweza kukamilisha taratibu za ununuzi wa vifaa vya uundaji wa *satellite* ndogo ya *CubeSats* kupitia mradi wa *UNOOSA* unaojulikana kama *KiboCUBE*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, usajili wa *satellite* umefanyika katika chombo kinachoratibu shughuli za anga za juu cha Kimataifa *ITU*. Tumeweza kuimarisha ushiriki wa Tanzania kikanda na Kimataifa ikiwemo kuweza kushiriki katika mikutano ya Umoja wa Posta Duniani, Umoja wa Mahusiano ya Simu Duniani: ambapo Tanzania ni Mjumbe wa Baraza la Utawala la *ITU* kwa miaka minne mpaka mwaka 2026, Baraza la Utawala na Baraza la Uendeshaji wa Posta kwa kipindi cha mpaka mwaka 2029.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *ITU* imemteua Mtanzania kuweza kuongoza Ofisi ya *ITU* Kanda ya Afrika. Tumeweza pia kuona kuongezeka kwa mapato ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka shilingi bilioni 56.3 mwezi Aprili, 2025 hadi shilingi bilioni 160.6 Machi, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza pia kukamilisha ujenzi wa kilometa 801 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupokea Mkongo wa Mawasiliano uliojengwa na umoja wa watoa huduma za mawasiliano *(Consortium Telco Operators)* wenye kilometa 1,193 na kufanya jumla ya kilometa zilizojengwa hadi sasa kufikia kilometa 15,167.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeunganisha wilaya 13 na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufanya jumla ya wilaya zilizounganishwa na Mkongo hadi sasa kufikia 122 kati ya 139 sawa na 87.8%. Tumesimamia utekelezaji wa hati ya maridhiano kati ya Serikali na umoja wa watoa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili mwaka 2026 *Consortium* imeweza kukabidhi umiliki wa miundombinu ya Mkongo wa Mawasiliano na kufanya malipo ya Dola za Kimarekani milioni 11.4 kati ya Dola za Kimarekani milioni 20 na kufanya uwekezaji kwenye Mkongo wa Taifa wenye thamani za Dola za Kimarekani milioni 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesimamia hati ya maridhiano kati ya Serikali na Kampuni ya *VTL* na kuweza kufanya maboresho katika kilometa 19,023 na kujenga minara 70 ya mawasiliano ya simu katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kufanya malipo ya awali ya shilingi bilioni 10.4 na Dola za Kimarekani milioni 2.2 kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuiunganisha Kongo *DRC* na Tanzania. Vilevile, tumeweza kuunganisha maeneo 50 ya umma na huduma ya *Wi-Fi* ya bure na kufanya jumla ya maeneo yaliyounganishwa kufikia 61 kati ya 120 sawa na 51% ya lengo lililokusudiwa. Tumesimamia maunganisho 132,793 ya lengo lililokusudiwa kwa ajili ya kufikia miundombinu ya *fiber* mlangoni ambapo jumla ya wateja 64,266 sawa na 51% wameunganishwa na huduma ya *fiber* mlangoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kufunga vifaa vya mikutano kwa njia ya *video* au *video conferencing facilities* katika vituo 98 vya Haki Jinai kwenye Ofisi za Taifa za Mashtaka vituo 20, Magereza 38, Jeshi la Polisi Bara vituo 34, Jeshi la Polisi Zanzibar vituo sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tumefunga vifaa hivyo vya *Video of conferencing* katika ofisi mbili za Wizara katika jengo letu la Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Tumekamilisha pia upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kuhifadhi *data* vya Dodoma na Mjini Magharibi Zanzibar. Tumegawa

vishikwambi 3,682 kwa watendaji wa Serikali za Mitaa, Shehia, waratibu wa Kitaifa na mikoa ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma kwa wananchi kidjitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kuunganisha mfumo wa Anwani na Makazi *NaPA* na mifumo mitatu ya kutolea huduma ambapo tayari kupitia mfumo wa *NBS* na mfumo wa ajira wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, umeweza kuunganishwa, na imesababisha mifumo 29 kuweza kuunganishwa na mfumo huu wa *NaPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeweza kufanya uhakiki wa anuani za makazi 48,492 katika halmashauri tatu za Jiji la Mbeya, Manispaa za Songea na Iringa na kufanya jumla ya anuani za makazi zilizosajiliwa kuongezeka kutoka 238,958 hadi 247,502 sawa na ongezeko la asilimia tatu nukta nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewezesha pia, kutoa barua za utambulisho 665,689 kidijitali kwa waombaji wapya wa mikopo ya elimu ya juu kupitia bodi ya mikopo na kufanya jumla ya barua za utambulisho 715,156 kutolewa kidijitali kupitia mfumo wa anuani za makazi. Idadi hii inajumuisha waombaji 32,083 wa ajira za Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tumekamilisha pia taratibu za upatikanaji wa eneo lenye ukubwa wa mita milioni 1.6 lililopo Nala, Dodoma, kwa ajili ya kujenga Chuo cha kisasa kabisa cha Taifa cha Teknolojia ya Kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumewezesha utoaji wa vifaa 1,371 vya TEHAMA kwa taasisi mbalimbali za Serikali, ili kuweza kuchochea matumizi ya TEHAMA nchini. Tumetoa elimu kwa umma kuhusu ulinzi na usalama wa mtandao kwa makundi mbalimbali ya kijamii, lakini vilevile tumewezesha ujenzi wa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Matukio na Makosa ya Mtandao unaotumiwa na Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi na usalama mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa leseni 1,048 za mawasiliano. Vilevile, tumefanya upimaji wa ubora wa

mawasiliano ya simu kwenye mitandao mitano ya *Vodacom, Airtel, Viettel, TTCL* na Honora katika mikoa 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar, ili kuhakikisha ubora wa maudhui yanayotolewa unaendana na ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendesha mnada wa uuzaji wa masafa ya mawasiliano yaliyowezesha Serikali kuweza kupata mapato ya shilingi bilioni 235.7. Aidha, masafa haya yatawezesha kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia ya *5G* nchini. Tumefanyia kazi matukio 198 yaliyoripotiwa kuwa ni viashiria vya uhalifu mtandaoni na kutoa ushauri kwa umma na wadau wa sekta ya mawasiliano, ili kuimarisha usalama mtandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefanya maboresho ya mfumo wa usafirishaji wa *SWIFTPST* kupitia Posta kwa lengo la kuongeza ufanisi na ubora wa huduma. Tumeboresha na kuongeza wigo wa usafirishaji wa sampuli za kimaabara kuanzia vituo vya afya ngazi ya kata hadi maabara kuu za upimaji nchini kutoka mikoa 12 hadi mikoa 31 sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesimamia ujenzi wa jukwaa la biashara mtandaoni kwa ajili ya kuwezesha wananchi wetu kuuza na kununua bidhaa na huduma mtandaoni. Tumewezesha ununuzi wa magari 12 kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya shirika la posta. Tumeboresha huduma za mawasiliano nchini kwa kusaini mikataba na watoa huduma za mawasiliano ikiwemo *TTCL*, *Airtel*, Honora na *Vodacom,* kwa ajili ya kujenga minara 287 kupitia mradi wa mawasiliano vijijini awamu ya kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 600 wa shule za umma za msingi na sekondari na kati ya walimu hao tajwa, 100 wanatoka Zanzibar na 500 wanatoka Tanzania Bara. Tumeweza kusajili kampuni changa 402 za TEHAMA, ili kuzitambua na kuzikuza, ili ziweze kukidhi mahitaji ya kupata mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa ukuaji sekta ya mawasiliano na teknolojia ya Habari, kwa hakika unachangiwa kwa asilimia kubwa na ushiriki wa sekta binafsi, hasa katika ujenzi

na usambazaji wa miundombinu ya mawasiliano. Mathalani, katika ujenzi wa minara ya mawasiliano, watoa huduma za mawasiliano Honora, *Airtel*, *Halotel*, *TTCL* na *Vodacom* wamekuwa wakichangia 60% ya gharama za ujenzi kwa kila mnara, tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, sekta binafsi pia, inashiriki katika kuchochea uchumi wa kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa mtumiaji wa mwisho au *last mile connectivity*, hali inayoongeza kasi ya upatikanaji wa huduma ya *internet*, ikiwemo majumbani pamoja na katika maeneo ya umma. Kampuni za sekta binafsi za mawasiliano zinazohusika na ujenzi wa minara, hadi mwezi Machi zimejenga jumla ya minara 9,124. Kati ya minara hiyo, 1,655 imejengwa kwa ushirikiano wa Serikali na sekta binafsi kupitia *UCSAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii imeweza kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za simu na *internet* kwa takribani wananchi milioni 46. Aidha, pamoja na kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano, minara hii imewezesha sana kupunguza gharama kwa waendeshaji wa mitandao na kuwezesha ujumuishaji wa kidijitali katika maeneo ya vijijini na pembezoni, ambapo hapo awali hayakuwa yakipata huduma za uhakika za mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoa huduma za mawasiliano kwa hakika wamekuwa na mchango mkubwa kwenye sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari ambapo wamewezesha utoaji wa mikopo ya ukuzaji wa biashara ndogo na za kati, utoaji wa ajira za kudumu na zisizo za kudumu kwa wananchi wetu, ufikishaji wa huduma za *internet* katika maeneo ya umma, lakini pia kufungua fursa za biashara mtandaoni. Hatua hii itaendelea kuwezesha kufikia malengo yaliyoainishwa katika Mkakati wetu wa Miaka Kumi wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu mengine ya sekta yetu ni kama ambavyo yameainishwa katika Kitabu cha Hotuba yangu, ukurasa wa 15 hadi 43 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Ninaomba kitabu chote kiweze kuingizwa katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 umezingatia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoyatoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano, tarehe 14 Novemba, 2025; Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 hadi 2028/2029; Dira yetu ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2026 mpaka 2031; Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; na pia, Maoni na Ushauri wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu; pamoja na ahadi, na maagizo mbalimbali ya Viongozi wetu Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vipaumbele vya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka ujao wa Fedha 2026/2027, tutajikita kutekeleza vipaumbele nane kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa miongozo inayosimamia sekta ya mawasiliano na teknolojia ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambapo tutasimamia utekelezaji wa mkakati wa uchumi wa kidijitali wa miaka kumi na tutakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakamilisha utungaji wa Sera Mpya ya Taifa ya *TEHAMA*, tutakamilisha utungaji wa Sera ya Taifa ya Anga za Juu, na pia Sera ya Taifa ya Kampuni Changa, tutakamilisha taratibu za uridhiwaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014, tutakamilisha taratibu za uridhiwaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Uhalifu wa Mtandao wa Mwaka 2025, na pia tutakamilisha Mikataba miwili ya Kimataifa ya Anga za Juu na kuendelea na taratibu za utungaji wa Sheria, anuani za makazi na Sheria ya *TEHAMA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha pili, tutaimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na posta nchini,

ambapo tutaimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na redio katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakamilisha ujenzi wa minara 636, tutaeendelea na ujenzi wa minara mingine mipya 287 nchini, ambapo itakamilika Machi, 2027, tutajenga minara mingine katika awamu ya 11, minara 280 katika maeneo ya kimkakati yenye changamoto za mawasiliano kwenye miundombinu ya reli ya *SGR*, *MGR* na *TAZARA*, Hifadhi za Taifa, pamoja na mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, tutaweka mazingira wezeshi, kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara mtandao nchini ambapo tutaratibu na kusimamia Mradi wa Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Bidhaa za Biashara Mtandao Nchini. Tutasimamia uundaji wa mfumo wa kidijitali utakaowezesha biashara mtandao na tutafanya tathmini ya mifumo ya kidijitali na kusajili majukwaa ya biashara mtandao na huduma za kielektroniki nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, tutaimarisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali ambapo tutaunganisha wilaya zetu katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Tutaunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kupitia Ziwa Tanganyika. Tutawezesha ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Dodoma na Zanzibar, tutawezesha usanifishaji na uboreshaji wa vifaa vya mikutano ya video katika wilaya 100 nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutawezesha kufikisha huduma za *Wi-Fi* katika maeneo 100 ya umma nchini, tutaratibu maunganisho ya *broadband* kwenye taasisi 100 za umma, Mji wa Serikali Mtumba na shule 100 za umma katika maeneo yetu ya Bunge na kuwezesha maunganisho 321,000 ya miundombinu ya huduma za *fiber*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha tano, tutaimarisha ulinzi wa usalama wa anga ya mtandao, ambapo tutaendelea kujenga uelewa kwa wananchi wetu kuhusu ulinzi wa taarifa na faragha zao na jinsi ya kukabiliana na matukio ya utapeli na wizi

mtandaoni, kuwezesha upatikanaji wa Mfumo wa Kitaifa wa ufuatiliaji wa matukio na makosa ya mtandao nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutatoa elimu juu ya miongozo ya miundombinu muhimu ya *TEHAMA* na kuimarisha ulinzi wa miundombinu hiyo pamoja na kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya Usalama wa Mtandao na kuandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mkakati wa usalama wa mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha sita ni kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa kampuni changa za TEHAMA au *ICT start-ups,* ambapo tutasimamia uanzishwaji wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali Nala. Tutawezesha uanzishwaji wa vituo saba vya kukuza ubunifu wa *TEHAMA*, tutafanya tafiti tatu za matumizi ya teknolojia za kidijitali zinazoibukia katika sekta ya uzalishaji na sekta ya huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutasimamia utekelezaji wa programu mbili za uwezeshaji wa wabunifu wa kampuni changa za *TEHAMA,* tutawezesha uanzishwaji wa vituo viwili vinavyotembea vya kupata taarifa za *TEHAMA* au *Mobile Information Access Centres.* Tutasajili kampuni changa 100 za ubunifu wa *TEHAMA* nchini na kuwezesha mafunzo kwa kampuni changa 25 za *TEHAMA* nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha saba, tutaimarisha uwekezaji katika *TEHAMA* na utekelezaji wa programu ya anga za juu, ambapo tutawezesha kurusha *satellite* moja katika anga za juu, tutaratibu mradi wa kurusha *satellite* ndogo ya mafunzo au *CubeSat* na kujenga uelewa kwa wananchi wetu kuhusiana na matumizi ya teknolojia ya anga za juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha nane, tutatoa elimu kwa umma kuhusu masuala yanayohusu mawasiliano na teknolojia ya habari, pamoja na teknolojia zinazoibukia, ambapo tutaelimisha umma kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kuhusu matumizi sahihi na salama ya mawasiliano na kuwajengea uelewa wananchi wetu kuhusu teknolojia zinazoibukia, ikiwemo akili unde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango mingine ya Wizara ni kama inavyoonekana na kufafanuliwa katika ukurasa wa 44 hadi 45 wa hotuba yangu. Kwa moyo wa dhati, ninapenda kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuweka kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hatua hii imewezesha Wizara yetu kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano wao wanaaoendelea kuutoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, natumia fursa hii tena kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Switbert Mkama, Mbunge na Naibu Waziri Wangu, kwa kuendelea kunisaidia katika kuiongoza Wizara yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, ninawashukuru sana kwa dhati Katibu Mkuu, Ndugu Mohammed Hamis Abdullah, na Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Nicholas Mkapa, kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninawashukuru sana Wakuu wa Idara na Vitengo wa Wizara yetu, Wenyeviti wa Bodi na Wakurugenzi wa Taasisi zinazosimamiwa na Wizara, pamoja na viongozi wa taasisi na watumishi wote wa Wizara yetu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawasihi waendelee kutekeleza majukumu yao kwa bidii, kwa uadilifu na moyo wa kujituma wakitambua kwamba, mchango wao ndiyo nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya Wizara yetu na Taifa kwa ujumla ya kuufikia uchumi wa kidijitali wenye tija. Mfumo jumuishi na endelevu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutumia fursa hii kuwatambua na kuwashukuru washirika wetu wa maendeleo tunaoshirikiana nao katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikiwemo Benki ya Dunia kupitia Dirisha la Wakala wa Maendeleo

ya Kimataifa *IDA*, Umoja wa Posta Duniani *UPU*, Umoja wa Mawasiliano Duniani *ITU*, Umoja wa Posta Afrika *PAPU*, Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika *ATU*, Jumuiya ya Mawasiliano ya nchi za Afrika Mashariki *EACO* na Jumuiya ya Wasimamizi wa Mawasiliano ya Kusini mwa Afrika *CRASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Umoja wa Watoa Huduma za Posta Kusini mwa Afrika *SAPOA*, Shirika la Maendeleo la Ufaransa *AFD*, Shirika la Watoto Duniani *UNICEF*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni *UNESCO*, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea *KOICA*, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan *JICA*, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Ujerumani, India, Estonia pamoja na Finland.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuzishukuru Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ikiwemo *EAC, SADC* na *EU* kwa ushirikiano wao katika masuala ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, Wizara ya mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa sekta yetu ya mawasiliano na teknolojia ya habari inachangia kikamilifu katika kufikia Dira 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, ninapenda kuwashukuru watoa huduma za mawasiliano kutoka katika kampuni za mawasiliano ya simu; Shirika la Mawasiliano Tanzania *TTCL*, *Airtel Tanzania*, *Vodacom Tanzania*, Honora Tanzania na *Viettel* kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutatua changamoto za mawasiliano nchini, kwa kufikisha huduma za mawasiliano kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutambua mchango wa kampuni changa pamoja na wabunifu nchini, ambao wamekuwa chachu katika maendeleo ya sekta za *TEHAMA* nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuwashukuru Taasisi za Fedha za *CRDB* na *NMB*, vyuo na taasisi zinazohusika na tafiti na programu mbalimbali za kuendeleza *TEHAMA*. Wabunifu wote wanaohusika na masuala ya kidijitali, ikiwemo Fintech, akili unde,

Meditech, kilimo, biashara, burudani na wadau wote muhimu kwa mchango kwa mchango wao katika kukuza ubunifu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninapenda kutambua mchango mkubwa unaotolewa na kampuni. Watoa huduma na wadau wote wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari ikiwemo kampuni za minara Tanzania *(HTTT)* pamoja na *TowerCo*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua mchango mkubwa unaofanywa na wakandarasi katika ujenzi wa miundombinu ya *TEHAMA,* wakiwemo kampuni ya *Huawei, Telecom Associates, Soft net* pamoja na *RadiFiber*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuzishukuru Wizara zote na Taasisi za Umma ikiwemo Ofisi ya Rais Utumishi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, Wizara yetu ya Mawasiliano Teknolojia ya Habari na Ubunifu kwa upande wa Zanzibar, *e-GA, EGAS, TCRA, NIDA, RITA, NEMC, TANROADS, TARURA, REA, TANESCO, TFS, TCAA, TAA, COSTECH* na wadau wote muhimu katika maeneo ya sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili siyo tu bajeti, hii siyo tu takwimu na jedwali, ni dira ya mustakabali wa uchumi wa kidijitali na mageuzi ya kidijitali kwa Taifa letu. Kupitia uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano, upatikanaji wa uhakika wa huduma za mawasiliano ya bei nafuu, upatikanaji wa vifaa vya kidijitali kwa bei nafuu na kuimarisha ujuzi wa *TEHAMA* kwa wananchi, tunajenga msingi wa uchumi shirikishi na wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo yetu ni bayana, kufikia angalau 55% ya wananchi kumiliki simu janja ifikapo mwaka kesho 2027, kupunguza gharama za huduma za simu na *internet* kwa kila Mtanzania na kusambaza nyaya za mkongo wa Taifa hadi vijijini, ili kila kijiji kiwe na fursa ya kuunganishwa na kujenga minara ya mawasiliano katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa na mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hizi tunaamini zitawawezesha vijana, wanawake, wazee, wakulima, wafugaji,

wavuvi, wafanyabiashara wa makundi mbalimbali na makundi mengine kuweza kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Bunge lako Tukufu, sekta binafsi, asasi zisizo za Kiserikali na washirika mbalimbali wa maendeleo kushirikiana nasi katika safari hii. Kwa mshikamano, uwajibikaji na ubunifu, tunaweza kuibadilisha Tanzania kuwa Taifa lenye nguvu za kidijitali, ambapo teknolojia siyo kwa wachache, bali ni haki na fursa kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhamira thabiti na mshikamano wa Taifa, bajeti hii itakuwa ni chombo cha kuleta maendeleo, uwazi na ustawi wa wananchi wetu kwa ajili ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiriwa kukusanya shilingi bilioni 160,369,242,000 ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Makadirio ya Matumizi katika Mwaka ujao wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi 222,589,451,000 kwa ajili ya kutekeleza majukumu na vipaumbele vya Wizara kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiriwa kutumia shilingi 13,146,172,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambayo ni sawa na asilimia tano nukta tisa ya bajeti iliyotengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha hizo, shilingi 6,371,830,000 ni kwa ajili ya mshahara na shilingi 6,774,342,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo au OC. Kwa upande wa matumizi ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiriwa kutumia shilingi 209,443,279,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na 94.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wabunge wataona hapa, tumeweka mkazo katika asilimia kubwa ya bajeti yetu katika kutekeleza bajeti ya maendeleo na asilimia ndogo sana katika matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 98,480,905,000 ni fedha za ndani na shilingi 110,962,374,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo ni http://www.mawasiliano.go.tz. Kwa unyenyekevu mkubwa, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA ANGELLAH JASMINE MBELWA KAIRUKI (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 2.1 Utangulizi

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/26. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27.

## 2.2 Shukrani na Pongezi

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa tatu wa Bunge la 13. Aidha, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu na kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27 ikiwa ni bajeti yangu ya kwanza tangu nilipoteuliwa kuongoza na kusimamia Wizara hii.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa heshima na taadhima ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua Mheshimiwa Dkt. Switbert Zacharia Mkama (Mb.) kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. ***Ninaahidi kwa Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu pamoja na Wananchi kwa ujumla kwamba nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu, uaminifu na kwa uwezo wangu wote katika kuendeleza Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ili kuwezesha Nchi kufikia adhma yake ya kuwa na Uchumi wa Kidijitali.***

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Wananchi zaidi ya **Milioni 31.9** katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 na kumuwezesha kuongoza Taifa letu katika kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya kauli mbiu ya ***"KAZI NA UTU, TUNASONGA MBELE*"**. Katika kipindi cha siku 100 tangu kuapishwa kwake tumeshuhudia jitihada mbalimbali zikiendelea kufanyika chini ya uongozi wake ikiwemo kuweka mazingira wezeshi yanayochochea ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika Ujenzi wa Miundombinu ya Mawasiliano kama vile Minara **758**, Uongezwaji Nguvu wa Minara **304,** Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano kwa kushirikiana na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano na Uunganishwaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo – DRC, hii inaonesha imani kubwa iliyopo kati ya wawekezaji na Serikali ya Awamu ya Sita.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza Miradi nane ya Maendeleo ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mawasiliano Vijijini, Tanzania ya Kidijitali, Anwani za Makazi na Postikodi, Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA, Kujenga Uwezo wa Taasisi Katika Utekelezaji wa Majukumu, Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA na Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali

ili kufikia matarajio makubwa aliyonayo Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha Huduma za Mawasiliano zinawafikia Wananchi wote kama ilivyofafanuliwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa na Wananchi wa Zanzibar kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi cha Awamu ya Pili. Vilevile, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.) kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni, ambayo imetoa Dira na Mwongozo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27. Hotuba hiyo imeeleza kwa kina mapitio ya uendeshaji wa shughuli za Serikali katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mipango ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27 pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025. Ninaahidi kuwa, Wizara ninayoiongoza itayafanyia kazi masuala yote yanayohusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kama yalivyoainishwa katika Hotuba na michango iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Hotuba hiyo.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatambua mchango wako kwa namna ambavyo umekuwa ukiibua mijadala mbalimbali ambayo ina lengo la kuboresha sekta ya TEHAMA. Na sote ni mashuhuda wa mabadiliko ambayo yametokana na mchango wako.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninampongeza Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.) kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika uongozi wenu mahiri umelifanya Bunge kuendelea kuwa chombo imara cha kutunga Sheria, kusimamia Serikali na kuwakilisha Wananchi kwa ufanisi.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, Niwapongeze Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini na Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuteuliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Aidha, ninawapongeza kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kukusaidia kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge lako Tukufu.

***11.*** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri wote kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara mbalimbali wanazozisimamia. Ninawaahidi ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yetu.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa napenda kuwapongeza: Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Tanganyika kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu pamoja na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati.

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa uchambuzi wao makini walioufanya na ushauri walioutoa wakati wa kupitia na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 068, kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27 na kupitisha Bajeti ya Wizara. Ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Wajumbe wa Kamati yamezingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2026/27. Vilevile, ninamshukuru Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, Katibu wa Bunge pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa uratibu wa shughuli za kila siku za Bunge.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee kabisa ninaomba kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kibamba kwa kunichagua kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu na kuniwezesha kuwa Mbunge wa Jimbo la Kibamba. Aidha, ninaomba kutoa shukrani za dhati kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kunichagua na kuniteua kuwa Mgombea wa CCM katika Jimbo la Kibamba katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025. Hii ni heshima kubwa na dhamana ya kipekee ambayo nitailinda kwa uadilifu na uwajibikaji mkubwa. vilevile, napenda kuwashukuru kwa moyo wa dhati wananchi wote wa Jimbo la Kibamba kwa kunipa kura nyingi na kuniamini kuwa mwakilishi wao. Imani yqo kwangu, Upendo, ushirikiano na mshikamano wao umekuwa nguzo ya mafanikio haya.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kumshukuru mume wangu mpenzi, Mheshimiwa Balozi Mbelwa Kairuki, pamoja na watoto wetu wapendwa Precious Kemilembe, Esther Kokubelwa na Hubert Mwesigwa kwa upendo na faraja yao kwangu wakati wote. Nawashukuru kwa kunivumilia ninapokuwa mbali nao, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ya kusimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Ninapohudumu katika Jimbo langu la Kibamba.

## 2.3 Salamu za Pole

***16. Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia, ndugu, jamaa, marafiki na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na Wapendwa Wetu: Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Ismani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Peramiho. Wizara inatambua mchango mkubwa uliofanywa na Waheshimiwa Viongozi hao hasa katika utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Aidha, nitoe pole kwa kuondokewa na Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum akiwakilisha Kundi la Wafanyakazi na Sekta Binafsi. ***Tunawaombea marehemu wote, Mwenyezi Mungu aziweke Roho zao mahali pema peponi, Amina!***

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuona umuhimu wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kuweka mazingira wezeshi yanayovutia uwekezaji ambayo yamewezesha upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kisekta ambayo utekelezaji wake unachochea ukuaji wa Uchumi wa Kidijitali.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Uongozi wa Mheshimiwa Rais, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepata mafanikio makubwa ikiwemo: Kukamilisha ujenzi wa Minara **758** katika Kata **688** pamoja na kuongeza nguvu Minara **304** katika Kata **231** iliyokuwa ya 2G kwenda 2G/3G na 4G ambapo miradi hii imekamilika kwa **asilimia 100** na ujenzi wa Minara hiyo unawanufaisha Wananchi takribani **Milioni 8.5** na kwa minara iliyoongezewa nguvu inawanufaisha Wananchi **Milioni 4.2.**

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inatekeleza Mradi wa Mawasiliano Vijijini wa ujenzi wa Minara **636** katika Kata **443** ambapo **Minara 456** sawa na **asilimia 72** imekamilika. Aidha, kati ya Minara **456** iliyokamilika, Minara **342** imewashwa na inatoa huduma kwa Wananchi na Minara **114** inatarajiwa kuwashwa Juni, 2026. Aidha, Minara **180** iliyobakia inatarajiwa kukamilika ifikapo Disemba, 2026. Kukamilika kwa Mradi huu kutawezesha Wananchi takribani **Milioni 2.5** kufikiwa na Huduma za Mawasiliano.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imekamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Wilaya **86** Nchini na kuunganisha Nchi saba kati ya nane. Kwa sasa Serikali imeanza utaratibu wa kuiunganisha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo – DRC katika Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia ufikishaji wa miundombinu ya Faiba Mlangoni ambapo ilikusudiwa kufanya maunganisho **279,795** hata hivyo hadi Machi, 2026 ujenzi wa njia za maunganisho **132,793** umekamilika na kuwezesha kutoa huduma kwa wateja **64,266** kati ya **126,740** sawa na **asilimia 51** ya lengo lililokusudiwa.

## 2.4 Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara

### 2.4.1 Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

**21.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mujibu wa Tangazo la Serikali **Na. 685** la tarehe **19 Disemba, 2025** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepewa majukumu nane kama ifuatavyo:

(i) Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera zinazohusu Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Posta na Mawasiliano ya Simu;
(ii) Kufanya tafiti za maendeleo na ubunifu kwenye TEHAMA;
(iii) Kuendeleza Wataalamu wa TEHAMA;
(iv) Kuanzisha na kusimamia Postikodi;
(v) Kusimamia ujenzi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
(vi) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa TEHAMA;
(vii) Kuboresha utendaji kazi na uendelezaji wa rasilimaliwatu ndani ya Wizara; na
(viii) Kusimamia Taasisi, Programu na Miradi ndani ya Wizara.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inasimamia Taasisi sita na Baraza moja. Taasisi hizo ni: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - TCRA; Shirika la Mawasiliano Tanzania - TTCL; Shirika la Posta Tanzania - TPC; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote - UCSAF; Tume ya TEHAMA - ICTC; Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi - PDPC na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC).

### 2.4.2 Majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Wizara

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu kuu la usimamizi wa Huduma za Mawasiliano kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 ambapo pamoja na mambo mengine, Mamlaka imekabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kutoa leseni za Watoa Huduma za Mawasiliano Nchini;

(ii) Kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayakufuatwa;
(iii) Kuweka viwango kwa bidhaa na huduma zinazosimamiwa kama gharama za maunganisho kati ya mtandao mmoja na mwingine;
(iv) Kulinda Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano;
(v) Kusimamia rasilimali adimu za mawasiliano ikiwemo masafa, namba za Postikodi na majina ya vikoa vya Kitaifa vya Intaneti;
(vi) Kufuatilia utendaji wa Sekta zinazosimamiwa na Mamlaka;
(vii) Kukuza ushindani katika Sekta;
(viii) Kusambaza taarifa zinazohusu kazi na majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; na
(ix) Kushauriana na mamlaka nyingine za usimamizi katika kutekeleza majukumu sawa na yale ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mawasiliano Tanzania lilianzishwa kupitia Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania, Sura ya 304. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Shirika limekabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Huduma za Mawasiliano ya Simu Nchini na utoaji wa Huduma ya Mawasiliano ya Simu kibiashara na kiuchumi;
(ii) Kutoa Huduma za Mawasiliano ya Simu kwa mujibu wa Sheria;
(iii) Kujenga na kuendesha Miundombinu ya Mawasiliano ya Kimkakati kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana;
(iv) Kutoa huduma ya miamala ya kifedha inayohusiana na Mawasiliano ya Simu;
(v) Kuendesha Mifumo na Huduma ya Mawasiliano ya Simu ikiwemo Mfumo wa TEHAMA ndani na nje ya Nchi;
(vi) Kutoa Huduma za Mawasiliano kwa njia ya sauti na picha;
(vii) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu TEHAMA kwenye Mashirika, Taasisi za Umma na kwa wajasiriamali; na
(viii) Kukuza uwekezaji wa Huduma za Mawasiliano ya Simu ndani na nje ya Nchi.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Posta Tanzania lilianzishwa kwa Sheria ya Shirika la Posta Tanzania, Sura ya 303 baada ya kuvunjwa kwa lililokuwa Shirika la Posta na Simu Tanzania. Shirika limekabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kutoa Huduma za Posta ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(ii) Kutosheleza mahitaji ya kitaifa ya Huduma za Posta za Kisekta, Viwanda, biashara na jamii kwa ujumla ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
(iii) Kutoa huduma za kifedha na uwakala kwa njia ya uhamishaji wa fedha kwa kutumia Mifumo ya Kielektroniki, ubadilishaji wa fedha au kwa njia nyingine zozote zitakazoonekana kufaa kwa Shirika; na
(iv) Kutoa huduma za Kaunta kwa ajili ya Jamii na Serikali kulingana na Malengo yaliyotajwa katika Sheria ya uanzishwaji wa Shirika.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulianzishwa kwa Sheria ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Sura ya 442 kwa lengo la kupeleka na kufikisha Huduma ya Mawasiliano kwa Wananchi waishio katika maeneo ya Mijini, Vijijini na maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa kushirikiana na Watoa Huduma za Mawasiliano. Mfuko umekabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa Huduma ya Mawasiliano katika maeneo ya Vijijini na maeneo ya Mijini yenye mawasiliano hafifu;
(ii) Kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi na Serikali katika utoaji wa Huduma za Mawasiliano kwa wote katika maeneo ya Vijijini na maeneo ya Mijini yenye mawasiliano hafifu;
(iii) Kuhamasisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo ya Vijijini na maeneo ya Mijini yenye mawasiliano hafifu;
(iv) Kutengeneza mfumo kwa ajili ya upatikanaji wa Mitandao ya Mawasiliano na huduma rahisi na zenye ufanisi katika uzalishaji na upatikanaji katika soko la kiushindani;
(v) Kuhamasisha utoaji wa huduma bora katika viwango nafuu na kuhakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

inapatikana Vijijini na sehemu za Mijini zenye mawasiliano hafifu kwa bei nafuu; na

(vi) Kuhakikisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kupitia ushiriki wa Sekta Binafsi.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya TEHAMA ilianzishwa kwa Amri ya Rais kupitia Tangazo Namba 532 lililochapishwa kwenye Gazeti la Serikali la tarehe 20 Novemba, 2015. Kwa mujibu wa Amri iliyoanzisha Tume ya TEHAMA, Tume imekabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kukuza uwekezaji katika TEHAMA;
(ii) Kujenga uwezo na kukuza utaalamu na viwango katika fani ya TEHAMA;
(iii) Kushauri na kushirikiana na wadau wengine kwenye masuala ya tafiti na kuweka viwango na mwelekeo;
(iv) Kuhifadhi na kuendeleza miundombinu na programu za TEHAMA; na
(v) Kufanya kazi nyingine zozote zitakazoainishwa na Sheria.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imeanzishwa kwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44. Kwa mujibu wa Sheria ya uanzishwaji wake, Tume imekabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa wakusanyaji na wachakataji;
(ii) Kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi;
(iii) Kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi na faragha za watu;
(iv) Kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri Ulinzi wa Taarifa Binafsi na faragha za watu;
(v) Kutoa elimu kwa Umma kwa kadri itakavyofaa;
(vi) Kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa;
(vii) Kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za Nchi nyingine zinazosimamia Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali; na

(viii) Kutekeleza majukumu mengine ya Tume kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria.

**29. Mheshimiwa Spika,** Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limeanzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172. Baraza limekabidhiwa majukumu yafuatayo:

(i) Kuwakilisha maslahi ya Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano zinazosimamiwa kisheria kwa kushauriana na TCRA, Waziri mwenye dhamana ya Mawasiliano na Mawaziri wa Sekta;
(ii) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni kuhusu masuala ya msingi ya watumiaji wa Huduma za Mawasiliano;
(iii) Kuanzisha kamati za watumiaji katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Sekta na kushauriana na Kamati hizo; na
(iv) Kufanya mashauriano na wahusika katika Sekta, Serikali na makundi mengine ya watumiaji wa huduma kuhusiana na masuala ya msingi ya watumiaji wa huduma zinazosimamiwa Kisheria.

## 2.5 Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, takwimu zinaonesha kuwa, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kukua na kutoa mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa kwa Mwaka 2024 ikilinganishwa na Mwaka 2023. Kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa cha Mwaka 2024 shughuli za Habari na Mawasiliano zilikua kwa **asilimia 14.3** ikilinganishwa na ukuaji wa **asilimia 7.6** Mwaka 2023. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa: Maeneo yaliyofikiwa na Miundombinu ya Mawasiliano; Matumizi ya Simu za Mkononi na Mitandao ya Kijamii; mikutano ya mitandaoni; na Matumizi ya malipo kupitia Mitandao ya Simu. Aidha, ukuaji huu umewezesha mchango wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika Pato la Taifa kuongezeka kutoka **asilimia 1.5** kwa Mwaka 2023 hadi **asilimia 1.6** kwa Mwaka 2024.

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni Sekta wezeshi na mtambuka inayowezesha utekelezaji

wa majukumu ya Sekta zingine kwa kutumia TEHAMA. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaendelea na uandaaji wa Akaunti ya Upimaji wa Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy Satelite Account – DESA) ili kuongeza wigo wa upimaji wa mchango wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwenye Pato la Taifa kwa lengo la kutambua kwa usahihi mchango halisi wa Sekta katika Pato la Taifa.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Benki Kuu ya Tanzania, Tume ya Taifa ya Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Shirika la Mawasiliano Tanzania, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Mamlaka ya Serikali Mtandao na Tume ya TEHAMA imeanza kukusanya takwimu zitakazotumika katika uandaaji wa Akaunti ya Upimaji wa Uchumi wa Kidijitali.

## 2.6 Upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano Nchini

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kukua, takwimu zinaonesha kuwa laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka **Milioni 90.4** Machi, 2025 hadi laini **Milioni 111.9** Machi, 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 23.8**. Watumiaji wa Intaneti wameongezeka kutoka **Milioni 49.3** Machi, 2025 hadi **Milioni 58.9** Machi, 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 19.5**. Watumiaji wa huduma za kutuma na kupokea pesa kwa njia ya Mtandao wa Simu wameongezeka kutoka **Milioni 66.5** Machi, 2025 hadi **Milioni 81.0** Machi, 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 21.8**. Aidha, Idadi ya Watoa Huduma wa Miundombinu ya Mawasiliano imefikia **52** Machi, 2026 ikilinganishwa na Watoa Huduma **38** Machi, 2025 hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 36.8**. Watoa Huduma za Ziada (Application Services and Value-Added Services) wamefikia **173** Machi, 2026 ikilinganishwa na Watoa Huduma **136** Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 27.2**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Takwimu hizi zinaonesha kuimarika kwa upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutokana na uwepo wa mifumo na mazingira wezeshi ambayo ni maono na Dira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano ambapo Kata **688** Nchini zimepelekewa Huduma za Mawasiliano kwa kujenga Minara ambayo imeweza kuwanufaisha wananchi takribani **Milioni 8.5**, ufikishaji wa huduma ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika Wilaya **86** kumewezesha na kurahisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wananchi pamoja na utambuzi wa makazi unaofanywa kupitia Mfumo wa Anwani za Makazi. Hatua hii imewezesha baadhi ya maeneo yaliyokuwa na changamoto za Mawasiliano kufikiwa na Huduma za Mawasiliano na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii na kiuchumi Kidijitali.

## 2.7 Huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, Huduma za Posta hususan usafirishaji wa vifurushi na vipeto zimeendelea kuimarika Nchini ambapo vifurushi na vipeto **142,496** vilitumwa ndani ya Nchi kwa Machi 2026 ikilinganishwa na vifurushi na vipeto **141,114** vilivyotumwa kwa Machi 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 1**. Aidha, kwa upande mwingine, vifurushi na vipeto **286,334** vilipokelewa ndani ya Nchi kwa Machi 2026 ikilinganishwa na vifurushi na vipeto **183,348** vilivyopokelewa kwa Machi 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 56.2**.

## 2.8 Hatua iliyofikiwa ya Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali wa Mwaka 2024 -2034 ambapo Wizara kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali umewezesha maboresho ya Miundombinu na Mifumo ya TEHAMA ambayo maboresho hayo ndiyo msingi wa utekelezaji wa Mkakati husika. Aidha, mkakati huu unatekelezwa na Sekta ya Umma na Binafsi kulingana na majukumu ya taasisi husika.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali unatekelezwa kwa ufanisi na kufikia malengo yaliyokusudiwa, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa

Mkakati ili kuiwezesha Serikali na Sekta Binafsi kutoa taarifa ya hatua iliyofikiwa kwa kila kiashiria katika utekelezaji wa Mkakati huo.

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kuratibu maboresho ya Mifumo mbalimbali Nchini ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali kwa kuwezesha Wananchi kupata Huduma za Mawasiliano na nyinginezo katika ubora kusudiwa. Wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za umma izimeweza kufanya maboresho ya Mifumo mbalimbali. Aidha, mkakati huu unatekelezwa na sekta binafsi kulingana na majukumu ya taasisi husika. Kwa umuhimu huo Serikali imeandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mkakati ili kuiwezesha Serikali na Sekta Binafsi kutoa taarifa ya hatua iliyofikiwa kwa kila kiashiria katika utekelezaji wa Mkakati huo na kuwezesha Nchi kuwa na mwelekeo unaoshabihiana katika kuhakikisha TEHAMA inachangia katika Pato la Taifa.

## 2.9 Utoaji wa Mitaji kwa Kampuni Changa (Startups) za TEHAMA

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika Oktoba, 2025, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliahidi ***Bilioni 200 kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuwezesha biashara ndogo, za kati na uendeshaji wa Kampuni Changa (Startups)***. Aidha, Kati ya Fedha hizo Shilingi **Bilioni 5** ni kwa ajili ya kuwezesha mitaji kwa Kampuni Changa za TEHAMA ili kukuza bunifu zao.

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kuwa Mheshimiwa Rais ametekeleza ahadi hii kwa kuwezesha upatikanaji wa Shilingi **Bilioni 5** kwa ajili ya mitaji ya kuwezesha uendeshaji wa Kampuni Changa za TEHAMA Nchini. Aidha, kwa sasa, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imekamilisha uandaaji wa Mwongozo utakaowezesha kuwapata wanufaika wa Mikopo.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** utoaji wa mikopo hii utafanywa na Benki ya NMB na inatarajiwa Kampuni Changa zisizopungua **50** za TEHAMA ambazo zitakuwa zimekidhi vigezo kwenye maeneo

yanayogusa masuala ya kidjitali ikiwemo bunifu za kifedha; Sheria (Legal Tech); Entertainment tech; Kilimo (Agri-Tech); Utalii (Tourism Tech); Bima (Insur- Tech); Elimu (Edu-Tech); Logistics-Tech; Mifumo ya huduma (SaS), e-commerce, n.k Maombi rasmi yatapokelewa kupitia mfumo wa kidijali ambao utaunganishwa na NMB kurahisisha zoezi la uchambuzi. Aidha, Mikopo hii inatarajiwa kutolewa Mei, 2026 kwa wanufaika wote watakaokuwa wamekidhi vigezo.

## SURA YA TATU

### 3.1 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2025/26

#### 3.1.1 Bajeti iliyoidhinishwa

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa **Shilingi 291,533,139,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 14,485,656,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 277,047,483,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 6,958,609,000** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 7,527,047,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 98,480,905,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 178,566,578,000** ni fedha za nje.

#### 3.1.2 Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilikadiria kukusanya **Shilingi 120,369,242,950** kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Hadi Machi, 2026 Wizara imefanikiwa kukusanya **Shilingi 160,698,818,453.40** sawa na **asilimia 133.5** ya lengo lililokusudiwa. Ufanisi huu umetokana na uwekezaji uliofanywa kwenye Miundombinu ya Mawasiliano ikiwemo kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambao umeunganisha Wilaya **86** Nchini na kuongeza uwezo wa njia za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

### 3.1.3 Mapokezi na Matumizi ya Fedha

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imepokea na kutumia **Shilingi 147,768,795,246.62** sawa na **asilimia 50.6** ya lengo lililokusudiwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,880,515,646.15** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 139,888,279,600.47** ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 4,100,186,167** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 3,780,329,479.15** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Vilevile, kwa upande wa fedha za Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 55,406,701,365.02** ni fedha za ndani na **Shilingi 84,481,578,235.45** ni fedha za nje.

## 3.2 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2025/26

### 3.2.1 Sehemu ya Mawasiliano

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Sehemu ya Mawasiliano imetekeleza yafuatayo:

***(i)*** **Ujenzi wa minara 758 katika Kata 688**

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imesimamia ujenzi wa Minara **758** katika Kata **688** Nchini ambapo hadi Machi, 2026 Minara yote imekamilika kwa **asilimia 100** na inatoa Huduma za Mawasiliano kwa Wananchi. Aidha, Wizara imekamilisha kuongeza nguvu Minara **304** katika Kata **231** iliyokuwa ya 2G kwenda 2G/3G na 4G sawa na **asilimia 100**.

***(ii)*** **Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika masuala ya Kikanda na Kimataifa, Wizara imeshiriki mikutano mbalimbali ikiwemo Mikutano ya Umoja wa Posta Duniani - UPU na Umoja wa Mawasiliano ya Simu Duniani - ITU ambapo Tanzania ni mjumbe wa Baraza la Utawala la ITU 2022 - 2026, Baraza la Utawala na Baraza la Uendeshaji wa Posta ya UPU

kwa kipindi cha 2021 – 2025 na imeshinda tena kuingia kwenye Mabaraza hayo kwa kipindi cha 2026 – 2029. Aidha, Tanzania imeshiriki kwenye Mikutano ya Baraza la uongozi la ITU na imechaguliwa kuingia kwenye Uongozi wa Kamati ya kuandaa Mpango Mkakati wa Baraza wa Mwaka 2028 – 2031. Pia, Mtanzania Dr, Emmanuel Manasseh amechaguliwa kuongoza Ofisi ya ITU Kanda ya Afrika. Katika Taasisi nyingine za Kimataifa, Tanzania ni Mjumbe wa Baraza la Utawala la Umoja wa Posta Afrika – PAPU wenye makao makuu Arusha, Tanzania na pia ni Mjumbe wa Baraza la Utawala la Umoja wa Mawasiliano Afrika – ATU 2022 – 2026

***(iii)* Utekelezaji wa Programu ya Anga za Juu**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa maelekezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais Mwaka 2022 ya Nchi kuwa na Satelaiti yake yanatekelezwa, Wizara imeanza taratibu za kuridhia Mikataba miwili ya Anga za Juu ambayo ni Mkataba wa Kanuni zinazosimamia shughuli za Mataifa katika Utafiti, Uchunguzi na Matumizi ya Anga za Juu wa Mwaka 1967 na Mkataba wa Usajili wa Vifaa, Vyombo Vilivyorushwa Katika Anga za Juu wa Mwaka 1975.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na maandalizi ya uridhiwaji wa Mikataba ya Anga za Juu iliyotajwa hapo juu, Wizara imekamilisha taratibu za Ununuzi wa vifaa vya uundaji wa Satelaiti ndogo ya CUBESAT kupitia Mradi wa UNOOSA unaojulikana kama KIBOCUBE pamoja na usajili wa Satelaiti umekamilika. Aidha, usajili wa Satelaiti umefanyika kupitia Shirika la ITU kwa kuwa ndio lenye dhamana ya usajili wa Satelaiti.

***(iv)* Uwekezaji katika TEHAMA**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhamasisha uwekezaji katika Sekta ya TEHAMA, Wizara imehuisha Wasifu wa Uwekezaji katika TEHAMA (ICT Investment Profile 2025) ambapo jumla ya miradi **21** imeainishwa ili kuendana na mabadiliko ya ukuaji wa Teknolojia yanayotokea Ulimwenguni. Aidha, Wasifu husika umesambazwa kwa wadau ikiwemo Tanzania Investment and Special Economic Zones Authority (TISEZA) na Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya Nchi

pamoja na Balozi za Nchi hizo zilizopo Nchini kwa lengo la kutangaza fursa zilizopo katika Sekta ya TEHAMA na tayari baadhi ya wawekezaji wameanza kuonesha nia ya kushirikiana na Serikali katika baadhi ya miradi.

**(v) Kukuza Biashara Mtandao**

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuweka mazingira wezeshi ya ukuaji wa Biashara Mtandao Nchini, Wizara imesimamia maboresho ya Mfumo wa Kidijitali uitwao Kipepeo unaoendeshwa na Shirika la Posta Tanzania utakaowezesha Biashara Mtandao ambapo ujenzi wa Mfumo huu umefikia **asilimia 90**. Aidha, majaribio ya Mfumo yanaendelea kufanyika kwa ajili ya kuwezesha Wananchi kuuza na kununua bidhaa na huduma Mtandaoni.

**(vi) Ukarabati wa Vituo 32 vya Huduma Pamoja**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha Huduma za Serikali zinapatikana katika dirisha moja, Wizara imeratibu ukarabati wa vituo **32** vilivyopo katika majengo ya Ofisi za Posta ili viweze kutoa Huduma za Serikali kupitia dirisha moja. Ukarabati huu unafanyika kwa awamu mbili. Awamu ya Kwanza inahusisha vituo **16** ambapo ukarabati umefikia **asilimia 81** na Awamu ya Pili ya vituo **16** imefikia **asilimia 41**. Kukamilika kwa utekelezaji wa Mradi huu kutarahisisha utoaji wa huduma kwa wakati na kwa gharama nafuu.

**3.2.2 Sehemu ya Miundombinu ya TEHAMA**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Sehemu ya Miundombinu ya TEHAMA imetekeleza yafuatayo:

**(i) Kusimamia Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano na Intaneti Nchini. Hadi Machi, 2026 jumla ya Kilometa **15,167** kati

ya **16,280** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zimejengwa sawa na **asilimia 93.2** ya lengo lililokusudiwa. Ujenzi huu umewezesha kufikisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye Wilaya **13** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 hivyo kufanya Wilaya zilizounganishwa kufikia **122** kati ya **139** sawa na **asilimia 87.8**.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Pamoja na kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ndani ya Nchi, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaendelea kusimamia ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye urefu wa Kilometa **186** ili kuweza kuunganisha Tanzania na Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo - DRC ambapo mradi huu unatarajiwa kukamilika Aprili, 2027. Kukamilika kwa Mradi huu kutaimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na DRC pamoja na kuongeza mapato yatokanayo na uuzaji wa Huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

***(ii)*** **Kufanya Maridhiano na Watoa Huduma za Mawasiliano**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inasimamia utekelezaji wa Hati ya Maridhiano kati ya Serikali na Umoja wa Watoa Huduma za Mawasiliano (Consortium of Telco Operators) uliosainiwa tarehe 25 Septemba, 2023. Aidha, hadi Aprili, 2026, *Consortium of Telco Operators* imeweza kukabidhi umiliki wa Miundombinu ya Mkongo wa Mawasiliano wenye Kilometa **1,193** kati ya **2,020**, kufanya malipo ya **Dola za Marekani Milioni 11.4** kati Dola za Marekani **Milioni 20** pamoja na kuanza kufanya uwekezaji kwenye Mkongo wa Mawasiliano wenye thamani ya Dola za Marekani **Milioni 13**. Utekelezaji wa makubaliano hayo ni wa miaka mitano na unatarajiwa kukamilika tarehe 24 Septemba, 2028.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inasimamia utekelezaji wa Hati ya Maridhiano kati ya Serikali na Kampuni ya Viettel Global Joint Stock ya Nchini Vietnam iliyosainiwa Oktoba, 2025 ambapo kampuni hiyo itapaswa kufanya maboresho ya Mkongo wa Mawasiliano wenye urefu wa **Kilometa 19,023** na kujenga Minara **70** ya Mawasiliano ya Simu katika maeneo ya Vijijini. Hadi Machi, 2026 Kampuni ya Viettel Global Joint Stock imekamilisha maboresho ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wenye Kilometa **1,808** na Minara **20**.

Utekelezaji wa Makubaliano hayo ni wa Miaka mitatu na unatarajiwa kukamilika Septemba, 2028.

***(iii)*** **Kuongeza uwezo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuongeza uwezo wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye njia kuu kutoka kiwango cha 200Gbps hadi kiwango kinachoanzia 400Gbps hadi 2,000Gbps na maunganisho ya Mipakani kutoka kiwango cha 100Gbps hadi 800Gbps, ili kuongeza kasi ya Mtandao Nchini. Aidha, Huduma ya Intaneti ya kasi imefikia **asilimia 94** kwenye maeneo ya makazi ya watu huku watumiaji wa Intaneti wakiongezeka na kufikia **asilimia 85.3**.

***(iv)*** **Kusimamia Ujenzi wa Miundombinu ya Faiba Mlangoni**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imesimamia Ujenzi wa Miundombinu ya Faiba Mlangoni ambapo hadi Machi, 2026 njia za maunganisho **132,793** kati ya **279,795** zimejengwa sawa na **asilimia 47.5**.

***(v)*** **Kusimamia Ujenzi wa Vituo vya Kuhifadhi Data**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imekamilisha kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Kuhifadhi Data vya Dodoma na Mjini Magharibi - Zanzibar. Aidha, taratibu za uridhiwaji wa miradi hii zinaendelea kupitia Tume ya Taifa ya Mipango. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivi kutaongeza wigo wa uhifadhi wa data pamoja na kuimarisha ulinzi na usalama wa data zilizohifadhiwa.

***(vi)*** **Kusimamia ufungaji wa vifaa vya mikutano kwa Njia ya Video**

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kupunguza gharama za uendeshaji wa Mikutano, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imekamilisha ufungaji wa vifaa vya mikutano kwa njia ya video (Video Conferencing Facilities) katika vituo **98** vya Haki Jinai kwa mchanganuo ufuatao: Ofisi za Taifa za Mashtaka vituo **20**; Magereza vituo **38**; Jeshi la Polisi Tanzania Bara vituo **34**; na Jeshi

la Polisi Zanzibar vituo sita. Aidha, Wizara imefunga vifaa hivyo katika Ofisi mbili zilizopo katika Jengo la Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

***(vii)*** **Kufikisha huduma ya Wi-Fi katika maeneo ya Umma**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imefikisha huduma ya Wi-Fi katika maeneo **50** ya Umma na kufanya jumla ya maeneo yaliyounganishwa kufikia **61** kati ya **120** sawa na asilimia **51** ya lengo lililokusudiwa. Huduma hii itasaidia ya kuhakikisha wananchi wanafikishiwa huduma za mawasiliano ili kurahisisha utoaji wa huduma mbalimbali za kijamii ambazo zitachochea kipato cha mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla wake na hivyo kuweza kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa kidijitali. Aidha, maeneo yaliyofikishiwa huduma ni pamoja na Masoko, Stendi Kuu za Mabasi, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Vyuo Vikuu na vya Kati, Vituo vya Mwendokasi na maeneo mengine ya Umma. Maeneo hayo yapo katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Geita, Pwani, Pemba, Unguja, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga. Utekelezaji wa Mradi huu unatarajiwa kukamilika Juni, 2027.

**3.2.3 Sehemu ya Uendelezaji wa Mifumo, Huduma za TEHAMA na Uzingatiaji**

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Sehemu ya Uendelezaji wa Mifumo, Huduma za TEHAMA na Uzingatiaji imetekeleza yafuatayo:

***(i)*** **Ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali – NDTI**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeanza taratibu za ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali - NDTI ambapo hadi Machi, 2026 Wizara imekamilisha upatikanaji wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba **1,619,000** lililopo Nala - Dodoma. Aidha, Upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Taasisi ya NDTI umekamilika ambapo kiasi cha **Dola za Marekani 194,132,332** zitatumika kutekeleza mradi.

### *(ii)* Ujenzi wa Miji Janja (Smart Cities)

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeingia Mkataba kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Miji Janja katika Mikoa ya Dodoma, Arusha, Mbeya na Dar es Saalam kwa lengo la kutathmini utayari wa Miundombinu ya TEHAMA kuwezesha uanzishwaji wa Miji Janja. Kukamilika kwa Mradi huu kutaongeza ufanisi wa utoaji wa huduma za jamii Kidijitali.

### *(iii)* Kusimamia Ukarabati wa Vituo vya Ubunifu

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imesimamia ukarabati wa vituo vitano vya ubunifu katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Tanga. Kukamilika kwa ukarabati wa vituo hivi utawezesha vijana kufanya tafiti kwa ajili ya kuboresha bunifu zao kwa maslahi mapana ya Nchi.

### *(iv)* Ujenzi wa Mifumo ya TEHAMA

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeratibu maboresho ya Mifumo **20** ya TEHAMA ya kutoa huduma kwa Wananchi kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi mbalimbali ikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa, Wakala wa Usajili, Ufilisi, na Udhamini, Baraza la Mitihani la Taifa, Wakala wa Vipimo, na Shirika la Madini la Taifa.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa huduma kwa Wananchi Jamii Portal na Mfumo wa Taifa wa kubadilishana taarifa Jamii XChange inayosimamiwa na Tume ya TEHAMA, Mfumo wa Huduma *Zanzibar Zan Portal* na Mfumo wa kubadilishana taarifa Zanzibar Zan XChange inayosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar-eGAZ; Mfumo wa Daftari la huduma za Serikali unaosimamiwa na OR UTUMISHI ; Mfumo wa huduma za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ZGSD unaosimamiwa na UTUMISHI ZANZIBAR, Mfumo wa Jamii Namba Gateway unaosimimamiwa na NIDA, Maboresho ya mfumo wa vifo na

vizazi unaosimamiwa na RITA, Maboresho mfumo wa NIDA kwa ajili ya Jamii Namba za watoto, Mfumo wa Afya Kidigitali - OR TAMISEMI, Mfumo wa Usajili wa wachakataji na watumiaji wa taarifa binafsi, Mfumo wa ubunifu na ugunduzi (startup and Innovation JamiiHunt) unaosimamiwa na Tume ya TEHAMA, Mfumo wa usajili wa wachimbaji wadogo, Mfumo wa Taifa wa Malipo (Jamii Pay/ Jamii Card), Mfumo wa upimaji na usimamizi wa mafuta Nchini na Mfumo wa uhakiki wa nyaraka za kutuma nje ya Nchi, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mfumo wa usimamizi wa madawa ya kulevya Nchini, Mfumo wa kupima ukomavu wa TEHAMA Nchini, Mfumo wa ufuatiliaji wa uchumi wa Kidijitali, maboresho ya Mfumo wa Usajili na Utambuzi wa Wataalamu wa TEHAMA – Tume ya TEHAMA na Mfumo wa Utambuzi wa Mteja na JamiiPass.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na maboresho hayo ya Mifumo, Wizara imekamilisha Ujenzi wa Mfumo wa Tembo ili kusaidia utekelezaji wa majukumu na kuboresha utendaji kazi ndani ya Wizara.

### *(v)* Utoaji wa Vifaa vya TEHAMA

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imekabidhi vifaa **1,371** vya TEHAMA kwa Taasisi mbalimbali za Serikali. Utoaji wa Vifaa hivi utawezesha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi husika Kidijitali.

### *(vi)* Mwongozo wa Uendelezaji wa Bunifu na Tafiti za TEHAMA

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeandaa Mwongozo wa Uendelezaji wa Bunifu na Tafiti za TEHAMA unaoainisha maeneo ya ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi. Utekelezaji wa Mwongozo huu utarahisisha uratibu wa utekelezaji wa masuala yanayohusu Tafiti na Bunifu za TEHAMA Nchini.

### *(vii)* Nyaraka za Kitaifa za usimamizi wa TEHAMA

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara imeandaa nyaraka

tano za Kitaifa za usimamizi wa TEHAMA ambazo ni: Mwongozo wa Taifa wa Ushirikishanaji na Ubadilishanaji wa Taarifa za Kielektroniki; Mwongozo wa Taifa wa Ujumuishaji wa Makundi Anuai katika Huduma za Kidijitali; Mwongozo wa TEHAMA wa Uzingatiaji na Viwango; Mwongozo wa Taifa wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya TEHAMA; na Mkakati wa Uendelezaji wa Matumizi Bora na Salama ya Akili Unde.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Wizara imeanza taratibu za kumpata Mshauri Elekezi wa kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Uzingatiaji wa Shughuli za TEHAMA. Kukamilika kwa Mwongozo huu kutatoa fursa kwa Wizara kusimamia miongozo ya TEHAMA iliyopo.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeandaa Mwongozo wa usimamizi wa TEHAMA uitwao *ICT Management Framework*. Mwongozo huu unalenga kuhakikisha kuwa TEHAMA inatumika kikamilifu ndani ya Wizara ili kuboresha utoaji wa huduma na kuhakikisha matumizi sahihi na salama ya mifumo na vifaa vya TEHAMA.

***(viii)*** **Muundo wa Kada za TEHAMA**

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imehuisha Muundo wa Kada za TEHAMA kwa kuboresha majukumu na fani zinazoendana na mabadiliko ya Kidijitali. Muundo huu utawezesha Wataalamu wa TEHAMA Serikalini kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia mabadiliko ya Teknolojia na mahitaji ya Soko yaliyopo sasa.

**3.2.4 Sehemu ya Ulinzi na Usalama wa TEHAMA**

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Sehemu ya Ulinzi na Usalama wa TEHAMA imetekeleza yafuatayo:

***(i)*** **Ununuzi wa Vifaa vya TEHAMA**

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika kukabiliana na changamoto za usalama mtandao

imewezesha ununuzi wa vifaa vya TEHAMA katika maabara za Jeshi la Polisi Tanzania Kitengo cha Uchunguzi wa Kidijitali (Cybercrime Unit) Dar es Salaam na Zanzibar kwa lengo la kuongeza uwezo wa kufanya uchunguzi wa uhalifu mtandaoni.

***(ii)* Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Ulinzi na Usalama wa Mtandao**

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza uhalifu mtandaoni, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Ulinzi na Usalama wa Mtandao kwa makundi mbalimbali ya Jamii ikiwa ni pamoja na Watumishi wa Umma, Wanafunzi, Wajasiriamali wa Kidijitali, vikundi vya kijamii kama waendesha magari na bodaboda, VICOBA na Wananchi kwa ujumla. Elimu hii imekuwa ikitolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo Redio, Televisheni, Mitandao ya Kijamii pamoja na kutembelea Shule za Msingi na Sekondari ambapo Wananchi takribani Milioni nne walifikiwa.

***(iii)* Kuandaa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Matukio na Makosa ya Mtandao**

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imewezesha uandaaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Matukio na Makosa ya Mtandao Nchini unaosimamiwa na kutumika na Jeshi la Polisi Tanzania. Mfumo huu utawezesha kuimarisha ulinzi na usalama mtandaoni kwa kuhakikisha mazingira salama ya matumizi ya TEHAMA.

***(iv)* Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Wizara kuhusu Miundombinu Muhimu ya TEHAMA**

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetoa mafunzo kwa Wataalam wa Wizara kuhusu Miundombinu Muhimu ya TEHAMA kwa kushirikiana na Wataalam kutoka Nchi za Estonia na Finland ambapo mafunzo haya yameongeza uwezo wa Wataalam kutambua na kulinda miundombinu muhimu ya TEHAMA, hivyo kuimarisha usalama wa Taifa, Uchumi wa Kidijitali, na utoaji wa huduma bora kwa Wananchi.

### *(v)* Kuanzisha Jumuiya za Usalama Mtandao

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeanzisha Jumuiya za Usalama Mtandao (Cyber Security Communities) katika Vyuo mbalimbali Nchini. Jumuiya hizo zinalenga kuwatambua vijana wenye uelewa na hamasa katika masuala ya Usalama wa Mtandao na kuwajenga kimaadili ili kuhimiza matumizi sahihi na salama ya Mtandao. Hadi Machi, 2026 Wizara imefanikiwa kuanzisha Jumuiya hizo katika Vyuo sita vya UDOM, UDSM, IAA, ATC, DIT na IFM. Aidha, Wizara imeanzisha jukwaa la Mawasiliano linalowaunganisha Viongozi wa Jumuiya za Usalama wa Mtandao katika Vyuo husika ili kuendelea kuhamasisha matumizi sahihi na salama ya Mtandao. Vilevile, Wizara inaendelea na jitihada za kuratibu uanzishwaji wa Jumuiya za Usalama Mtandao katika Vyuo mbalimbali Nchini.

### 3.2.5 Utekelezaji wa Majukumu Mengine ya Wizara

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu mengine kama ifuatavyo:

(i) Kukamilisha taratibu za ndani ya Serikali kwa ajili ya kuridhiwa kwa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014;

(ii) Kukamilisha uandaaji wa Waraka wa Baraza la Mawaziri (BLM) kuhusu Mapendekezo ya Kutunga Sera Mpya ya TEHAMA ya Mwaka 2026 pamoja na Mkakati wa Utekelezaji na kuwasilisha katika ngazi mbalimbali za Serikali kwa ajili ya kuridhiwa. Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa Andiko Dhana la utungwaji wa Sheria ya TEHAMA ya Mwaka 2026 na kuwasilisha kwa wadau kwa ajili ya kutoa maoni;

(iii) Kukamilisha uandaaji wa Waraka wa Baraza la Mawaziri (BLM) kuhusu Mapendekezo ya Kuhuisha Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 Toleo la 2026 ambapo pamoja na masuala mengine itajumuisha Miongozo itakayosaidia kusogeza Huduma za Posta kwa Wananchi katika maeneo ya Vijijini na yasiyo na mvuto kibiashara;

(iv) Kupandisha Vyeo Watumishi **44** baada ya kutumikia Vyeo walivyonavyo kwa muda wa miaka mitatu na kukidhi matakwa ya miundo ya Utumishi;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa Watumishi **89** kulingana na kada zao. Kati ya Watumishi hao, **78** wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na **11** wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya Nchi;

(vi) Kukamilisha kuandaa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano wa Mwaka 2026/27 – 2030/31;

(vii) Kusimamia ujenzi wa jengo la Ofisi za Wizara zilizopo Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ambapo hadi Machi, 2026 ujenzi wa jengo umefikia **asilimia 99**. Kazi inayoendelea sasa ni kufanya *landscaping* eneo la nyuma ya jengo. Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika Mei, 2026;

(viii) Kuanza taratibu za utungwaji wa Sheria ya Anwani za Makazi ya Mwaka 2026 pamoja na Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali - NDTI; na

(ix) Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini wa masuala ya TEHAMA (National ICT M&E Framework).

### 3.2.6 Mchango wa Sekta Binafsi katika utekelezaji wa Bajeti ya Wizara

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari unachangiwa kwa asilimia kubwa na Ushiriki wa Sekta Binafsi katika ujenzi na usambazaji wa Miundombinu ya Mawasiliano. Mathalani katika ujenzi wa Minara ya Mawasiliano, Watoa Huduma za Mawasiliano (Honora, Airtel, Halotel, TTCL na Vodacom) huchangia **asilimia 60** ya gharama za ujenzi kwa kila mnara. Pamoja na hayo, Sekta Binafsi zinashiriki katika kuchochea Uchumi wa Kidijitali kwa kuwezesha maunganisho ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa mtumiaji wa mwisho (Lastmile Connectivity) hali inayoongeza kasi ya upatikanaji wa Huduma ya Intaneti ikiwemo majumbani na maeneo ya Umma.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni za Sekta Binafsi za Mawasiliano na zinazohusika na ujenzi wa Minara ya Mawasiliano zimejenga Jumla ya Minara **9,124** kufikia Machi, 2026 kati ya minara hiyo Minara **1,653** imejengwa kwa Ushirikiano na Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF). Hatua hii imewezesha kuongeza wigo wa upatikanaji wa Huduma za Simu na Intaneti kwa Wananchi takribani **Milioni 46.** Aidha, pamoja na kuongeza wigo wa upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano, Minara hii imewezesha kupunguza gharama kwa waendeshaji wa mitandao na kuwezesha ujumuishaji wa Kidijitali hasa katika maeneo ya Vijijini na pembezoni ambayo hapo awali hayakuwa na huduma za uhakika za Mawasiliano.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Watoa Huduma za Mawasiliano wamekuwa na mchango mkubwa kwenye Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Nchini kwa kuwezesha yafuatayo: Utoaji mikopo inayowezesha ukuaji wa biashara ndogo na za kati; Utoaji wa ajira za kudumu na zisizo za kudumu kwa Wananchi; Ufikishaji wa Huduma ya Intaneti katika maeneo ya Umma; na Kufungua fursa za Biashara Mtandao. Hatua hii itawezesha kufikia malengo yaliyoainishwa kwenye Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali (2024 – 2034).

## 3.3 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**86.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **Bilioni 277,047,483,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi saba ya Maendeleo. Kati ya miradi hiyo, mitatu inatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani, mitatu inatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani na nje na mradi mmoja unatekelezwa kwa kutumia fedha za nje. Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 139,888,279,600** sawa na **asilimia 50.4**. Hali ya utekelezaji wa kila mradi ni kama ifuatavyo;

### 3.3.1 Mradi wa Mawasiliano Vijijini

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu na kusimamia ujenzi wa Miundombinu ya Mawasiliano Vijijini. Mradi huu unahusisha ujenzi wa Minara **636,** ambapo **621** ni ya Simu na **15** ni ya Redio.

Mkataba wa ufundi wa mradi huu ulisainiwa tarehe 23 Oktoba, 2023 baina ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mkandarasi China Technical Import and Export Corporation (CNTIC). Mradi huu unatekelezwa kwa muda wa miezi 24 kuanzia tarehe 09 Disemba, 2024 hadi 08 Disemba, 2026 kwa gharama ya **Dola za Marekani 108,579,160** ambazo ni Mkopo wenye Masharti Nafuu kutoka Benki ya Exim ya China. Aidha, Mkataba wa fedha ulisainiwa tarehe 27 Septemba, 2024 baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Benki ya Exim ya China.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mradi wa Mawasiliano Vijijini umetengewa Bajeti ya **Shilingi 131,077,920,208**. Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea **Shilingi 39,225,668,288.55** sawa na **asilimia 29.9** ya lengo lililokusudiwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Minara **456** kati ya **636** iliyopangwa kujengwa sawa na **asilimia 72.** Kati ya Minara iliyokamilika **441** ni ya Simu na **15** ni ya Redio. Hadi Machi, 2026 Minara **328** ya Simu na Minara **14** ya Redio imewashwa na inatoa huduma kwa Wananchi;

(ii) Kuwezesha ugomboaji wa vifaa kwa ajili ujenzi wa Minara ya Mawasiliano;

(iii) Kuwezesha mafunzo kwa Wataalamu **259** wanaosimamia Mradi wa Mawasiliano Vijijini. Kati ya Wataalamu hao, **72** wameshiriki mafunzo nje ya Nchi (China) na **187** wameshiriki mafunzo ndani ya Nchi;

(iv) Kuandaa Andiko la utekelezaji wa Mradi wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya Pili utakaohusisha ujenzi wa Minara **339**. Kati ya Minara tajwa, **327** ni ya Simu na **12** ni ya Redio. Aidha, mradi huu utajumuisha maunganisho **300,000** ya wateja wa faiba (FTTH);

(v) Kufanya tathmini kwa kushirikiana na UCSAF ili kubaini maeneo yenye changamoto za Mawasiliano na kuandaa

Mpango Kazi wa kutatua changamoto hizo kwenye Mikoa **31** Nchini; na

(vi) Kuandaa Mkakati wa Miaka Mitano 2025 – 2030 wa kufikisha Huduma za Mawasiliano ya Simu kote Nchini kwa kushirikiana na wadau wa Mawasiliano (MNOs, UCSAF na TCRA).

### 3.3.2 Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Anwani za Makazi ni miundombinu ambayo kwa pamoja inatambulisha mahali halisi mtu ama kitu kilipo, iwe ni nyumbani, ofisini au eneo la biashara. Kufuatia maendeleo ya teknolojia, miundombinu hii huambatishwa na mifumo ya Kidijitali ili kuimarisha utendaji kazi katika utekelezaji na matumizi ya Mfumo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kutoa huduma kwa wananchi ikiwemo Barua ya Utambulisho Kidijitali na Programu Tumizi ya NaPA. Mradi huu unatekelezwa Nchini kwa kutumia Fedha za Ndani. Hata hivyo, Serikali kupitia Wizara ya Fedha ipo katika mazungumzo na wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwemo nchi ya Korea Kusini kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa fedha zitakazowezesha utekelezaji wa mradi husika.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mradi wa Anwani za Makazi na Postikodi umetengewa Bajeti ya **Shilingi 26,842,400,000**. Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea **Shilingi 4,144,593,000** sawa na **asilimia 15.4** ya lengo lililokusudiwa. Aidha, **Shilingi 2,013,879,894** zimetolewa kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali kuwezesha utekelezaji wa shughuli za mradi. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Ununuzi wa Vishikwambi **3,482** kwa ajili ya Watendaji wa Serikali za Mitaa ili kuongeza kasi ya utoaji huduma kwa Wananchi Kidijitali. Aidha, Wadau wamehamasishwa kuchangia Vishikwambi **200** na ahadi ya Vishikwambi **1,500** na kufanya jumla ya vishikwambi vilivyopatikana kuwa **3,682** kati ya Vishikwambi **21,872** vinavyohitajika kwa ajili ya Wadau wa Mfumo wa Anwani za Makazi, Watendaji wa Kata, Mitaa, Vijiji na Shehia. Vilevile, Wizara imeandaa Mwongozo wa Usimamizi

na Matumizi ya Vishikwambi husika na kusambazwa kwa walengwa;

(ii) Kuunganisha Mfumo wa NaPA na mifumo mitatu ya kutolea huduma ambayo ni *Exchange Gateway* wa TBS, Tanzania *Intergrated Statistical Portal* wa NBS na Mfumo wa Ajira wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na kupelekea jumla ya Mifumo **29** kuunganishwa na Mfumo wa NaPA;

(iii) Kufanya uhakiki wa anwani **48,492** katika Halmashauri tatu za Jiji la Mbeya, Manispaa za Songea na Iringa. Katika uhakiki huo jumla ya anwani mpya **8,094** ziliweza kusajiliwa na kufanya anwani zilizokusanywa katika Mikoa husika kuongezeka kutoka anwani **238,958** zilizokuwepo awali hadi **247,052** sawa na ongezeko la **asilimia 3.4**;

(iv) Kuwezesha utoaji wa barua za utambulisho **655,689** Kidijitali kwa waombaji wapya wa mikopo inayotolewa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hadi Machi, 2026 jumla ya barua za utambulisho **715,196** zimetolewa Kidijitali kupitia Mfumo wa Anwani za Makazi. Idadi hii inajumuisha waombaji **32,083** wa ajira kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Aidha, juhudi za kuhamasisha watumiaji wengine kutumia Mfumo zikiwemo Taasisi za kifedha zinaendelea;

(v) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi ya Mfumo wa NaPA kupitia *Outreach programs,* maonesho, vipindi vya Redio, Televisheni na Mitandao ya Kijamii ikiwemo *Instagram na Youtube*;

(vi) Kufanya maboresho ya Mfumo wa NaPA ili kuendana na mahitaji ambapo maboresho yaliyofanyika ni pamoja na:

(a) Kuboresha *NaPA Data Collection Tool* ili iweze kutengeneza na kuonesha taarifa za kijiografia za majengo na viwanja yaani *building footprints* na *plots polygons* ili kuwezesha ukusanyaji wa kodi ya majengo;

(b) Kuboresha moduli ya ukusanyaji na uhuishaji wa taarifa za Anwani za Makazi nje ya mtandao;

(c) Kuboresha moduli ya usimamizi wa wakusanya taarifa ili wasiweze kukusanya na kuhuisha taarifa nje ya eneo la kazi;
(d) Uandaaji wa *Application Progamming Interface* (API's) zinazotumika kuunganisha mifumo; na
(e) Uchambuzi wa mahitaji ya kuboresha kanzidata ya mfumo (System Database Revamping).

(vii) Kujenga uwezo kwa Watendaji wa Serikali za Mitaa **5,559** kuhusu matumizi ya Mfumo wa Anwani za Makazi;

(viii) Kuandaa Wiki ya Anwani za Makazi iliyofanyika tarehe 2 – 8 Februari, 2026. Aidha, Wizara imefanya Kongamano la masuala ya Anwani za Makazi ambalo lilihudhuriwa na washiriki **1,200** katika siku ya kilele kutoka ndani na nje ya Nchi. Lengo la kongamano hili ni kuwa na Jukwaa la kila Mwaka na kualika Nchi mbalimbali kuja Tanzania kujifunza utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi na kuifanya Tanzania kuwa kinara wa utekelezaji ndani ya Bara la Afrika;

(ix) Kushiriki kwenye kongamano la *Global Address Innovation Conference* lililofanyika Septemba, 2025 Goyang - Korea Kusini. Kupitia kongamano hili Wataalamu wa Mfumo wa Anwani za Makazi wamepata uzoefu kuhusu utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi; na

(x) Kuliwezesha Shirika la Posta Tanzania magari **12** ili kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

### 3.3.3 Mradi wa Tanzania ya Kidijitali

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Tanzania ya Kidijitali unatekelezwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe 29 Septemba, 2021 hadi tarehe 31 Oktoba, 2026 kwa fedha za mkopo wenye thamani ya **Dola za Marekani Milioni 150** kutoka Benki ya Dunia.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Utekelezaji wa Mradi huu unahusisha maeneo makuu manne ya Ikolojia ya Kidijitali (Digital Ecosystem), Maunganisho ya Kidijitali (Digital Connectivity), Mifumo ya utoaji huduma Kidijitali (Digital Platforms and Services) na Menejimenti ya Mradi (Project Management). Mradi huu unalenga kuongeza upatikanaji wa huduma bora na za kiwango cha juu za Intaneti yenye kasi kwa Serikali, Wafanyabiashara na Wananchi na kuboresha uwezo wa Serikali wa kutoa huduma za Umma za Kidijitali.

**93.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mradi wa Tanzania ya Kidijitali umetengewa Bajeti ya **Shilingi 28,146,257,792.** Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea **Shilingi 49,883,879,923.30** sawa na **asilimia 177.2** ya lengo lililokusudiwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilika kwa upembuzi yakinifu, usakinishaji, uanzishwaji na utumiaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA;

(ii) Kuwezesha ujenzi wa mifumo miwili Zanzibar ya *Zanzibar Government Service Directory (ZGSD)* na *Zanzibar Data Exchange Platform* (ZAN- XCHANGE);

(iii) Kuandaliwa kwa Rasimu ya Mwongozo wa Kitaifa wa Tafiti na Bunifu pamoja na Mkakati wake wa Mawasiliano (Communication Strategy);

(iv) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa Watumishi **516** wa kada ya TEHAMA Nchini;

(v) Kuwezesha uhakiki wa Anwani za Makazi katika Halmashauri tatu za Jiji la Mbeya, Manispaa ya Iringa na Songea;

(vi) Kuwezesha ujenzi wa Minara **437** kati ya **758** Nchini;

(vii) Kuwezesha ukarabati wa vituo **32** vitakavyotumika kutolea huduma za Serikali katika eneo na dirisha moja; na

(viii) Kuwezesha uundaji wa jukwaa la Biashara Mtandao na uanzishwaji wa Kituo cha Ubunifu cha Biashara Mtandao.

### 3.3.4 Mradi wa Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Park)

**94.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mradi wa Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA umetengewa Bajeti ya **Shilingi 12,800,000,000.** Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea **Shilingi 7,310,360,000** sawa na **asilimia 57.1** ya lengo lililokusudiwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha taratibu za umiliki wa eneo la mita za mraba **1,619,000** lililopo Nala, Dodoma kwa ajili ya Ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali - NDTI;

(ii) Kukamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Taasisi ya NDTI ambapo **Dola za Marekani 194,132,332** zinatarajiwa kutumika;

(iii) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa kushirikiana na Wadau wengine ikiwemo OR - UTUMISHI, PDPC na OWM - TAMISEMI kupitia Redio, Televisheni, Mitandao ya Kijamii, kutembelea Shuleni na Mitaani ambapo takribani Wananchi **Milioni 4** wamefikiwa;

(iv) Kuendelea na majadiliano na Benki ya Exim kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Taasisi ya NDTI;

(v) Kuanzisha ushirikiano na Chuo Kikuu cha Hanyang, Korea ya Kusini kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Wataalamu wa NDTI;

(vi) Kuwezesha utoaji wa mitaji kwa Kampuni Changa za TEHAMA; na

(vii) Kuwezesha uandaaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Matukio na Makosa ya Mtandao Nchini unaosimamiwa na kutumika na Jeshi la Polisi.

### 3.3.5 Mradi wa Kujenga uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu unatekelezwa na Wizara kwa lengo la kuwajengea uwezo Watumishi wa Wizara wakiwemo Viongozi na Maafisa kupitia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuwezesha kufikia malengo ya uanzishwaji wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, Mradi huu unalenga kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi kwa Watumishi wa Wizara.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mradi wa Kujenga uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu umetengewa Bajeti ya **Shilingi 3,030,905,000.** Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea **Shilingi 3,165,971,434.51** sawa na **asilimia 104.5** ya lengo lililokusudiwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Ununuzi wa magari mawili aina ya *Toyota Coaster* na moja aina ya *Toyota Land Cruiser Hard Top* kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara;

(ii) Kuwezesha uandaaji wa Rasimu ya Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Wizara 2026/27 – 2030/31;

(iii) Kuwezesha ziara ya mafunzo Nchini Thailand kwa timu ya wataalamu wa Wizara kwa ajili ya kupata uzoefu wa uandaaji wa Akaunti Maalum ya Upimaji wa Uchumi wa Kidijitali. Mafunzo haya yamefanyika tarehe 14 – 20 Disemba, 2025. Aidha, zoezi la kukusanya Data zitakazotumiwa katika uandaaji wa akaunti tajwa linaendelea;

(iv) Kuandaa Daftari la Vihatarishi la Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2025/26;

(v) Kutoa mafunzo kwa waratibu **12** wa vihatarishi wa Wizara. Mafunzo haya yalifanyika tarehe 4 – 9 Agosti, 2025 Jijini Arusha;

(vi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi sita ya maendeleo ambayo ni: Mawasiliano Vijijini; Tanzania ya Kidijitali; Anwani za Makazi na Postikodi; Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano; Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA; na Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA;

(vii) Kufanya vikao viwili vya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara 2021/22 – 2025/26 na Utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali 2024 - 2034;

(viii) Kujenga uwezo kwa Watumishi **11** wa Wizara kuhusu ukusanyaji wa takwimu za kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Mwaka 2024 – 2034. Aidha, wawakilishi **52** kutoka Wizara 26 walijengewa uwezo wa kuandaa takwimu za msingi za Mkakati na namna bora ya kuwasilisha taarifa za utekelezaji wake;

(ix) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 – 2025 kwa kukusanya na kuchambua taarifa za utekelezaji hadi 2025 na kuwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu;

(x) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Mwaka 2024 - 2034 na kuandaa Mfumo wa Kielektroniki utakaotumika na Sekta zote; na

(xi) Kufanya uchambuzi wa Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2026 – 2050) ili kubaini Maeneo ya Kimkakati na Afua zinazohusu Wizara.

### 3.3.6 Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA unahusisha ukuzaji Uchumi wa Kidijitali, kuibua bunifu za Kampuni Changa za TEHAMA pamoja na ujenzi wa Vituo vya  Bunifu za TEHAMA; kufanya

tathmini za maendeleo ya sekta ya TEHAMA na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya uundaji wa bidhaa za TEHAMA.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA umetengewa Bajeti ya **Shilingi 2,100,000,000.** Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea **Shilingi 1,240,319,484.15** sawa na **asilimia 59.1** ya lengo lililokusudiwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ukarabati wa jengo lililopo Upanga Jijini Dar es Salaam linalotumika kwa ajili ya Ofisi za Tume ya TEHAMA na kukuza bunifu za TEHAMA (Startups);
(ii) Kuanzisha madarasa manne ya kukuza TEHAMA katika Shule nne za Sekondari zilizopo katika Wilaya za Ilala, Rufiji, Kilombero na Malinyi. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kukarabati madarasa husika, kuweka samani na kusimika vifaa vya TEHAMA;
(iii) Kukamilisha ukarabati wa Kituo cha Upatikanaji wa Taarifa za TEHAMA (Information Access Centre) Dodoma kwa kushirikiana na Taasisi ya *National Information Society* kutoka Korea Kusini; na
(iv) Kukamilisha taratibu za awali za uanzishwaji wa vituo viwili vinavyotembea (Mobile Information Access Centers) vya upatikanaji wa taarifa za TEHAMA.

### 3.3.7 Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ni njia inayowezesha Mawasiliano kupita na kusafiri kwa kasi, kwa ubora wa hali ya juu na kwa uhakika kwa kutumia mfumo wa mwanga na tabia zake halisi. Mkongo wa Mawasiliano una uwezo wa kusafirisha Mawasiliano kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na Teknolojia nyingine zilizopo kama waya wa shaba, Satelaiti na siwaya/mawimbi/redio. Aidha, Mradi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ulianza kutekelezwa Mwaka 2009 ukiwa na awamu tano za utekelezaji. Awamu ya kwanza na ya pili zilihusisha uunganishaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwenye Makao Makuu ya Mikoa na kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Mikongo ya baharini iliyokuwepo. Aidha, awamu

ya tatu inayoendelea ni kuuunganisha Wilaya zote na Mkongo wa Taifa na kujenga vituo vitatu vya kuhifadhi data vya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umetengewa Bajeti ya **Shilingi 73,050,000,000.** Hadi Machi, 2026 Wizara imepokea **Shilingi 34,917,487,469.96** sawa na **asilimia 47.8** ya lengo lililokusudiwa. Fedha hizo zimetumika kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Kilometa **801** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano sawa na **asilimia 100** ya lengo lililokusudiwa;

(ii) Kuunganisha Taasisi za Haki Jinai na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo Vituo vya Polisi **49** kati **64**, Ofisi za Taifa za Mashtaka **8** kati ya **8** pamoja na Ofisi za Magereza **30** kati ya **96** zimeunganishwa. Aidha, Ofisi **47** kati ya **118** za TARURA zimeunganishwa. Vilevile, taratibu za ununuzi wa vifaa **100** vya *Video Conference* za Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaendelea na zoezi hili linatarajia kukamilika ifikapo Juni, 2026;

(iii) Kufanya malipo ya awali ya Shilingi **Bilioni 10.4** na **Dola za Marekani Milioni 2.2** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na kugharamia Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika;

(iv) Kuanza upembuzi yakinifu wa utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Maendeleo ya Kidijitali (National Digital Development Program) ambayo inalenga kuimarisha mfumo wa Kisheria, Kikanuni na Kitaasisi Kidijitali, kuboresha Miundombinu ya TEHAMA na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma bora kwa Wananchi kwa njia ya Kidijitali;

(v) Kusimamia maunganisho ya njia za Mkongo wa Mawasiliano **132,793** kati ya **279,795** sawa na **asilimia 47.5** ya lengo lililokusudiwa kwa ajili ya kufikisha miundombinu ya Faiba Mlangoni. Katika maunganisho hayo wateja **64,266** kati ya **126,740** wameunganishwa na huduma ya faiba mlangoni sawa na **asilimia 51**;

(vi) Kufanya ukaguzi wa njia **12** ambazo ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umekamilika ili kuhakikisha ubora wa

kazi iliyofanyika. Maeneo yaliyofanyiwa ukaguzi ni pamoja na: Dodoma - Kibaya – Kilindi, Kondoa - Handeni – Tanga, Shinyanga - Bariadi, Bunda - Musoma, Mbeya – Chunya – Makongolosi – Kambikatoto - Itigi, Kyaka Substation - Karagwe - Rusumo, Geita - Ushirombo, Kahama (Msalala) - Bukene, Tabora – Sikonge - Rungwa, Sikonge - Inyonga, Tabora - Urambo – Nguruka – Uvinza, Kigoma – Kidahwe;

(vii) Kufanya ukaguzi wa maunganisho ya mwisho (Lastmile connectivity) katika Ofisi **190** za Haki Jinai zikiwemo Vituo **100** vya Jeshi la Polisi, Ofisi **70** za Magereza na Ofisi **20** za Taifa za Mashtaka kwa kushirikiana na Wataalamu kutoka Taasisi za Haki Jinai ili kujiridhisha endapo maunganisho ya mwisho yaliyofanywa na Shirika la Mawasiliano Tanzania yamezingatia ubora na vigezo vinavyotakiwa;

(viii) Kuandaa Mpango Kabambe wa Miundombinu ya Kitaifa ya TEHAMA wa Mwaka 2026 – 2036;

(ix) Kukamilisha usanifu wa mfumo jumuishi wa Kitaifa kwa ajili ya usimamizi na uratibu wa Miundombinu ya TEHAMA uitwao *Digital ICT Infrastructure Management System* kwa ajili ya kukusanya taarifa za Miundombinu ya TEHAMA ili kuwezesha Wizara kupata taarifa za maendeleo ya Miundombinu ya TEHAMA Nchini; na

(x) Kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Kuhifadhi Data za mtandao Dodoma na Mjini Magharibi.

## 3.4 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI KWA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2025/26

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zilikadiria kukusanya **Shilingi 689,038,108,270.** Hadi Machi, 2026 Taasisi zimekusanya **Shilingi 546,686,947,873.36** sawa na **asilimia 79.3** ya lengo lililokusudiwa.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa kila Taasisi ni kama ifuatavyo:

### 3.4.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania – TCRA

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mamlaka ya Mawasilano Tanzania ilipanga kukusanya **Shilingi 245,989,519,796** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ada za leseni, ada za matumizi ya masafa, mrabaha, ada za usimikaji na ukarabati wa mitambo ya Mawasiliano, ada za uingizaji na usambazaji wa vifaa vya TEHAMA. Hadi Machi, 2026 TCRA imekusanya **Shilingi 262,541,403,514.40** sawa na **asilimia 106.7** ya lengo lililokusudiwa.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ni kama ifuatavyo:

***(i)*** **Utoaji wa Leseni na Rasilimali za Mawasiliano**

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa Huduma za Mawasiliano, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuimarisha Mfumo wa Utoaji Leseni na Rasilimali za Mawasiliano ambapo hadi Machi, 2026, Mamlaka imetoa leseni **1,048** ambapo kati ya hizo, **431** ni leseni za rasilimali namba (Numbering licences), **399** ni leseni ndogondogo (Class licences), **98** ni hati (Certificates) na **82** ni leseni kubwa (Individual licences). Hatua hii inaongeza wigo wa upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano kupitia Watoa Huduma waliopatiwa Leseni.

***(ii)*** **Kudhibiti Ulaghai katika Mitandao ya Mawasiliano**

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** kukua kwa Teknolojia kunapelekea baadhi ya Wananchi wasiokuwa na nia njema na Nchi yetu kufanya matukio ya utapeli. Ili kudhibiti matukio hayo, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuboresha na kusimamia uendeshaji wa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Mawasiliano (Communications Monitoring System) ambao unasimamia na kudhibiti Huduma za Mawasiliano ya Simu Nchini. Mfumo huu, umeiwezesha Mamlaka kubaini Simu za ulaghai ikiwemo utapeli kwa njia ya mitandao. Katika kipindi cha Machi 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka imebaini na kufungia jumla ya laini za Simu **62,879,** pamoja na kuzuia kufanya usajili wa laini mpya za Simu kwa

Vitambulisho vya Taifa **60,177** vilivyohusika katika matukio ya ulaghai.

**107.** ***Mheshimiwa Spika***, Sambamba na hatua hizo, Mamlaka imeendelea kushirikiana na Watoa Huduma za Mawasiliano ya Simu katika kutoa elimu kwa Umma kuhusu matumizi sahihi na salama ya Huduma za Mawasiliano, ikiwemo kuhakikisha kuwa namba **100** ndiyo inayotumika kwa Mawasiliano kati ya Mtoa Huduma na wateja, namba ***106#** inatumika kuangalia na kuhakiki namba zilizosajiliwa kwa Kitambulisho cha Taifa cha mteja na namba **15040**, inatumika kutoa taarifa za namba zilizotumika kufanya ulaghai ili ziweze kuchukuliwa hatua stahiki. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imekuwa ikishirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kutoa takwimu na uchambuzi wa maeneo yanayoonekana kuwa na majaribio mengi ya kufanya ulaghai, ili kuwezesha hatua madhubuti za udhibiti kuchukuliwa.

***(iii)*** **Usimamizi wa Mawasiliano ya Simu na Intaneti.**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kufanikisha usimamizi wa Mawasiliano Nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuboresha Mfumo wa kuhakiki Simu za ndani na za Kimataifa ili kupata takwimu za Mawasiliano yanayofanyika ndani na nje ya Nchi kwa kila Mtoa Huduma kwa ngazi ya Mkoa na Wilaya. Kupitia Mfumo huu, Serikali imeweza kupata takwimu sahihi za Mawasiliano ya Simu ambapo jumla ya Simu za Kimataifa zilizoingia Nchini kwa Machi, 2026 zilikuwa ni dakika **Milioni 16.1** ikilinganishwa na dakika **Milioni 12.9** kwa Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 24.8**. Kwa upande wa Mawasiliano ya Simu za sauti za Kimataifa zinazotoka hapa Nchini kwenda Nchi nyingine kwa Machi, 2026 zilikuwa ni dakika **Milioni 55.7** ikilinganishwa na dakika **Milioni 42.2** kwa Machi, 2025 sawa na ongezeko la **asilimia 32**.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Mawasiliano ya sauti kwa Simu za ndani za mtandao mmoja (on-net calls) dakika **112,954,285,698** zimeweza kuhesabiwa kuanzia Machi 2025 hadi Machi 2026. Takwimu zinaonesha kuongezeka kutoka dakika **7,012,477,246** kwa Machi 2025 hadi dakika **7,837,852,021** kwa

Machi 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 11.8**. Kwa Mawasiliano ya sauti kwa Simu za mtandao mmoja kwenda mwingine (off-net) kulikuwa na dakika **110,885,471,766.** Takwimu zinaonesha ongezeko kutoka dakika **6,953,125,110** kwa Machi 2025 hadi dakika **7,628,733,376** kwa Machi, 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 9.7**.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kufuatilia mwenendo wa miamala ya fedha mtandao inayofanyika Nchini ambapo takwimu zinaonesha kuwa idadi ya miamala imeongezeka kutoka **Milioni 476.7** kwa kipindi cha Julai 2025 hadi **Milioni 742.7** Machi 2026 sawa na ongezeko la **asilimia 55.8**. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa matumizi ya malipo kwa njia ya mtandao.

***(iv)*** **Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Huduma za Mawasiliano**

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Watoa Huduma za Mawasiliano wanatoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo, TCRA imeendelea kufanya ukaguzi katika mikoa yote Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, matokeo ya ukaguzi huchapishwa katika taarifa za kila robo Mwaka kupitia tovuti ya TCRA.

***(v)*** **Upimaji wa Ubora wa Huduma za Mawasiliano**

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Huduma za Mawasiliano zinazotolewa zinazingatia viwango na ubora uliowekwa kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanya upimaji wa ubora wa Mawasiliano ya Simu kwenye mitandao mitano ya Vodacom, Airtel, Viettel, TTCL na Honora katika Mikoa **31** ya Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, TCRA imefanya ufuatiliaji kwa Watoa Huduma **443** ili kuhakikisha ubora wa maudhui yanayotolewa. Kati ya Watoa Huduma hao, **224** ni wa Redio, **35** ni wa Televisheni; na **184** ni wa Maudhui Mtandaoni. Vilevile, kwa Watoa Huduma waliobainika kukiuka masharti ya leseni wameelekezwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Matakwa ya leseni.

***(vi)*** **Ukaguzi wa vifaa vya Kielektroniki**

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kupunguza athari zitokanazo na matumizi ya vifaa vya kielektroniki, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanya ukaguzi wa vifaa vya kielektroniki **423** kwa ajili ya matumizi ya ndani ya Nchi. Kati ya vifaa hivyo, **357** vilikidhi vigezo na kuidhinishwa kwa matumizi. Aidha, vifaa **66** vipo katika hatua mbalimbali za uidhinishaji.

### *(vii)* Upangaji na Usimamizi wa Rasilimali za Mawasiliano

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea na usimamizi wa rajisi ya majina ya vikoa vya dot tz ambayo ni rasilimali inayowezesha Mawasiliano ya njia ya mtandao wa Intaneti. Hadi Machi, 2026, Idadi ya majina ya vikoa vilivyosajiliwa imefikia **38,409**. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imehuisha Orodha ya Postikodi zinazotumika katika Anwani za Makazi na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 9,331 la tarehe 18 Julai, 2025. Vilevile, katika kipindi husika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetenga masafa maalum yanayotumika na Viongozi Wakuu wa Nchi za nje wanaokuja Nchini kwa ziara za kikazi. Sambamba na hayo, TCRA imewezesha masafa yaliyopangwa kwa matumizi ya 5G kutolewa kwa njia ya ushindani ambapo kampuni za Viettel (T) PLC, Honora (T) PLC na Vodacom (T) PLC ziliweza kushinda na kupatiwa masafa husika.

### *(viii)* Kuweka mazingira wezeshi ya Uchumi wa Kidijitali

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na jitihada za kufikia Uchumi wa Kidijitali, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetoa rasilimali namba za Mawasiliano bure kwa ajili ya majaribio kwa Wabunifu wa TEHAMA watano waliohitaji kufanya majaribio kwenye bunifu zao. Aidha, TCRA imefanya stadi ya Mapitio ya Mfumo wa Kisheria na Udhibiti katika Sekta za Posta, Utangazaji, Mawasiliano ya Simu na Intaneti ambazo zitasaidia kuboresha mazingira ya Uchumi wa Kidijitali Nchini.

### *(ix)* Kuimarisha Mifumo ya Kiudhibiti

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Mawasiliano (Communications Monitoring System) hususan katika uundaji wa

moduli ya Usimamizi wa Takwimu za Matumizi ya Huduma za Intaneti (Over the Top Services Monitoring) ambayo utekelezaji wake umekamilika na kuanza kutumika rasmi, kufanya maboresho katika moduli ya Usimamizi wa Ubora wa Huduma za Mawasiliano (Quality of Service Monitoring) ili kuwezesha usimamizi wa huduma zinazotolewa katika Minara ya 5G na kuboresha Moduli ya ufuatiliaji wa usajili wa laini za Simu ili kuendana na maboresho ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu usajili wa laini za Simu za Mwaka 2025.

***(x)*** **Kufuatilia, kujibu na kuripoti matukio ya Usalama wa Kimtandao**

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanya tathmini ya Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA na kutoa ushauri jinsi ya kurekebisha na kulinda Mifumo na Miundombinu ya Mtandao dhidi ya mashambulio mtandaoni. Hadi Machi, 2026, Mamlaka ilifanyia kazi matukio **198** yaliyoripotiwa kuwa na viashiria vya uhalifu mtandaoni na kutoa ushauri kwa Umma na Wadau wa Sekta ya Mawasiliano ili kuimarisha usalama mtandaoni. Aidha, katika kuimarisha usalama wa kimtandao, Mamlaka imeanza utekelezaji wa awali wa Mfumo wa Usimamizi wa Usalama wa Taarifa unaozingatia viwango vya Kimataifa vya ISO/IEC 27001.

### 3.4.2 Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL

**118. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Shirika lilipanga kukusanya **Shilingi 305,092,154,592** kutokana na Huduma za Mawasiliano, ukodishaji wa vifaa vya Mawasiliano, upangishaji wa majengo na ruzuku kutoka Serikali Kuu. Hadi Machi, 2026 Shirika limekusanya **Shilingi 180,769,753,741** sawa na **asilimia 59.3** ya lengo lililokusudiwa.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania ni kama ifuatavyo:

### *(i)* Uunganishaji wa Wilaya na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mawasiliano Tanzania limefanikiwa kuunganisha Wilaya **13** ambazo ni Sikonge (Tabora), Urambo (Tabora), Kilwa (Lindi), Inyonga (Katavi), Bariadi (Simiyu), Bukombe (Geita), Chunya (Mbeya), Karagwe (Kagera), Chemba (Dodoma), Butiama (Mara), Gairo (Morogoro), Mkinga (Tanga) na Maswa (Simiyu) na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufanya jumla ya Wilaya zilizounganishwa kufikia **122** kati ya **139** sawa na **asilimia 88**.

### *(ii)* Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mawasiliano Tanzania limekamilisha taratibu za Ununuzi kwa ajili kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo - DRC. Hadi Machi, 2026 Shirika limefanya malipo ya awali ya Shilingi **Bilioni 10.4** na Dola za Marekani **Milioni 2.2** kwa ajili ya kutekeleza mradi. Kukamilika kwa utekelezaji wa Mradi huu kutaimarisha ushirikiano baina ya Tanzania na DRC pamoja na kuongeza mapato yatokanayo na uuzaji wa Huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

### *(iii)* Kuunganisha Wateja na Huduma za Faiba Mlangoni

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** matumizi ya Intaneti ni nyenzo muhimu katika kufikia Uchumi wa Kidijitali. Katika kuongeza kasi ya matumizi ya intaneti kwa gharama nafuu, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kuunganisha Wateja Majumbani na Maofisini kupita Huduma ya Faiba Mlangoni. Hadi Machi, 2026 Shirika la Mawasiliano Tanzania limefanikiwa kujenga njia za maunganisho ya Faiba Mlangoni **132,793** kati ya njia **279,795** sawa na **asilimia 47.5** katika ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Mbeya, Mjini Magharibi (Unguja), na Mwanza. Aidha, hadi Machi, 2026 Shirika limeunganisha jumla ya wateja **64,266** wa Faiba Mlangoni sawa na **asilimia 51** ya lengo la kuunganisha wateja **126,740.**

***(iv)*** **Kuunganisha maeneo ya Umma na huduma ya Wi-Fi**

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imedhamiria kufikisha Huduma za Wi – Fi katika maeneo ya Umma ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma Kidijitali. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania imefanikiwa kufikisha huduma ya Wi-Fi katika maeneo ya Umma **50** hivyo kufanya jumla ya maeneo yaliyounganishwa kufikia **61** kati ya **120** sawa na **asilimia 51** ya lengo lililokusudiwa. Maeneo yaliyofikishiwa huduma ni pamoja na Masoko, Stendi Kuu za Mabasi, Hospitali za Rufaa za Mikoa, Vyuo Vikuu na vya Kati na maeneo ya Umma. Maeneo hayo yapo katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Geita, Pwani, Pemba, Unguja, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Tabora na Tanga.

***(v)*** **Ujenzi wa Vituo vya Kuhifadhi Data Dodoma na Mjini Magharibi**

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** maendeleo ya TEHAMA yamepelekea kuongezeka kwa taarifa zinazozalishwa kidijitali. Pamoja na uwepo wa kituo cha kuhifadhi data Dar es Salaam, ongezeko la mahitaji ya kuhifadhi data limepelekea uhitaji wa ujenzi wa vituo vipya vya kuhifadhi data ili kukidhi mahitaji yaliyopo sasa. Katika kuendelea kutoa huduma za kuhifadhi data za Serikali na Sekta Binafsi, Serikali imekamilisha kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Kuhifadhi Data Dodoma na Zanzibar - Mjini Magharibi.

**3.4.3 Shirika la Posta Tanzania – TPC**

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Shirika lilipanga kukusanya **Shilingi 43,653,957,000** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ambavyo ni Huduma za EMS, Barua, Huduma za Usafirishaji, Biashara Mtandao, Huduma za Kifedha na Uwakala, Kubadili fedha za Kigeni (Bureau de Change) na Miliki za Shirika. Hadi Machi, 2026 Shirika limekusanya **Shilingi 35,718,323,007.88** sawa na **asilimia 81.8** ya lengo lililokusudiwa.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa na Shirika la Posta Tanzania ni kama ifuatavyo:

### *(i)* Kuboresha Mfumo wa Kidijitali wa Usafirishaji wa *SwifPack*

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Huduma za usafirishaji Kidijitali, Shirika la Posta Tanzania limefanya maboresho ya Mfumo wa Usafirishaji wa *SwifPack* katika moduli ya mtumiaji na dereva kwa lengo la kuongeza ufanisi na ubora wa huduma baada ya kupokea maoni ya watumiaji (Riders and Customers feedback). Aidha, Mfumo huu kwa sasa unafanya kazi kikamilifu na kampeni mbalimbali za matangazo zinaendelea kufanyika ili kuvutia watumiaji wengi zaidi;

### *(ii)* Kuboresha Duka Mtandao la Posta

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwezesha ukuaji wa Biashara Mtandao Nchini, Shirika la Posta Tanzania limekamilisha maboresho ya Duka Mtandao liitwalo Kipepeo ikiwemo kuliunganisha Duka Mtandao na mifumo ya malipo, mifumo ya usafirishaji, mifumo ya biashara kwa biashara, biashara kwa wanunuzi, kutumia Sarafu za Nchi mbalimbali, mwonekano wa duka lenyewe na kuboresha dashibodi kwa ajili ya kufuatilia mtiririko wa huduma kwa wateja. Maboresho yaliyofanyika yanalenga kuwawezesha Wananchi na Wajasiriamali kununua na kuuza bidhaa mtandaoni;

### *(iii)* Kuboresha na Kupanua Huduma ya Usafirishaji wa Sampuli

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa Huduma ya upimaji na usafirishaji wa Sampuli za Kimaabara, Shirika la Posta Tanzania kwa kushirikiana na Wizara ya Afya limeboresha Huduma ya Usafirishaji wa Sampuli kwa kuwasajili wasafirishaji **845** na kutengeneza Mfumo wa Ufuatiliaji wa Usafirishaji wa Sampuli. Aidha, Shirika limeongeza wigo wa usafirishaji wa Sampuli za Kimaabara Nchini kutoka Mikoa **12** ya awali hadi Mikoa **31**.

### *(iv)* Kutengeneza Mfumo wa Malipo Jumuishi

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuimarisha ujumuishaji wa Huduma za Kifedha Nchini, Shirika la Posta Tanzania limetengeneza Mfumo wa Malipo Jumuishi (Ppay) ambapo hadi Machi, 2026 hatua mbalimbali zimekamilika ikiwemo, upatikanaji wa leseni ya kutoa Huduma za Kifedha kutoka Benki Kuu ya Tanzania. Aidha, hatua inayoendelea ni usanifu na ujumuishaji wa mfumo na kuunganisha Mifumo na Taasisi za Kibenki pamoja na Wadau wengine wanaotoa huduma katika Sekta ya Huduma za Kifedha.

### *(v)* Kuboresha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo Watumishi

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuendelea kuimarisha Rasilimaliwatu na kuboresha Mazingira ya Ufanyaji Kazi, Shirika la Posta Tanzania limekarabati **Ofisi 65** za Posta za Wilaya na Ununuzi wa vitendea kazi. Aidha, Shirika limetekeleza Programu **19** za Mafunzo kwa Watumishi **412** kati ya **530** waliokusudiwa sawa na **asilimia 77.7**. Mafunzo haya yanalenga kuongeza ufanisi wa utendaji kazi kwa Watumishi wa Shirika.

### 3.4.4 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote – UCSAF

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulipanga kukusanya **Shilingi 65,696,337,542** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni ruzuku kutoka Serikalini, tozo ya huduma, ruzuku kutoka TCRA na Wadau wa Maendeleo. Hadi Machi, 2026 UCSAF imekusanya **Shilingi 61,186,243,405.93** sawa na **asilimia 93.1** ya lengo lililokusudiwa.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ni kama ifuatavyo:

### *(i)* Ujenzi wa Minara 758 katika Kata 688

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa tarehe 13 Mei, 2023 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania alishuhudia utiaji saini wa ujenzi wa Minara **758** katika Kata **688** Nchini. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imekamilisha ujenzi wa Minara **758** katika Kata **688** Nchini sawa na **asilimia 100** ambapo hadi Machi, 2026 Minara yote iliyopangwa kujengwa imekamilika na inatoa Huduma za Mawasiliano kwa Wananchi. Aidha, katika kuongeza matumizi ya intaneti Nchini, Wizara imekamilisha kuongeza nguvu Minara **304** katika Kata **231** iliyokuwa ya 2G kwenda 2G/3G na 4G sawa na **asilimia 100**. Kukamilika kwa mradi huu, kumewezesha Wananchi zaidi ya **Milioni 8.5** katika Mikoa yote **26** ya Tanzania Bara kufikiwa na Huduma za Mawasiliano.

***(ii)*** **Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu 600 wa Shule za Umma**

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unatekeleza Mradi wa Upelekaji wa Vifaa vya TEHAMA kwa Shule za Umma za Msingi na Sekondari. Utekelezaji wa Mradi huu unaenda sambamba na utoaji wa mafunzo kwa Walimu wanaohusika na ufundishaji wa TEHAMA Mashuleni. Hadi Machi, 2026 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umefanikiwa kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu **600** wa Shule za Umma za Msingi na Sekondari. Kati ya Walimu tajwa, **100** wanatoka Zanzibar na **500** wanatoka Tanzania Bara.

***(iii)*** **Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano kwenye maeneo yenye changamoto ya upatikanaji wa Mawasiliano ya Simu**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulikusudia kujenga Minara **287** Nchini ili kutatua changamoto za Mawasiliano. Hadi Machi, 2026 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umesaini Mikataba na Watoa Huduma za Mawasiliano (TTCL, Airtel, Honora na Vodacom) kwa ajili ya ujenzi wa Minara **287** kwenye Kata **287** ambapo utekelezaji unaendelea kupitia Mradi wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya **10** na unatarajia kukamilika tarehe 4 Machi, 2027.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, UCSAF imeainisha maeneo mengine **280** ya kimkakati yenye changamoto ya Mawasiliano

kwenye miundombinu ya reli (SGR/MGR na TAZARA), Hifadhi za Taifa na Mipaka ya Nchi. Uhakiki wa maeneo haya umekamilika na taratibu za Ununuzi zinaendelea kwa ajili ya ujenzi wa Minara kupitia Mradi wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya **11**.

***(iv)*** **Kuboresha upatikanaji wa matangazo ya Redio Jamii**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imekamilisha Ujenzi wa majengo ya kuhifadhi mitambo ya Mawasiliano pamoja na misingi ya Minara ya Mawasiliano. Aidha, ujenzi wa Minara ya kurusha matangazo ya Redio Jamii katika Mikoa ya Morogoro na Simiyu umeanza kwa kumwaga zege katika nguzo zinazobeba Minara.

***(v)*** **Kutoa vifaa vya TEHAMA Kwenye Shule 10 za Umma zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu**

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unatarajia kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA katika Shule 10 za Umma zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambazo ni Musoma Tech (Musoma), Mustapha Sabodo (Mtwara), Malangali (Iringa), Moshi Sekondari (Moshi), Buhongwa (Nyamagana), Mlingano (Muheza), Kantalamba (Sumbawanga), Mubaba (Biharamulo), Tanga Tech (Tanga) na Kigoma Girls (Uvinza) zitanufaika na Mradi huu.

### 3.4.5 Tume ya TEHAMA – ICTC

**140.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Tume ya TEHAMA ilikadiria kukusanya **Shilingi 6,850,114,300** kutoka katika vyanzo vya mapato ya Tume na Serikali Kuu. Hadi Machi, 2026 Tume imekusanya **Shilingi 3,205,217,984.15** sawa na **asilimia 46.8** ya lengo lililokusudiwa.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa na Tume ya TEHAMA ni kama ifuatavyo:

***(i)*** **Kuimarisha Ushirikiano katika Sekta ya TEHAMA**

***142. Mheshimiwa Spika,*** Tume ya TEHAMA imefanya majadiliano na Vyuo vitano ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo

Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar kwa ajili ya kujadili maeneo ambayo yatapewa kipaumbele kwenye ushirikiano ikiwemo kukuza ujuzi wa Kidijitali, kukuza ubunifu pamoja na kujenga uwezo wa Wataalamu wa TEHAMA. Majadiliano haya yatawezesha uandaaji wa Mkakati wa ushirikiano kati ya Tume ya TEHAMA na Vyuo Vikuu Nchini.

***(ii)* Kuanzisha vituo vya kutengeneza na kukarabati vifaa vya TEHAMA**

**143. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya TEHAMA kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali inaendelea na ukarabati wa majengo yatakayotumika kwa ajili ya vituo vya kukarabati na kutengeneza vifaa vya TEHAMA Nchini. Majengo yapo katika ofisi za TIRDO kwa Mkoa wa Dar es Salaam na ofisi za SIDO kwa Mkoa wa Arusha. Uanzishwaji wa vituo hivi unalenga kuboresha upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA kupitia kuongeza muda wa matumizi wa vifaa vya TEHAMA wakati vinapofikia mwisho wa matumizi yake na hivyo, kuwezesha vifaa hivyo kupatikana kwa bei nafuu hususani kwa watumiaji waliopo vijijini na maeneo ya pembezoni.

***(iii)* Kusajili Wataalamu wa TEHAMA na Kampuni Changa za TEHAMA Nchini**

**144. *Mheshimiwa Spika,*** Tume ya TEHAMA imeendelea kushirikiana na wadau katika kuendesha programu za kuendeleza kampuni changa ikiwemo kutoa mchango wa kitaalamu na rasilimali katika kuwezesha programu hizo ambapo Tume ya TEHAMA imeanzisha Kanzidata maalum ya Usajili wa Kampuni Changa za TEHAMA. Hadi kufikia Machi, 2026 Kampuni Changa za TEHAMA **402** zilizo katika hatua mbalimbali za ukuaji kuanzia hatua ya ubunifu hadi kutoa huduma zimesajiliwa. Aidha, kati ya hizo Kampuni Changa **164** zilifikia kiwango na kukidhi vigezo vya kuingia kwenye programu za uendelezaji na uwezeshwaji kupitia Tume ya TEHAMA.

***(iv)* Kuanzisha modeli ya Kitaifa ya Akili Unde (AI) ya Lugha ya Kiswahili (National Kiswahili Large Language Model).**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuunda modeli kubwa ya lugha ya Kiswahili "Swahili Large Language Model" hapa Nchini. Aidha, uwepo wa *Swahili Large Language Model* utarahisha matumizi halisi ya Akili Unde kwa kutumia Kiswahili fasaha. Kupitia moduli hii ya Kiswahili, Sekta itaweza kuimarisha ujumuishaji Kidijitali kwani Wananchi wote, wakiwemo wale wa Vijijini wataweza kutumia Huduma za TEHAMA zitokanazo na matumizi ya Akili Unde katika lugha wanayoielewa, kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi na mafunzo kwa kutumia Akili Unde, kuboresha upatikanaji wa data za Kiswahili kwa wabunifu, kuhifadhi lugha za asili na maarifa ya asili katika ulimwengu wa Kidijitali.

***(v)* Kukuza na kuvutia uwekezaji wa TEHAMA**

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya TEHAMA imefanya kongamano la tisa la Mwaka la TEHAMA lililofanyika Januari, 2026 ambapo washiriki **860** kutoka ndani na nje ya Nchi walishiriki na Jukwaa la kwanza la Akili Unde (AI) lililofanyika Julai, 2025 ambapo wadau **300** kutoka ndani na nje ya Nchi walishiriki. Aidha Kongamano na Jukwaa lililoandaliwa yalilenga kuhamasisha matumizi ya TEHAMA, kukuza ujuzi na kuchochea ubunifu katika TEHAMA ili kubainisha fursa zilizopo katika Sekta ya TEHAMA.

### 3.4.6 Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi – PDPC

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26 Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ilikadiria kukusanya **Shilingi 21,046,025,040.00** kutoka katika mapato ya ndani na Serikali Kuu. Hadi Machi, 2026 Tume imekusanya **Shilingi 2,593,046,220.00** sawa na **asilimia 12** ya lengo lililokusudiwa.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ni kama ifuatavyo:

### *(i)* Kusajili Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeendelea na usajili wa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi ambapo hadi Machi, 2026 Taasisi **4,283** zimesajiliwa. Usajili huu unafanya jumla ya Taasisi zilizosajiliwa kufikia **12,214**. Aidha, Tume imefanya maboresho kwenye Mfumo wa Usajili - RCMIS kwa kupunguza mlolongo wa usajili na kuboresha moduli ya usajili kutoka kurasa nane hadi mbili na kuongeza kasi ya mfumo katika uzalishaji wa taarifa. Hatua hii imerahisisha zoezi la usajili kwa Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi.

### *(ii)* Kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inatekelezwa kama ilivyokusudiwa, Tume imeandaa Mfumo wa Ukaguzi kwa Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi utakaowezesha kufanya ukaguzi kwa wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi. Mfumo huu unatumika kufanya doria mtandaoni hivyo kurahisisha zoezi la ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022.

### *(iii)* Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ina jukumu la kutoa Elimu kwa Umma kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Tume imetoa mafunzo kwa Maafisa **1,267** wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi, imefanya vipindi **51** vya Televisheni na **26** vya Redio, imetoa machapisho mawili kuhusu Sheria ya ulinzi wa taarifa Binafsi, imetoa taarifa kwenye magazeti **25** na vyombo vya habari **108** vya mtandaoni, imeshiriki na kutoa mawasilisho **33** kwenye mikutano/warsha, imeshiriki maonesho mawili kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi, imechapisha vipeperushi **742** kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kusambaza kwa Wadau na imetoa taarifa nne kwa Umma kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

***(iv)*** **Kufanya Tafiti za Bunifu**

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imefanya tafiti mbili zinazohusu masuala ya Uchambuzi wa utayari wa Kitaasisi katika uzingatiaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 na Matumizi bora ya Teknolojia Zinazoibukia kwenye Ulinzi wa Taarifa Binafsi ikiwemo Akili Unde (AI). Tafiti hizo zipo katika hatua za mwisho za uchapishaji katika majarida ya Kimataifa.

***(v)*** **Kuanzisha na kuimarisha mahusiano ya Kikanda na Kimataifa katika masuala yanayohusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi**

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume inashirikiana na Nchi nyingine za Jumuiya ya Kikanda na Kimataifa katika masuala yanayohusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Katika eneo hili Tume imeshiriki Kikao cha Kikundi Kazi cha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) cha kuandaa Sheria ya Ubadilishanaji wa Taarifa Binafsi ndani ya Jumuiya, imeshiriki katika Mafunzo ya Kujengewa Uwezo wa Usimamizi wa Taarifa na Sera ya Usimamizi wa Taarifa ya Umoja wa Afrika (AU Data Policy Framework), imeshiriki Vikao na Wadau wa Maendeleo wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (Agence Française de Développement – AFD) vinavyohusu utekelezaji wa Mradi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Kidijitali (NDDP) na imejiunga na Mtandao wa Mamlaka za Ulinzi wa Taarifa Binafsi Barani Afrika.

***(vi)*** **Kujenga uwezo kwa Watumishi katika masuala ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ndani na nje ya Nchi**

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imewezesha jumla ya Watumishi **11** kujengewa uwezo katika maeneo mbalimbali yanayohusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi ndani na nje ya Nchi. Watumishi hao wameshiriki mafunzo katika Nchi za Uswisi, Nigeria, Rwanda, Kenya, Madagascar, Sierra Leone na Ujerumani. Tume itaendelea kuwajengea uwezo Watumishi wake ili waweze kutoa huduma kwa viwango vilivyokusudiwa

**(vii) Kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na faragha za watu**

**155.** ***Mheshimiwa Spika***, Tume imepokea ripoti ya uvunjifu wa misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi (data breach) kutoka kwa Taasisi saba na imepokea na kushughulikia malalamiko **55** ya ukiukwaji wa misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Aidha, Tume imetoa ushauri katika ripoti za uzingatiaji kwa Taasisi **900,** ushauri wa Sera za Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Taasisi ishirini na mbili **22** na imetoa vibali **38** vya kusafirisha Taarifa Nje ya Nchi.

### 3.4.7 Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano - TCRA – CCC

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2025/26, Baraza lilipanga kukusanya **Shilingi 710,000,000** kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania - TCRA kama tengeo la kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza. Hadi Machi, 2026 Baraza limepokea **Shilingi 672,960,000** sawa na **asilimia 94.78** ya lengo lililokusudiwa. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 532,500,000** sawa na **asilimia 75** ni tengeo kutoka TCRA na **Shilingi 140,460,000** sawa na **asilimia 19.8** ni michango kutoka kwa wadau.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli zilizotekelezwa na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano ni kama ifuatavyo:

**(i) Kuwezesha Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano**

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limefanikiwa kuwezesha Kamati **20** za watumiaji wa Huduma za Mawasiliano zilizopo katika Mikoa ya Arusha, Tanga, Iringa, Mbeya, Morogoro, Lindi, Mtwara, Mwanza, Kagera, Dodoma, Kigoma, Pwani, Tabora, Mjini Magharibi, Kaskazini Unguja, Kusini Pemba, Simiyu, Ruvuma, Manyara na Rukwa. Kuwezeshwa kwa kamati hizo kunalenga kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao ya kutoa elimu kwa Umma, kuhamasisha na kupokea maoni ya watumiaji.

***(ii)*** **Kuanzisha Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano**

**159.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeanzisha Kamati Mbili za watumiaji wa Huduma za Mawasiliano katika Mikoa ya Singida na Kusini Unguja. Aidha, Wajumbe wa Kamati wamejengewa uwezo kuhusu utekelezaji wa majukumu yao ikiwemo kutoa elimu kwa Umma, kuhamasisha na kupokea maoni ya Watumiaji. Kuanzishwa kwa Kamati hizi kunafanya jumla ya Kamati zilizoanzishwa Nchini kufikia **22** ambapo **18** zipo Tanzania Bara na nne zipo Zanzibar.

***(iii)*** **Kutoa elimu ya watumiaji wa Huduma za Mawasiliano**

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeandaa na kusambaza Machapisho **5,246** kati ya **10,000** sawa na **asilimia 52.5** yaliyokusudiwa ya utoaji elimu kwa watumiaji wa Huduma za Mawasiliano katika maeneo ya Ulinzi wa Mtoto mtandaoni, Haki na Wajibu kwa Mtumiaji wa Huduma za Mawasiliano, umakini wa Watumiaji katika matumizi ya Huduma za Mawasiliano na machapisho ya nukta nundu ambayo ni maalumu kwa Watumiaji wenye ulemavu wa kuona.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Baraza limeendelea kutoa elimu kuhusu Huduma za Mawasiliano ikiwemo fursa zinazopatikana kupitia TEHAMA, namna ya kutatua changamoto wanazopata watumiaji wakati wa matumizi ya Huduma za Mawasiliano, uhamasishaji matumizi sahihi ya huduma ikiwemo kulinda Miundombinu ya Mawasiliano pamoja na namna ya kuwasilisha maoni na changamoto kwa Baraza.

**162.** ***Mheshimiwa Spika***, Vilevile, Baraza limefanikiwa kufanya mikutano ya elimu **138** ambayo imefanyika katika Mikoa **20**, Vipindi **25** vya Redio na Televisheni pamoja na kurusha matangazo **2,408** ya kuelimisha na kuhamasisha kuhusu masuala muhimu yenye maslahi kwa Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano kupitia Redio zilizopo katika Mikoa sita ambayo ni Kigoma (KICORA FM), Ruvuma (Hekima FM), Pwani (Chalinze FM), Mwanza (Afya Redio FM), Lindi (Mtama FM) na Mjini Magharibi (Coconut FM). Aidha, elimu kupitia Mitandao ya Kijamii ya Instagram, Facebook na YouTube imeendelea kutolewa.

### *(iv)* Matumizi ya Mfumo wa E - Mrejesho na Mtumiaji App

**163.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza katika kutekeleza majukumu yake limefanikiwa kuwahudumia Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano kupitia Mfumo wa E – Mrejesho. Aidha, Baraza limeanzisha na kuzindua Mfumo wa Kidijitali wa kuhudumia Watumiaji ujulikanao kama Mtumiaji App ambapo hoja **578** zilizowasilishwa kwa Baraza kupitia mfumo huo zilipokelewa na kufanyiwa kazi na Watumiaji waliweza kupata mrejesho wa utatuzi wa hoja hizo.

### *(v)* Kufanya mashauriano na Wadau wa Sekta ya Mawasiliano

**164.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limefanya mashauriano na Wadau wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ikiwemo TCRA, UCSAF, TAMNOA na Wadau wa Utangazaji. Mashauriano hayo yanahusu masuala mbalimbali yenye maslahi ya watumiaji wa Huduma za Mawasiliano kwenye maeneo ya TEHAMA, Utangazaji, Posta, Usafirishaji wa vifurushi na vipeto. Kufanyika kwa mashauri hayo kumewezesha kuwa na ushirikiano katika kutekeleza baadhi ya majukumu ya Baraza pamoja na kupunguza changamoto za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano.

### *(vi)* Kujenga uwezo kwa Watumishi wa Baraza

**165.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limefanikiwa kuwajengea uwezo Watumishi wawili ili kuwaongezea ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao hususani katika matumizi ya Mifumo ya TEHAMA pamoja na masuala ya Kihasibu ili kuboresha utendaji kazi katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

## SURA YA NNE

## 4.0 MAKADIRIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2026/27

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27

umezingatia yafuatayo: Maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 14 Novemba, 2025; Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27 - 2028/29; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050; Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 - 2030/31; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025; Maoni na Ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu; pamoja na Ahadi na Maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

## 4.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27

**167*. Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele nane kama ifuatavyo:

(i) Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa Miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
(ii) Kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Posta Nchini;
(iii) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Biashara Mtandao Nchini;
(iv) Kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa Uchumi wa Kidijitali;
(v) Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Anga ya Mtandao;
(vi) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa Kampuni Changa (Startups);
(vii) Kuimarisha uwekezaji katika TEHAMA na utekelezaji wa Programu ya Anga za Juu; na
(viii) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu masuala yanayohusu Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Teknolojia zinazoibukia.

### 4.2 Majukumu yatakayotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27

### 4.2.1 Majukumu yatakayotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** majukumu yatakayotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27 yamefafanuliwa katika maeneo yafuatayo;

#### 4.2.1.1 Sehemu ya Mawasiliano

**169.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuendelea na taratibu za utungwaji wa Sera ya Anga za Juu ya Mwaka 2026;
(ii) Kukamilisha taratibu za utungwaji wa Sheria ya Anwani za Makazi ya Mwaka 2026;
(iii) Kukamilisha mapitio ya Sera ya Posta ya Mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2026 pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake;
(iv) Kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Redio Nchini katika maeneo yasiyo na mvuto kibiashara;
(v) Kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Posta Nchini kwa kuongeza wigo wa upatikanaji wa Huduma za Msingi za Posta;
(vi) Kutekeleza Mkakati wa Kuimarisha Ushiriki wa Tanzania Kikanda na Kimataifa katika Sekta ya Mawasiliano;
(vii) Kushiriki na kutoa michango ya kuwezesha maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano Duniani;
(viii) Kuimarisha utekelezaji, uendelezaji na matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Anwani za Makazi kwa kuboresha Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi;
(ix) Kuandaa Mpango Mahsusi wa Kitaifa wa Mfumo wa Anwani za Makazi;
(x) Kuendelea na uratibu wa mradi wa kurusha Satelaiti ndogo ya mafunzo - CUBESAT;
(xi) Kuendeleza Wataalam wa Sekta ya Mawasiliano kwa kutoa mafunzo kuhusu teknolojia zinazoibukia;

(xii) Kusimamia utendaji wa TCRA, UCSAF, TPC, TCRA - CCC pamoja na Watoa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Posta;
(xiii) Kusimamia uundaji wa Mfumo wa Kidijitali utakaowezesha Biashara Mtandao (e-Commerce);
(xiv) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Mawasiliano Vijijini;
(xv) Kuratibu Wiki ya Anwani za Makazi itakayofanyika tarehe 2 – 8 Februari, 2027;
(xvi) Kusimamia Utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano ya Simu wa Mwaka 2026 – 2031;
(xvii) Kuandaa kongamano la Kimataifa la Uwekezaji katika Mawasiliano na Anga za Juu; na
(xviii) Kuratibu na kusimamia Mradi wa Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Bidhaa za Biashara Mtandao Nchini.

**4.2.1.2 Sehemu ya Miundombinu ya TEHAMA**

**170.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kusimamia ufanisi wa Miundombinu Muhimu ya TEHAMA ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data, Mikongo ya Baharini, Vituo vya Maunganisho ya Intaneti na Miundombinu ya Saini za Kielektroniki;
(ii) Kusimamia utendaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania - TTCL;
(iii) Kusimamia ujenzi wa Miundombinu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
(iv) Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Brodibendi pamoja na Mpango Kabambe wa Miundombinu ya TEHAMA (ICT Infrastructure Masterplan 2026 - 2036);
(v) Kusimamia utekelezaji wa Miongozo ya Miundombinu ya TEHAMA;

**4.2.1.3 Sehemu ya Uendelezaji wa Mifumo, Huduma za TEHAMA na Uzingatiaji**

**171.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuandaa Miongozo mitano ya usimamizi na uzingatiaji wa Huduma za TEHAMA;
(ii) Kuratibu utekelezaji wa Miongozo mitatu ya TEHAMA;
(iii) Kuanzisha Mpango wa Kitaifa wa Mageuzi ya Kidijitali;
(iv) Kuwezesha uuzaji wa Mifumo ya Huduma za TEHAMA nje ya Nchi;
(v) Kuratibu uanzishwaji wa Vituo saba vya ubunifu vya TEHAMA;
(vi) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali 2024 – 2034;
(vii) Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Tafiti na Bunifu za TEHAMA 2026 – 2031;
(viii) Kusimamia utekelezaji wa programu mbili za uwezeshaji wa wabunifu na Kampuni Changa za TEHAMA;
(ix) Kusimamia uanzishaji wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali itakayojengwa Nala, Dodoma;
(x) Kuratibu Mikutano **10** ya Kikanda na Kimataifa ya TEHAMA; na
(xi) Kusimamia utendaji wa Tume ya TEHAMA.

### 4.2.1.4 Sehemu ya Ulinzi na Usalama wa TEHAMA

**172.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kutoa mafunzo ya Usalama wa Mtandao kwa Watumishi **80** wa Serikali na **20** wa Sekta Binafsi;
(ii) Kutoa elimu na uhamasishaji kwa Umma kuhusu Usalama wa Mtandao;
(iii) Kuhuisha Sheria ya Makosa ya Mtandao ya Mwaka 2015;
(iv) Kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati wa Usalama wa Mtandao;
(v) Kutoa elimu ya Miongozo ya Miundombinu Muhimu ya TEHAMA;
(vi) Kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya Usalama wa Mtandao; na
(vii) Kusimamia utendaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

### 4.2.2 Miradi itakayotekelezwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itatekeleza Miradi nane ya Maendeleo ili kuendelea kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano itakayochochea matumizi ya TEHAMA na hatimaye kufikia adhma ya Serikali ya kuwa na Uchumi wa Kidijitali unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.2.1 Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

**174.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 103,600,425,000** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Shughuli zitakazotekelezwa kwenye mradi huu ni:

(i) Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;
(ii) Kuunganisha vituo **20** na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
(iii) Kuwezesha ujenzi wa Vituo viwili vya Taifa vya Kuhifadhi Data za Intaneti katika Mkoa wa Dodoma na Zanzibar;
(iv) Kuratibu na kusimamia vituo saba vya mabadilishano ya Intaneti;
(v) Kuwezesha maunganisho ya mwisho (Last Mile Connectivity) katika Shule **100**;
(vi) Kuwezesha ufikishwaji wa Huduma ya Wi-Fi katika maeneo **100** ya Umma Nchini;
(vii) Kuwezesha ujenzi wa Miundombinu ya Kitaifa ya Taarifa Muhimu (National Critical Information Infrastructure) katika maeneo **100** ya Umma;
(viii) Kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Brodibendi pamoja na Mpango Kabambe wa Miundombinu;
(ix) Kuwezesha maboresho ya Kituo cha Taifa cha kuhifadhi Data kilichopo Kijitonyama, Dar es Salaam;
(x) Kusimamia utekelezaji wa ujenzi wa Miundombinu ya Mkongo wa Mwisho (Last Mile Optic Fiber) kwa Taasisi **100** za Haki Jinai, Taasisi za Ulinzi na Usalama (Mahakama, TAKUKURU, Polisi, Magereza, JWTZ, Usalama) na Taasisi zingine za Serikali; na

(xi) Kuwezesha usakinishaji na uboreshaji wa vifaa vya mikutano ya video (Video Conference) katika Wilaya **100**.

#### 4.2.2.2 Kuimarisha uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu

**175.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 3,200,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Majukumu. Fedha hizo zimekusudia kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuendelea na maandalizi ya Akaunti Maalum ya Upimaji wa Uchumi wa Kidijitali;
(ii) Kuwezesha maandalizi ya Daftari la Vihatarishi la Wizara na kutoa mafunzo kwa wamiliki na waratibu wa vihatarishi;
(iii) Kufanya *benchmarking* katika Nchi mbili kwa ajili ya kupata uzoefu wa kuandaa Akaunti ya Maalum ya Upimaji wa Uchumi wa Kidijitali;
(iv) Kutoa mafunzo kwa Watumishi **25** ili kuratibu utekelezaji wa Akaunti Maalum ya Upimaji wa Uchumi wa Kidijitali;
(v) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na Maagizo ya Serikali;
(vi) Kusimamia utekelezaji wa Ajenda ya Utafiti ya Wizara;
(vii) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini kwenye miradi nane ya Wizara; na
(viii) Kuwezesha Ununuzi wa vitendea kazi vya Watumishi ikiwemo magari ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

#### 4.2.2.3 Mfumo wa Anwani za Makazi

**176.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara imekadiria kutumia **Shilingi 16,149,040,000** kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi. Fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha taratibu za utungwaji wa Sheria ya Anwani za Makazi ya Mwaka 2026;

(ii) Kujenga uelewa kwa jamii kuhusu utekelezaji, matumizi na manufaa ya Mfumo wa Anwani za Makazi Nchini;
(iii) Kuandaa Mpango Kabambe wa matumizi ya Taarifa za Anwani za Makazi;
(iv) Kuwezesha upatikanaji wa vitendea kazi vya TEHAMA kwa ajili ya Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi;
(v) Kujenga uwezo kwa Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Wadau kuhusu Mfumo wa Anwani za Makazi;
(vi) Kuboresha Programu Tumizi na Kanzidata ya Mfumo wa Anwani za Makazi;
(vii) Kutengeneza moduli tatu za Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi; na
(viii) Kuwezesha uunganishaji wa Mfumo wa NaPA na mifumo mitano ya kutolea huduma.

#### 4.2.2.4 Mawasiliano Vijijini

**177.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 40,007,673,000** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Mawasiliano Vijijini. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Minara **636** Nchini;
(ii) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Mawasiliano ya Simu wa Mwaka 2026 – 2031;
(iii) Kuratibu upembuzi wa pamoja (Joint Survey) kubainisha maeneo yenye changamoto za huduma ya Mawasiliano katika Mikoa **31** Nchini;
(iv) Kuwezesha Mafunzo ya usimamizi kwa Wataalamu wanaosimamia mradi.

#### 4.2.2.5 Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Parks)

**178.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 13,728,556,000** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya

Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukuza Ujuzi na Maarifa ya Kidijitali kwa Wananchi;
(ii) Kufanya mafunzo kuhusu Teknolojia zinazoibukia ikiwemo Akili Unde;
(iii) Kuratibu utekelezaji wa Miongozo mitatu ya TEHAMA;
(iv) Kuanzisha Mpango wa Kitaifa wa Mageuzi ya Kidijitali;
(v) Kuratibu uanzishwaji wa Vituo saba vya ubunifu vya TEHAMA;
(vi) Kujenga uelewa kwa Wananchi kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Anga za Juu;
(vii) Kuandaa na Kuwezesha Utekelezaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Uzingatiaji wa TEHAMA;
(viii) Kuwezesha utekelezaji wa Mfumo wa Jamii Stack na kuboresha Mfumo wa TEMBO *Portal*;
(ix) Kuratibu uzingatiaji na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mifumo ya Kitaifa ya TEHAMA;
(x) Kusimamia utekelezaji wa programu mbili za uwezeshaji wa wabunifu na Kampuni Changa za TEHAMA;
(xi) Kuwezesha kuunganisha Mifumo **110** ya TEHAMA katika majukwaa ya Kitaifa ya data X-Change katika Taasisi za Umma na Binafsi;
(xii) Kufanya mafunzo ya Usalama wa Mtandao kwa Watumishi **100** wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;
(xiii) Kufanya kampeni **10** kwenye vyombo vya habari kuhusu Usalama wa Mtandao; na
(xiv) Kuwezesha uundwaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa matukio na makosa ya mtandao Nchini.

#### 4.2.2.6 Tanzania ya Kidijitali

**179.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 12,157,585,000** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Tanzania ya Kidijitali. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuwezesha ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali na Kituo cha Ubunifu pamoja na vituo vitano katika kanda tano Nchini;

(ii) Kuwezesha ununuzi, usambazaji, ufungaji wa vifaa vya TEHAMA na kuanza matumizi ya vifaa hivyo katika vituo vitano vya Kanda;
(iii) Kuwezesha ununuzi, usambazaji, ufungaji na matumizi ya miundombinu ya Anwani za Makazi Nchini;
(iv) Kuwezesha uanzishwaji wa vituo **32** vya Huduma Pamoja Nchini;
(v) Kukamilisha usakinishaji, uanzishwaji na matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Usimamizi wa Taarifa za Takwimu za TEHAMA (Jamii Data Lake) Nchini; na
(vi) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidijitali 2024 – 2034.

#### 4.2.2.7 Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA

**180.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 2,100,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuanzisha vituo viwili vinavyotembea vya upatikanaji wa taarifa za TEHAMA Nchini (ICT Mobile Information Access Centers);
(ii) Kufanya tathmini ya Mifumo ya Kidijitali na usajili wa majukwaa ya Biashara Mtandao na Huduma za Kielektroniki Nchini;
(iii) Kufanya tafiti tatu za matumizi ya Teknolojia za Kidijitali zinaozoibukia katika Sekta za Uzalishaji na Huduma;
(iv) Kuandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Vituo vya Ubunifu na Vituo vya Kukarabati Vifaa vya TEHAMA Nchini;
(v) Kufanya utafiti wa Mnyororo wa Thamani wa Uchakataji Taka za Kielektroniki;
(vi) Kufanya mapitio ya Mfumo wa Kitaifa wa Maendeleo ya Ujuzi katika TEHAMA (ICT Skills Development Framework);
(vii) Kujenga uwezo wa Wataalam wa ndani katika kusimamia Miradi ya TEHAMA; na
(viii) Kuanzisha Modeli ya Kitaifa ya Akili Unde (AI) ya Lugha ya Kiswahili (National Swahili Large Language Model).

#### 4.2.2.8 Ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali – NDTI

**181.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 18,500,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali. Fedha hizo zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuwezesha utungwaji wa Sheria ya Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali;
(ii) Kuwezesha ujenzi wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali;
(iii) Kuandaa Mtaala wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali;
(iv) Kufanya *benchmarking* katika Nchi mbili kwa ajili ya kupata uzoefu wa uanzishwaji wa Taasisi ya NDTI; na
(v) Kujenga uelewa kwa Watumishi nane wa Taasisi ya NDTI.

### 4.2.3 Mipango na Bajeti za Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/27

**182.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27 Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari zinakadiria kukusanya **Shilingi 921,119,791,807.89** na kutumia **Shilingi 877,688,851,568.76** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Mchanganuo wa mapato na matumizi ya kila Taasisi ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.3.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania – TCRA

**183.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepanga kukusanya **Shilingi 235,400,000,000**—na kutumia **Shilingi 235,400,000,000** ambapo **Shilingi 185,450,000,000**—ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ikiwemo Mishahara na Matumizi Mengineyo na **Shilingi 49,450,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**184.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kuendelea kutoa mafunzo kwa Watumishi **252** ili kuwajengea uwezo katika usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano;
(ii) Kuweka mazingira wezeshi ya Uchumi wa Kidijitali kwa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za Mawasiliano;
(iii) Kuimarisha ukusanyaji wa Ada za kiudhibiti ili kuhakikisha usimamizi wa huduma bora za Mawasiliano;
(iv) Kuendelea kutoa elimu kwa watumiaji na Wadau wengine wa Huduma za Mawasiliano ili kuongeza uelewa kuhusu haki na wajibu wao;
(v) Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa Huduma za Mawasiliano ili kuhakikisha huduma zinatolewa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na kwa kuzingatia Masharti ya leseni;
(vi) Kufuatilia matukio ya usalama mtandaoni na kuchukua hatua stahiki ili kupunguza au kuondoa uwezekano wa kushambuliwa kwa mifumo;
(vii) Kuendelea kuimarisha Mifumo ya usimamizi ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na usimamizi wa Sekta ya Mawasiliano;
(viii) Kufanya tafiti tatu ili kufanya maboresho yanayostahili katika kuisimamia Sekta ya Mawasiliano kwa ufanisi;
(ix) Kuendelea na kampeni ya kuhamasisha uanzishwaji wa Vilabu vya Kidijitali Shuleni ili kukuza uelewa wa masuala ya TEHAMA;
(x) Kuimarisha shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini kwenye miradi na shughuli zilizopangwa ili kuongeza ufanisi;
(xi) Kusimamia na kutekeleza Mwongozo wa Mazingira, Jamii na Utawala (Environmental, Social, and Governance) kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa, pamoja na kuanza maandalizi ya kupata uthibitisho wa mfumo wa usimamizi wa mazingira (ISO 14001), sambamba na kuimarisha usimamizi wa hatari za kimazingira, kijamii na kiutawala katika Sekta ya Mawasiliano;
(xii) Kuanzisha na kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Usalama wa Taarifa (Information Security Management System – ISMS) kwa kuzingatia viwango vya ISO/IEC 27001, sambamba na kuimarisha usimamizi wa hatari za usalama wa TEHAMA katika Sekta ya Mawasiliano.
(xiii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la TCRA Dodoma na Zanzibar; na
(xiv) Kuimarisha ushiriki wa TCRA kwenye Taasisi **10** za Kikanda na Kimataifa.

### 4.2.3.2 Shirika La Posta Tanzania – TPC

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Shirika la Posta Tanzania limepanga kukusanya **Shilingi 50,933,863,225** na kutumia **Shilingi 49,353,956,977** ambapo **Shilingi 18,000,000,000** ni kwa ajili ya Mishahara **Shilingi 26,853,956,977** ni kwa ajili ya gharama za uendeshaji na **Shilingi 4,500,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**186.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Shirika la Posta Tanzania limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuboresha Mfumo wa Posta Kiganjani kuwa jukwaa jumuishi linalounganisha huduma zote za Posta Kidijitali;
(ii) Kutekeleza miradi **10** ya uendelezaji viwanja kupitia *Joint Venture* katika Maeneo ya Kimkakati;
(iii) Kuzindua na kuendesha Kituo cha Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TPC - Virtual Academy) kitakacholenga kuimarisha Uongozi, ubora wa huduma na utaalamu wa Huduma za Posta ndani ya Shirika;
(iv) Kusimamia uendeshaji wa vituo **32** vya Huduma Pamoja vitakavyoanzishwa kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali;
(v) Ununuzi wa magari **12** na pikipiki **20** za umeme kwa ajili ya usafirishaji wa vifurushi na mizigo;
(vi) Kuanzisha vituo vitano vya ukusanyaji mizigo katika maeneo ya kimkakati ikiwemo Stendi za Mabasi na Masoko makubwa Nchini; na
(vii) Kufanya kampeni nne kuhusu huduma zinazotolewa na Shirika la Posta ikiwemo kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Usafirishaji Kidijitali (SwifPack).

### 4.2.3.3 Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano – TCRA CCC

**187.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano linakadiria kukusanya **Shilingi 919,015,000** na kutumia **Shilingi 919,015,000** kwa ajili ya Mishahara na kugharamia utekelezaji wa shughuli za Baraza.

**188. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuwezesha mafunzo kwa Watumishi wawili wa Baraza;
(ii) Kuanzisha Kamati za Watumiaji katika Mikoa ya Shinyanga na Kaskazini Pemba;
(iii) Kujenga uwezo kwa Kamati za Watumiaji katika Mikoa **24** kuhusu masuala mbalimbali yanayojitokeza katika Sekta ya Mawasiliano;
(iv) Kuwezesha na kusimamia Kamati za Watumiaji katika Mikoa **24** kutekeleza Mpango Kazi wa Mwaka wa Fedha wa 2026/27;
(v) Kuandaa Mkakati wa Mawasiliano na Uhamasishaji wa Baraza wa Mwaka 2027/28 – 2031/32;
(vi) Kuandaa na kusambaza machapisho ya elimu kwa Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano yakiwemo ya wenye mahitaji maalumu (nukta nundu);
(vii) Kuboresha na kutumia Mifumo ya Kidijitali ya kuwahudumia Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (E-mrejesho na Mtumiaji App/Portal);
(viii) Kutoa elimu ya uhamasishaji na kupokea maoni ya Watumiaji kupitia Redio, Televisheni, Mitandao ya Kijamii, Maonesho na Matukio ya Kitaifa.
(ix) Kuendelea kufanya maboresho ya utendaji kazi wa Baraza kwa kukamilisha Kanuni za Uendeshaji wa Baraza
(x) Kuendelea kuwasilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kushauriana na Serikali, TCRA, watoa huduma na wadau wengine, na
(xi) Kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo (induction) Wajumbe wapya wa Baraza.

**4.2.3.4 Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL**

**189. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Shirika limepanga kukusanya **Shilingi 524,652,058,739.13** na kutumia Shilingi **482,801,024,748**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 314,582,769,607.43** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 168,218,255,140.59** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**190.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Shirika la Mawasiliano Tanzania limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuboresha huduma na kuongeza mauzo kutoka vyanzo vya ndani kufikia Shilingi Bilioni **411.7**;
(ii) Kujenga maunganisho **321,000** ya Miundombinu ya Huduma za Faiba Mlangoni;
(iii) Kuunganisha wateja **128,800** na Huduma ya Faiba Mlangoni;
(iv) Kuunganisha wateja **912,700** wa Huduma za Mawasiliano ya Simu;
(v) Kuunganisha maeneo **100** ya Umma na Huduma ya Wi-Fi;
(vi) Kuunganisha vituo **20** na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;
(vii) Kutoa mafunzo kwa Watumishi **340** wa Shirika ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma;
(viii) Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuunganisha Tanzania na Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo; na
(ix) Kufanya kampeni nne kuhusu huduma zinazotolewa na Shirika la Mawasiliano Tanzania.

### 4.2.3.5 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote – UCSAF

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Mfuko unatarajia kukusanya **Shilingi 93,976,905,177** na kutumia **Shilingi 93,976,905,177**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 59,702,774,787** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi 34,274,130,390** ni kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo.

**192.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukamilisha ujenzi wa Minara ya Mawasiliano kwenye Kata **567** zenye changamoto ya upatikanaji wa Mawasiliano ya Simu na Intaneti;
(ii) Kuboresha upatikanaji wa matangazo ya Redio ya Taifa - TBC katika Mikoa mitano yenye usikivu hafifu ambayo ni; Manyara, Mtwara, Mwanza, Ruvuma na Kilimanjaro;
(iii) Kuanzisha vituo **31** vya kutolea Huduma za Posta (Universal Postal Outlets);

(iv) Kutoa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha utoaji wa Huduma za Posta;
(v) Kuunganisha Huduma za Intaneti (Wi-Fi) kwenye maeneo **100** ya Umma Nchini;
(vi) Kuboresha vituo vya kubadilishana Intaneti (Internet Exchange Points - IXPs) kwenye vituo sita vilivyopo Zanzibar, Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Mbeya na Arusha;
(vii) Kupeleka Huduma za Faiba (Last-Mile Fiber Connectivity) kwenye Halmashauri **10**;
(viii) Kuanzisha Redio Jamii katika Wilaya tano ikiwemo;
(ix) Kuanzisha Maabara za TEHAMA kwenye Shule **250** za Umma;
(x) Kutoa vifaa vya TEHAMA kwenye Shule **10** za Umma zenye Wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
(xi) Kujenga miundombinu ya TEHAMA kwenye Vyuo **15** vya Mafunzo ya Ufundi (Vocational Training Centres);
(xii) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Walimu **700** wa Shule za Umma;
(xiii) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Wanafunzi **250** wa Kike;
(xiv) Kukarabati vituo **10** vya TEHAMA (Telecenters) vilivyopo Unguja na Pemba; na
(xv) Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Afya Mtandao (Telemedicine).

#### 4.2.3.6 Tume ya TEHAMA – ICTC

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Tume imepanga kukusanya **Shilingi 6,490,443,666.76** na kutumia **Shilingi 6,490,443,666.76.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,100,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na **Shilingi 4,390,443,667** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ikiwemo Mishahara na Matumizi Mengineyo.

**194.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Tume ya TEHAMA imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali 2024 – 2034 Nchini.
(ii) Kufanya tathmini ya mwenendo wa ukuaji wa Sekta ya TEHAMA Nchini;

(iii) Kusajili na kuendeleza Wataalamu **600** wa kada za TEHAMA Nchini;
(iv) Kusajili Kampuni Changa **100** za Ubunifu wa TEHAMA Nchini;
(v) Kuandaa Majukwaa mawili ya uwekezaji katika TEHAMA kwa ajili ya kuhamasisha uwekezaji katika TEHAMA;
(vi) Kuandaa vipaumbele vya Utafiti katika TEHAMA vya Mwaka 2026 - 2030;
(vii) Kuandaa matukio ya kuhamasisha na kukuza matumizi ya TEHAMA Nchini;
(viii) Kuwezesha mafunzo kwa Kampuni Changa **25** za TEHAMA Nchini;
(ix) Kujenga uwezo kwa Watumishi **20** wa Tume ya TEHAMA; na
(x) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na shughuli za Taasisi.

#### 4.2.3.7 Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi – PDPC

**195. *Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Tume imepanga kukusanya **Shilingi 8,747,506,000** na kutumia **Shilingi 8,747,506,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 6,497,506,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,250,000,000** kwa ajili ya Shughuli za Maendeleo.

**196. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kusajili Wakusanyaji na Wachakataji **30,000** wa Taarifa Binafsi;
(ii) Kuimarisha Mifumo ya usajili, ushughulikiaji wa Malalamiko na Rejista ya Wakusanyaji na Wachakataji wa Taarifa Binafsi;
(iii) Kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Wakusanyaji na Wachakataji **5,000** wa Taarifa Binafsi;
(iv) Kushughulikia malalamiko yanayohusu uvunjifu wa misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka kwa wahusika wa taarifa;
(v) Kufanya tafiti moja na kutoa machapisho mawili kuhusu masuala ya Teknolojia na Ulinzi wa Taarifa Binafsi;
(vi) Kununua magari matatu kwa ajili ya matumizi ya Tume;
(vii) Kuandaa Mwongozo mmoja wa Utafiti na Ubunifu kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi;

(viii) Kuwajengea uwezo Watumishi **36** wa Tume katika masuala ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi;
(ix) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022; na
(x) Kuanza ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume, Dodoma.

## SURA YA TANO

### 5.1 SHUKRANI

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa moyo wa dhati napenda kumshukuru tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuweka kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Hatua hii imewezesha Wizara kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, napenda kutumia nafasi hii tena kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano wao wanaoendelea kutoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu.

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho lakini sio kwa umuhimu, nitumie fursa hii tena kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. Switbert Zacharia Mkama (Mb.)**, Naibu Waziri kwa kuendelea kunisaidia katika kuiongoza Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, ninawashukuru kwa dhati Katibu Mkuu, **Ndugu Mohammed Khamis Abdulla** na Naibu Katibu Mkuu, **Ndugu Nicholaus Merinyo Mkapa** kwa kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo wa Wizara, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Viongozi wa Taasisi pamoja na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa. Ninawasihi waendelee kutekeleza majukumu yao kwa bidii, uadilifu na moyo wa kujituma wakitambua kuwa mchango wao ni nguzo muhimu katika kufanikisha malengo ya Wizara na Taifa kwa ujumla ya kufikia Uchumi wa Kidijitali wenye tija, jumuishi na endelevu kwa maendeleo ya Nchi yetu.

**199.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutumia fursa hii kuwatambua na kuwashukuru Washirika wa Maendeleo tunaoshirikiana nao katika utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo ambao ni: Benki ya Dunia (WB) kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa (IDA); Umoja wa Posta Duniani (UPU); Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU); Umoja wa Posta Afrika (PAPU); Jumuiya ya Mawasiliano ya Afrika (ATU); Jumuiya ya Mawasiliano ya Nchi za Afrika Mashariki (EACO); Jumuiya ya Wasimamizi wa Mawasiliano ya Kusini mwa Afrika (CRASA); Umoja wa Watoa Huduma za Posta Kusini mwa Afrika (SAPOA); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Shirika la Watoto Duniani (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA), Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Korea ya Kusini, Ujerumani, India, Estonia na Finland.

**200.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kuzishukuru Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ikiwemo: Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); Jumuiya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC); Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU) kwa ushirikiano wao katika masuala ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Aidha, Wizara ya Mawasiliano na Teknoloia ya Habari itaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inachangia kikamilifu katika kufikia Dira 2050.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ningependa kuwashukuru Watoa Huduma za Mawasiliano kutoka katika kampuni za mawasiliano ya simu ambazo ni Shirika la Mawasilinao Tanzania (TTCL), Airtel Tanzania, Vodacom Tanzania na Honora Tanzania, na Viettel kwa kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutatua changamoto za Mawasiliano Nchini kwa kufikisha Huduma za Mawasiliano kwenye maeneo husika.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutambua mchango wa Kampuni Changa pamoja na Wabunifu Nchini ambao wamekuwa chachu katika maendeleo ya Sekta ya TEHAMA Nchini; Taasisi za fedha za CRDB na NMB; Vyuo na Taasisi zinazohusika na Tafiti na programu mbalimbali za kuendeleza

TEHAMA; wabunifu wote wanaohusika na masuala ya Kidijitali kama vile Fintech, Akili Unde, Meditech, Kilimo, Biashara, Burudani na wadau wote muhimu kwa mchango wao katika kukuza bunifu Nchini. Vilevile, natambua mchango mkubwa unaotolewa na Kampuni, Watoa Huduma na Wadau wote wa Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ikiwemo Kampuni za Minara Tanzania, HTT na TOWERCO. Pia, natambua mchango mkubwa unaofanywa na wakandarasi katika ujenzi wa Miundombinu ya TEHAMA wakiwemo Kampuni ya Huawei, Telecom Associate, Softnet, pamoja na Raddy Fibre.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kuzishukuru Wizara na Taasisi za Umma ikiwemo Ofisi ya Rais – UTUMISHI, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu – SMZ, e-GA, eGAZ, ZICTIA, NIDA, RITA, NEMC, TANROADS, TARURA, REA, TANESCO, TFS, TCAA, TAA, COSTECH na wadau wote muhimu katika maendeleo ya Sekta**.**

## 5.2 MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KATIKA MWAKA WA FEDHA WA 2026/27

### 5.2.1 Makadirio ya Makusanyo ya Mapato

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiria kukusanya **Shilingi 160,369,240,000** ambazo zitatokana na mauzo ya Huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

### 5.2.2 Makadirio ya Matumizi

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 222,589,451,000** kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu na vipaumbele vya Wizara kwa mchanganuo ufuatao;

**5.2.3 Matumizi ya Kawaida**

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiria kutumia **Shilingi 13,146,172,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 5.9** ya Bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 6,371,830,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Shilingi 6,774,342,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**5.2.4 Matumizi ya Miradi ya Maendeleo**

**207.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha wa 2026/27, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakadiria kutumia **Shilingi 209,443,279,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 94.1** ya Bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 98,480,905,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 110,962,374,000** ni fedha za nje.

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo ni http://www.mawasiliano.go.tz.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wako. Sasa ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kwa niaba yake Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Abubakari Asenga. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso Mbunge, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukukufu taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inahusu utangulizi ambapo inahusisha misingi na muundo wa taarifa. Sehemu ya pili ni kuhusu uchambuzi na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2026/2027. Sehemu ya nne inahusu maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa Serikali na sehemu ya tano ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa pamoja kwa bajeti na maoni ya ushauri wa mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarehe 16 Mei, 2025 wakati Bunge lako Tukufu likipitisha Bajeti ya Wizara Fungu Na. 68 kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na mapendekezo katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji kwa bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati imepitia taarifa ya utekelezaji wa maoni,

ushauri na mapendekezo ya Kamati na kubaini kuwa, sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Kamati na kuna baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati ambao utekelezaji wake ni endelevu. Hata hivyo, Kamati inasisitiza Serikali kufanyia kazi ushauri uliotolewa katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

(i) Kamati ilishauri Serikali kuongeza jitihada za kupambana na uhalifu wa kimtandao, ikiwa ni pamoja na wizi wa kimtandao ili kuzuia jumbe fupi zinazotumwa bila idhini au matakwa ya mteja. Kamati imebaini bado tatizo hilo ni kubwa na kumekuwa na malalamiko mengi miongoni mwa wananchi kuhusu utapeli na wizi mitandaoni.

(ii) Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha za miradi ya maendeleo zinatolewa kama zilivyoidhinishwa kwa ajili ya kuhakikisha miradi inatekelezwa na kukamilika kwa wakati. Hata hivyo, Kamati imebaini ucheleweshaji wa fedha hizo, kwa kuwa hadi tarehe 26 Machi, 2026, Wizara ilikuwa imepokea 49.2% tu ya fedha hizo. Aidha, Kamati imefanya juhudi za kukumbusha malipo ya fedha za miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 89.6 toka Hazina kwa zaidi ya miezi miwili bila mafaniko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Serikali kuzingatia ushauri wa Kamati ya Bunge katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka 2025/2026 kuhusu ukusanyaji wa maduhuli.

(i) Kamati imebaini kwamba, Wizara hii ilihidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 120.3 ambapo hadi kufikia Februari, 2026 imekusanya shilingi bilioni 149.2 sawa na 124% ya lengo.

(ii) Upande wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii zilikadiriwa kukusanya shilingi bilioni 689.04 hadi kufikia Februari, 2026, taasisi hizo zilikusanya shilingi bilioni 516.3 sawa na 74.9% ya lengo.

(iii) Imebaini kuwa, kuna baadhi ya taasisi abazo hazikuwa na makusanyo ya kuridhisha hadi kufikia Februari, 2026 ikiwa ni pamoja na Tume *ya TEHAMA* 32.3% na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi asilimia nane nukta nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara na taasisi zilizofanya vizuri kwenye makusanyo na inaendelea kuishauri Serikali kufanya ufuatiliaji wa taasisi zenye makusanyo hafifu ili kuongeza maduhuli ya Serikali.

(iv) Uchambuzi kuhusu upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2026. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 291.53. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 14.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 277.05 ni kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2026 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 142.3 sawa na 48.8% ya lengo. Upatikanaji wa fedha kwa Wizara hii hauridhishi, kwani fedha iliyopokelewa ilikuwa ni chini ya wastani wa 66.7% ni mpangokazi wa utekelezaji wa bajeti. Kama Serikali inataka kuhakikisha Wizara hii inafanikiwa, inapaswa kutoa fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili Wizara itekeleze majukumu yake na vipaumbele vyake kwa ufanisi.

(v) Ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanya ziara ili kujionea utekelezaji wa miradi iliyopo chini ya Wizara, iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026. Ukaguzi ulifanyika kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (1). Miradi iliyokaguliwa ni pamoja na Mradi wa Mkongo wa Taifa, Kituo cha Taifa cha Kutunza Data *(NIDC)*, Ujenzi wa Minara 758 na Maabara ya Uidhinishaji wa Vifaa vya Mawasiliano ya Kielectoniki *(TAL)*. Taarifa zaidi kuhusu miradi hiyo inapatikana katika ukurasa wa 14 hadi 21 wa taarifa ya Kamati.

(vi) Masuala mahsusi yaliyobainika katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

a) Nafasi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* katika kulinda usalama wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba, 2025 zilizuka ghasia ambazo ziliondoa utulivu na kutishia amani na mshikamano wa Taifa letu. Hata hivyo, pamoja na vyombo vya Ulinzi na Usalama nchini, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* ilihakikisha inakuwa sehemu ya kurejesha hali ya utulivu, amani na mshikamano katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* ilichukua hatua ya haraka ya kuzima mtandao wa *internet* ili kuzuia usambazaji wa taarifa potofu zenye nia ya kuchochea ghasia nchini. Aidha, *TCRA* ilihakikisha kuwa vyombo vya habari nchini vinatoa taarifa ambazo hazileti hofu na kuzua taharuki kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ni ya kizalendo kwani inatambua kuwa jukumu la ulinzi na usalama wa Taifa letu siyo wa vyombo vya dola peke yake. Kamati inaipongeza Bodi, Menejimenti na Watumishi wote wa *TCRA* kwa kutambua wajibu wao katika kudumisha umoja, amani na mshikamano nchini yetu, hakika uzalendo wenu ni wa kupigiwa mfano katika Taifa letu.

b) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano wa kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeanza ujenzi wa Mkongo wa Taifa kuunganisha kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC)*. Ujenzi huo unaunganisha Mji wa Kigoma - Tanzania na Kalemie *(DRC)* kwa umbali wa Kilometa 183 kupitia Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utagharimu Dola za Marekani milioni 11.5 hadi kukamilika kwake. Serikali imekwishatoa shilingi bilioni 10.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa huku Dola za Marekani milioni 4.3 zikitolewa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa

mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/2027 ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huu kutaongeza nafasi na ushawishi wa Tanzania kwenye tasnia ya TEHAMA kikanda na kuchangia fedha za kigeni, kupitia mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa. Aidha, mradi huu utaongeza manufaa ya kiusalama na kibiashara kwa Taifa letu kutokana na nafasi yetu kijiografia.

c) Shirika la Posta Tanzania *(TPC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania ni moja ya taasisi chini ya Wizara hii, likiwa na jukumu la msingi la kutoa huduma za usafirishaji na usambazaji wa vipeto, vifurushi na mizigo ndani na nje ya nchi, kwa njia ya kawaida na njia ya haraka. Shirika linatekeleza majukumu yake chini ya Sheria Na. 19 ya Shirika la Posta Tanzania ya Mwaka 1993.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Shirika la Posta nchini linakabiliwa na changamoto kubwa ya madeni na upungufu wa mtaji, hali inayopunguza ufanisi katika kuhudumia wananchi. Shirika pia linakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya kutolea huduma, pamoja na maslahi yasiyoridhisha kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa iwapo Serikali itachukua hatua ya kugeuza deni la Shirika kuwa mtaji *(capitalization)*, Shirika litaanza kujiendesha kwa faida na kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, Shirika likiongezewa mtaji linaweza kuongeza mapato yake, kukarabati miundombinu yake na kuboresha maslahi ya watumishi wake.

d) Ulinzi wa Taarifa Binafsi

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ulimwengu wa uchumi wa kidijitali, taarifa ndiyo bidhaa inayouzwa na kununuliwa. Kwa hiyo, ulinzi wa taarifa binafsi kwa wananchi, taasisi na Serikali ni suala la kipaumbele katika ustawi wa nchi pamoja na ulinzi na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa, bado wananchi wengi wakiwemo watumishi wa umma na wale wa sekta binafsi, hawajapata elimu ya kutosha kuhusu utunzaji na matumizi sahihi katika taarifa nchini. Hali hii imesababisha upatikanaji holela wa taarifa za taasisi za umma na binafsi mitandaoni bila kuwa na udhibiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya jambo hili zimeanza kuonekana, siku za hivi karibuni picha zinazodhalilisha watu zinatumwa katika mitandao na kushabikiwa na baadhi ya watu. Madhara ya picha hizi ni pamoja na msongo wa mawazo unaotokana na unyanyasaji wa kijinsia na kisaikolojia, hali inayoweza kusababisha muathirika wa picha hizi kuchukua hatua ya kujidhuru au kulipiza kisasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa taasisi za umma, kuna baadhi ya taarifa za siri za Serikali zimekutwa kwenye mitandao ya kijamii, hali inayoondoa utulivu katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, kumekuwa na taarifa potofu kuhusu baadhi ya viongozi wa Serikali, zikiwa na lengo la kuzusha hofu na kuleta taharuki miongoni mwa jamii. Hali hii isipodhibitiwa haraka inaweza kuleta madhara zaidi kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

e) Nafasi za vijana katika uchumi wa kidijitali

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatekeleza Mkakati wa Miaka Kumi wa Uchumi wa Kidijitali 2024/2034. Pamoja na wadau wengine, mkakati huo unalenga kutoa nafasi kwa vijana nchini, kunufaika na fursa za kiuchumi kupitia majukwaa ya kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha vijana wananufaika na fusra za mkakati huo, Wizara imeanza ujenzi wa vituo vya kuendeleza ubunifu katika TEHAMA *(ICT Park)* kwenye Mikoa Nane nchini. Vilevile, Wizara imekamilisha Sera ya Taifa ya Kampuni Changa ya mwaka 2026 *(National Start-up Policy, 2026)* kwa ajili ya maoni ya wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua kuwa Serikali imepeleka shilingi 5,000,000,000 kwa ajili ya mikopo kwa vijana katika Wizara hii. Kamati inaona kuwa fedha hizi hazitoshi kwa

sababu kuna fursa kubwa ya ubunifu, vipaji, ujasiriamali na kampuni changa ipo katika majukwaa ya kidijitali hasa mitandao ya kijamii. Aidha, vijana ndiyo nguzo na wahusika wakuu katika maendeleo ya *TEHAMA* na utekelezaji wa mkakati wa uchumi wa kidijitali.

(vii) Makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara Fungu Na. 68 imepanga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 160.37 sawa na ongezeko la 33.23% ukilinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara zinakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 921.12 sawa na ongezeko la 33.7% ukilinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Ni maoni ya Kamati kuwa lengo hili litafikiwa kwa sababu ya mwenendo mzuri wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara na Taasisi zake umeanza kuonekana.

(viii) Makadirio ya Matumizi ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 222.59. Bajeti hii imeshuka kwa 23.65% ukilinganisha na Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanya uchambuzi wa tathmini hii ya kina kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati imebaini kushuka kwa bajeti kumechangiwa na mambo mambo matatu kama ifuatavyo:-

(i) Uamuzi Madhubuti wa Serikali katika kudhibiti na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ili kuhakikisha fedha zinaelekezwa kwenye shughuli zenye tija katika kuhudumia ustawi wa wananchi.

(ii) Kukamilika kwa baadhi ya miradi ikiwemo ujenzi wa minara 758 katika kata 713 kwenye maeneo mbalimbali nchini.

(iii) Kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza Serikali kwa hatua ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, pamoja na kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika kugharamia miradi ya maendeleo.

(ix) Maoni na ushauri.

a) Maoni ya jumla.

(i) Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuzisimamia taasisi zilizo chini ya Wizara hii katika ukusanyaji wa mapato ili ziweze kujiendesha na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija bila kutegemea Mfuko Mkuu wa Serikali.

(ii) Serikali iendelee kusimamia na kuweka mazingira ya kuwezesha taasisi za umma na binafsi kutoa huduma bora za mawasiliano na matumizi ya TEHAMA nchini.

(iii) Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge na kusimamia kikamilifu miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara hii ili iweze kukamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa.

(iv) Serikali ihakikishe inakamilisha kwa haraka Muswada wa Sheria ya TEHAMA ya Mwaka, 2026 ambayo utachochea ubunifu, ajira na usalama katika matumizi ya TEHAMA nchini.

Maoni Mahsusi.

(i) Kamati inashauri kuwa, Serikali ichukue hatua ya kuitambua Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* kama chombo cha kimkakati katika ulinzi na usalama wa Taifa, na kuhakikisha kuwa taarifa zilizowasilishwa kwa mamlaka hii kama viashiria vya uvunjifu wa amani katika vyombo vya dola zinafanyiwa kazi kwa uzito unaostahili.

(ii) Ipange na kutekeleza mkakati wa kuzuia na kupambana na uhalifu wa kimtandao ikiwa ni pamoja na wizi wa mitandaoni. Nguvu zaidi zielekezwe katika mikoa yenye matukio mengi.

(iii) Ifanye tathmini kuhusu matumizi ya vifurushi vya data na muda wa maongezi na kuja na utaratibu utakaomwezesha mteja kutumia kifurushi chake mpaka kitakapoishia, badala ya sasa ambapo anatumia hadi muda wa kifurushi utakapoishia.

b) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa Serikali iongeze kasi katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kati ya Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, hali itakayoboresha mazingira ya kibiashara baina ya nchi zetu na kuongeza fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma za Mkongo. Ihakikishe kuwa Wilaya zote nchini zinaunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, pamoja na kuunganisha taasisi za umma na binafsi kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na utoaji huduma nchini.

c) Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuwa: -

(i) Itoe shilingi 100,000,000,000 kwa ajili ununuzi wa vifaa vipya pamoja na upanuzi wa eneo la utoaji wa huduma ya upangishaji wa nafasi yaani *(colocation)* hatua itakayoongeza ufanisi katika matumizi ya kituo.

(ii) Ianze mara moja ujenzi wa vituo vya kuhifadhi taarifa jijini Dodoma na Zanzibar ili kuhakikisha kuna utunzaji endelevu wa taarifa zinazozalishwa na kutumiwa nchini.

d) Shirika la Posta Tanzania (TPC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuwa:-

(i) Ifanye tathmini na kugeuza madeni ya Shirika la Posta kuwa mtaji *(capitalization)* ili liweze kujiendesha kwa faida na kutoa gawio la Serikali,

(ii) Iboreshe miundombinu ya kufanyia kazi suala la maslahi ya watumishi wa Shirika la Posta nchini ili kuongeza motisha na kuleta ufanisi katika utendaji wa Shirika hilo.

e) Ulinzi wa Taarifa binafsi

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuwa:-

(i) Iandae mkakati wa kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya mitandao na madhara ya kuweka taarifa binafsi katika mitandao ya kijamii, ili kuhakikisha jamii inazingatia faragha na kupunguza uhalifu na unyanyasaji wa kimtandao nchini.

(ii) Itoe elimu na mwongozo mahususi kwa watumishi wa umma na sekta binafsi kuhusu umuhimu wa kutunza taarifa binafsi za wateja, pamoja na taasisi wanazozifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria, watumishi watakaobainika kushindwa kutekeleza masharti ya mwongozo huo.

f) Vijana na Uchumi wa Kidijitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuwa:-

(i) Itoe kipaumbele kwa maoni ya vijana katika Sera ya Kampuni Changa za mwaka 2026, pamoja na kuonesha fursa zinazopatikana katika utekelezaji wa mkakati wa uchumi wa kidijitali kwa makundi mbalimbali ya vijana nchini.

(ii) Ikamilishe ujenzi wa kituo kikuu na vituo vidogo vya kuendeleza ubunifu katika *TEHAMA (ICT Park)* ili kuwapa vijana nafasi kukuza ubunifu na ujuzi wa matumizi ya TEHAMA katika sekta mtambuka za kijamii na kiuchumi nchini.

(iii) Ibainishe na kuvitambua vituo binafsi vinavyokuza ubunifu na ujuzi katika *TEHAMA* na kuviwezesha katika mtaji na

malezi ili kuhakikisha matumizi sahihi ya ujuzi na ubunifu kiuchumi na kuzingatia maadili ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)*. Kamati inashauri kuwa, Serikali: -

(a) Ihakikishe kunakuwa na watoa huduma zaidi ya mmoja katika minara 758 iliyojengwa nchini kwa ajili ya kuwapa wananchi fursa ya kuchagua huduma na kuimarisha ushindani katika sekta ya mawasiliano;

(b) Ifanye malipo ya shilingi 31,642,735,500 kwa watoa huduma waliojenga minara 758 kwa ajili kuepusha riba inayoweza kuchangiwa na kuchelewesha malipo hayo;

(c) Iboreshe usikivu wa Redio Jamii na Redio ya Taifa katika maeneo ya mipakani kwa ajili ya kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kuwa na taarifa sahihi kuhusu Taifa letu; na

(d) Ifanye tathmini na kuongeza nguvu kwenye minara kutoka 2G kwenda *3G/4G/5G* hasa maeneo ya vijijini ili kutoa fursa ya kupata taarifa kupitia huduma za mtandao wa *internet*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa namna ya kipekee ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu, na kwa maelekezo yake ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna anavyomsaidia kutekeleza majukumu yake kama Spika wa Bunge hili, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia

ya Habari pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Ninaomba niwatambue Wajumbe hao, wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso; na kutokana na muda sitasoma majina yao, hivyo ninaomba yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mheshimiwa Angela Jasmin Mbelwa Kairuki, kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chake cha utekelezaji wa majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Switbert Zacharia Mkama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawashukuru watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bwana Mohammed Khamis Abdullah. Kamati inatambua na kuthamini mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya sekta ya mawasiliano na TEHAMA katika ujenzi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bwana Baraka Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Kamati kuhusu hoja. Baada ya maelezo hayo, ninaomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi (Fungu 68) ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**30 APRILI, 2026**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI (FUNGU 068) KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 121 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 [Kanuni za Bunge] naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **(Fungu 068)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, bila kuathiri masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

a) Sehemu ya kwanza ni utangulizi kuhusu muundo wa taarifa na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

b) Sehemu ya pili ni uchambuzi wa utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kutathimini uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati, makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

c) Sehemu ya tatu ni uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027;

d) Sehemu ya nne ni majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na Sehemu ya tano ni hitimisho.

1.2 Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge. Katika kushughulikia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **(Fungu 068)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea dondoo (extracts) na randama ya Wizara kwa ajili ya Uchambuzi wa Bajeti [Kanuni ya 118 (1)];

b) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026 [Kanuni ya 120 (1)]; na

c) Kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na kufanya ulinganisho wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 [Kanuni ya 120 (2)].

**SEHEMU YA PILI**

**2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

**2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 16 Mei, 2025, Bunge lilipokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **(Fungu 068)** kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika kikao hicho, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliwasilisha maoni yake kuhusu Bajeti ya Wizara hiyo katika maeneo tisa (09) ili kutimiza masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri

uliotolewa na Kamati. Vilevile, Serikali imeendelea kuchukua hatua zaidi kwa kuwa maoni mengine utekelezaji wake ni endelevu. Hata hivyo, baadhi ya maoni na ushauri uliotolewa haukufanyiwa kazi kwa ukamilifu, na kwa sababu hiyo Kamati inapenda kuweka msisitizo kuhusu umuhimu wa utekelezaji wake kama ifuatavyo: -

(a) Kamati ilishauri Serikali kuongeza jitihada za kupambana na uhalifu wa kimtandao ikiwa ni pamoja na wizi wa mitandaoni na kuzuia jumbe fupi zinazotumwa bila idhini au matakwa ya mteja. Pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali kupambana na kudhibiti uhalifu na wizi mitandaoni, Kamati imebaini bado tatizo hilo ni kubwa kwa sababu kumekuwa na malalamiko mengi miongoni mwa wananchi kuhusu utepeli na wizi mitandaoni; na

(b) Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha za miradi ya maendeleo zinatolewa kama zilivyoidhinishwa kwa ajili ya kuhakikisha miradi inatekelezwa na kukamilika kwa wakati. Hata hivyo, Kamati imebaini ucheleweshaji wa fedha hizo, kwa kuwa hadi tarehe 26 Machi, 2026, Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 49.22** tu ya fedha hizo. Aidha, Wizara imefanya juhudi za kukumbushia malipo ya fedha za Miradi ya Maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni 89.6** toka hazina kwa zaidi ya miezi miwili bila mafaniko.

### 2.2 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 120,369,242,950/=** ambapo hadi kufikia Februari, 2026 makusanyo yalikuwa yamefikia jumla ya **Shilingi 149,236,990,425.18,** sawa na **asilimia 124** ya lengo. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara zilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 689,038,108,270/=** ambapo hadi kufikia Februari, 2026, taasisi hizo zilifanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 516,290,129,193.48** sawa na **asilimia 74.90** ya lengo lililokusudiwa. Taswira ya makusanyo ya mapato kwa Wizara na taasisi zake yameanishwa katika **Kielelezo Na. 1**.

**Kielelezo Na. 1: Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Februari, 2026**

| Wizara/Taasisi | Makadirio ya Makusanyo 2025/2026 (Shilingi) | Makusanyo hadi Februari, 2026 (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|
| WMTH (Fungu 068) | 120,369,242,950.00 | 149,236,990,425.18 | 124.00 |
| TCRA | 245,989,519,796.00 | 262,541,403,514.40 | 106.70 |
| TCRA – CCC | 710,000,000.00 | 606,223,832.00 | 85.40 |
| TTCL | 305,092,154,592.00 | 156,652,028,275.00 | 51.30 |
| TPC | 43,653,957,000.00 | 31,245,061,464.00 | 71.60 |
| UCSAF | 65,696,337,542.00 | 61,186,243,405.93 | 93.10 |
| ICTC | 6,850,114,300.00 | 2,214,348,534.15 | 32.30 |
| PDPC | 21,046,025,040.00 | 1,844,820,168.00 | 8.80 |
| **JUMLA** | **809,407,351,220.00** | **665,5271,19618.66** | **82.22** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Wizara na taasisi zake kwa namna ilivyotekeleza jukumu la ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi mkubwa. Hata hivyo, katika uchambuzi wake Kamati imebaini kwamba, baadhi ya taasisi chini ya Wizara zimekuwa na mwenendo usioridhisha katika ukusanyaji wa mapato.

**Mheshimiwa Spika,** taasisi za Wizara ambazo zimekusanya mapato kwa kiwango cha chini ni Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na Tume ya TEHAMA (ICTC). Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imekusanya kiasi cha **Shilingi 1,844,820,168.00** sawa **asilimia 8.80** tu ya lengo huku Tume ya TEHAMA ikikusanya **Shilingi 2,214,348,534.15** ambayo ni **asilimia 32.30** tu ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi na tathmini ya kina, Kamati imebaini kuwa taasisi hizi zilipanga malengo makubwa (overambitious) bila kuzingatia uhalisia wa uwezo wa kitaasisi katika kukusanya mapato. Vilevile, Kamati imebaini kuwa taasisi

hizi ni changa na hazina teknolojia na rasilimali watu wa kutosha wa kuwezesha kufikia vyanzo vyao vya mapato vilivyoanishwa.

### 2.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Matumizi hadi Februari, 2026

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari **(Fungu 068)** iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 291,533,139,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi Februari, 2026, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 142,297,189,687.73** sawa na **asilimia 48.80** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kamati haikuridhishwa na upatikanaji wa fedha kwani kiasi hicho ni pungufu ukilinganisha na mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti ulioripotiwa ambao ni **asilimia 66.67** kama ilivyoainishwa katika **Kielelezo Na. 2.**

**Kielelezo Na. 2: Mwenendo wa Mapokezi ya Fedha za Matumizi toka Hazina hadi Februari, 2026**

| Bajeti (Matumizi) | | Kilichoidhinishwa 2025/2026 (Shilingi) | Kilichopokelewa 2026 (Shilingi) hadi Februari, | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Kawaida | **Mishahara** | 6,958,609,000.00 | 2,528,229,184.42 | 36.33 |
| | **OC** | 7,527,047,000.00 | 3,390,702,520.82 | 45.05 |
| | **Jumla (A)** | **14,485,656,000.00** | **5,918,931,705.24** | **40.86** |
| | | | | |
| Maendeleo | **Ndani** | 98,480,905,000.00 | 51,896,679,660.04 | 52.70 |
| | **Nje** | 178,566,578,000.00 | 84,124,788,444.85 | 47.11 |
| | **Jumla (B)** | **277,047,483,000.00** | **136,378,257,982.49** | **49.22** |
| **JUMLA KUU (A+B)** | | **291,533,139,000.00** | **142,297,189,687.73** | **48.80** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina katika mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi hadi Februari, 2026, kama ifuatavyo:-

(i) Fedha za Mishahara (P.E) zimepokelewa kwa **asilimia 36.33** ikilinganishwa na **asilimia 66.67** ya mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti. Kamati imebaini kuwa Wizara ilipanga kupokea watumishi wa kuhamia na kuajiri watumishi wapya kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa TEHAMA kwenye Wizara na Taasisi zake. Hata hivyo, hadi kufikia Februari, 2026, Wizara haikuwa imepokea watumishi hao;

(ii) Fedha za Matumizi Mengineyo (OC) zilikuwa zimepokelewa kwa **asilimia 45.05** ikilinganishwa na **asilimia 66.67** ya mpango kazi wa utekelezaji wa bajeti. Fedha hizi ndio hutumika katika kuendesha shughuli za ofisi kama vile ununuzi wa vifaa, malipo ya watumishi katika usimamizi wa miradi uwandani, malipo ya kazi zinazofanyika muda wa ziada pamoja na ununuzi wa mafuta na vipuri vya magari. Kwa hiyo mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha hizi unaweza kuathiri ufanisi katika utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya Wizara; na

(iii) Katika **asilimia 49.22** ya bajeti iliyopokelewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha za ndani ni **asilimia 52.70**, huku fedha za nje zikiwa ni **asilimia 47.11** ya bajeti iliyoidhinishwa. Hatua hii inaonesha kuwa upatikanaji wa fedha za maendeleo sio wa kuridhisha hali ambayo imechangia katika kuzorota kwa kasi ya baadhi ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo usioridhisha wa upokeaji wa fedha kutoka hazina kwenye utekelezaji wa shughuli za Wizara unaweza kuwa kikwazo kwa Wizara na taasisi zake katika kukuza sekta ya TEHAMA na Uchumi wa Kidijitali nchini. Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zake.

### 2.4 Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo
### 2.4.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2025/2026. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kutathmini hali ya mapokezi ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi katika Mkoa wa Dar es Salaam kati ya tarehe 17 na 18 Machi, 2026.

### 2.4.2 Miradi Iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

**(a) Mradi Na. 4283 – Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (NICTBB)**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu unasimamiwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Lengo la mradi ni kuwezesha, kuimarisha na kuunganisha mawasiliano katika Mikoa, Wilaya na vituo vya mpakani mwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026, mradi huu ulitengewa **Shilingi 73,050,000,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wake. Hadi tarehe 17 Machi, 2026, ambapo Kamati ilitembelea na kufanya ukaguzi wa mradi huo, **Shilingi 32,619,102,051.93** sawa na **asilimia 44.7** pekee ndio zilikuwa zimepokelewa toka hazina.

**Mheshimiwa Spika**, kupitia fedha hizo, Shirika limefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuunganisha baadhi ya Taasisi za Haki Jinai na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo Vituo vya Polisi **49**, Ofisi za Taifa za Mashtaka **8** na Ofisi za Magereza **30** zimeunganishwa;

(ii) Kusimamia maunganisho **105,000** kati ya **279,795** sawa na **asilimia 37.5** ya lengo lililokusudiwa kwa ajili ya kufikisha miundombinu ya Faiba Mlangoni;

(iii) Kukamilisha ujenzi wa Kilometa **801** za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(iv) Kufanya ukaguzi wa njia **12** ambazo ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano umekamilika ili kuhakiki ubora wa kazi iliyofanyika; na

(v) Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Ofisi 47 za TARURA.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa ajili ya mradi huu kwani Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ndio njia kuu ya mawasiliano katika kukuza uchumi wa kidijitali na kuhakikisha usalama wa nchi. Aidha, Serikali inanufaika na ukusanyaji wa mapato kwa uuzaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**(b) Mradi wa Upanuzi wa Eneo la Huduma ya Upangishaji wa Nafasi (Colocation) katika Kituo cha Taifa cha Kutunza Data (NIDC)**

**Mheshimiwa Spika**, kituo hiki ni sehemu ya Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kilianzishwa mwaka 2015. Kituo hiki kinatoa huduma za upangishaji wa nafasi (colocation), uhifadhi wa taarifa (Storage) na huduma ya uwekaji wa tovuti mitandaoni (Web Hosting).

**Mheshimiwa Spika,** Kituo kinatoa huduma kwa wateja **211** ikiwa ni pamoja na taasisi za umma na binafsi nchini. Ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wateja, kituo hiki kinatakiwa kufanyiwa ukarabati na ununuzi wa vifaa vipya.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Kituo kimetengewa jumla ya **Shilingi Biloni 5.13** kwa ajili kutekeleza mradi wa upanuzi wa eneo la utoaji wa huduma ya upangishaji

wa nafasi (colocation)**.** Mradi huo upo katika hatua ya upembuzi yakinifu na hadi Kamati inatembelea ukaguzi wake, Kituo kilikuwa hakijapokea fedha yoyote kwa ajili ya mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati, Kituo hicho kinahitaji **Shilingi Bilioni 70**. Vilevile, Kamati ilibaini kuwa pamoja na uwezeshaji unaotolewa na Wizara mara kwa mara, Kituo kinakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya Mawasiliano na Vifaa ambayo inaweza kutatuliwa kama Kituo kitapata **Shilingi Bilioni 30**.

**(c) Mradi Na. 4280 – Ujenzi wa Minara 758**

**Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa minara hii umefanyika katika kata **713** nchini na umetekelezwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali. Lengo la mradi huu ilikuwa ni kuhakikisha Watanzania Milioni 8.5 wanafikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu umegharamiwa na Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia kwa jumla ya **Shilingi 125,958,353,000/=** na ulianza kutekelezwa tarehe 13 Mei, 2023. Hadi Februari, 2026 Watoa Huduma wamelipwa jumla ya **Shilingi 94,315,617,500/=** sawa na **asilimia 74.6** ya gharama za mradi ambapo minara yote **758** imekamilika kujengwa na inatoa huduma za mawasiliano kwa wananchi. Aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** alifanya uzinduzi wa minara hii tarehe 10 Aprili, 2026 Jijini Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huo umetekelezwa katika mikoa yote 26, Wilaya 128, kata 713 na vijiji 1400 nchini. Ili kujiridhisha kama utekelezaji wa mradi huu umezingatia thamani ya fedha na ubora, tarehe 18 Machi, 2026, Kamati ilitembelea na kukagua Ujenzi wa mnara wa mawasiliano katika kata ya Kibada, Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar Es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa mnara huo umefanywa na Kampuni ya Vodacom kama mtoa huduma na unahudumia wananchi 28,188 katika vijiji vya Dawasco na Fullshangwe. Ujenzi wa mnara

huo umekamilika na umegharimu jumla ya **Shilingi 89,715,000/=** ukiwa na teknolojia ya 2G/3G/4G.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na ubora wa mradi ikiwa ni pamoja na ubora wa mawasiliano wanayoyapata wananchi husika. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto ya wananchi kukosa nafasi ya kuchagua huduma kwani wanalazimika kutumia huduma ya mtoa huduma aliyepewa kujenga mnara katika eneo husika. Aidha, watoa huduma waliotekeleza mradi wanadai **Shilingi 31,642,735,500/=** hali ya kuwa wamemaliza ujenzi wa minara kwa mujibu wa mikataba yao.

**(d) Mradi wa Maabara ya Uidhinishaji wa Vifaa vya Mawasiliano ya Kielectroniki (TAL)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetekelezwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kuwa vifaa vya mawasiliano vya kieletroniki vinakidhi viwango vya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetekelezwa kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 7.527** ambapo **Shilingi Bilioni 1.496** ni kwa ajili ya usanifu na ujenzi wa jengo la Maabara ya Uidhinishaji wa Vifaa vya Mawasiliano, na **Shilingi Bilioni 6.031** ni gharama ya ununuzi wa mitambo na usimikaji. Vifaa vinavyopimwa ni pamoja na simu za mkononi, vishikwambi na kompyuta mpakato katika teknolojia za 2G/3G/4G/5G na kuendelea.

**Mheshimiwa Spika**, hadi tarehe 18 Machi, 2026, wakati Kamati inatembelea na kuukagua, mradi huu ulikuwa umekamilika na tayari ulikuwa unafanya kazi. Maabara hii kwa sasa inapima mawimbi ya radio (*Radio Frequency*) na kiwango cha mionzi (*Specific Absorption Rate*). Katika kupima Mawimbi ya Radio, maabara inakagua iwapo kifaa husika kinaweza kutumia masafa ya mawasiliano kwa mujibu wa viwango vya nchi na Kimataifa. Aidha, katika upimaji wa mionzi, maabara inapima athari za mionzi inayotolewa na kifaa husika kama imekidhi viwango vya kutumika nchini.

**Mheshimiwa Spika,** hadi mwezi Februari, 2026, maabara hiyo imefanikiwa kupima sampuli za vifaa **272** kwa modeli mpya zilizowasilishwa na watengenezaji. Katika vifaa hivyo, sampuli **6** hazikukidhi vigezo vya kutumika hapa nchini. Kamati inaipongeza Serikali kwa maabara hii ambayo inahakikisha vifaa vya kieletroniki vinavyotumika nchini vimezingatia viwango vya ubora wa Kitaifa na Kimataifa.

### 2.5 Masuala Mahsusi Yaliyobainika Katika Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

#### a) Nafasi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika Kulinda Usalama wa Nchi

**Mheshimiwa Spika**, katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba, 2025 zilizuka ghasia ambazo ziliondoa utulivu na kutishia amani na mshikamano wa Taifa letu. Hata hivyo, pamoja na vyombo vya Ulinzi na Usalama nchini, Mamalaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilihakikisha inakuwa sehemu ya kurejesha hali ya utulivu, amani na mshikamano katika Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** TCRA ilichukua hatua ya haraka ya kuzima mtandao wa internet ili kuzuia usambazaji wa taarifa potofu zenye nia ya kuchochea ghasia nchini. Aidha, TCRA ilihakikisha kuwa vyombo vya habari nchini vinatoa taarifa ambazo hazileti hofu na kuzua taharuki kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** hatua hii ni ya kizalendo kwani inatambua kuwa jukumu la ulinzi na usalama wa Taifa letu sio wa vyombo vya dola pekee. Kamati inaipongeza Bodi, Menejimenti na Watumishi wote wa TCRA kwa kutambua wajibu wao katika kudumisha umoja, amani na mshikamano nchini. Hakika uzalendo wenu ni wa kupigiwa mfano katika Taifa letu.

#### b) Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imeanza ujenzi wa Mkongo wa Taifa kuunganisha kati ya Tanzania

na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC). Ujenzi huo unaunganisha mji wa Kigoma (Tanzania) na Kalemie (DRC) kwa umbali wa Kilometa 183 kupitia Ziwa Tanganyika.

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu utagharimu **Dola za Marekani 11,568,429/=** hadi kukamilika kwake. Serikali imekwishatoa **Shilingi Bilioni 10.4** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa huku **Dola za Marekani Milioni 4.3** zikitolewa kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa mradi huu kutaongeza nafasi na ushawishi wa Tanzania kwenye tasnia ya TEHAMA kikanda na kuchangia fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa. Aidha, mradi huu utaongeza manufaa ya kiusalama na kibiashara kwa Taifa letu kutokana na nafasi yetu kijiografia.

### c) Shirika la Posta Tanzania (TPC)

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Posta Tanzania ni moja ya taasisi chini ya Wizara ikiwa na jukumu la msingi la kutoa huduma za usafirishaji na usambazaji wa vipeto, vifurushi na mizigo ndani na nje ya nchi kwa njia ya kawaida na ya haraka. Shirika hili linatekeleza majukumu yake chini ya Sheria Na. 19 ya Shirika la Posta Tanzania ya Mwaka 1993.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, Shirika la Posta nchini linakabiliwa na changamoto kubwa ya madeni na upungufu wa mtaji hali inayopunguza ufanisi katika kuhudumia wananchi. Shirika pia linakabiliwa na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya kutolea huduma pamoja na maslahi yasiyoridhisha kwa watumishi wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa iwapo Serikali itachukua hatua ya kugeuza deni la Shirika kuwa mtaji (Capitalization), Shirika hili litaanza kujiendesha kwa faida na kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake. Vilevile, Shirika hili likiongezewa mtaji linaweza kuongeza mapato yake pamoja, kukarabati miundombinu yake na kuboresha maslahi ya watumishi wake.

### d) Ulinzi wa Taarifa Binafsi

**Mheshimiwa Spika**, katika ulimwengu wa uchumi wa kidijitali taarifa ndio bidhaa inayouzwa na kununuliwa. Kwa hiyo, ulinzi wa taarifa binafsi kwa wananchi, taasisi na Serikali ni suala la kipaumbele katika ustawi wa nchi pamoja na ulinzi na usalama wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa, bado wananchi wengi wakiwemo watumishi wa umma na wale wa sekta binafsi hawajapata elimu ya kutosha kuhusu utunzaji na matumizi sahihi ya taarifa nchini. Hali hii imesababisha upatikanaji holela wa taarifa za taasisi za umma na binafsi mitandaoni bila kuwa na udhibiti wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika,** athari ya jambo hili imeanza kuonekana, kwa kuwa siku za hivi karibuni picha zinazodhalilisha watu zinatumwa katika mitandao na kushabikiwa na baadhi ya wananchi. Madhara ya picha hizi ni pamoja na msongo wa mawazo unaotokana na unyanyasaji wa kijinsia na kisaikolojia hali inayoweza kusababisha muathirika wa picha husika kuchukua hatua ya kujidhuru au kulipa kisasi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa taasisi za umma, kuna baadhi ya taarifa na siri za Serikali zimekutwa kwenye mitandao ya kijamii hali inayoondoa utulivu katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, kumekuwa na taarifa potofu kuhusu baadhi ya viongozi wa Serikali zikiwa na lengo la kuzusha hofu na kuleta taharuki miongoni mwa jamii. Hali hii isipodhibitiwa haraka inaweza kuleta madhara zaidi kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

### e) Nafasi ya Vijana Katika Uchumi wa Kidijitali

**Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza Mkakati wa miaka kumi wa Uchumi wa Kidijitali 2024-2034. Pamoja na wadau wengine, mkakati huo unalenga kutoa nafasi kwa vijana nchini kunufaika na fursa za kiuchumi kupitia majukwaa ya kidijitali.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuhakikisha vijana wananufaika na fusra za mkakati huo, Wizara imeanza Ujenzi wa Vituo vya Kuendeleza

Ubunifu katika TEHAMA (ICT Park) kwenye Mikoa Nane (08) nchini. Vilevile, Wizara imekamilisha Sera ya Taifa ya Kampuni Changa ya Mwaka 2026 (*National Startup Policy, 2026*) kwa ajili ya maoni ya wadau.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa Serikali imepeleka **Shilingi Bilioni 5** kwa ajili ya mikopo kwa vijana katika Wizara hii. Kamati ina maoni kuwa fedha hizi hazitoshi kwani, kwa sasa fursa kubwa ya ubunifu, vipaji, ujasiriamali na kampuni changa ipo katika majukwaa ya kidijitali hasa mitandao ya kijamii. Aidha, vijana ndio nguzo na wahusika wakuu katika maendeleo ya TEHAMA na utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

### 3.1 Mpango na Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (**Fungu 068**) itatekeleza vipaumbe na majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi 2025-2030, Mpango wa Nne wa Mendeleo ya Taifa (FYDP IV) wa Mwaka 2026l2027-2030/2031 na Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Mwaka 2024-2034.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti inayoombwa na Wizara ina lengo la kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya Wizara kama ifuatavyo: -

a) Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa Miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari;
b) Kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Posta kote Nchini;
c) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Biashara Mtandao Nchini;
d) Kuimairisha miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa Uchumi wa Kidijitali;

e) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuchochea ubunifu na kuimarisha ustawi wa Kampuni Changa (Startups);
f) Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Anga ya Mtandao; na
g) Kuimarisha utekelezaji wa Programu ya Anga za Juu.

### 3.2 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 160,369,240,000/=** sawa na ongezeko la **asilimia 33.23** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Aidha, taasisi zilizo chini ya Wizara zinakadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 921,119,791,807.89** sawa na ongezeko la **asilimia 33.70** ukilinganisha na mwaka wa fedha 2025/2026. Ni maoni ya Kamati kuwa lengo hilo la mapato litafikiwa kwa sababu ya mwenendo mzuri wa makusanyo ya maduhuli kwa Wizara na taasisi zake.

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Makadirio ya Matumizi kwa Bajeti ya Mwaka 2025/2026 na 2026/2027**

| Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 068) | | Bajeti 2025/2026 (Shilingi) | Bajeti 2026/2027 (Shilingi) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Kawaida | Mishahara | 6,958,609,000.00 | 6,371,830,000.00 | -8.43 |
| | OC | 7,527,047,000.00 | 6,774,342,000.00 | -10.00 |
| | **Jumla (A)** | **14,485,656,000.00** | **13,146,172,000.00** | **-9.25** |
| | | | | |
| Maendeleo | Ndani | 98,480,905,000.00 | 98,480,905,000.00 | 0.00 |
| | Nje | 178,566,578,000.00 | 110,962,374,000.00 | -37.86 |
| | **Jumla (B)** | **277,047,483,000.00** | **209,443,279,000.00** | **-24.40** |
| **JUMLA KUU (A+B)** | | **291,533,139,000.00** | **222,589,451,000.00** | **-23.65** |

### 3.3 Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara hii inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 222,589,451,000/=.** Bajeti

hii imeshuka kwa **asilimia 23.65** ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026. **Kielelezo Na. 3** kinaonesha ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** katika kufanya uchambuzi na tathmini ya kina kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati ilipata matokeo yafuatayo:-

(i) Fedha za Matumizi ya Kawaida zimepungua kwa **asilimia 9.25** ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha. Hatua hii imetokana na uamuzi madhubuti wa Serikali katika kudhibiti na kupunguza matumizi yasiyo yalazima ili kuhakikisha fedha zinaelekea kwenye shughuli zenye tija katika huduma na ustawi wa wananchi;

(ii) Fedha za Miradi ya Maendeleo zimepungua kwa **asilimia 24.40** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2025/2026. Hali hii imetokana na kukamilika kwa baadhi ya miradi ikiwemo ujenzi wa minara 758 katika kata 713 kwenye maeneo mbalimbali nchini;

(iii) Fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazijapungua huku fedha za nje zikipungua kwa **asilimia 37.86** kulinganisha na mwaka wa fedha unaoisha. Hali hii imechangiwa na kukamilika kwa baadhi ya miradi iliyokuwa inagharamiwa na fedha za nje. Vilevile, mradi wa Tanzania ya Kidijitali unaotekelezwa kwa fedha za Benki ya Dunia ulipokea **Shilingi 49,883,879,923.30** katika mwaka wa fedha 2025/2026 sawa na **asilimia 177.20** ya bajeti iliyoidhinishwa ya **Shilingi 28,146,257,792.00**/=. Kwa hiyo utekelezaji wa mradi huu na miradi mingine inayotegemea fedha za nje haitaathirika; na

(iv) Minaradi yote ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara imeongezewa fedha kwa ajili ya utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2026/2027 ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha, ikiwa ni pamoja na Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa hatua ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima pamoja na kupunguza utegemezi wa fedha za nje katika kugharamia miradi ya maendeleo. Hata hivyo, miradi hiyo itakamalika kwa wakati na kuleta tija kwa wananchi iwapo Serikali itazingatia kutoa fedha za maendeleo kwa wakati kama zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka unaoisha pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (**Fungu 068**) kwa mwaka wa fedha 2026/2027, sasa naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

### 4.1 Maoni ya Jumla

a) Serikali iweke mikakati madhubuti na kuzisimamia taasisi zilizo chini ya Wizara hii katika ukusanyaji wa mapato ili ziweze kujiendesha na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija bila kutegemea mfuko mkuu wa Serikali;

b) Serikali iendelee kusimamia na kuweka mazingira ya kuwezesha taasisi za umma na binafsi kutoa huduma bora za mawasiliano na matumizi ya TEHAMA nchini;

c) Serikali ihakikishe inatoa fedha za maendeleo kama zilivyoidhinishwa na Bunge na kusimamia kikamilifu miradi ya kimkakati inayotekelezwa na Wizara hii ili iweze kukamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa; na

d) Serikali ihakikishe inakamilisha kwa haraka Muswada wa Sheria ya TEHAMA ya Mwaka, 2026 ambayo utachochea ubunifu, ajira na usalama katika matumizi ya TEHAMA nchini.

## 4.2 Maoni Mahsusi

### a) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ichukue hatua ya kuitambua TCRA kama chombo cha kimkakati katika ulinzi na usalama wa Taifa, na kuhakikisha kuwa taarifa zinazowasilishwa na Mamlaka hii kama viashiria vya uvunjifu wa amani katika vyombo vya dola zinafanyiwa kazi kwa uzito unaostahili;

(ii) Ipange na kutekeleza mkakati wa kuzuia na kupambana na uhalifu wa kimtandao ikiwa ni pamoja na wizi mitandaoni. Aidha, nguvu zaidi ielekezwe mikoa ya Dar Es Salaam, Morogoro, Mbeya na Rukwa ambapo matukio haya ni mengi; na

(iii) Ifanye tathmini kuhusu matumizi ya vifurushi vya data na muda wa maongezi na kuja na utaratibu utakaomwezesha mteja kutumia kifurushi chake mpaka kitakapoisha badala ya sasa ambapo anatumia hadi muda wa kifurushi utakapoisha

### b) Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iongeze kasi katika ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kati ya Tanzania na Jahmhuri ya Kidemokrasia ya Kongo hali itakayoboresha mazingira ya kibiashara baina ya nchi zetu na kuongeza fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma za Mkongo; na

(ii) Ihakikishe kuwa Wilaya zote nchini zinaunganishwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pamoja na kuunganisha taasisi za umma na binafsi kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na utoaji huduma nchini.

**c)Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Itoe **Shilingi Bilioni 100** kwa ajili ununuzi wa vifaa vipya pamoja na upanuzi wa eneo la utoaji wa huduma ya upangishaji wa nafasi (colocation) hatua itakayoongeza ufanisi katika matumizi ya kituo; na

(ii) Ianze mara moja ujenzi wa vituo vya kuhifadhi taarifa jijini Dodoma na Zanzibar ili kuhakikisha kuna kuwa na utunzaji endelevu wa taarifa zinazozalishwa na kutumiwa nchini.

**d) Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ifanye tathmini na kugeuza madeni ya Shirika la Posta kuwa mtaji (capitalization) ili liweze kujiendesha kwa faida na kutoa gawio Serikalini; na

(ii) Iboreshe miundombinu ya kufanyia kazi pamoja na maslahi ya watumishi wa Shirika la Posta nchini ili kuongeza motisha na kuleta ufanisi katika utendaji wa Shirika hilo.

**e) Ulinzi wa Taarifa binafsi**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Iandae mkakati wa kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya mitandao na madhara ya kuweka taarifa binafsi katika mitandao ya kijamii ili kuhakikisha jamii inazingatia faragha na kupunguza uhalifu na unyanyasaji wa kimtandao nchini; na
(ii) Itoe elimu na mwongozo mahususi kwa watumishi wa umma na sekta binafsi kuhusu umuhimu wa kutunza taarifa binafsi za wateja pamoja na taasisi wanazozifanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwachukulia

hatua za kisheria watumishi watakaobainika kushindwa kutekeleza masharti ya mwongozo huo.

**f) Vijana na Uchumi wa Kidijitali**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Itoe kipaumbele kwa maoni ya vijana katika Sera ya Kampuni Changa 2026, pamoja na kuonesha fursa zinazopatikana katika utekelezaji wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali kwa makundi mbalimbali ya vijana nchini;

(ii) Ikamilishe ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo Vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Park) ili kuwapa vijana nafasi kukuza ubunifu na ujuzi wa matumizi ya TEHAMA katika sekta mtambuka za kijamii na kiuchumi nchini; na

(iii) Ibainishe na kuvitambua vituo binafsi vinavyokuza ubunifu na ujuzi katika TEHAMA na kuviwezesha katika mtaji na malezi ili kuhakikisha matumizi sahihi ya ujuzi na ubunifu kiuchumi na kuzingatia maadili ya Taifa.

**g) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

Kamati inashauri kuwa, Serikali:-

(i) Ihakikishe kunakuwa na watoa huduma zaidi ya mmoja katika minara 758 iliyojengwa nchini kwa ajili ya kuwapa wananchi fursa ya kuchagua huduma na kuimarisha ushindani katika sekta ya mawasiliano;

(ii) Ifanye malipo ya Shilingi **31,642,735,500/=** kwa watoa huduma waliojenga minara 758 kwa ajili kuepuka riba inayowezakuchangiwa na kuchelewesha malipo hayo;

(iii) Iboreshe usikivu wa Redio Jamii na Redio ya Taifa katika maeneo ya mipakani kwa ajili ya kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kuwa na taarifa sahihi kuhusu Taifa letu; na

(iv) Ifanye tathmini na kuongeza nguvu kwenye minara kutoka 2G kwenda 3G/4G/5G hasa maeneo ya vijijini ili

kutoa fursa ya kupata taarifa kupitia huduma za mtandao wa internet.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge kwa Ufanisi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. **Mwenyekiti**
2. Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. **Makamu**
3. Mhe. Kapt. Said Hassan Ali Mwinyi, Mb. Mjumbe
4. Mhe. Condester Michael Sichalwe, Mb. Mjumbe
5. Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb, Mb. Mjumbe
6. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. Mjumbe
7. Mhe. Nuru Issa Kashakari, Mb. Mjumbe
8. Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako, Mb. Mjumbe
9. Mhe. Isack Joseph Copriano, Mb. Mjumbe
10. Mhe. Eng. Johnston J. Mutasingwa, Mb. Mjumbe
11. Mhe. Sara Msafiri Ally, Mb. Mjumbe
12. Mhe. John Stephano Luhende, Mb. Mjumbe
13. Mhe. Ibrahim Mohamed Shayo, Mb. Mjumbe

14. Mhe. Kellen Rose Rwakatare, Mb. Mjumbe
15. Mhe. Fatma Ally Rembo, Mb. Mjumbe
16. Mhe. Saidi Salim Hamad, Mb. Mjumbe
17. Mhe. Mgore Miraji Kigera, Mb. Mjumbe
18. Mhe. Hija Hassan Hija, Mb. Mjumbe
19. Mhe. Nabil Ahmed Abdallah, Mb. Mjumbe
20. Mhe. Hamis Mwagao Tabasamu, Mb. Mjumbe
21. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abdood, Mb. Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Waziri wa Wizara hii Mhe. Angela Jasmin Mbelwa Kairuki, (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri, Mhe. Switbert Zacharia Mkama (Mb). Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndg. Mohammed Khamis Abdullah. Kamati inatambua na kuthaamini mchango wa watendaji hao katika Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano na TEHAMA katika ujenzi wa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

### 5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya **Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (Fungu 068)** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu**
30 Aprili, 2026

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa uwasilishaji wa taarifa ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye hatua ya pili ya uchangiaji wa hoja iliyopo mbele yetu. Tunaanza na Mheshimiwa *Engineer* Saidi Salim Hamad, atafuatiwa na Mheshimiwa Eric James Shigongo, na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga ajiandae.

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuchangia katika Wizara yetu hii ya Mawasiliano. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninakishukuru Chama changu cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti, wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuamini kuwa Wabunge katika hili Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiofichika, Wizara hii ya Mawasiliano inafanya kazi kubwa sana. Nami nichukue nafasi hii kuupongeza uongozi wa Wizara hii chini ya Waziri wetu, Mama Kairuki, kwa kweli hongera sana na anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia kwangu kwa kuanza mchango wangu wa kwanza kwenye *data centre* yetu ya Taifa tulionayo. Duniani kote kuna *class* nne za *data centre* ambapo *the highest class* ni *class four* na *lowest* ni *class one*. *Data centre* yetu hii ya Tanzania iko katika *category* ya *class three* au *Q4*. Haya ni maendeleo makubwa sana ya ki-*data centre* ambayo tunapaswa kuji-*proud*. *Only thing* ambayo inapelekea *data centre* yetu isifikie ile *class four* ambayo inamilikiwa na Mataifa makubwa yaliyoendelea duniani kama Marekani, China na Mataifa mengine ni kwamba *data centre* yetu hii ya Tanzania hatuna *alternative power supply* ukiacha *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama leo tunaanzisha gridi mpya ya Taifa ya umeme au tuna *alternative power source, let us say* ya ki-*solar,* basi *data centre* yetu kwa vifaa na *infrastructure*

ambazo ziko pale na teknolojia inayotumika pale ina-*shift* kutoka *class three* kuja *class four*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Wizara ya Mawasiliano ikae kitako na Wizara ya Nishati kutafuta *alternative power source* ya kuihamisha *data centre* yetu hii kutoka *class three* kuja *class four* ili nasi tuwe tuna *data centre* ambayo inaendana na nchi ambazo zinaendelea duniani na Tanzania izidi kupaa katika hii sekta ya kimawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye wasilisho la Kamati ya Miundombinu hapa lililowasilishwa juu ya Wizara hii, *data centre* yetu hii tuko nayo kwa takribani miaka 10. Vifaa vyetu vya *storage capacity* tumeshafanya matumizi nayo *for more than 90%.* Sasa hivi nchi yetu inakwenda kwa mujibu wa uchumi wa kidigitali. Kwa hiyo tunahitaji *storage capacity* nyingine mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasilisho la Kamati hapa linasema kwamba Serikali iitengee Wizara hii kwa dharura ya kipekee kabisa shilingi bilioni 100 ili kuweza kujengwa *data centre* nyingine *as soon as possible* kabla *storage capacity* hii haijafikia *100%*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hii *data centre* ndiyo *engine* ya mawasiliano yetu na *storage* zetu na *server* zetu zote za *TRA*, mifumo yetu ya kiafya *data* zote ziko pale. Kwa hiyo, na mimi ninaunga mkono hoja hii ya kwa dharura yake kabisa, ku-*speed up*, kuwezeshwa Wizara hii kupatiwa hii shilingi bilioni 100 kuweza kujengwa *data centre* nyingine mpya haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *data centre* mpya ambayo itajengwa, niweze kushauri jambo lifuatalo. Tunaona vita vinavyoendelea duniani, licha tu ya kwamba wana-*target* kwenye *infrastructure* za umeme, lakini vilevile wana-*target infrastructure* za kimiundombinu ya kimawasiliano kama hii. *Data centre* yetu sisi ipo Dar es Salaam ambayo tupo nayo, *data centre* nyingine ambayo tutaijenga basi tutafute eneo lingine kama Dodoma au Arusha. Hii ni kwa ajili ya *security purpose*. Hata wahalifu wanapotaka kutufanyia uhalifu, basi *data centre* moja ipo Dar es Salaam, moja ipo Mbeya, moja ipo Dodoma inakuwa ni nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hii *data centre* ningependa kuishauri Wizara hii, kwa nini sasa tusijikite kwenda kwenye *cloud computing*? Tukiacha kuwa na hii *data centre* ambayo iko *physical* pale, tuhame. Sasa hivi dunia inaenda kwenye *cloud computing*. Tukienda kwenye *cloud computing* kwanza tunakwenda kwenye *low cost*, tunakwenda ku-*generate saving* ya kutumia fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwenye *cloud computing* tunaenda kwenye *flexibility of the data*. Sasa mtu, mfano *TRA* akitaka *data* zake kuna baadhi ya mambo inamlazimu aende pale pale kwenye *data centre*, lakini ikiwa tuna *cloud computing* hata awe wapi duniani anaweza ku-*access data* zake. Kwa hiyo, *flexibility* ya *data* inakuwa ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri hata kwenye *security*, kwamba tukiwa *tuna cloud computing* sasa tunajua *data centre* yetu iko Dar es Salaam, na yeyote anayetaka kufanya uhujumu wa *data centre* yetu anajua *physical location* yetu iko sehemu fulani. Kwa mfano, *disaster* kama za *earthquake*, Mungu atunusuru, mambo ya shoti za umeme, mafuriko kutokea kuweza kuathirika *data centre* kwa mambo kama haya yanapotokea ni rahisi, lakini tukienda kwenye *cloud computing* mambo kama hayo *never happen*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kupata shoti za umeme, hatuwezi kuathiriwa na mafuriko, hatuweze kuathiriwa na *disaster* nyingine zozote zile. Kwa hiyo, ninaishauri hii Wizara licha ya kwamba tunataka kuja na *data centre* nyingine, lakini vilevile tuanze kufikiria na ku-*shift* kutoka hizi *physical data centre* kwenda kwenye *cloud computing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie mchango wangu mwingine kwenye hii Wizara kupitia Mkongo wetu wa Taifa. Nchi yetu ya Tanzania tunaji-*proud* kwa kwenda vizuri kwenye diplomasia ya kiuchumi *(economic diplomacy)*. Mkongo wetu wa Taifa kwa wasilisho lililowasilishwa hapa tumeshaunganisha nchi saba ambazo ni hizi nchi zetu za maziwa makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kenya inatumia Mkongo wetu wa Taifa, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi nchi saba zilizotuzunguka zinatumia Mkongo wetu huu wa Taifa. Mpaka sasa tumesha-*generate income* ya shilingi bilioni 319 kupitia Mkongo huu ambao wameunganisha hizi nchi zetu jirani. Kwa hiyo, kwenye *economic diplomacy* tumpongeze sana Mheshimiwa Kairuki na Wizara yake, wanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi moja ambayo ni *potential* sana imeorodheshwa hapa, bado Mkongo huu wa Taifa haujafika, *which is DRC*. Hivyo basi, ninapenda kushauri, kwa kuzingatia kwamba nchi hii ina raia zaidi ya milioni 100, haraka sana iwezekanavyo twende tukatafute maokoto kupitia hii nchi. Tupeleke Mkongo haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hizi nchi ndogondogo tumesha-*generate* zaidi ya shilingi bilioni 319, kwa nini *DRC* tumechelewa muda wote huu? Ninaomba Mheshimiwa Waziri kwa kipekee kabisa aende akaunganishe Mkongo haraka sana tuweze kupata fedha nyingi kupitia nchi hii ili nchi yetu izidi kupaa kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kuchangia kuhusiana na *TCRA*. Ni ukweli usiofichika kwamba bado Watanzania wanalia na uhalifu wa kimtandao ambao unaendelea. Sisi hatuna *doubt* juu ya miundombinu waliyonayo *TCRA*, hatuna *doubt* juu ya *technical team* waliyonayo *TCRA*, hatuna *doubt* juu ya teknolojia wanazozitumia *TCRA,* wako vizuri, lakini kuna sehemu moja *I think* hapa kuna tatizo. *TCRA* wako na *Cyber Security* ambao ni *regulator,* lakini wata-*capture* mwizi, wata-*capture* taarifa zao, wata-*capture* uhalifu ulipofanyika kila kitu, baada ya kukusanya *data* zote hizi kwa mujibu wa Kitengo chao cha *Cyber Security* wanachukua na wanapeleka *Cyber Crime* ambacho kipo kwenye Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi nalo lipo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa *in between* kutoka kwenye *Cyber Security,* kutoka *TCRA* ikapanda daladala au bodaboda zikapelekwa huku kwenye *Cyber Crime* hapa katikati, hapa *in*

*between* kuna mapepo yanakuwa yanachanganya changanya mambo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, tuna kikosi cha bandari kiko pale, kwenye reli tuna kikosi cha Polisi kiko pale, *airport* tuna kikosi cha Polisi kiko pale, Bungeni tuna Askari Polisi wako hapa, Mahakamani kuna Askari Polisi wako pale, kwa nini *TCRA* ambao ni *Cyber Security* tusichukue *Cyber Crime* ya Jeshi la Polisi tukaenda tuka-*imbed* pale pale, akakamata mwizi mwenyewe *TCRA?* Tukabadilisha sheria, akawa ana-*regulate* sheria pale pale, na kama kuna *issue* ya *law enforcement* ifanyike pale pale *TCRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi, ninaamini kwamba uhalifu wa kimitandao hautapungua, bali utatokomea kabisa, kuliko tukienda kwa mwendo huu ambao kwa kweli Watanzania wanaumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuchangia kuhusiana na Mfuko wetu wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)*. Minara hii inasaidia sana, lakini bado tuna shida kwenye mipaka yetu baina ya Tanzania na Msumbiji kama kule Mtwara na sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa pale mpakani, mnara wetu upo, umejengwa na Wizara ya Mawasiliano, lakini una-*capture* mawasiliano ya nchi jirani. Kwa nini kama kuna teknolojia ambazo ni dhaifu tunazozitumia? Ninaishauri Serikali kupitia minara ambayo inajengwa, twende tukaboreshe *quality* ya minara yetu. Tukikaa mipakani, kwa nini tuvute mawasiliano kupitia mitandao mingine, kupitia nchi jirani, minara yetu isiwe *more powerfully* na *strong* zaidi ili tuweze kupata mapato yanayotokana na mipaka hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi tulichopita, Taifa letu hapo Oktoba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SAIDI SALIM HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Eric James Shigongo, ajiandae Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kusimama ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo mema ambayo ameyafanya katika Jimbo letu la Buchosa. Tumejengewa minara ya mawasiliano kwenye visiwa vyetu. Hivi sasa mawasiliano yameboreka sana. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba tu Mheshimiwa Waziri akipata mnara mwingine mahali popote, bado sehemu ya Iligamba kuna changamoto kubwa kidogo ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri alianza kwa kumshukuru mume wake leo, na mimi nimshukuru mke wangu. Ninaomba nimshukuru sana mke wangu Veneranda Ephrem Kavishe kwa namna ambavyo analea familia yangu mimi nikiwa hapa Bungeni, pia kwa namna ambavyo anasimamia biashara zangu. Mama nakushukuru sana, Mungu akubariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la Mungu linasema katika Danieli 12:4 kwamba, "Lakini ewe Danieli yafunge maneno haya ukakitie muhuri kitabu, hata wakati wa mwisho: wengi wataenda mbio huko na huko na maarifa yataongezeka."

Mheshimiwa Mwenyekiti, maarifa yameongezeka. Mungu aliiona dunia tunayoishi sasa wakati wa Danieli. Aliona kutakuwa na *Instagram*, aliona kutakuwa na *Imo,* aliona kutakuwa na *Snapchat*, kutakuwa na *TikTok;* aliona toka kule, lakini huku anaweka hayo mawazo ndani ya akili za wanadamu, wanatengeneza mambo ambayo Mungu aliyaona muda mrefu uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika ulimwengu huu ambao unabadilika kwa kasi katika ulimwengu huu ambao maarifa yameongezeka, teknolojia imebadilika, watu wamebadilisha namna ya kuwasiliana, watu wamebadilisha namna ya kufanya biashara, namna ya kutibu watu, kila kitu kimebadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyozungumza ndani ya ukumbi huu leo, watumiaji wa *smartphone* katika nchi yangu ya Tanzania ni 41%, watumiaji wa simu za mkononi ambazo huko nyuma zilikuwa hazipo kwa ujumla wao ni 87%, watumiaji wa mitandao ya kijamii ni milioni 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia imebadilika na mimi niseme wazi, mimi ni mdau mkuu wa mawasiliano kwa miaka mingi. Nimefanya kazi kwenye eneo hili kama mfanyabiashara wa mawasiliano kwa miaka mingi. Sasa Tanzania imepiga hatua kubwa sana kwenye eneo la mawasiliano. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima ya Mawasiliano. Ninaipongeza sana *TCRA* kwa kazi nzuri ambayo inaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa na mazungumzo marefu kidogo na Mkurugenzi wa *TCRA* ambaye amemaliza muda wake. Nilikuwa na mazungumzo naye kwenye maeneo matatu, kama ananisikia ataelewa ninachokizungumza. Nilizungumza naye juu ya malalamiko na manung'unuko ya watu wetu. Mimi kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania niko hapa kuwawakilisha watu wa nchi yangu. Niko hapa kuwawakilisha wananchi wa Buchosa na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ninyi humu ndani ni mashahidi, na mimi sijaja hapa kumshtaki mtu, lakini ninatimiza wajibu wangu. Wananchi wangu wanalalamika juu ya mambo makubwa matatu; *data* ni kitu ambacho sasa hivi ni *basic need,* ni mahitaji ya muhimu kwa kila mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji hewa, chakula, malazi na ninaona kuna jambo la nne linaongezeka kwenye maisha ya mwanadamu kwamba mwanadamu ili aishi, anahitaji *data*. Sasa

wanasema *data* ni *expensive*. *Data* zina gharama kubwa, na kinachowasikitisha wananchi wetu kweli, cha kwanza ni pale anaponunua bando la siku saba, halafu inafika siku saba bando halijaisha, halafu *data* zilizobaki zinapotea. Wanalalamika, hawana furaha, hawana amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu ameamua kuwapa wananchi wake tabasamu, wananchi hawana tabasamu kwenye eneo hili. Umenunua bando la siku saba, siku saba zikifika umebakiza *GB* mbili zinapotea, zinakwenda wapi? Wananchi wanauliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, umenunua bando la siku saba, lakini siku saba hazifiki. Waheshimiwa Wabunge nikiwauliza hapa ndani, nani alishawahi kununua bando la siku saba ikafika siku saba? Hakuna. Wengi mtasema inategemea na matumizi ya mtu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaponunua king'amzi cha Azam cha siku 30, siku 30 zinafika. Ofisini kwangu ninaponunua *Wi-Fi* ya mwezi, inafika mwezi, sana sana nikitumia vibaya inapunguza *speed,* lakini mwezi unafika. Wananchi wangu wanasema hapo kuna jambo haliko wazi, lazima jambo liwekwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanasema, kuna jambo haliko wazi. Siwezi kusema kuna wizi, sina uhakika, lakini kuna jambo haliko wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tunaponunua *bundle* ya kuongea *(voice);* ukiongea na *bundle* ya *voice* ikiisha ile *bundle*, wanahamia moja kwa moja kwenye *wallet* yako kwenye fedha za kwenye simu yako, wanaanza kuzitumia bila wewe ku-*opt*, siyo sawa. Nimenunua *bundle* ya kutumia kwa siku tano, ikiisha usiende kwenye fedha zangu kwenye *wallet* bila kuniuliza, niulize mimi nikubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu wanalalamika. Nimezungumza hili na Mkurugenzi aliyepita, akanipa kijana nikaongea naye, hatukufikia vizuri hatima yake. Ninafahamu, kampuni za simu zinahitaji faida na zinapataje faida, zinapata

faida kwa kitu kinaitwa *ARPU (Average Revenue Per User)*. Yaani mtu mmoja anatumia kiasi gani, *the higher the ARPU* ndiyo wanapata faida, ikiwa chini wanapata hasara. Wanafanya kila kinachowezekana kuona kwamba watu wanaendelea kutumia *data* ili waweze kupata faida, hakuna ubaya, wanapata faida wanalipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni moja, ninaponunua *bundle*; nikusomee kitu kimoja hapo. South Africa, nchi ambayo ina kampuni ya *Vodacom* kama sisi, wananchi walilalamika kama ninavyozungumza mimi, wakalalamika wakatishia kwenda mahakamani. Wiki iliyopita, *ICASA (Independent Communications Authority of South Africa)* imepitisha *regulation* mpya ya kwamba kuanzia mwakani tarehe 23 Januari, 2027 *bundle* haliozi, *bundle* halichachi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo siyo yangu, Waziri aende mtandaoni akasome na data ninayo hapa inasema hivi, "*ICASA moves to allow rollover of unused mobile data*". Yaani kinachofanyika ni *rollover*. Data imebaki una-*rollover*, unaenda nayo kwenye masaa mengine unanunua hapo mbele. Wananchi wa nchi yangu hawataki kuona *bundle* yao inapotea, wanahisi wanaibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri, muda hautoshi, ushauri wangu wa kwanza, tunacho kitu kinaitwa *TCRA-CCC*, *(TCRA Consumer Consultative Council* - Baraza la Walaji). Naliomba Baraza la Walaji litimize wajibu wake kwa kuwatetea wananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko hapa nisimamie *interest* za watu, kuna uwazi hauko wazi, nisimamie mambo yawe wazi watu waelewe, *bundle* lao linakwenda wapi? Wananchi wananung'unika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninashukuru sana kampuni za simu zinafanya kazi kubwa, hamna ubaya, wanatoa mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Ninaomba kitu kimoja muhimu, wafikirie kufanya kama wenzao South Africa wanavyofanya, wafanye *rollover* ya *bundle*. Kenya

wanafanya, Uganda wanafanya, Rwanda wanafanya, *what is wrong with* Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, huu wangu ni ushauri, *rollover* ifanyike, *bundle* ikifika mwisho, sijalitumia, nihame nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, ninamwomba dada yangu, amekuja kwenye hii Wizara aache alama, aache Watanzania wamkumbuke kwamba alipokuwepo Angela *bundle* lilishuka likawa bei rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna umaskini mwingine mpya, umaskini wa data. Mtu akiwa hana data anakuwa maskini, mtoto wetu hawezi ku-*post*, hawezi kufanya chochote mtandaoni, kwa sababu hana data. Kama tunataka ku-*promote digital economy* data iwe *affordable*, *data* iwe *cheaper*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha, ahsante sana kwa kunipa muda na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, wajiandae Mheshimiwa Joseph Enock Tama na Mheshimiwa Sara Msafiri Ally.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara nyeti ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu kwamba, Wizara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Jinsi dunia inavyokimbia katika teknolojia ya kila siku, kila siku ukiangalia katika mitandao ya kijamii utakutana na vifaa vipya vya kiteknolojia, ambavyo vinabadilika. Dunia sasa inaelekea kwenye maeneo ambayo hakuna tena kugusa vitu. Unaonyesha kwa ishara vitu vinafunguka na vitu vinafanya matumizi. Unaweza kuwa uko Bungeni, unaiendesha nyumba yako kiusalama, unazima *TV*, unazima vifaa vya umeme kwa sababu ya teknolojia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumesimama hapa, ikiwa minara 758 imekamilika. Juzi Mheshimiwa Rais alikuja pale *Jakaya Convention* na Wizara iliandaa tukio zuri sana la kidijitali. Ma-*screen* makubwa tuliona mambo mazuri sana. Inawezekana leo watu wasione jambo hilo la minara 758 kukamilika. Kaka yangu Mheshimiwa Ado yuko hapa atakuwa shahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakirejea huko nyuma, kelele zilizokuwa zikipigwa kuhusu tatizo la mawasiliano katika nchi hii, kiasi kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, hasa hii ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kusimamia kutafuta fedha, kutafuta mikopo na kujenga minara hii leo inakamilika, lazima tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake, katika nchi yetu sasa hivi tumefikia kwamba, tulivyo navyo ndani hatutaki kuviongezea tozo tupate mapato, hatutaki Serikali yetu ikope na kila siku tunatoa changamoto hapa za kutaka fedha, tutaendeshaje nchi? Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, leo tuna minara 758. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilombero, Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Katurukila kule nimepata mnara, Mpanga, Kisawasawa nimepata mnara na Lumemo nimepata mnara. Ninaishukuru sana Serikali, ninaishukuru sana Wizara hii. Ninaomba tu changamoto zinazotokana na minara hiyo kwa sababu mingine ni mipya imefunguliwa hivi karibuni zipatiwe tiba. Mfano, katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, Kata ya Lumemo, Diwani wangu Frank Ngawa ananiambia mnara uliojengwa pale una changamoto ya mawasiliano mpaka mtu awe karibu zaidi ndio anapata mawasiliano vinginevyo hapati mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niko hapa ninaunga mkono mapendekezo yote ya Kamati na kuhakikisha kwamba, tunaboresha kuipelekea Wizara hii fedha kwa wakati ili isaidie maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie, Wizara hii ya Mawasiliano ndiyo ambayo inakagua simu zetu zote tulienda

kutembelea pale. *Dealer* yeyote wa simu anayeingiza simu nchi hii anatakiwa kuchukua *sample* ya simu kuzipeleka pale. Pale wana kimiminika maalum ambako wanaingiza simu, hicho kimiminika kina-*sense* kama binadamu, kinasema simu hii ni mbovu ama si mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipopeleka pesa kwa wakati katika Wizara hii, zitaingia simu mbovu hapa ndiyo tunapata mambo ya kansa, maana yake huko mtandaoni kuna habari nyingi sana za kuhusu ukiongea na simu weka mbali, sijui usivae *headphone* sijui usifanye namna gani. Kwa hiyo, hii ninasema ni Wizara muhimu sana kuhakikisha tunaipa fedha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wabunge wengine walivyomaliza kuchangia hapa, ninataka kusema *TCRA* iundiwe Kamandi Maalum ya Polisi. Ninaunga mkono hoja hiyo, ili kuhakikisha kwamba inaweza kuchukua ushahidi wa kitaalam ule, kuusimamia polisi moja kwa moja kwa polisi ambao watakuwa wa *TCRA* ili kuhakikisha kwamba ushahidi ule haupotei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hapa pia, Mheshimiwa Waziri yuko hapa, kwa sababu Halmashauri yangu ya Mji wa Ifakara imetajwa huko, inaongoza katika utapeli wa kimtandao. Ninaishi Ifakara lakini si kweli jambo hili. Tunaonewa na Mheshimiwa Waziri ninaomba anilinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi vijana wetu ni wakulima wazuri Ifakara, wanafanya kazi kwa bidii, lakini laini zikikamatwa Ifakara, zimesajiliwa Ifakara, watu wanatapeliwa Mwanza, wanatapeliwa Kigoma, wanatapeliwa wapi.  Sitetei uhalifu, kama Mbunge ninawapenda wananchi wangu na ninawapenda vijana. Kama kuna wachache wahalifu watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Ndiyo maana nimemwomba Mheshimiwa Waziri semina ile tukajifungie na vijana, waseme ukweli kwa wale ambao wanahusika na changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema kwa ufupi, vijana wa Kilombero ni vijana wa bidii sana. Tuwasaidie basi kuwapa, *ICT Park*. Nimeona katika bajeti Waziri anajenga *ICT Park* katika mikoa

nane. Sasa kama wamei-*list* Halmashauri ya Ifakara inaongoza katika jambo hilo ambalo mimi sina uthibitisho nalo, basi watuwekee *ICT Park,* kituo cha kompyuta vijana wakaonyeshe utundu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake vijana wa Ifakara ni wajanja kweli. Sasa wewe ndugu yangu, mwananchi unaambiwa tuma kwenye namba hii, unatuma. Sasa kijana atafanyaje endapo huku kuna mambo mengine yameziba ziba. Ninasema sitetei uhalifu, lakini ninaomba njia mbadala. Kama kuna vijana kama hao wapo Ifakara, tuwajengee *centre ICT Park* nzuri, tuweke mtandao, tuweke *computer*. Vijana waweze kubadilisha ubunifu wao na utundu wao, uende katika njia mbadala kuliko kusema tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja Afande *OCD* pale mkubwa alikuwa anatuambia vizuri sana. Siyo kwamba kweli hapa kuna tatizo hilo la kiasi hicho cha utapeli. Kuna watu wa mitandao ya simu watuambie, kwa nini laini za utapeli za huko duniani, nchini huko kote, mikoa yote, zinaonekana zinasajiliwa pale. Ina maana kuna *gap* la usajili. Ninataka kuja na mapendekezo ya jambo hili, yako mapendekezo kwamba hii mitandao ya simu laini wasiziachie achie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakuwaje na laini ambayo haijasajiliwa kwa *NIDA* na alama ya kidole inamtapeli mtu, tunaacha? Sheria yetu inasema ili kesi iende mahakamani lazima uwe umepoteza pesa, kupata zile jumbe peke yake hakutoshi kuipeleka kesi mahakamani. Kwa hiyo, tunachoomba kwanza, ni kwamba, tubadilishe sheria. Hata hawa watuma jumbe hawa *TCRA* wafungie hizi laini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwa bahati nzuri aliyekuwa Mkurugenzi wa *TCRA* alikuwa anafanya kazi nzuri sana, ukimtumia meseji anai-*block* ile laini pale pale. Siyo wananchi wote wana uwezo wa kumtumia meseji na kuna maneno unaweza kuyafungia na wamefanya hivyo unaona hata wale watu wa mtandao sasa hivi kuna maneno wakikuandikia kwenye sentensi unaona kuna maneno mengine ambayo hayatokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tumepoteza shilingi bilioni 20 kwenye utapeli wa kimtandao. Kwa hiyo, ni sehemu ambayo Mheshimiwa Waziri kwa kweli anatakiwa aweke nguvu kubwa sana kuhakikisha tunakomesha jambo hili. Kuna akina mama huko vijijini, wajane, watu wa kawaida wanatapeliwa pesa nyingi sana. Nimeona juzi Tabora *RC* anakamata vijana wamemtapeli mama shilingi milioni 40 kwenye akaunti. Utapeli wa mitandao ya simu lazima tuweke kikosi madhubuti cha kuhakikisha kwa kweli tunaondoa jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili, kuwe na dawati, kama tunashindwa kuweka kamandi, basi kituo cha polisi, kuna dawati la jinsia tumeweka pale. Kuwe na dawati la askari wanaoenda mafunzo maalum ya utapeli wa kimtandao na wanapewa *access* kwenye *computer*. Mtu ameibiwa simu akiripoti, simu yake inajulikana iko wapi, duniani sasa hivi kila kitu kiko katika mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anaweza akaripoti ameibiwa simu mwezi mzima, inatafutwaje simu na wakati ukiiwasha tu tunajua simu iko wapi. Tunasema tubadili sheria, laini zote zinazotuma meseji zifungiwe na siyo lazima mpaka mtu awe amepoteza pesa. Tutoe elimu mashuleni kwa vijana wetu. Tuwaambie vijana, sheria inasema, shilingi 100,000 ya utapeli ni miaka saba jela, watu wajue kwenye mashule. Watu wa *TCRA* kitengo cha elimu kipewe pesa, kipewe magari, kizunguke kwenye mashule kutoa elimu, kwamba ukishiriki utapeli shilingi 100,000 ni miaka saba jela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kwa kumalizia ninataka kuzungumzia Shirika la Posta. Shirika la Posta kama lingewezeshwa vizuri, kama ilivyosoma taarifa; madeni ya Serikali, Serikali ichukue deni la Shirika la Posta, isaidie Shirika la Posta kujenga miundombinu. Sasa hivi tunatuma sana vipeto kupitia mabasi ya watu binafsi, ninaona biashara inavyokuwa kubwa, ni aibu Shirika letu la Posta kuyumba. Leo kuna kampuni hapo ukitaka gari kupeleka sehemu fulani unaitumia ile kampuni, iko duniani huko inaitwa *Bolt*, lakini Shirika la Posta walisha-*develop application* kama ile. Kutokana na kipato kuwa duni hawana uwezo, wameshindwa kuendeleza *Bolt* yao ambayo jina limenitoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiiwezesha vijana wa *ICT* wa nchi hii kama alivyofanya Waziri wa ujenzi ametoa ofa kwa vijana kuandika *paper* kuhusu foleni ya Dar es Salaam. Waziri atangaze vijana wa *University* of Dar es Salaam, vyuo vya teknolojia, vyuo vikuu vya nchi hii. Watengeneze *application* kama *Bolt*, tunaweka *Bolt* pesa, pesa zinaenda nje ya nchi. Kila anayelipia *Bolt* pesa zinaenda nje. Tunashindwa kuweka ramani za Jiji la Dar es Salaam peke yake katika *application* ya Tanzania, ambayo mimi niki-*request* pikipiki inakuja katika *app* ya nchi yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujifunze basi hata kwa Nchi marafiki kama China, tufanye pesa hizi zibaki. Hawa watu kwa kamisheni wanakusanya mabilioni ya pesa. Tuliwezeshe Shirika letu la Posta na kuhakikisha kwamba inafanikiwa kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili la Posta lina ofisi karibu kila halmashauri na kila wilaya. Sasa hivi kulikuwa na nyumba ya Posta pale Ifakara sasa hivi wana uwezo wa kuweka *ATM*, lakini mtu alikuwa anaenda kuchukua kipeto chake Posta badala ya kutuma kwenye usafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Enock Tama.

**MHE. JOSEPH E. TAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuiona siku ya leo pamoja na Wabunge wenzangu kuhudhuria Bungeni hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhana hiyo hiyo ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nianze na maneno yake matukufu kutoka kwenye Biblia Takatifu. Kitabu cha Mwanzo 41 mstari wa 38, nanukuu: “Farao akawaambia watumwa wake, tumpate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake?” Hakika,

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametuletea Waziri Angellah Kairuki mwenye roho ya Mungu ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya na Wabunge wenzangu watakuwa mashuhuda. Mama huyu ni msikivu, mnyenyekevu, hodari na mchapakazi kwelikweli. Watu kama hawa wanahitaji kutiwa moyo, hakika, hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. Aendelee kuchapa kazi na msaidizi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Wizara kutuletea bajeti ambayo 94.1% imejielekeza kwenye miradi ya maendeleo, ni kitu chema sana na ninaiona kesho iliyo njema kwa Taifa letu. Kweli tumepiga hatua kubwa sana kwenye teknolojia ya habari, ni kweli tulipotoka ni mbali, mafanikio ni makubwa. Hakika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana kwenye Sekta hii ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye mambo machache ili kuwashawishi Wabunge wenzangu tuunge mkono kwa 100% bajeti hii ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara imejenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano zaidi ya kilometa 801, ambapo wanufaika ni wilaya 121. Kwa kweli ni kazi kubwa sana, inayostahili kuungwa mkono. Wilaya zilizobaki ni 18, ushauri wangu kwa Wizara, wapeleke haya mambo mbiombio na hizi wilaya 18 zilizobaki zifikishiwe huduma kwa kuungwa kwenye Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kwa kufanya hivyo, tutamtendea haki Mtanzania, kwa kufanya hivyo tutawatendea haki wananchi waliomwamini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaotoka kwenye majimbo ya vijijini, tusipomshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tutakuwa ni wachoyo wa fadhila. Tarehe 10 Aprili, 2026, Waheshimiwa Wabunge wote ni mashahidi. Mheshimiwa Rais wetu alizindua ujenzi wa minara 758. Mawasiliano vijijini ilikuwa ni changamoto, leo hii minara hii inakwenda kuhudumia kata 713. Si jambo dogo, kata hizi zinakwenda kutabasamu. Hongera sana

kwa Wizara, hongera sana kwa Serikali, hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo la minara, Wizara imetueleza, kwamba upo uendelezaji wa ujenzi wa minara 636. Hii ni *commitment* ya hali ya juu. Tabasamu linakwenda kwenye kata 443, tabasamu linakwenda kwenye vijiji 636. Loh! Hili si jambo dogo. Tumpate wapi mtu kama huyu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajaishia hapo kwenye eneo la minara. Kitendo cha kuongezea nguvu minara 304 ni jambo jema sana. Wale waliokuwa kwenye *2G*, leo hii wanatabasamu kwa *4G,* ni jambo jema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani, sote tunatabasamu na *WhatsApp*, ni Wizara ya Mawasiliano, tunatabasamu na *Facebook*, Wizara ya Mawasiliano, tunatabasamu na *Instagram*, Wizara ya Mawasiliano, kama hatutapitisha kwa 100% bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano tutalaaniwa. Mimi siko tayari kuwa sehemu ya wale waliolaaniwa. Hakika Wizara wanachapa kazi, kwa kutukumbuka sisi wa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo wamefanya vizuri Wizara hii, wameongeza ajira. Vijana wetu wengi, Watanzania wengi wamejiingiza kufanya biashara kupitia mitandao. Leo hii tunaagiza nguo na vifaa kwa mtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatusafiri kwenda Dar es Salaam kutoka Kaliua kufuata bidhaa. Hata ndugu yangu Mheshimiwa Ado anakubaliana na mimi, hasafiri kutoka Tunduru kufuata saa ghali aliyoivaa Dar es Salaam. Anaagiza, analetewa, anapokea, ni matunda ya Wizara. Tuwaunge mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho; kwa sababu, tumeelezwa mipango mizuri ya uendelezaji wa ujenzi wa minara ili kuhakikisha ya kwamba mpaka kufika 2030 nchi nzima changamoto ya mawasiliano ya simu, changamoto ya mawasiliano ya redio, Wizara itakuwa imetupa majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara, kwenye Jimbo langu la Kaliua, kuna Kijiji cha Shera, Kijiji cha Igombe, Kijiji cha Luyembe, Kijiji cha Mwaraja, Kijiji cha Mpongolo na Kijiji cha Isunda havina minara ya simu. Kwa kasi ileile, kwa *speed* ileile na mimi leo ninawaambia wananchi wangu wa Jimbo la Kaliua, ninakwenda kupitisha bajeti hii nikiamini kwamba 2030 wote tutatabasamu; wananchi watatabasamu na mimi Mbunge nitatabasamu kwa sababu kazi iliyofanywa ni njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, tunakushukuru kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, ajiandae Mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara hii; Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya na kutupa ushirikiano sisi Waheshimiwa Wabunge kwenye kutekeleza majukumu yetu. Tunashukuru sana na tunawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee niipongeze Wizara kwa kuvuka malengo ya makusanyo yaliyopangiwa shilingi bilioni 120 ilikuwa ni malengo, lakini mpaka tunaenda mwezi huu wa Aprili, Wizara imeweza kukusanya shilingi bilioni 160 zaidi ya 133% ya malengo waliopangiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi niiombe Serikali itoe fedha zote zilizoombwa na Wizara hii kwa kuwa inatoa huduma kwa wananchi na inafanya biashara tunapata mapato mengi na makubwa ambayo inaenda kuleta mabadiliko kwenye miradi mbalimbali ya kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda niipongeze Serikali kwa kuhakikisha kwamba miradi mingi ndani ya Wizara hii, fedha za ndani zimetengwa na zimetolewa kwa zaidi ya 52% ya bajeti kwenye fedha za maendeleo na ndiyo maana leo kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama hapa anapongeza kazi

kubwa iliyofanywa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha huduma za miundobinu ya kiteknolojia na mawasiliano tunajua fedha za nje zimetoka lakini kwa kiwango kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara na Serikali kwenye miradi yetu ya kimkakati kwa hali ya mabadiliko ya kiuchumi, basi tuhakikishe fedha za ndani tunazokusanya tuweke nguvu kwenye miradi yetu hii ya kimkakati ambayo inatuletea mapato mengi sana kwenye miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu walioongea Serikali imejenga minara ya simu 758 kwenye vijiji 1,400 Jimbo langu la Mvomero lina vijiji 140, ni maeneo machache sana. Tunahitaji kama minara 43 Jimbo zima la Mvomero liwe na mawasiliano ya uhakika ya interneti na minara ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Wizara katika mpango unaokuja waweke kwenye maeneo haya 43 ya Jimbo la Mvomero ili wananchi wanaolima kokoa na mazao mengine ya biashara waweze kuwa na uhakika wa kutafuta masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee kuhusu Mkongo wa Taifa. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alivyoingia madarakani alikuta wilaya 36 tu ndani ya nchi hii ndio zina mkongo wa mawasiliano, lakini kwa kipindi kifupi Mheshimiwa Dkt. Samia ameweza kufikisha mkongo wa mawasiliano kwenye wilaya 122 na ameahidi Mheshimiwa Rais kupitia bajeti hii tunayoipitisha mwisho wa bajeti wa mwaka huu anakwenda kumalizia wilaya zilizobaki 17. Kwa hiyo, wilaya zote zitapata huduma ya *internet* za uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa mapinduzi makubwa ya kiteknolojia ambayo amewekeza kuhakikisha tunaleta mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali ninajua kwamba tuna mradi wa ujenzi wa mkongo huu wa mawasiliano, Mkongo wa Taifa kule *DRC* Congo na Kigoma, basi Serikali sasa itoe fedha

ikamilishe ili zile nchi saba ambazo tumezifikia tuongeze na DRC Congo kwa sababu ni eneo letu la kimkakati la kiuchumi tuweze kupata mapato kupitia mkongo huu kwa sababu tunauza huduma hizi za mawasiliano kwenye nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuongelea kuhusu mifumo ya uendeshaji na mifumo ya malipo ya kidijiti au ya *electronics* ambayo ipo kwenye taasisi mbalimbali za umma. Unakuta Wizara ina mifumo ya malipo ya kieletroniki zaidi ya 10 na mengine zaidi. Kwa mfano TAMISEMI kuna TAUSI lakini kule kuna za ukitaka kutafuta pasipoti kuna mifumo hiyo. Hivyo, swali ninalojiuliza kila siku mifumo hii yote inasimamiwa na taasisi gani? Mifumo hii nani anaipima? Kwa sababu wananchi wanaenda kupata huduma ukifika unaambiwa mfumo haufanyi kazi unacho ninachofanya ni kurudi tu nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kuona mifumo hii yote ya Serikali ya malipo na uendeshaji ya *electronics* iwe chini ya Wizara hii itatusaidia waweze kupata utaalam ambao ume-*advance* zaidi. Tunaona mifumo iko mpaka kwenye halmashauri, lakini tunashangaa kwa sababu ukienda kwa mfano idara ya sheria utakuta kuna changamoto za kimikataba. Mifumo hiyo imepanda mpaka kuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwenye uhasibu mifumo imepanda mpaka kuna Mhasibu Mkuu wa Serikali na sekta zingine huko na idara zingine, lakini mifumo ya mawasiliano kila mtu anaamua anachoona, anaanzisha mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nani tunamuuliza mifumo hii tukienda kwenye taasisi hiyo tunaambiwa mfumo una shida? Kwa hiyo nii Serikali ili kuongeza ufanisi na kupima mifumo hii kwamba inaleta matokeo mazuri kwenye huduma hizi za mawasiliano kwa wananchi, basi mifumo hii sasa ikasimamiwe na Wizara hii na hii itatusaidia kupunguza masuala mengine ya wizi na ukiukaji wa kimaadili na upotevu wa vitu vingine kwa kuwa sasa inapimwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapenda mifumo hii na hatuwezi kuondokana na mifumo hii kutokana na teknolojia ya sasa, lakini kuiacha mifumo hii ianze tu inavyoanza inaishia inavyoishia bila kuwa na msimamizi, nadhani sasa hivi ni muda sasa muafaka

tuwe na mifumo hii ambayo huyu Mhasibu wa Halmashauri akitaka kuulizia mfumo huu umemsumbua au mtu wa *IT* wa halmashauri, basi kuna *appeal* huko juu ya kwenda kuja kumsaidia, wasiende kumuuliza yule aliyetengeneza mfumo au akarudi kwa *consultants*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini ucheleweshaji wa mifumo hii wakati wananchi wanataka huduma inasababisha kupoteza mapato ya Serikali kwa sababu unaenda kupanga foleni kulipa kodi unafika pale unaambiwa mfumo hakuna rudi na hela, sasa unaenda mara mbili, mara tatu na hakuna mtu anayefurahishwa na mambo ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi *bureaucracy* zikiwa nyingi na changamoto ambazo hazina majibu ya kudumu wananchi hawa tutakuwa tunawalaumu wanaenda huko hawapati huduma hizo za malipo. Kwa hiyo, turasimishe mifumo hii kuanzia ngazi za Halmashauri za Serikali za Mitaa mpaka ngazi ya juu kwenye Wizara husika na taasisi ikitaka kuanzisha mfumo lazima upitiwe tujiridhishe uwezo wake katika utoaji wa huduma ili kupunguza changamoto hizi za kukosekana kwa mifumo lakini na kuongeza mapato yetu mifumo ifanye kazi kipindi chote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono na niendelee kuipongeza Wizara nimpongeze Mheshimiwa Rais na niwaombe vijana wa Tanzania mkongo huu wa mawasiliano uliowekwa kwenye wilaya zote tutumie fursa hii kujiendeleza ni fedha nyingi ya walipakodi, fedha ya Serikali imewekezwa huko. Sasa tusibadilishe mawasiliano haya yakawa adha tukafanye maendeleo, tukaipongeze Serikali uwekezaji huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na wilaya 36 tu lakini Mheshimiwa Dkt. Samia amefikisha kila wilaya ili wananchi hawa vijana wanaofanya biashara ndogo ndogo hizi kama walivyoongea wenzangu waweze ku-*test* na kutafuta masoko na bei za mazao. Kwa hiyo, niwasihi sana tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, tuendelee kuipa fedha nyingi za kibajeti Wizara hii kwa sababu inafanya huduma na kufanya biashara inatuletea mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja mheshimiwa Suleiman Mohamed Rashid.

**MHE. SULEIMAN MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuwa mchangiaji wa hotuba ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Awali yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii bila kuwasahau wadau mbalimbali wa sekta ya mawasiliano pamoja na teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ni mmoja kati ya mdau namba moja wa uchumi wa kidijiti na ninampongeza kwa namna ambavyo ametambua umuhimu wa uchumi wa kidijiti. Tunaweza kuona hayo katika Dira yetu ya Maendeleo ya 2050, kwenye ukurasa wa tatu ambapo alisisitiza mageuzi ya kidijitali yaweze kufanyika kwa kiwango wa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, isitoshe Mheshimiwa Rais wakati anahutubia Bunge letu hili la Kumi na Tatu, moja ya maeneo ambayo aliweza kuyazungumzia kwenye kitabu chake cha Hotuba ukurasa wa 34 ni suala zima la mkakati wa uchumi wa kidijiti. Siyo hivyo tu ameonyesha dhamira ya kuona kuna haja ya kuwa na chuo maalumu kinachohusiana na masuala ya teknolojia ya kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya 2025 - 2030 ameonyesha nia ya kutaka Tanzania iwe kitovu cha masuala haya ya kidijiti Afrika Mashariki pamoja na Kusini. Nami nikiri ni kwamba sekta hii ya mawasiliano, sekta hii ya habari imekuwa ni sekta muhimu sana na sekta iwezeshe kwenye masuala yetu haya ya uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mifano hai ya nchi ambayo wanaweza kutumia sekta hii katika masuala mazima ya uchumi

kwa mfano, Nchini China unaweza ukaona sekta hii imeweza kuchangia 43% ya pato la Taifa wenye wastani wa dola trilioni 7.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchini Kenya sekta hii imechangia 9.24 kwenye pato la Taifa. Siyo hivyo tu, utapokwenda Rwanda sekta hii inachangia 4.5%, lakini Tanzania sekta hii inachangia 1.5% kwenye pato la Taifa. Nitajikita kwenye changamoto ambazo tunakabiliana nazo kama Taifa letu, namna gani ambavyo tumeshindwa kufikia malengo ambayo Mheshimiwa Rais ameonyesha dira ya uchumi ya kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya sehemu ambayo nimeiona kuwepo kwa ushuru wa bidhaa, dhana kubwa ya ushuru wa bidhaa ni kuzuia matumizi ya bidhaa ambayo tunaweza kufikiria ikawa ina *harmful* kwa mwananchi. Ushuru huu wa bidhaa huwa analipa mlipaji ambaye ni mwananchi, ambaye ni mtumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia kiwango cha ushuru wetu wa bidhaa ni 17% ikiwa na maana kwamba tutapokuwa tunanunua vocha ya shilingi ushuru wa bidhaa tunachajiwa shilingi 170, hapo hatujakatwa *VAT* na hapo hapo ndani ya ushuru wa bidhaa hii 17% ndani yake mna *VAT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia stadi ya nchi nyingine kama Malawi ushuru wa bidhaa kwenye masuala haya ni 10% tu, ukienda Kenya ushuru wa bidhaa ni 15%, ukienda South Africa ushuru wa bidhaa ni 0%. Hapa unaweza ukaona namna gani Tanzania tunakabiliana na changamoto kubwa sana ambayo imekuwa ni kikawazo kikubwa kwenye suala zima la uchumi huo wa kidijiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la gharama za uendeshaji wa minara maeneo ya vijijini pia unaweza ukaona namna ambavyo gharama za uendeshaji wa minara hii inakuwa ni kubwa sana kiasi cha kwamba inakuwa haina uwiano baina ya gharama ambazo zinapatikana na mapato ambayo wenzetu wenye sekta ya mawasiliano ambayo wamewekeza wanaweza kupata. kwa hiyo, unaweza ukaona miongoni mwa kikwazo kikubwa sana katika maeneo yetu ya vijijini kuweza kutumika

ipasavyo mitandao yetu hii na kuweza kufaidika kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la uchache wa minara, Tanzania tumebarikiwa tuna kilometa za mraba 947,000 lakini wastani wa minara ambayo tunayo kwa idadi ni minara 10,000 tu. Unaweza ukaona ni kwamba kila mnara moja unahudumia kilometa za mraba 94.7, wakati wenzetu Kenya minara ambayo wanayo ni minara 9,000, lakini wastani wa kilometa za mraba ni 64,400. Unaweza ukaona kwamba wastani wa kila mnara moja unahudumia kilometa za mraba 64.4. Kwa hiyo, unaweza ukaona namna gani ambavyo tumekuwa na changamoto kwenye suala hilo la minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nilitaka nilizungumzie miongoni mwa changamoto hii kubwa katika masuala haya ya uchumi kidijiti; ni suala la usalama wa mtandao. Bila shaka wenzangu wameelezea kwa umakini sana. Unaweza ukaona aina mbalimbali za uhalifu ambazo zinajitokeza katika mitandao yetu hii. Tunapotarajia kuelekea kwenye uchumi wa kidijiti tunatarajia kwamba aina za biashara zetu zote ziweze kufanyika kupitia mitandao, lakini usajili wa watu wenyewe wa mikoa hawaaminiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni zenyewe ambazo tunatarajia ziweze kufanya biashara hizo zimekuwa hazina uhakika kutokana na uhalifu. Kwa hiyo, unaweza ukaona kwamba Taifa letu pamoja na mipango mizuri na dhamira ambayo anayo Mheshimiwa Rais, lakini bado tuna changamoto hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni changamoto ambayo tunayo ni suala la uelewa mdogo wa teknolojia ambayo baadhi ya wananchi wetu wengi hasa wa maeneo vijijini hawaelewi umuhimu na faida ya suala hili la kiteknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa miongoni mwa changamoto kubwa sana ni Sera yetu ya Taifa ya 2016, pamoja na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa kwamba

bado wapo katika mapitio, lakini sera hii ambayo tunayo sasa ambayo ndiyo tunaitumia na ndiyo tumeanza nayo kutekeleza Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi na ndiyo ambayo tumeanza nayo kutekeleza Mpango wetu wa Miaka Mitano ambayo tumetohoa kwenye Dira yetu ya Taifa 2050, bado haitambui kwenye suala la *AI,* bado haitambui suala la *blockchain,* lakini pia haitambui masuala la *cloud computing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya yote nilitaka nitambue kwamba pamoja na jitihada na dhamira ambayo Mheshimiwa Rais ameonyesha, lakini kama ni Taifa tunakabiliana na changamoto hizo. Katika hili ninapenda nitoe ushauri wangu; la kwanza, kwenye kupunguza ushuru wa bidhaa niombe sana Serikali ione haja na umuhimu kwamba ili tuweze kumpa *purchasing power* mwananchi wetu ya kuweza kununua vocha tupunguze hii angalau itoke angalau 17% twende 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika kipindi cha ushindani na tuikiri kwamba *counterpart* wetu tumjue ni nani na yeye yupo hali gani ili na sisi tuwe katika *safe side* ya kuwa tuna uhakika wa kuweza kufanya biashara hii. Niombe sana tupunguze ushuru huu wa bidhaa kutoka 17% angalau tuweze kufika 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka nitoe ushauri kwa Serikali kwenye suala la ushirikishwaji sekta ya binafsi, tuna makampuni tofauti ya simu ambayo yameonyesha nia na dhamira ya uwekezaji katika sehemu mbalimbali ya katika masuala ya minara na maeneo mengine. Tuombe Serikali iendelee kufungua fursa watengeneze mdahalo tutengeneze Kamati Maalum ambazo zitaweza kuwa na mkakati mahususi kwa maeneo ambayo tumeshindwa kufika ili tufike na kufikisha huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka nishauri Serikali pamoja na hotuba ambayo Mheshimiwa Waziri ameweza kuitoa hapa ya kuona sasa wanafikiria katika matumizi haya ya *satellite,* ninajua kwamba baadhi ya sheria zetu zinakinzana kwenye zana hii ya suala la *satellite,* ulimwengu ndipo unapoelekea, hatuwezi sisi Tanzania tukaishi kama Kijiji, ni vyema tukafikiria kwa namna gani na muda sahihi ya kuweza kutumia hizi

*satellite*, *satellite* ambazo zitaweza kutumika kwa maeneo ambayo yasiyofikika, lakini itaweza kuboresha maeneo ya kupatikana kwa huduma hizi za *internet* na huduma nyingine hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la kukuza elimu ya kidijiti, tuone mitaala yetu ya elimu tuone tunaboresha vipi na kuweza kuona tunaweza kutoa elimu ya suala la kidijiti, lakini pia tuweze kuwa na *program* maalum. Zamani tulikuwa tuna *DJ*, tunamwita *DJ Roving* ambaye alikuwa akipita mitaani huku wakati wengine vipaji vyetu viko mitaani tusikae sana maofisini, tufanye *survey* katika maeneo tofauti ambayo tutaweza kukutana na wadau na kuweza kuwapa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa kwenye ushauri wangu kwenye suala hili la *IT hub*. Ni vyema na amefika wakati Dar es Salaam kule tulianzisha *Silicon Dar* lakini kuna umuhimu sasa kuona kila mkoa tuweze kuwa na *IT hub* na *IT* hizi *hub* zitakuwa zina majukumu tofauti moja ni kuwatambua watu wetu wa TEHAMA*;* lakini la pili, tutaweza kuwaongoza namna gani bora kuweza kutumia masuala haya ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, tutaweza ku-*develop* mambo mbalimbali yanayohusiana na masuala ya TEHAMA kama ni Taifa, ni vyema tufike wakati kwamba tusiwe tuna-*import* mifumo kutoka Mataifa mbali na ni vyema tukawa tunazalisha sisi wenyewe kupitia wataalam wetu wa hapa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, nimepitia bajeti yetu hapa na imeonekana bajeti yetu imepungua kwa 23% na miongoni mwa hoja ambayo ilitolewa ni kuweza kupunguza matumizi ambayo hayana faida. Tunapokuwa tunapitisha bajeti ndani ya Bunge lako hili tunatarajia kwamba Serikali ikasimamie juu ya matumizi hayo. Mimi binafsi ninamba sana kwamba bajeti hii iweze kuongezeka ili changamoto ambazo tumezioanisha zote ifike wakati ziweze kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mwera, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zetu kwa mchana wa leo na watakaoanza kuchangia jioni ataanza Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mheshimiwa Emmanuel Khambay na orodha itaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; wote mnatangaziwa kuwa leo siku ya Alhamisi tarehe 30, 2026 kutakuwa kuna semina kuhusu Mradi wa Gridi ya Maji ya Taifa itakayotolewa na Wizara ya Maji. Semina hii itafanyika Ukumbi wa Msekwa mara baada ya kumaliza kikao Chama Cha Mapinduzi. Wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninaomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.59 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Isack Joseph

Copriano, Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe na Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa wajiandae.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi kukushukuru kwa kunipa fursa ili kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Mawasiliano. La kwanza, ninaomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kusimama mahali hapa kwa ajili ya huu mchango ambao ninaotaka kuutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kwanza kabla sijaenda kwenye mchango wangu niwashukuru sana au niipongeze sana Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya na niwapongeze sana wataalam kwa sababu tulivyopata fursa ya kutembelea kama Kamati, tulipata watalaam ambao wana weledi wa kutosha na walikuwa wakieleza kiundani juu ya utendaji kwenye mashirika ambayo yapo chini ya Wizara hii ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, lakini kipekee nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumteua na kumpa Wizara hiyo na anajua ana uwezo mzuri kwa sababu hakuna Wizara ambayo amekwenda akapwaya. Ninaamini ana makusudi ya kumpeleka Wizara hiyo kwa sababu kuna mambo ambayo anataka kuona yanakwenda. Ninajaribu kutafakari mara zote nikijaribu kuangalia baadhi ya Mawaziri, hakika Mheshimiwa Rais kwenye upande huu, Manaibu na Mawaziri wote ametutendea haki

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na *TTCL*. La kwanza, ningeshauri tuone ni jinsi gani tutaendelea kuwekeza *TTCL*. Kwa sababu tunajua miaka ya nyuma kila ukisikiliza taarifa ya *TTCL* ni hasara, lakini ni mikakati mizuri tu haikuwepo. Kwa jinsi walivyojipanga Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu na viongozi wote huko, wamejipanga vizuri, lakini tunatamani sana watoke hapo walipo waende zaidi kwa sababu wanaweza kwenda zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijaribu kusikiliza wataalam, nilipata nafasi siku ile ya kusikiliza walikuwa wakieleza mambo

mazuri ambayo wanaweza kuyafanya punde pale Serikali itakapowawezesha na kuhakikisha kwamba inawajengea uwezo. Ninafikiri tutengeneze nafasi kwa sababu *TTCL* ndiyo mtandao ambao kimsingi ni wa Watanzania *per se* kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukifanya kila juhudi ya kuwekeza, kutengeneza mitambo mizuri na kusimika minara ya kutosha, basi wale wengine wote watakuja kukodisha kule na tutapata fedha. Hata unaweza usiwe na simu, usiwe na nini lakini ukafanya uwekezaji mzuri wale wenzetu wa mitandao wakaja wakawekeza kule, tutapata fedha za kutosha na Serikali itapata kodi ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ninapata shida moja tu wakati mwingine Mheshimiwa Waziri na baadaye akihitimisha atatueleza labda vizuri, suala la wizi mitandaoni. Ni jambo ambalo tumezungumza sana na anakumbuka hata kwenye Kamati tumezungumza sana. Ninajiuliza hao wenzetu wenye mitandao hivi hawajui kadi walizo-*produce* kwenye taasisi labda *Vodacom, Tigo* na wengine, hawajui kadi walizonazo? Hawajui mkoa huu tumepeleka kadi ngapi? Hawajui wilaya hii tumepeleka watu gani wa kusajili watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajiuliza, ninajitafakarisha sana labda nao ni sehemu, mimi sina maana hiyo; lakini ni lazima Mheshimiwa Waziri aweke mguu chini na ninamwamini kwamba ataweka mguu chini huu wizi wa mitandao angalau upungue kwa asilimia kubwa kwa sababu umekuwa ni jambo ambalo linawaumiza Watanzania sana. Ukijaribu kuangalia; hata ukiangalia maeneo mengi Mheshimiwa Rais alisema anatamani kuwaachia Watanzania tabasamu na watu wakisikia anazungumza suala la tabasamu wanafikiri tunazungumza kwa sababu tunazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi sana yamezungumzwa hapa juu ya matumizi haya ya kadi. Unapoweka *bundle* unaambiwa *bundle* lako hili ni la siku saba. Bahati mbaya umeenda huko vijijini, umekaa *bundle* lile wanachukua. Mheshimiwa Waziri *bundle* ni hela, ni sawa unapokwenda sokoni kununua mboga au mahitaji, ukanunua

fedha zikabaki yule muuzaji akakwambia nipe na hizi kwa sababu zote ulishapangia matumizi wakati unakuja sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lazima tufike mahali kama ni sheria, sheria ibadilike. Ukienda kwenye tathmini ukafanya ulinganisho mtaani na kuuliza Watanzania wengi wanalalamika juu ya *bundle*. Mtu anakwambia unaenda kwenye mtandao fulani unasema bundle ya mwezi, *bundle* ya wiki mbili. Basi umenunua *bundle* la shilingi 20,000 hata haifiki nusu mwezi limekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri lazima akae chini na haya mashirika kuhakikisha suala la *bundle* la Watanzania kama hajatumia si hela yake? Kwa nini asiwekewe akaendelea kutumia? Kwa nini uchukue? Kwa sababu ndiyo sababu wao wanakuwa na tabia ya kusema tumetengeneza faida, lazima watengeneze faida. Kwa nini watengeneze faida? Si wanachukua hela yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri lazima kwenye hili aweke mguu chini na ndiyo sababu Mheshimiwa Rais amemleta hapo alete tabasamu kwa Watanzania kuhakikisha fedha zao za *bundle* hazichukuliwi jamani. Lazima hili tuzungumze. Ukizungumza huko mtaani wanakwambia *bundle* langu nimeweka la shilingi 2,000. Hebu niambie mwananchi pale Monduli au pale Mfereji, nikupe kata moja huko chini, amenunua *bundle* lake la shilingi 2,000, kuna mahali Mheshimiwa Waziri hakuna *network* amekaa huko amerudi kwenye *network* baada ya siku tatu anakuta *bundle* halipo, anatakiwa kununua nyingine tena. Ni vyema wakaweka mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekazia hapo kwa sababu ni jambo ambalo linawaumiza Watanzania wengi na mimi nimeendelea kusisitiza Mheshimiwa Rais amemleta Waziri makusudi hapa ili alete tabasamu kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Rais ya ufunguzi wa Bunge alitaja kabisa pale, ukienda kusoma kwamba lazima tuhakikishe tunajenga chuo. Ukisoma kwenye ilani na ukisoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kujenga uwezo

wa kufundisha watu kujua maana ya mtandao, kuwafundisha Watanzania na ile ni ajira. Tutakapowafundisha Watanzania wengi watapata ajira kwenye mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukitaka kitu chochote unaagiza kwenye mtandao, ukitaka nini unaagiza kwenye mtandao. Ni vyema tukahakikisha kwamba mitandao yetu hii tunakwenda kuwafundisha Watanzania wengi ili wafanye biashara. Waziri atengeneze chuo kama Mheshimiwa Rais alivyoi-*table* kwenye hotuba yake kwamba tunakwenda kujenga chuo kwa ajili ya kuwaelimisha Watanzania kujifunza suala la kimtandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, Wilaya yangu ina vijiji 63, vitongoji 236, tarafa tatu na kata 20. Mheshimiwa Waziri ninashukuru kwa sababu kuna mnara amenijengea kule Selela lakini kuna maeneo ambayo bado hayajafikiwa na minara hiyo. Kata ya Naalarami, Kata ya Mfereji, Kata ya Engaruka, Kata ya Mswakini na Kata ya Lemooti. Nimwombe, tupate minara ili Watanzania wafaidi matunda ya nchi yao kwa sababu watakapopata kazi hiyo ya kupiga simu wanafaidi matunda ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri la mwisho, ninajua muda umekwisha. Suala la *center,* pale tulifika na wataalam wakatueleza kinaga ubaga kwamba inafika mwisho mwisho. Tuiombe Serikali ipeleke fedha, ile ndiyo roho ya nchi yetu siyo mpaka i-*collapse* ndiyo sasa tuanze kutafuta fedha za kupeleka kwa ajili ya kufanya yale marekebisho. Niiombe Serikali wakati tunakwenda kwenye bajeti tuombe bajeti ya dharura tupeleke pale ili tutengeneze ile *center* yetu iwe salama kwa ajili ya masilahi ya nchi yetu na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na ninaunga mkono hoja kwa 100%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack Copriano, ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, Mheshimiwa Johnston Mutasingwa na Mheshimiwa Mgore Miraji wajindae.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwenye maandiko matakatifu Kitabu cha Ayubu 27:4 kinasema hivi: "Hakika midomo yangu haitanena yasiyo haki, wala ulimi wangu hautatamka udanganyifu." Ninaomba Mungu anisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini kipekee ninaomba niipongeze Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki. Hongera Mheshimiwa kwa kazi nzuri lakini hongera pia na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Menejimenti yote ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ripoti ambayo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha na nipende kwenye upande wa makusanyo wa mauzo kupitia Mkongo wa Taifa ambao wameweza kukusanya 133.4% mpaka kufikia mwezi Machi, 2026. Pia, wameweza kutandaza Mkongo wa Taifa kwa kilometa 15,167 kati ya 16,280 ambayo imefikisha 93% ya mtandao wa mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kuboresha mawasiliano nchini, mijini na vijijini, hali ambayo inaleta mfumo wa mawasiliano ya teknolojia ya kisasa kama yaliyokuwepo duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 10 Aprili, 2026 Mheshimiwa Rais alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa minara 758 pamoja na maunganisho ya mkongo wa mawasiliano katika wilaya 85 nchini. Ninaomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha anaitekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa kufikisha malengo hayo, lakini pia katika kuitekeleza kupitia mawasiliano nayo pia inaleta tija ya ajira, fursa za ajira kwa vijana ambapo Ilani ilikuwa inaelekeza kufikia mwaka 2030 basi ajira milioni 8.5 ziwe zimepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande huo wa kuleta mawasiliano hususani mawasiliano ya simu hizi za mikononi. Kuna

tatizo ambalo limejitokeza na tatizo hilo ni wizi wa mtandao. Wizi wa mtandao *(cyber-criminal)* na jinsi ya kuzuia. Kumekuwa na wimbi kubwa la wizi wa mitandao, lakini kwa upande mkubwa *TCRA* na Polisi wanajitahidi kudhibiti wizi huo wa mtandao kwa asilimia kubwa sana, lakini wizi huo bado unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutatua hali hiyo, ningeomba kwanza Wizara labda ingekabiliana katika hali ya usajili. Usajili huu ufanyike kwa kutumia *e-sim line* badala ya kutumia zile *physical line* kwa sababu usajili huu kwenye *physical line* wezi (*freelancers)* ambao ndiyo wanatumika sasa kufanya hiyo kazi wanasajili laini zaidi ya moja ndiyo inavyoonekana. Wanasajili laini zaidi ya moja na siyo kwa mlengwa ambaye amefuata huduma ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsi gani wanatumia? Wana njia nyingi za kutumia, lakini ninafikiri mojawapo huwa wanatumia sana eneo la kusema mtandao haupatikani. Sasa maelezo yao mtandao haupatikani wanaokwenda pale ni *innocent* hawaelewi kitu chochote, wazee pamoja na akina mama. Anaambiwa mtandao haupatikani yeye anakaa anasubiri kumbe wale wanasajili laini zaidi ya moja kwa jina la yule mlengwa. Kwa hiyo, sasa ninafikiri kwenye kusajili upande wa hii *e-sim* utasaidia, lakini wakati huo huo Serikali ina uwezo wa kuwaanzishia hawa wanaosajili vituo kama vile mawakala wa pesa badala ya kuwa wanarandaranda mitaani kusajili basi wawe na vituo maalum kufanya usajili ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hii inaonekana ndiyo inasababisha wizi mkubwa wa wa mtandaoni watu wanaibiwa sana. Sasa hivi dunia imekuwa kijiji kila kitu kinafanyika kwenye simu ya mkononi. Manunuzi yote yanafanyika kupitia simu za mikononi, hizo pesa zinakuwepo kwenye simu za mikononi, lakini ndiyo saa zote hizo pesa tunaibiwa. Unaambiwa tuma pesa, rusha pesa umekwenda dukani unataka kulipa pesa ile imekwishayeyuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri kwa kutumia njia hii, Serikali ikijipanga na kutekeleza kwa njia hiyo hapo ya kusajili kwanza kuwapatia vituo wale wanaosajili, lakini pia kutumia hizo *e-sim line*

badala ya zile *physical line* ninafikiri itakwenda kuokoa hili janga la wizi wa mitandaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali hususan kupitia *TTCL* kwa kusimamia uboreshaji wa Mkongo wa Taifa nchi nzima pamoja na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF)*. Ninaomba kuipongeza sana *TTCL*, lakini pia wakati huo huo ninaipongeza *TTCL* kwa kufanya kazi zake vizuri hasa kwa kufanya kazi kwa niaba ya Serikali kuhakikisha inapeleka mawasiliano katika maeneo tofauti lakini hasa kui-*cover* nchi nzima, lakini pia kupeleka nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa ninapenda kuwapongeza zaidi kwa kuja na huduma mpya ya teknolojia mpya wanaita ya *GPON* ambayo ni *Gigabit Passive Optic Network* ambayo inasambaza huduma nyingi kwa wakati mmoja na eneo moja, lakini pia mteja anapata huduma zaidi ya moja katika kutumia teknolojia hii hapa. Ninawapongeza sana *TTCL* waendelee kuchapa kazi, lakini waendelee kuwaletea Watanzania huduma hii. Pia, ninaomba kuwapongeza waendelee na kasi ya kusimamia mawasiliano hayo kupitia huo mkongo na kupeleka mawasiliano nje ya nchi kama ilivyo sasa wanavyoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau, ninaiomba pia Serikali iongeze kasi katika kuongeza zile *data center* ambayo *data center* ninafikiri iko Dar es Salaam, lakini kwenye ripoti ya Wizara inaeleza itajenga *data center* Dodoma pamoja na Zanzibar ambapo upembuzi yakinifu umeshafanyika. Kwa hiyo kasi ya kuanzisha au kujenga vituo vile ifanyike kwa haraka sana ili kuokoa gharama za umeme kupitia mitambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais maana amehakikisha analeta tabasamu kwa Watanzania wa mijini na vijijini, ili kuweza kutumia mawasiliano haya ya simu pamoja na *internet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaamini muda wangu nimeutumia vizuri. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Johnston Mutasingwa, Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera na Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, wajiandae.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru sana Mungu aliyetujalia afya njema na sasa tuko hapa tunaendelea na kipindi chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru sana Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Angela Kairuki, kwa kazi njema anayoifanya, pamoja na Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu. Ninawashukuru wataalam wote wa Wizara hii na wa taasisi zote kwa kweli, wanafanya kazi nzuri. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ninaweza nikasema ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu. Kwa sasa mambo mengi sana yanabadilika, kutoka kutumia *hardware*, inakuja kwenye *software*, njia ngumu zinakuja kwenye njia tuseme rahisi sana, ambazo ni *soft*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiweza kutimiza malengo ya Wizara hii, hasa Serikali, kwa kuipa pesa kutimiza miradi yake kwa wakati mambo mengi yataenda kufanyika vyema na kuwa ni taasisi ambayo inaisaidia Serikali sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi tukiya-*digitalise* kwenye mfumo wa *digital ways,* hata kukusanya kodi, hata kufanya kila kitu vilevile, tunaweza tukafanya kitu kikubwa sana ambacho kinaweza kikasaidia nchi yetu. Kwa mfano, sasa hivi Mheshimiwa Waziri wanaenda kufungua hii akaunti ya uchumi wa kidijitali *(DESA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *DESA* ni kitu kizuri sana Wizara ikikifanya kwa wakati na tukaendana na nchi nyingine, kama zinavyofanya. Kwa sasa tuko chini sana, lakini *DESA* itasaidia sehemu moja muhimu ambayo Serikali na nchi nyingine zinatumia. Umuhimu mkubwa wa *DESA* ni kukusanya data,

takwimu na kama tutaweza kukusanya takwimu sahihi, tutakwenda kufanya maamuzi sahihi katika sekta zetu, lakini *DESA* inaweza ikawa kipimo cha kupima hata taasisi na Wizara nyingine zinafanyaje kazi, zimepata nini. Hata kwenye kutunga sera zetu, tutatunga kwa *data* ambazo ni sahihi na hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwa na *data* sahihi utafanya mambo sahihi. Hata bajeti yetu inategemea sana *population, population* ni *data* ambazo tunazo. Kwa hiyo, ninaomba sana kuhakikisha hii *DESA* tunaipa kipaumbele na umuhimu wake wote utakaokwenda kufanya kazi kwenye kujua uchumi wetu, *GDP* yetu, inapandaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajua kwenye sera zetu tunazipandaje. Tutajua kubaini fursa za uwekezaji, vyote hivi tutaweza kuvijua na kuvifanyia kazi, kama tutaimarisha *DESA* na kukahakikisha inafanya kazi *effectively*. Kwa hiyo, nawaomba sana. Hii *DESA* iende sambamba, Mheshimiwa Waziri ninashauri hapa sasa hivi, twende tunahama kwenye mfumo hata wa kuanza baadhi ya miji kwa kuanza kununua vitu kwa kadi, za kuchanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya jambo hili tutaokoa kodi nyingi sana za Serikali, itaisaidia sana hata Serikali kukusanya mapato makubwa. Nchi zilizoendelea watu wameacha kununua vitu sokoni kwa kwenda na pesa mkononi, lakini mtu akiwa na kadi anaweza akachanja sehemu kununua mchicha, Serikali inapata kodi yake stahiki kwa wakati. Hii tunaweza tukatoa mikoa au wilaya chache tukafanya utafiti, tukaona hili suala linaweza likasaidiaje katika ukusanyaji wa kodi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara kwa kuongeza minara, wameweka minara mingi sana, kwa hili ninamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa kwenye minara. Vijijini saa hizi kila mtu anaperuzi na simu yake. Sasa tumeweka minara sehemu ambazo kuna makazi ya watu, lakini ninavyoelewa mawasiliano ni usalama, mawasiliano ni ulinzi, mawasiliano ni uokozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipata pancha huko porini ni rahisi kumfikia mtu akaja kukufuata, akakusaidia. Sasa ninaomba twende *along the road, trunk roads* zote, tuhakikishe mitandao inapatikana mtu anapokuwa kwenye basi. Kutoka eneo A kwenda eneo lingine tuhakikishe njia nzima unapatikana mtandao. Kwa mfano, sisi kwetu kule Kagera, mtu akitoka Karagwe kwenda Benako kuna Pori la Kimisi, katikati pale hakuna mtandao huwa unakata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tujitahidi hata maeneo ambako magari yanapita, tuweze kuona kama tunaweza kuweka mitandao ikasaidia watu, lakini hata sisi tunapokuwa tunatoka Bukoba kwenda Mwanza kwenye meli, kuna sehemu hapa katikati mitandao huwa inakata kwa hiyo, tujitahidi. Maeneo kama hayo, inaweza ikatumika kama sehemu ya uokozi, kama tatizo litatokea mtu akafanya mawasiliano ni rahisi sana kuja kuokolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimoja kizuri sana kinaitwa *Cyber* Mlangoni. Hiki kitu naomba mkitangaze sana, ili watu muwapelekee mkongo mlangoni na kuwaelewesha ina faida gani, tangazeni fursa mlizonazo, hii itaongeza uchumi na itasaidia. Ukiangalia vijana wengi sana sasa hivi wamemaliza shule, wako nyumbani, kila kitu hata mikopo ya Serikali inatangazwa kwenye *internet*. Sasa tuwasaidie vijana na watu wengine kwa kuwapelekea mkongo mlangoni, itasaidia sana. Moja, utamsaidia yule, lakini utatusaidia na sisi kuongeza mapato katika Wizara yetu, ila ninawashukuru sana, pale kwetu Bukoba Mjini maeneo ya Kashai, wametuwekea *Wi-Fi* kwenye soko na Rwamishenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ni zuri sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu, kuna vijana wamemaliza shule, lakini mtu hawezi kununua bando la shilingi 2,000. Wakiweka hivi vituo au *center* za *Wi-Fi* mtu anakuwa na 500 yake, anaweza kujua nini cha kufanya na ikamsaidia, ile 500 ya bei nafuu ya *TTCL*. Kwa hiyo, ninawaomba maeneo mengi sana waende wanaweka hivyo vifaa, hasa vijijini. Aende kwetu Kanazi Kijijini kule, wawekee; kuna vijana, kuna mtoto wa mkulima amemaliza shule amerudi kijijini, hawezi kabisa kununua bando, lakini anahitaji ajira kwa hiyo,

ninaomba Wizara hii iwe mkombozi kwa vijana, sisi ambao tumetoka vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya. Ombi langu ni, Serikali itoe pesa kwa miradi yenu waliyonayo, ili waweze kuitekeleza kwa wakati na kuboresha vituo vyetu vya *data centre;* kununua vifaa vya kisasa tuendane na hali ilivyo ya kiuchumi, ya kitaaluma na mambo yanavyozidi kubadilika. Hii Wizara ndiyo inaweza kabisa kuunganisha taasisi zote zikasomana. Wawe na mfumo mmoja, nenda *TANROADS, TRA, TARURA*, Maliasili, kote, tuna wataalam wazuri, vijana wengi sana wazuri wanasoma *TEHAMA,* tuwatumie hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiwatumia, watatusaidia kuunganisha mifumo yetu. Tutatoka kwenye kuwa na mifumo mingi. Kwa mfano, saa hizi unaweza ukakuta mtu anaenda kulipia gari, atalipa kodi kama nane. Kwa nini tusiende kwa *TEHAMA?* Kwa kutumia mfumo wenu, mtu akalipa kodi moja ya gari halafu tukawa na *system* ndani inayosambaza kodi kwenye taasisi zingine kuliko mtu kwenda analipa huku, anaenda huku analipa? Tukifanya hivyo, tutafanya biashara zetu kwa usahihi na uharaka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo yote, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tumpitishie Mheshimiwa Waziri bajeti yake kwa kishindo, ili aende akatimize majukumu yake na kulitumikia Taifa. Baada ya kusema hayo, ninaunga hoja mkono na Mungu awabariki sana. Ahsanteni.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mutasingwa. Nilimtaja Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mheshimiwa Said Ali Mbarouk na Mheshimiwa *Eng*. Mwanaisha Ulenge, ajiandae.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu kwenye Taifa letu. Kwanza kabisa ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuchagulia wawakilishi na viongozi wazuri ambao ni Waziri wetu Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki na Naibu wake Mheshimiwa Switbert Mkama pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano Mohammed

Abdulla. Wamefanya kazi kubwa na nzuri ambayo inaweza kuonekana na kusaidia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni mashahidi, sasa hivi duniani kote teknolojia ndiyo inayoshika kasi. Ninaomba niweze kuwakumbusha, tarehe 29 Oktoba, Wizara ya Mawasiliano na Habari ndio imeweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kujua nini ambacho kinaenda kufanyika katika Taifa letu. Wizara hii imeweza ku-*monitor,* kuzuia na kupunguza athari kubwa ambazo zingeweza kuendelea kutokea. Hivyo ninawaomba Waheshimiwa Wabunge tuungane kwa pamoja kuendelea kuishauri Serikali na kupitisha bajeti hii, ili Wizara ikaendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuongelea Shirika letu hili la *TTCL. TTCL* imekuwa inafanya vizuri sana na hapa ninamwomba Waziri wa Mawasiliano aweke jicho lake haswa, *TTCL* ijiendeshe kibiashara. Tuna mitandao mingi sana ya simu; tunayo *Vodacom*, tunayo *YASS*, tunayo *Airtel*, tunayo *Zantel,* tunayo *Halotel.* Wenzetu wamekuwa wanafanya vizuri na wanapata faida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi, *TTCL*, tulenge kujiendesha kibiashara, ili tuweze kutoka hapa tuende mbele. *TTCL* imeweza kufanya vizuri kwa kuja na *product* nzuri ya *Fiber* Mlangoni. *Fiber* Mlangoni kuunga ni shilingi elfu hamsini na tano, unatumia mwezi mzima, familia nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kidijitali sasa hivi, watoto wetu wanasoma kupitia mitandao, wanatumia *internet.* Kazi zinafanyika kupitia *internet.* Hata Serikali wakitangaza *tender NeST*, ni internet inatumika. Hivyo basi, kwa kupitia *Fibe*r Mlangoni tunaweza kufanya kazi nzuri sana. Changamoto inakuja huko kwetu vijijini, watu hawajui kitu kinaitwa *Fiber* Mlangoni. Tufanye matangazo, kama wenzetu wanavyofanya matangazo, biashara yoyote ile ni *advertisement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunayo hapa *SGR station* yetu, ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Twende tukaweke *advertisements* pale, *billboards* zioneshe, "Tuna *TTCL Fiber* Mlangoni. Tuna *TTCL*

*Fiber* Mlangoni, *Triple Hub,* ili watu waweze ku-*join* na kufanya vizuri."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wametoka kuchangia kuhusiana na vifurushi. Unajiunga kifurushi cha *Vodacom* bando la shilingi elfu kumi siku saba, lakini siku mbili limeisha. Ila ukiwa na *TTCL Fiber* Mlangoni, elfu hamsini na tano, ukiweka *Triple hub* elfu sabini na tano, unatumia mwezi mzima. Hivyo, ninaomba tuwaeleweshe wananchi wetu, tufanye matangazo, tufanye *promotion* za kutosha, ili tuweze kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapahapa tuna Shirika letu la Posta, ni kama shirika ambalo limesahaulika. Posta inafanya vizuri sana, lakini ninaomba Serikali iliwezeshe Shirika la Posta, ili liweze na lenyewe kujitangaza, wananchi wajue kwamba, Posta ipo na inatoa huduma gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ndugu zetu wako vijijini huko Musoma, Nyakatende huko, mtu hajui biashara ya kutuma mizigo sijui kwenye jamvi wala wapi, wamesahau habari ya Posta. Ninaomba Mheshimiwa Waziri, hili walishikie kidedea, warudi kutangaza kwamba, Shirika la Posta lipo, linafanya kazi nzuri na linatuma *parcel*. Tunaona mfano mzuri *DHL* wana-*deliver* mizigo vizuri na wanafanya biashara yao, wanaingiza fedha nyingi sana. *Why not* Posta isifanye hivyo? Ninawaomba tuwa-*motivate* na kuwasaidia, Posta, waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niweze kuchangia kwenye suala la *TCRA*. Katika kipindi Taifa letu lipo kwenye janga ni kipindi hiki, watu wanadhalilisha watu kupitia mitandao kwa kiasi kikubwa sana. Mtu anachukua kichwa cha Mheshimiwa Mgore, huku chini anaweka kitu kingine, halafu *sometimes* unakuta hata nguo hakuna! Mtu akiangalia anajua huyo ni Mheshimiwa Mgore, lakini *TCRA* wapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TCRA* ninaendelea kuwaomba na kuwasisitiza, tujitahidi ku-*coordinate* pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani, ili adhabu kali ziweze kutolewa na sheria kali ziwekwe kwa watu ambao wanatumia hii mitandao vibaya. Mtu anatukana viongozi wa Serikali, mtu anadhalilisha mtu, lakini

hakuna hatua zinazochukuliwa, wote wanachukulia *business as usual,* lakini tuki-*stick* vizuri ku-*coordinate* kati ya *TCRA* na Wizara ya Mambo ya Ndani na hatua kali zikachukuliwa, kama siyo kumaliza, tutaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa sana huu wizi wa mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Waziri, hapa wengi wetu wamesafiri kwenda nje, hata Kenya tu hapa karibu, ukienda kupata laini ya simu ni kazi. Utafanya *roaming* ya simu yako ama utatumia *internet* peke yake. Kwa nini Tanzania mtu mmoja unamkuta ana laini 10, anazipatapataje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ondoka hapa nenda *USA*, laini ni hiyohiyo moja, kama huwezi kutumia *internet* utaazima simu ya mwenyeji wako. Ninawaomba Wizara ya Mawasiliano hili waliangalie kwa jicho la tatu, ili kuhakikisha mtu *at least maximum* ya kuwa na laini ni mbili ama tatu. Mtu una laini 10 unafanya biashara gani? Ndiyo maana watu wanakuwa wakidhalilishwa, wanatukanwa kwa sababu, laini za simu zinapatikana hovyohovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kupongeza Wizara ya Mawasiliano, ninawapongeza kwa kiasi kikubwa sana. Wameonesha ni namna gani wanataka kujiendesha sasa kibiashara. Wameweza kuvuka lengo katika ukusanyaji wa mapato yenu, toka shilingi bilioni 120.3 mlizokusudia mpaka shilingi bilioni 149.2. Wameweza kuongeza watumiaji wa mtandao wa *TTCL* kutoka 66% mpaka 88%. Hiyo ni *improvement* kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Serikali yangu sikivu chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wawawezeshe hawa Wizara ya mawasiliano, ili waendelee kufanya vizuri kazi yao, kwa weledi. Bajeti hii waliyoiomba iweze kupitishwa kwa sababu, nchi yetu inategemea mawasiliano kuliko chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ukiongelea mambo ya kufanya *tendering* ya kazi, sasa hivi ukienda kwenye hospitali zetu, tunatumia mambo ya *digital*, yote ni mawasiliano. Bila kuwa na mawasiliano hatuwezi kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa *TANROADS*, watu wa *TARURA,* watu wa Uchukuzi; hapa ukitaka kukata tiketi ya *SGR* lazima utatumia mtandao hivyo, mawasiliano ndiyo kitovu cha nchi yetu. Mawasiliano ambayo wanaendelea kufanya, Wizara hii ya mawasiliano, yanaendelea kutuonesha kwamba, sasa hivi Tanzania tunaendelea kupiga hatua. Hapa ninaendelea kuwapongeza kwa minara 758 ambayo imeweza kujengwa na kuzinduliwa, ili hata huko vijijini watu waweze kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga hoja hii mkono na Waheshimiwa Wabunge tupitishe bajeti hii, ili Waziri wa Mawasiliano aweze kufanya kazi yake vizuri. Aendelee kulinda nchi yetu na kusimamia Taifa letu kwa weledi unaotakiwa. Ahsanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngore Miraji Kigera. Nilimtaja Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge na Mheshimiwa Zeyana Abdallah Hamid, wajiandae.

**MHE. SAID ALI MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi na uzima kuweza kuchangia machache sana katika bajeti ya Wizara hii muhimu sana ya Mawasiliano. Wizara hii, kama walivyosema wenzangu wengine wengi, ndiyo Wizara muhimu sana katika maendeleo ya nchi. *Internet* leo siyo anasa, ni jambo muhimu sana katika maendeleo ya uchumi wa nchi, kwenye maisha kwa wananchi, kwa nchi mbalimbali na kwamba, umuhimu wake katika nchi, wenzetu wanazipima nchi kwa namna ambavyo *internet* ziko madhubuti katika nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi Taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunapaswa kuwa tunaongoza katika kanda na katika Bara la Afrika. Sasa ninaomba sana jitihada ifanywe kufika huko. Bahati mbaya hali ilivyo sasa si hivyo; kwamba, wanapotu-*rate*, wanapotuweka katika viwango, tunaonekana tunapitwa na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu mmoja amesema mchana hapa, Kenya wako mbele, Nchi ya Rwanda nayo

inatupita, tunaambiwa hata Uganda watu tuliwasaidia kujikomboa, lakini katika hili wako mbele, sasa hii siyo hali nzuri. Ukiangalia Afrika zaidi, utaona katika *top ten*, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatuonekani kama tupo. Ombi langu ni kwamba Serikali Waziri na Msaidizi wake Naibu Waziri isaidie kupiga hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo litawezekana kibajeti, lazima Wizara hii isaidiwe kibajeti, vinginevyo tutakuwa tunafanya siasa kubwa lakini *in reality* hatuko. Katika bajeti, kitabu cha Waziri, nilikuwa nikimsikiliza sana mchana hapa alivyokuwa anasoma, hilo linathibitishwa katika *paragraph* ya 42, *page* ya 15 ya kitabu chake Mheshimiwa Waziri. Mwaka jana 2025/2026 bajeti ya maendeleo ilikuwa shilingi 277,047,483,000, lakini mwaka huu Waziri anatuomba tumuidhinishie bajeti ya maendeleo ya shilingi 209,443,277,000. Maana yake ni nini? Amepunguza bajeti ya maendeleo kwa shilingi 67,000,000,000, sasa sidhani kwamba Serikali iko makini na hili suala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sisi tunapitwa na nchi jirani katika suala la *strength of internet* na mambo mengine, sisi tunapunguza bajeti ya maendeleo. Nilidhani Waziri angesaidiwa kuongeza bajeti ya maendeleo kuliko ile ambayo alikuwa nayo mwaka jana. Ningetegemea angeongezewa bajeti ya maendeleo angalau shingi 100,000,000,000 zaidi ili kumsaidia Rais Samia katika lile lengo la kuongeza masuala ya *internet* na mawasiliano katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisikiliza wakati wa maswali asubuhi, Wabunge wengi wanazungumzia na wanaomba kujengewa minara katika Majimbo yao na katika maeneo yao ili wananchi wao waweze kufaidika na masuala ya *ICT* na mambo mengine, sasa bajeti ya maendeleo mwaka huu imepunguzwa kwa shilingi 67,000,000,000. Ninaomba akija Waziri hapa atueleze ni sababu zipi kama yeye mwenyewe ameomba au Serikali imemlazimisha kupunguza bajeti ya maendeleo katika suala hili muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nimeliona na ningeomba pia maelezo ya Wizara ni *TCRA* imepanga kukusanya

shilingi 285,400,000,000, jambo zuri sana. Hata hivyo, lile ambalo wamelipanga kwa shughuli za maendeleo ni shilingi 49,450,000,000. Maana yake ni nini? *Only twenty percent* ya bajeti ambayo imepangwa kukusanywa ndiyo inakwenda katika shughuli za maendeleo, 80% inakwenda katika shughuli za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu siyo utaratibu mzuri wa kusimamia mashirika, Mashirika yanapaswa angalau 30% ndiyo iende, angalau ikizidi hapo itakuwa ni bora zaidi, lakini kama unakusanya shilingi 235,000,000,000 na kwa ajili ya maendeleo unawekeza shilingi 49,000,000,000, huo siyo utaratibu mzuri na ninaomba Mheshimiwa Waziri hili alisimamie vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Zanzibar tungetarajia kwamba *TCRA* ibane matumizi kidogo, iwekeze katika fungu la maendeleo ili na sisi tupate mgawo mzuri kutokana na kile ambacho wameki-*save,* lakini sasa kama wanaweka 20% tu katika suala la maendeleo, ni suala ambalo lina mtihani kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaomba nilitilie mkazo, wenzangu wengi wamelizungumza na hili niliwahi kulizungumza Zanzibar. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu - Zanzibar, sasa hili nilihoji nikaambiwa aah! Wewe Mbunge nenda ukalihoji Bungeni. Kwa hiyo, ninaomba nipate nafasi kidogo nilizungumze, wenzangu wengi wamelizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala lile ambalo mwananchi wa kawaida wa kijijini, mimi ninatoka Jimbo la Gando, ananunua vocha ya shilingi 2,000, ananunua bando la shilingi 2,000 anategemea atumie kwa muda wa wiki moja. Sasa kwa sababu ya *fluctuation* ya *internet* na mambo mengine, hapati huduma, ametumia labda asilimia hamsini ya vocha yake au bando yake, baada ya wiki anaambiwa imeisha. Sasa hili linaathiri Watanzania wengi Bara na Visiwani. Jambo hili linasababisha wananchi wetu wapoteze pesa nyingi na wanaofaidika ni makampuni ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali isikubali kuona kwamba wananchi wake wanapata hasara na wanaofaidika ni makampuni ya simu *billions* kwa mwaka, nina uhakika, nimefanya

mahesabu kidogo, lakini ni mabilioni ya shilingi wananchi wanapunjwa wanaofaidika ni makampuni ya simu. Sasa hapa ni lazima kuwe na sera, kuwe na mwongozo na kuwe na utaratibu ambao wananchi wetu wanyonge hawatapunjwa, hawatadhulumiwa pesa zao katika matumizi ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, leo sitaki niseme sana, ni suala la sekta ya habari na sekta ya mawasiliano. Hapa waandishi wa habari wanasimamiwa na Wizara ya Habari, lakini wakati huo huo huduma nyingi wanazipata *TCRA* ambayo iko chini ya Wizara ya Ndugu yangu Mheshimiwa Angellah. Sasa kunakuwa na matatizo, huku kuna miongozo na huku kuna miongozo mingine. Kuna wakati wanapata adhabu za *TCRA* ambazo kwa kweli zina matatizo. Ninaomba Serikali iangalie kama kuna uwezekano wa kuunganisha mambo haya ya maudhui na huduma za Wizara ya Habari, ingewasaidia sana watu wetu wa sekta ya habari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, pia utaratibu wa *TCRA* wa kuadhibu kidogo uwe suala la kuwafundisha zaidi na kuwapa taaluma kuliko kuwa na bakora ya kuadhibu kidogo, tutapoteza watu, watu wana familia wamewekeza pale, ndiyo kazi yao, ukifungia chombo cha habari maana yake unasababisha wananchi wetu wapate matatizo mbalimbali ya maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nizungumze hayo na mwisho kabisa ninaomba sana suala la mgao wa fedha zinazotokana na sekta ya mawasiliano baina ya nchi hizi mbili, baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, liwekwe vizuri ili na Zanzibar tupige hatua kubwa katika masuala haya ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa muda wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Said Ali Mbarouk. Nilimwita Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid na baadaye ajiandae Mheshimiwa Simai Mohammed Said.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Ninamshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa jioni ya leo. Kipekee pia ninachukua fursa hii kuipongeza Serikali yetu ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri inayofanya katika sekta hii ya mawasiliano na teknolojia ya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kwa hakika ku-*make it very clear*, dada yangu Angellah Kairuki, wewe ni mfano halisi wa *beauty with brain*. Sijawahi kuona mahali ambapo umewekwa na ukacheza chini ya viwango, unatupa fahari kubwa wanawake, ndugu zako tunaokuangalia endelea kuchapa kazi. Vilevile, ninawapongeza Watendaji kwa kazi kubwa na nzuri wanazofanya kuhakikisha Taifa letu linakwenda kunufaika na uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee niseme wazi hapa, Tume ya TEHAMA inafanya kazi nzuri kwa kweli, ukilinganisha na Bodi ya Wahandisi na ninamwona pale Mheshimiwa Ulega ananisikiliza, Tume ya TEHAMA ni changa sana nchini lakini leo ina kongamano la 10 la Tume ya TEHAMA Nchini. Inawaandaa wataalam wa ki-TEHAMA kwa ajili ya *emerging technologies* lakini Bodi ya Wahandisi haijajipanga kisawasawa kuhakikisha kwamba Taifa letu tunakwenda kwenye Dira ya 2050 na miradi ya kimkakati ipo mingi, lakini bado tunacheza chini ya viwango. Ninaipongeza sana Tume ya TEHAMA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza sana vilevile, Serikali kwa kazi kubwa inayofanya kwa kuanzisha *initiatives* mbalimbali ambazo zinapelekea twende kwenye kuhakikisha tunakwenda kwenye uchumi wa kidijitali. Nimeona mikakati ile ya 2024-2030. Ninawapongeza sana kwa hatua mbalimbali ambazo wamechukua ikiwemo uwepo wa hiyo *data centre* kwa maana ya kituo cha ulinzi wa taarifa, vilevile, kuanzishwa kwa sheria ile ya mwaka 2022 ya taarifa binafsi. Vilevile, kwa kuwepo kwa sheria ya mwaka 2015 ya *cyber security*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubali, roho ya uchumi wa kidijitali ni taarifa. Ninaiona changamoto kubwa mbele yetu

ya *misinformation* na *disinformation*. Kumekuwa na wimbi kubwa la upotoshaji wa maudhui, kumekuwa na wimbi kubwa la kuenezwa taarifa za uzushi nchini kupitia *online platforms*, majukwaa ya kimtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *TCRA* kuondosha tu maudhui mitandaoni haitoshi, ni lazima twende katika mkakati wa kuhakikisha *online platforms* zinakuwa *held responsible whenever* kunapokuwa na maudhui ambayo ni hatarishi, maudhui ambayo yanachochea chuki, maudhui ambayo yanaleta mgongano katika Taifa letu. Tunaomba hili lifanyike sasa hivi, tunahitaji Tanzania yetu iendelee kuwa nchi na kisiwa cha amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu *emerging technologies* kama hiyo *artificial intelligence* inachangia mno, mno katika kuhakikisha kunakuwa na upotoshaji wa habari. Tunaomba sasa waje na miongozo, *ethical guidelines to prevent misuse* ya *artificial intelligence* nchini. Bila kuweka miongozo Taifa letu hatuta-*realize* maendeleo ya uchumi wa kidijitali. Tunaomba sasa Serikali iweke mikakati mahsusi na ifanye hivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kitengo cha *cyber security* kipo, lakini *cyber security* iongezewe nguvu, kuwepo na dawati maalum ambalo litahusika na suala zima la kushughulikia upotoshwaji wa habari na uenezwaji wa habari za kizushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli tunashuhudia hata nchi za Ulaya haya mambo yanatokea, lakini wenzetu wamepiga hatua. Nimeona Tume ya Umoja wa Ulaya mwaka huu 2026 wameanzisha *Digital Services Act* ambayo ni sheria mahsusi kabisa ya kuhakikisha mitandao ya kijamii inakuwa *held responsible*. *Twitter* au *X* ni miongoni mwa mtandao ambao umeshtakiwa na Tume ya Umoja wa Ulaya kwa kuruhusu maudhui ambayo yanaleta uchonganishi na maudhui ya kizushi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiruhusu jambo hili kuna watu ambao siyo *genuine*, watu wa hovyo wanaonekana kama watu wa maana sana kwenye Taifa hili kwa sababu tu wameshikilia mitandao ya kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakwenda kulifanya Taifa hili watu wa maana sana wakisimama waonekane siyo wa maana kwa sababu hatuwezi ku-*held responsible online platforms* ambazo zinaleta habari za uzushi, habari za uchonganishi na kufanya mambo ambayo kwa kweli yanapelekea hatari kubwa kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia hasara ambayo Taifa limeingia, angalia migongano ambayo Taifa limeingia, yote ni kwa sababu ya majukwaa ya kijamii ambayo hayapati kushughulikiwa ipasavyo. Tunaomba sasa, ni wakati sahihi Serikali wasimamie jambo hili liweze kutokea. Tunatamani kuona mtandao fulani sasa umewajibishwa kwa ajili ya kuleta taarifa chonganishi na kwa ajili ya kuleta migongano katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile niseme, tumeanzisha kituo cha kulinda *data* nchini. Kituo kile kiukweli tunajitahidi katika Afrika kinakuwa kama cha sita hivi, lakini bado idadi ya vituo ni vichache. South Africa inaongoza Afrika nzima, vituo vile ni vingi sana. Sisi tuna vituo *almost* 10 au 11, tunatamani kama Taifa tunapoelekea kwenye uchumi wa kidijitali vituo hivi viongezwe. Tunahitaji viongezwe na hatimaye tuwe na *National Data Centre*, kituo cha kitaifa ambacho kitakuwa ni *backup* ya vituo vingine vyote ambavyo vipo nchini. Jambo hili lifanyike ili Taifa letu liende kunufaika na uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mkoa wa Tanga tunashukuru sana, kwa kuhakikisha tumepata minara, kule Kwekivu, Kilindi kulikuwa na changamoto kubwa sana, lakini tumenufaika. Tunaomba sasa watuweke katika mkakati wa kuhakikisha kule Rwande tunapata na kule Saunyi tunapata. Kuna hali ngumu ya kimtandao kwa kweli. Tunaomba sana Serikali watuangalie katika jicho la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Tanga Mjini vilevile,kilianzishwa kile kituo cha *ICT Hub* ambapo vijana wa Tanga Mjini na wenyewe watapata fursa ya kuweza kufanya zile *startups* na kuweza kushiriki kwenye uchumi wa kidijitali ipasavyo. Tunaomba sasa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hoja yake, tusikie kituo kile

pale Tanga Mjini kimefikia wapi? Tunahitaji kujua, tuone vijana wa Tanga sasa na wenyewe wakishiriki katika kutengeneza vifaa ya kidijitali na vitu vingine vinavyohusika kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Eng*. Mwanaisha Ulenge. Nilimtaja Mheshimiwa Zeyana Abdallah Hamid, Mheshimiwa Simai Mohammed Said na Mheshimiwa Alan Thomas Mvano wajiandae.

**MHE. ZEYANA ABDALLAH HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa wasilisho tulilolipata leo kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ninaipongeza sana Wizara pamoja na Kamati kwa kutuletea mapendekezo haya ya bajeti na ninaomba nichangie bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utangulizi ninaomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono yake kwenye sekta hii ya TEHAMA kiasi ambacho tumeishuhudia ikiwa imetekelezwa kwa ufanisi mkubwa sana kipindi cha ilani na maono yanayoendelea sasa hivi kupitia *Vision 2050* tunaona Tanzania inakwenda kabisa kwenye uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza sana Wizara ya Mawasiliano chini ya uongozi wa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki na ninapongeza sana kwa kutupeleka kinaga ubaga kwenye hatua baada ya hatua. Leo nitapenda kuchangia yale ambayo kwa haraka haraka nimeona ni mafanikio makubwa ambayo tunahitaji kuyaongezea nguvu na kuiombea Wizara hii ipewe bajeti inayoelekeza utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mafanikio yaliyoonekana kwenye kuongezeka kwa minara. Minara hii imekwenda ku-*cover* Kata nyingi sana Tanzania. Tumeona mafanikio kama haya kwenye maji, kwenye umeme, lakini mafanikio tunayoyaona leo kwenye hii minara yanatuambia kwamba Tanzania iko tayari

kwenye *infrastructure* ya kuweza kufanikisha yale ambayo tulikuwa tunayadhania Tanzania ya kidijitali ije kutupa. muunganiko wa vijiji na miji ni kitu muhimu sana katika kuleta *coverage* ya kimtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona namna Mkongo wa Taifa unavyokwenda kuleta ile *backbone* ya *digital infrastructure* na kuenea kwa *internet*. Matumizi ya *internet* tumeona kutokana na *data* zilizonyeshwa watumiaji wameongezeka kwa 23%. Matumizi ya uchumi wa kidijitali yamekuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kata ambazo zinaendelea na kuimarika kwa 73% ni kuonyesha kabisa Wizara imejipanga kumaliza tatizo la upatikanaji wa *internet* mahsusi inayohitajika kwenye uchumi wa kidijitali. Tumeona namna Wizara imejipanga katika usalama, ishu za udhibiti na usalama wa huduma pamoja na kuelekeza nchi kwenye maendeleo ya uchumi wa kidijitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia tuyaangalie mafanikio haya katika kunyanyua sekta mbalimbali. Inaonekana wazi kabisa mafanikio ya Wizara ya TEHAMA yanatuwezesha katika sekta za kilimo, sekta za usafiri na namna ambavyo uchukuzi na sisi tunaona mifano mbalimbali tunavyobadilika kimatumizi na *internet* inavyoendelea kutumika kwa kasi kubwa kuleta maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia tuyaangalie mafanikio haya katika kunyanyua sekta mbalimbali. Inaonekana wazi kabisa kuwa mafanikio ya Wizara ya TEHAMA yanatuwezesha katika sekta za kilimo na sekta ya usafiri. Sisi tunaona mifano mbalimbali ya namna tunavyobadilika kimatumizi na *internet* inavyoendelea kutumika kwa kasi kubwa kuleta maendeleo ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa sekta ya TEHAMA ni marafudu; na Wizara imetuionesha kinagaubaga; kutoka asilimia saba kwenda 14%. Hizi ni pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wetu ambaye ametuonesha kwamba njia ya kutoka kimaisha

ni kwenda kwenye uchumi wa kidigitali na Wizara haijaliangusha hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanahitaji shilingi milioni 111, ambalo ni ongezeko kubwa sana la matumizi na kuimarika. Kwa mfano Mradi mzima wa *Digital Tanzania* tunaendelea kutazama mafanikio yake. Ubunifu huu umepelekea uanzishwaji wa *startups*, *startups* ambazo sisi pia tunazitegemea kuzishusha katika vyuo na vyuo vikuu. Wabunifu wadogowadogo nao wamekwenda kufuata mkondo wa kitaifa kwenye ubunifu ambao unakwenda kuwa *applied* kwenye sekta za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachoendelea sasa tunakiona kina *unfold* ni uchochezi wa teknolojia hii. Kwa maana hiyo basi, kuna kila haki ya kuipa nguvu Wizara hii kwa sababu uchochezi huu ndiyo ambao unakwenda ku-*cover* sekta zote kwa wakati mmoja. Mafanikio yanajibu *investment* ambayo inafanyika kwenye habari, na habari ni *capital*. Inakuja kutupa sisi *power*, inakuja kutupa *decision making,* inatuepusha kufanya hasara. Kwa sababu tumezoea saa nyingine tunafanya kwa kujaribu, lakini data ndizo ambazo zinatupa uhakika wapi pa ku-*invest*, vipi vya ku-*invest* na kiasi gani cha ku-*invest*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kugusa moja kwa moja kwenye kipengele cha akili mnemba *(artificial intelligence)*. Wizara imetushika mkono leo kutuonesha na wao wamejipanga vipi kwenye akili mnemba. Dunia nzima inaangalia akili mnemba kwa namna ambayo *parliaments* nazo zitasaidia kuhakikisha kwamba nchi zinapita sambamba na *development* ya *AI*. *AI has been very fast* namna inavyotengenezwa, *so fast* kiasi ambacho hata akili ya binadamu inashindwa kuifukuzia namna inavyo-*unfold*, namna inavyotumika, namna tunavyoweza kujilinda au kuzilinda taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *speed* kama hii tunategemea sana wizara iweze kuwezeshwa kwenda sambamba na kidunia kwa namna ambavyo nchi inabaki kuwa salama, nchi inaweza kushika maendeleo. Kwa kasi sana kuliko uwezo wa binadamu kuweza ku-*interpret*, inamaanisha nini maendeleo yanayoendelea. Sipendi kuhisi kama yanatupita,

lakini tayari ukiangalia kwenye *development* zilizokuwepo ndani ya nchi, ndani ya vyuo, tunakwenda nazo sambamba. *AI* sasa hivi Tanzania inatumika katika namna tofauti, *projects* za wanafunzi zinaonesha kwamba tayari inafundishwa katika viwango hivyohivyo vya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichopenda kwenye mchango huu wa leo ninaomba nikiwasilishe ni kwamba tunajikita kuitengeneza *AI* ya Kiswahili, *AI* ya Kiswahili si tu kuwa fahari ya Kiswahili na sisi ni Watanzania, lakini hii ndiyo nyenzo jumuishi kwa Watanzania walio wengi. Sisi ni Waswahili lakini kuna watu ambao wana miradi mizuri yenye maendeleo, lakini kikwazo cha lugha kinawafanya washindwe kuitumia teknolojia hii ya habari ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, wanapotuwekea *large language modules* za Kiswahili, wanatuambia Mtanzania yeyote ama kasoma, hajasoma, yupo mjini, yupo vijijini, *as long as* ana mradi mkubwa, mdogo, ataweza kutumia taarifa hizi ambazo wanasayansi wanazichakata katika lugha tofauti, Watanzania watazipata kwa Kiswahili ambacho Wizara inatuletea. Hii ni jumuishi, hii ni kuonesha kwamba kila Mtanzania atafaidika na rasilimali hii ambayo tunaiwekeza kwenye *digital economy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira hii ya Wizara inatuonesha kwamba jamii yetu inaelekea kuwa jamii iliyowezeshwa kwenye maendeleo ya kidigitali; na inaweza kabisa kwa sababu tunaona *data* zinakusanyika nyingi kwa wakati mmoja. Nitazungumzia sekta ya afya, *data* za afya zinakusanyika *in million studied*. Bila kutumia *infrastructure* madhubuti kama hii ambayo tumeiona leo katika wasilisho, ni wazi kabisa hatuwezi kutoboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike wakati, badala ya kutumia dakika 10 kukata tiketi ya *SGR*, nitumie sentensi tu, 'Nahitaji tiketi kesho saa 2.00 asubuhi'. Hivi sasa teknolojia hii tunayo na hivi sasa ninaamini Wizara imeshajipanga hivyo, ukiangali lile wasilisho. Tuna wanafunzi ambao wakipewa *homework* hii, ni siku mbili tu wanatuletea *project* ambayo kila mtu anaweza kukata tiketi kwa kutumia *voice note*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *what about* kwenye *health care*? *Health care* yenyewe, mgonjwa anapoanza kuingia tu, kipimo chake kimoja hata kama ni kipimo kimoja cha damu kina majibu kumi. Kila kipimo kina *dimensions* 20 na kile ni cha mtu mmoja. Kuna wagonjwa wangapi wanaonekana kwa wakati mmoja? Kuna mifumo mingapi inaweza ikahitajika kuunganika mpaka matibabu ya mtu mmoja tu yakamilike. Tuipe umuhimu Wizara hii kwa sababu inakwenda kutuwekea sawa mambo mengi ambayo tulidhania ni *future,* lakini ni *present*, mambo mengi ambayo tulidhania Tanzania haijafikia wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kusema hapa, hii ndiyo awamu tunayoondokana na umaskini na hii ndiyo mifano halisi iliyotuonesha kwamba Serikali ipo tayari kwa mabadiliko haya. Ukiangalia yaliyochangiwa leo, hakuna eneo ambalo nimeliona lime-*fall short* kwamba hapa labda hatujaweka tafakuri ya kina na kwa hili ninaipongeza sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa *data* ndiyo ambao utahakikisha *data sets* zetu ziko safi, ziko sahihi, ziko kamilifu, zipo tayari kutumika; na *infrastructure* ambazo hii Wizara inatuwekea ndizo zitazi-*supply* Tanzania nzima. Hii si kazi ndogo, hii ni kazi kubwa na tayari wamejipanga ukitazama namna ambavyo Tume ya TEHAMA inafanya kazi. Kunahitajika mashirikiano makubwa sana *cross-cuttingly* kwa Wizara tofauti. Wizara ya Afya, nitatolea mfano kwa sababu ndiyo Kamati yangu, inahitaji sana *digital infrastructure* ambayo ipo *robust*, ipo *healthy*, inaweza kufikika mahali popote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii minara ndiyo imekuja kutuonesha huo mtandao upo imara na unaweza kufanikiwa. Kinachobakia sasa hivi ni *cosmetics*, kuunganisha zile *tips,* lakini misingi imara imewekwa vizuri na tumeisoma, kwa hiyo tuipongeze na tuiongezee nguvu iweze kufanikiwa kwa muda mfupi ikiwezekana. Fedha zipatikane kwa wakati; tunawapongeza kwa maono yao, tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuvusha kwenye zama za kiza na kwenye nuru ya *digital economy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Zeyana Hamid. Nilimtaja Mheshimiwa Simai Mohammed Said, Mheshimiwa Alan Thomas Mvano na Mheshimiwa Juma Kawamba ajiandae.

**MHE. SIMAI MOHAMMED SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia kuweza kufika hapa na kuweza kutoa mawazo yangu, lakini kuweza kumchangia Mheshimiwa Waziri. Mara nyingi huwa ninasononeka ikiwa mzungumzaji aliyemaliza, ameshusha nondo siyo za kutosha. Sasa ninafikiria, ninayefuata hapa hata ninachokisema Waheshimiwa Wabunge wenzangu ninatumaini tu watanisikiliza. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninakuja Dodoma nilimtafuta Mheshimiwa Waziri nikimwomba atakayenisaidia kufunga mtandao katika nyumba ambayo ninaishi ili niweze kusimamia majukumu yangu. Nikampigia simu, nikamtafuta, nikapita, nikahangaika, mwisho nikamkuta nje hapo Bungeni; lakini hadi leo huo mtandao bado sijaupata. Sasa ninajiuliza, ikiwa mimi mmoja Mheshimiwa Mbunge, mtu mmoja katika watu Tanzania milioni 60 ninajenga mategemeo kama haya; mwenye dhamana na watendaji wake huko chini wawe wepesi katika kutegemea jinsi gani mifumo na kuunganishwa na mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana huko nikiamini mtu kama Mheshimiwa Profesa Mkenda kutoka Wizara ya Elimu wana matarajio hayohayo wawekewe mifumo yote pamoja na kuunganishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninataka kusema tu Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana kuwa mwepesi; kwa sababu suala la Wizara yake ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari; pamoja na kuwa sisi kule Zanzibar tunayo, inaitwa ya Ubunifu; lakini ninajua ubunifu umo ndani ya Wizara yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zeyana amezungumza pia suala la *startups***.** Hao ni wabunifu wanahangaika, wanapokuja na mawazo, Wizara yake ni lazima wawe wepesi kuwasikiliza. Dunia ya sasa kwa hali inavyokwenda, wazo dogo tu basi linaweza likazaa vitu vizito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili hawa waweze kufaidika, hawa watu wenye *startups*, tunahitaji kuwa na vitu vifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wanaweza wakaweka katika *legal framework* ikawa vizuri, lakini pia wengine hawa wanakuwa hawana elimu ya kutosha, lakini wanamtegemea yeye. Wanahitaji kuwe na maeneo kama ya *incubation*, sera rafiki, wasiwe na *stress* lakini pia *access to financial services*. Kwa hiyo ni muhimu sana hawa vijana ambao tunawazungumzia, wanapopiga hodi katika Wizara yake, basi mapokezi yake yawe vile kama mtu ambaye anakwenda kuposa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ukitaka kuposa, huendi saa nane za mchana, unakwenda magharibi au alasiri; mtu amekwishakula, amekwishasali, amekwishapumzika, anapewa kahawa yake. Kwa hiyo hawa vijana wanaokuja katika Wizara yake ni lazima kutoka *point A – Z* mapokezi yao yawe mazuri. Pia lazima tuhakikishe kwamba tunajua kuwa huo mfumo wote tunaotaka wa *digital economy*, *this ministry will be the epicenter*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo atakayoisimamia, kazi atakazozifanya, ushauri atakaoutoa; mimi nitaisubiri Wizara ya Utalii. Huko kuna mambo kibao yanakuja; tunategemea hasa katika masuala ya mifumo. Kuanzia *security*, *how to board a plane.* Kila kitu kitategemea jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wataweza kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu pia kinaudhi sana; kila ukitaka kujisajili ili upate simu ya kadi mpya ni lazima uwe na kadi ya *NIDA*. Ni vizuri kweli mtu kumtambua. Sisi kwetu Zanzibar tuna kadi ya Uzanzibari, lakini ninalosema hili ninataka mnifahamu. Kule Zanzibar mimi ninao watu kutoka Tanzania Bara kibao, wazee wao wamekuja amekwishafariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu atoke leo aende zake hadi Sumbawanga, aende zake hadi Kigoma, aje Lindi au wapi kutafuta cheti cha kuzaliwa. Hana kadi ya *NIDA,* lakini anayo kadi ya Uzanzibari na tunamtambua kama Mzanzibari lakini hawezi kupata kadi ya *NIDA*, hawezi kwenda mahali popote akafanya mambo ambayo yatamwendea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba, Mheshimiwa Waziri ajitahidi sana apange utaratibu ili kadi ya Mzanzibari itumike katika usajili wa kununua kadi za simu au wanataka *offline*, haya. Pia kuna mgao, mgao wa Zanzibar. Amezungumza Mheshimiwa Said Ali Mbarouk, Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi ambaye ni Mwakilishi wa Gando pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya *TCRA* kwenye mgao si kwamba tukizungumza hapa kujaribu kuja na maneno maana yake sisi Wazanzibari;haturidhiki na Maisha, ninaomba tuondoe dhana hiyo potofu. Tunachokizungumza ni vizuri Wazanzibari na Watanzania wakajua katika mapato yanayopatikana na *TCRA* Zanzibar wanafaidika vipi kwa sababu na wao wana Serikali ya kuiendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo atakapokuja hapa, atueleze ili na sisi Waheshimiwa Wabunge watano tutapokwenda katika Baraza la Wawakilishi katika ripoti zetu tunaweza kusema kwamba kweli Mheshimiwa Waziri alijibu na tumechukua hizi taarifa tumewaleteeni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Serikali mpokee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kuna huu Mfuko wa Mawasiliano ambao kuna *one percent* wanakuwa wanachangia hizi kampuni. Inajengwa minara maeneo tofauti, lakini tunapoamua kujenga minara kupeleka katika maeneo tofauti, Zanzibar isiwekwe katika kapu moja. Sisi pia tuna maeneo tunahitaji huduma, waiangalie Zanzibar, waipe *assessment* yake kwa haki iliyokuwepo. Hatuwezi tukasema kwamba hapa tunakwenda kama ilivyo kwenye suala la elimu, Tanzania kuna watu milioni 60 sisi tuko *1.8,* unaambiwa *division one* waliopata Tanzania nzima tunatoa wote kapu hilo moja, utakuta pale wako

wawili tu wa *ratio*. Kama ukisema huyu kapata *1.7, 1.3,* sisi tutakuwa tuko wangapi kwa sababu tuko kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ni lazima linapofanyika jambo, na sisi tuangaliwe. Hata kwenye suala la polisi kwa mfano, unasema tunahitaji polisi, polisi Zanzibar wapo wengi, lakini Zanzibar tunategemea *tourism*. Ulinzi na usalama wa wageni na mali zao ni cha msingi. Kwa hiyo katika hili, ni vizuri Waziri akaangalia na Zanzibar, akaipa nafasi yake. Hata katika hilo suala la kadi nililozungumza, hilo linanigusa sana na ningependa kuona haya mambo yanafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia kwamba, katika hizi kazi zote tulizozungumza katika suala la *data literacy*, hizi *smartphones*, matumizi yake; lakini mchangiaji mmoja ameongea katika mambo tunayoyaona. Ninapata tabu sana. Kuna maeneo ukienda nje kuna matumizi ya vitu wanasema *under 18 is not allowed*; *tobacco*, vilevi na maeneo mengine. Hata hivyo ninajiuliza, mbona humu katika mitandao, humu ndani kuna vitu vingi sana na vizito, tunavidhibiti vipo sisi kwa watoto wetu? Ninaanza kuona katika *TV* sasa hivi kuna nchi wanaanza kutoa taarifa *under 16,* au ngapi, watu wapate kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wakati mwingine mwanangu au pengine majirani zangu watoto wao wana *information* kwa umri wao, kwa malezi yao, kwa jinsi sisi Watanzania tulivyolelewa, mbali ya dini zetu na madhehebu tulipotoka, mengine siyo kwa muda huu wanaotakiwa waone. Kwa hiyo ni lazima udhibiti uwepo. Kama mtu ameamua kuibiaibia, sijui ameingia kwenye *VPN*, yaani hapo amejilazimisha; lakini kuwe kuna *control*. Hakuna nchi yoyote duniani hata katika kibiashara, *you cannot expand without control*. Hata uwe binadamu kama unataka kula nyama, chakula cha asubuhi ule manyama, mchana ule nyama na usiku utatapika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tufanye mambo yetu kwa mpango. Kwa hiyo kwa kweli mimi yangu yalikuwa ni hayo. Ninamkumbusha Mheshimiwa Waziri kwa sababu Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu, tumekwishafanya kazi pamoja, *I hope* hataninunia akiniona na leo au kesho atanipelekea

mtandao. Ajue tu kwamba Watanzania wanamtegemea yeye katika suala zima la kutupelekea hizi huduma na mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sizuii fungu, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia; lakini nitafurahi pia atakapokuja, Watanzania na Wazanzibari alete yale maelezo katika bajeti yake. Ninashukuru sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Simai Mohammed Said. Nilimtaja Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Kawamba na Mheshimiwa Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia wasilisho la Bajeti ya Wizara hii muhimu sana ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kutujalia afya njema na Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kulijalia amani Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile kutoa pongezi zangu nyingi sana kwa Serikali yetu hii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kwa Mheshimiwa Waziri wetu Kairuki na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kweli kazi kubwa inafanyika, tunaona kwa macho, tunawapongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. Bila mawasiliano kwenye maisha hakuna kitu kinachoweza kufanyika. Kwa hiyo tunawapongeza sana kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo, pongezi zangu zinaendana na kwamba kumekuwa na jitihada kubwa sana za Serikali kwenye usambazaji na ujenzi wa minara ndani ya Taifa letu. Hata katika Mkoa wetu wa Kigoma tayari tunaona jitihada kubwa zinazofanyika; na ninatoa pongezi nyingi sana kwa Serikali kwa kazi kubwa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkongo wa Taifa umefika katika Mkoa wa Kigoma na Wilaya ya Kakonko ni moja kati ya wilaya ambazo zinanufaika sasa na Mkongo huu wa Taifa. Kwa hiyo

ninatoa pongezi nyingi na ninaamini kazi kubwa hii inayoendelea kufanyika ni kwa manufaa mapana ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo, yapo mambo machache ambayo ningependa kuyasema, ambayo wananchi wa Kakonko wangependa kuona yanafanyika kwenye eneo hili la mawasiliano na teknolojia. Eneo la kwanza, pamoja na kwamba sisi ni eneo la mipakani na nchi jirani, yapo maeneo kadhaa ambayo bado yana changamoto kidogo ya mawasiliano. Maeneo hayo ni kama maeneo ya Kata ya Nyamtukuza, kwenye maeneo ya Nyamwironge, Rutenga na Kavungwe, vilevile maeneo ya Ruhuru na Nyabenge, maeneo hayo bado yana changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Rugenge, Mugunzu, Kanyonza na Kihomoka, yote hayo bado yana changamoto. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu tayari anatambua na ninatambua kwamba katika mpango huu na bajeti hii na sisi tumeguswa, ndiyo maana nilianza na shukrani nyingi sana. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba basi maeneo haya kwa kuzingatia unyeti wa kuwa maeneo ya mipakani tupewe kuipaumbele kwa ajili ya kujengewa minara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, zipo shule ambazo ziko katika maeneo ya jirani na ulipopita Mkongo wa Taifa. Kwa hiyo pia niombe nafasi hii, kwamba Serikali ione namna ya kutusaidia kufikisha huduma hii ya *internet* kwenye shule za sekondari kama Sekondari ya Kanyonza, Sekondari ya Wasichana ya Kakonko na Shule ya Sekondari ya Dkt. Mpango ambazo ziko jirani kabisa na unapopita Mkongo huu wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwamba tunakoelekea sasa ni kwenye mageuzi ya matumizi ya teknolojia; na ili tuweze kufanya hivyo ni lazima tuwe na sababu za makusudi za kuhakikisha wanafunzi wetu katika shule zetu wanawezeshwa katika kusoma na kupata uelewa katika matumizi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningependa kuomba pia katika eneo hili kwamba Wizara iangalie namna ya kufanya

kuzifikia shule zetu hasa hasa shule za sekondari ili nazo angalau ziweze kupata vifaa vya TEHAMA, wanafunzi wetu waweze kujifunza na kukuza uelewa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, ukiangalia katika Wilaya yetu ya Kakonko kuna shule moja ya Kayonza Sekondari ina wanafunzi 890, lakini shule hiyo ina *computer* moja tu. Katika ushindani wa teknolojia hii tuliyonayo ni kwamba lazima tuwe na sababu za makusudi kama Wizara kuona namna ya kupeleka vifaa hivi katika shule zetu ili watoto wetu waweze kujifunza na mwisho wa siku, basi waweze kuja kulikomboa Taifa katika eneo hili la teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo ambayo yanagusa maeneo makubwa ya nchi yetu. Eneo hili ninapenda kuchangia kwa kutoa mawazo yangu kwamba, eneo la kwanza tumekuwa tukishuhudia minara inajengwa, lakini inatolewa huduma ya mtandao mmoja peke yake. Kwa hiyo niombe Serikali kupitia Wizara, kwamba ione namna ya kufanya maeneo yote ambayo yana minara, basi minara ile itumiwe na watoa huduma wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Nyamwilonge kuna minara lakini huduma inayopatikana ni ya *TTCL* peke yake. Kama jambo hili likifanyika maana yake *Vodacom* wataweka huduma yao, *Airtel* wataweka huduma yao, *Yas* wataweka huduma yao na wananchi wa maeneo hayo watapata huduma hiyo. Kwa hiyo, ninadhani hili jambo ni muhimu kuliangalia ili wananchi wetu waweze kupata huduma vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kama nilivyosema maeneo ya mipakani nimesema Kakonko, lakini natambua kwamba tuna maeneo mengi ya mipakani, basi maeneo hayo yaimarishiwe miundombinu hii ya mawasiliano ili mambo yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu ni kwamba, ili tuweze kwenda kwenye ushindani huu lazima tukubali kwamba elimu lazima itolewe. Kwa hiyo, Wizara lazima iwe tayari kutenga fedha, kujiandaa kuwa na mpango mzuri wa kutoa elimu juu ya matumizi salama ya teknolojia hii ya habari. Kwa hiyo, jambo hilo ni

muhimu. Vilevile matumizi ya mitandao kibiashara, haya mambo ni lazima Wizara iangalie

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kushauri kwamba tumeona wenzetu wa kuzuia na kupambana na rushwa wana *club* katika shule za sekondari huko. Tumeona watu wa mazingira wana *club* zao huko. Kwa hiyo, ninashauri kwamba pamoja na mambo mengine tunayokwenda kuyafanya Wizara pia ione sababu ya kuanzisha *club* za ubunifu kwenye shule zetu za sekondari na shule za msingi ili watoto wetu waanze sasa kuwa na chachu ya kuwa wabunifu. Jambo hilo ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kwamba tunatambua sasa hivi sasa dunia iko kwenye akili mnemba *(Artificial Intelligence)*. Hapa ningependa kushauri kwamba pamoja na jitihada nzuri sana ambazo zinaendelea kufanyika, lakini ninadhani ni muhimu sana tuwe na *innovation centers* katika maeneo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie Dar es Salaam tuwe na *Innovation Center* (Kituo cha Ubunifu) kimoja, tuje Kanda ya Kati hapa Dodoma tuwe na Kituo cha Ubunifu, tuangalie Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Magharibi na Kanda ya Kusini. Haya mambo ni muhimu kwa sababu tukifanya hivyo tutakuwa na uwezo wa kuwachukua vijana na kuwaweka pamoja na mwisho wa siku wanaweza wakawa tayari kuweka mchango wao na tukapata mawazo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, basi nitumie nafasi hii vilevile kutoa pongezi nyingi tena kwa kweli Wizara hii inafanya kazi kubwa. Tumeona maeneo mengi ya nchi yetu yana mawasiliano mazuri. Kwa hiyo, tuwatie moyo Mawaziri wetu. Pia, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ninaamini mambo yatakwenda vizuri na tuko tayari kupitisha bajeti hii kwa kishindo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Juma Kawamba, ajiandae Naibu Waziri Mheshimiwa Switbert Zacharia Mkama na baadaye Mtoa hoja, Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki ajiandae.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amejalia jioni hii ya leo tumekutana hapa kwenye Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitoe pongezi za kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kuiongezea fedha hii Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Kwa kweli Mheshimiwa Rais ni mzalendo na ni mwanamawasiliano kweli kweli. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuipongeza Wizara ya Mawasilino na Teknolojia ya Habari kwa kazi nzuri ambazo wanaendelea kufanya kwani sisi Wabunge wote tunaona na tunaona kwa macho siyo mambo ya kuhadithiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu. Pamoja na kazi nzuri ambazo Wizara inafanya, lakini ndani ya Jimbo langu la Igalula bado kuna maeneo hayajafikiwa na huduma hii ya mawasiliano kikamilifu. Hata hivyo, sina shaka na Wizara hii tayari nimeshayaorodhesha na nimeshampa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Ninaamini maeneo haya yatafanyiwa kazi kikamilifu kwani wananchi wa Igalula hawataki tu mawasiliano, wanataka mawasiliano ya uhakika Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutoa ushauri. Wao kama Wizara ya Mawasilino na Teknolojia ya Habari waendeleze kasi ya

kuongeza minara nchini. Kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano wa *UCSAF* wahakikishe maeneo yote yanafikiwa na huduma ya mawasiliano nchini kwani huduma hii haitachochea tu huduma ya mawasiliano bali inachochea na kasi ya ukuaji wa uchumi nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niongelee suala la huduma ya mawasiliano katika huduma za kijamii hasa sisi ambao tunapatikana maeneo ya vijijini. Ukienda zahanati unakuta kuna huu mfumo ambao unaitwa *Got-HOMIS* unakuta wakati mwingine mfumo huu haupatikani, watu wanaenda hospitali unakuta nyakati za usiku, lakini unakuta mfumo huu haupatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta zahanati haiwezi kutuma taarifa zetu kwenye kituo cha afya na kituo cha afya hakiwezi kutuma taarifa kwenye hospitali ya wilaya na hospitali ya wilaya haiwezi kutuma taarifa kwenye hospitali ya mkoa. Kwa hiyo, ninaomba kama Wizara ihakikishe mifumo hii inasomana. Kila siku Mheshimiwa Rais anaendelea kusisitiza tuhakikishe mifumo inasomana hasa katika maeneo muhimu kama haya maeneo ya sekta ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu anakwenda hospitali usiku lakini anakuta pale mfumo hamna. Sasa unakuta madaktari wale wanamtibu hivyo hivyo, lakini jinsi ya ku-*keep* zile *records* kuna maeneo mengine unakuta wanashindwa. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara iharakishe huduma hizi za mawasiliano hasa kwenye vituo vya afya kuhakikisha zinapatikana masaa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie kwenye suala la vifurushi vya *internet*. Licha ya umuhimu wa huduma hii ya vifurushi vya *internet,* lakini bado imekuwa ghali na inawaathiri sana vijana na hasa wanafunzi. Tunaona japokuwa na umuhimu wa huduma hii ya *internet,* lakini bado wanafunzi wetu nchini wanashindwa kuimudu huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Wizara ianzishe vifurushi maalum kwa ajili ya wanafunzi kama jinsi ilivyokuwa zamani kwa sababu wanafunzi wengi wanashindwa kujifunza kikamilifu na wanashindwa kujitanua kwa ajili ya kwenda kupambana na

huduma zingine kama vile kujikimu kiuchumi na uchumi wa kidijiti. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara tuhakikishe tunaenda kuanzisha vifurushi maalum kwa ajili ya wanafunzi kwa sababu sisi sote tunatambua wanafunzi wanashindwa kumudu hudumu hizi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nichangie kwenye suala la minara ambayo imeshajengwa zamani iende ikaongezewe nguvu, iende ikatoe huduma kwenye kasi ya *4G* na *3G*. Maeneo haya yanapatikana hasa maeneo ya Mjini unakuta minara ipo lakini imezidiwa. Kwa hiyo, unakuta kwa mfano Mji huu wa Dodoma kuna muda mawasiliano ya Tigo yanapatikana kwa shida sana. Kwa hiyo, ninaiomba kama Wizara ihakikishe inakwenda kuiongezea minara hii iendane na ongezeko la watu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini ninaipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambazo inazoendelea kufanya. Hizi changamoto ambazo nimeziorodhesha hapa ninaomba Wizara izifanyie kazi kwa maslahi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru.

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya Mafunzo. Tunao wanafunzi 50 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, jiandae Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kuchangia kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetuwezesha kuwa hapa leo tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake kubwa kwangu kwa kuniteua kuwa msaidizi wake kama Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Imani hii ni deni kubwa

kwangu na nitalilipa deni hili kwa kufanya kazi kwa uaminifu, kwa uwezo wangu wote, kwa akili yangu yote na nguvu yangu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yao ya kuiongoza nchi yetu. Ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kazi nzuri anayofanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimpongeze pia na kumshukuru Waziri wangu Mheshimiwa Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki kwa malezi mazuri, miongozo, ushirikiano na upendo anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu na ukizingatia kwamba mimi ni mgeni katika nyanja ya siasa amekuwa Mwalimu wangu mzuri katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia sana watumishi wote wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mohammed Khamis Abdulla na Naibu Katibu Mkuu kwa mapokezi mazuri waliyotupatia tulipowasili Wizarani kwa uchapakazi mzuri, kwa weledi, kwa upendo na ushirikiano mzuri wanaotupatia ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na kwa wepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru pia Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu kwa ushirikiano wanaotupatia mimi pamoja na Mheshimiwa Waziri usiokuwa na mipaka ambao umetuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kazi tuliyopangiwa kwa wepesi na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Ukerewe walionichagua kwa kura nyingi za heshima. Ninawaahidi utumishi uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru pia familia yangu mke wangu Matilda, watoto wangu: Sebastian, Alexander, Benjamin na Collins kwa kuniunga na kuwa bega kwa bega na mimi katika safari yangu hii ya kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais kwa kuitendea haki sekta hii ya mawasiliano na teknolojia ya habari. Kiukweli Mheshimiwa Rais amekuwa mdau mkubwa katika sekta hii kwa uwekezaji mkubwa alioufanya ambao unaiwezesha sekta hii kupaa na kuwa nguzo kuu ya uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, ninapenda kuchangia katika maeneo makuu mawili hasa hasa ujenzi wa miundombinu: Mkongo wa Taifa wa Mawasilino na Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano. Niruhusu nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, majibu ya hoja zote kwa kina tutayawasilisha kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuonyesha umuhimu wa Wizara na Serikali kuendelea kukamilisha Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasilino kwa kukamilisha Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kuunganisha Wilaya 17 zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kazi hii tunaianza kuitekeleza katika bajeti hii ambayo leo watutapitishia na tutahakikisha kwamba Wilaya zote nchini zinapata Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika muda mfupi ujao. Pia na taasisi zote muhimu za Serikali na za watu binafsi, Taasisi za kimkakati zote tutahakikisha zinafikiwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge pia walishauri tuongeze kasi ya kupeleka Mkongo wa Mawasiliano *DRC*. Ninapenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba suala hili sisi Wizara na Serikali kwa ujumla tunalipa umuhimu mkubwa na tutalitekeleza kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, nipende kuwajulisha kwamba tayari tumejipanga kuanza uzinduzi wa hii safari ya kupeleka Mkongo wa Taifa Nchini *DRC* tarehe 26 Mei, katika Mkoa wa Kigoma. Tunatarajia kama kila kitu kitakuwa kama tulivyopanga ifikapo

Mwezi Aprili, 2027, tutakuwa tumekamilisha zoezi la kuufikisha Mkongo wa Taifa nchini *DRC* ambao tunatarajia kwamba utagharimu takribani pesa za Kitanzania shilingi bilioni 31 na pesa hii tunategemea kuwa imelipwa ndani ya miaka mitano tangu baada ya kukamilika kwa mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa minara ya mawasiliano. Kwa sasa Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba ifikapo Mwaka 2030 tuwe tumekamilisha Ujenzi wa Minara katika maeneo yote yenye changamoto. Hii inathibitishwa kwamba katika Mwaka huu wa Fedha tunaokwenda nao 2025/2026, Serikali inatekeleza awamu mbili za ujenzi wa minara, awamu ya tisa ambayo inahusiana na ujenzi wa minara 636, awamu ya 10 inayohusu minara 287 na awamu ya 11 ambayo itahusisha minara 280.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo hayatafikiwa na hizi awamu kuna mpango mkakati wa miaka mitano ya ujenzi wa minara ambayo tunakusudia kuyafikia maeneo yote ambayo yana changamoto ya minara. Ifikapo mwaka 2030 tutakuwa tumekamilisha. Maeneo yote yenye changamoto tutakuwa tumeyafikia: kila eneo la Mbunge, kila Jimbo, kila Kata tutakuwa tumeifikia na tutahakikisha kwamba Wabunge wanapokwenda kufanya kampeni mwaka 2030, sekta ya mawasiliano haitakuwa kikwazo kwenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea vilevile kufanya tathmini ya maeneo mengine yenye changamoto na tutaendelea kuyatekeleza awamu kwa awamu kwa kadiri hali ya fedha itakavyokuwa inaruhusu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana na ninaomba niseme kwamba ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipatia Wizara yangu bajeti ya

kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ambayo tunaiomba leo imeelekezwa katika kuimarisha uwekezaji kwenye miundombinu ya TEHAMA na hasa Ujenzi na Uendelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Ujenzi wa Minara ya Mawasiliano kupitia Miradi ya Wizara Nane na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, aidha kupitia uwekezaji huu tunaamini utawezesha sekta yetu ya mawasiliano na teknolojia ya habari kuweza kukua kwa kasi, kuongeza upatikanaji wa huduma za kidijiti na hatimaye kuweza kufikiwa kwa lengo la Serikali la kuwa na uchumi wa kidijiti.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha Hotuba yangu katika Bunge lako Tukufu. Aidha, nikushukuru pia kwa kuniruhusu kuweza kuihitimisha Hotuba yangu mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru vilevile Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Selemani Kakoso, Mwenyekiti wetu wa Kamati na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa mchango mzuri na maelekezo ambayo yamesaidia sana kuboresha utekelezaji wa shghuli za sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari.

Mheshimiwa Spika, kadhalika ninatoa shukurani zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, akiwemo na Mheshimiwa Paresso, ambaye aliongoza kikao asubuhi ya leo na wote kwa kuweza kunisikiliza kwa makini na kwa michango yao kwa hoja ambazo tunaamini tutakapozitekeleza zitaweza kufikia malengo ya Wizara ninayoiongoza.

Mheshimiwa Spika, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, takribani 16 ambao wameweza kuchangia kwa kuzungumza, lakini vilevile kwa wale ambao wamekuwa wakiwasiliana nasi kuweza kutupatia maoni mengine ya ziada.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, michango ya Waheshimiwa Wabunge, imejikita kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, imejikita katika ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano ikiwemo ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, ujenzi wa Minara ya Mawasiliano, ujenzi wa vituo vya kuhifadhia *data*, usalama mtandao, utapeli mtandaoni, elimu kwa umma, vifurushi, mchango wa sekta ya mawasiliano kwenye pato la Taifa, utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, elimu shuleni pamoja na masuala mengine kadha wa kadha.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kipekee kumshukuru Naibu Waziri kwa mchango mzuri alioutoa leo hii hapa, amenipunguzia kazi kwa kujibu baadhi ya hoja, ninamshukuru sana kwa mchango huu sawia. Kipekee nimshukuru sana kwa namna anavyoendelea kunisaidia kazi, kwa hakika Mheshimiwa Rais, alinitendea haki kuweza kunipatia aina ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa aina yake. Kipekee niwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Ukerewe kwa kuona jembe hili ambalo kwa sasa linatusaidia sana pia katika Wizara yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru sana Katibu Mkuu, ndugu yangu Abdullah pamoja na Naibu Katibu Mkuu, ndugu yangu, Mkapa na Menejimenti nzima, Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Bodi, Wakuu wetu wote wa Taasisi, Wataalam katika Taasisi zetu, watoa huduma wetu wa Mawasiliano, wakandarasi wetu pamoja na wengine wote wanaotusaidia katika ujenzi wa Minara na huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nitoe ufafanuzi kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, majibu mengine ambayo tutakuwa hatujayajibia hapa kutokana na ufinyu wa muda, tuwaombe Waheshimiwa Wabunge waridhie nitayawasilisha pia kwa maandishi ili tuweze kuyatolea majibu na ufafanuzi wakina.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa

kuonesha umuhimu kwa Wizara na Serikali kuendelea kukamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa kukamilisha ujenzi wa Mkongo wa Taifa katika kuunganisha wilaya 17 zilizosalia nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma za mawasiliano zinapatikana kwa wananchi, Wizara yangu itaendelea kufanya uwekezaji katika miundombinu ya TEHAMA ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano zinaimarika nchi nzima na hii inajumuisha kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kuhakikisha unafika katika wilaya zilizobakia, kuunganisha katika Taasisi mbalimbali za umma na binafsi, kuunganisha katika shule kama ambavyo tumemsikia Mbunge wa Kakonko akisemea, hivyo kupunguza gharama za mawasiliano na kuongeza ufanisi wa huduma.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza, kuiunganisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwa uamuzi huu utasaidia sana kuongeza mapato yetu ya Serikali, lakini kuwa na matumizi sawia na sahihi ya Mkongo kama ambavyo Taifa lilikusudia katika ujenzi huu. Tunaamini kupitia takwimu zilizopo, marejesho ya uwekezaji ndani ya miaka mitatu, uwekezaji wa shilingi bilioni 31 utakaokuwa umefanyika utakuwa umesharudi na hatimaye fedha itakayofuata hapo itakuwa ni faida.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tutaendelea na ujenzi wa Minara na kama ilivyoelezwa lengo letu ni kuhakikisha kwamba isitokee tunafika mwaka 2030 kuna maeneo ambayo bado katika nchi yetu wanajikuta wametengwa kwa kukosa mawasiliano. Tunatambua mawasiliano sasa hivi ni kila kitu katika huduma za kijamii, katika biashara pamoja na masuala mengine kadha wa kadha lakini pia katika suala zima la ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, kama Wizara vilevile tutaendelea kufanya tathmini ya maeneo yote nchini yenye changamoto ya

mawasiliano na kuhakikisha tunayaingiza katika mpango wa ujenzi wa minara kupitia awamu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa hoja imejitokeza ya vituo vya kuhifadhi *data*; Wizara yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tutaendelea kufanya maboresho ya kituo cha Taifa cha kuhifadhi *data* kilichopo Dodoma, kilichopo Dar es Salaam Kijitonyama kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa *data* zinazohifadhiwa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara itaanza ujenzi wa vituo viwili vya kuhifadhi *data* vilivyopo Dodoma na Dar es Salaam ili kuongeza wigo wa kuhifadhi taarifa zinazoendelea kuzalishwa kila siku.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya kuweza kuongeza nguvu katika suala zima la kuongeza vifaa katika *data centre* yetu ya Dar es Salaam, ninapenda kuwahakikishia na kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwa mwaka ujao wa fedha tutatumia takribani shilingi bilioni 9.7 ambapo tutatumia shilingi bilioni nne kutoka katika Wizara na shilingi bilioni 5.7 tutaweza kutoa kupitia Shirika letu la Mawasiliano Tanzania kupitia vyanzo vya ndani vya shirika, ikiwemo mapato yanayotokana na uuzaji wa huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mahitaji ya muda mrefu kama ambavyo Kamati yetu imelieleza vizuri sana, tutaendelea kuona ni namna gani tunajenga majengo mapya yatakayojengwa Jijini Dodoma na Zanzibar; ambapo kwa upande wa *data centre* ya Zanzibar tayari eneo limepatikana la hekta 71, litajulikana kama *Dunia Cyber City*. Ninadhani kwa upande wa Zanzibar wanalifahamu, lakini kwa upande wa Dodoma tayari pia tumeshapata eneo Njedengwa la mita za maraba takribani 16,626.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *data centre* tayari Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeshatenga kiasi cha fedha takribani shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa mradi huo. Kwa upande wa Dodoma tunaendelea na uratibu wa ufuatiliaji wa ujenzi husika na tunaamini tutaweza kufikia katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upanuzi wa *data centre* ya Dar es Salaam kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge, wamesemea; umuhimu wa kupata takribani shilingi 100,000,000,000 kuweza kupanua uwezo wa kuweza kuhifadhi taarifa katika kituo chetu cha kuhifadhi *data*.

Mheshimiwa Spika, kwanza tuwashukuru kwa namna ambavyo waliweza kutoa hoja hii; lakini tukushukuru Mheshimiwa Spika, pia kwa namna ambavyo kupitia Kamati yako ya Uongozi na mashauriano ambayo yalifanyika na Serikali angalau tumeona sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha kwa mwaka ujao wa fedha kupitia kifungu kidogo katika fedha zetu za miradi ya maendeleo, tumetenga takribani shilingi 30,000,000,000 ambazo zitaelekezwa katika ujenzi wa *data centre* kwa upande wa Dar es Salaam na tunaamini hatua kwa hatua basi tutaweza kufikia zile shilingi 100,000,000,000.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Kamati kwa kuliona hili, lakini zaidi tukushukuru Mheshimiwa Spika kwa uongozi wako na tuwashukuru pia Wizara ya Fedha kwa kuona umuhimu wa Kituo hiki cha Kuhifadhi *Data* kwa Dar es salaam na baadaye kuhamia Dodoma pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, tutaendelea kuimarisha usalama mtandao ili kulinda mifumo ya TEHAMA, taarifa na miundombinu ya kidijiti dhidi ya mashambulizi ya kimtandao, udukuzi na matumizi mabaya ya teknolojia.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali tunaendelea kuimarisha mifumo ya ulinzi, tunaendelea kutoa elimu kwa umma haswa watumiaji wetu, lakini vilevile tunaendelea kuweka mifumo na taasisi madhubuti kwa ajili ya kushughulikia vitisho mbalimbali vinavyoweza kujitokeza na vinavyojitokeza kwa wakati mwingine na kimtandao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utapeli mtandaoni kama Wizara tumeendelea kushughulikia masuala ya utapeli mtandaoni kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano nchini katika kukabiliana na vitendo vya udanganyifu vinavyofanyika kupitia

mitandao ikiwemo jumbe za uwongo, wizi wa taarifa binafsi, lakini vilevile wizi na utapeli wa fedha kwa njia za kidijiti.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua ambazo tutaendelea kuzichukua ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa kushirikiana na watoa huduma wetu, lakini kuona ni namna gani watumiaji pia wa mitandao hii wanaweza kuuhisha taratibu mbalimbali za kiusalama kama ambavyo watoa huduma wetu wameweka *a two multiple factor* kwa ajili ya *security*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo vile vile kuhusiana na mchango wa sekta ya Mawasiliano kwenye pato la Taifa: ninashukuru baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wameweza kuelezea umuhimu wa kuwa na *digital economy satellite account* ikiwemo shemeji yangu Mheshimiwa Mutasingwa, Mbunge wa Bukoba Mjini na kama ambavyo nimeeleza katika hotuba yangu. Ukiangalia katika mchango wa sekta ya TEHAMA katika pato la Taifa kama tulivyoeleza, kwa mwaka 2023 ilikuwa ni asilimia 7.6 lakini unauona umepanda mpaka 14.6% kama ukuaji, lakini mchango wenyewe kwa sasa tupo katika asilimia 1.6.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika yapo mengi ambayo yamefanyika kupitia mchango wa sekta ya TEHAMA na ndiyo maana sasa tunaamini tutakapokuwa na *account* mahususi ya upimaji wa uchumi wa kidijitali, asilimia hii itaweza kukua na itaweza kuongezeka ili kuweza kuonesha mchango sahihi wa sekta yetu ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu huo, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari itaendelea na taratibu za uandaaji wa akaunti ya upimaji wa uchumi wa kidijiti au *DESA* ili kuweza kuongeza wigo wa upimaji wa mchango wa sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari katika pato la Taifa ili kuweza kutambua kwa usahihi mchango halisi wa sekta katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili tumeanza kuchukua hatua tukitambua kwamba uandaaji wa akaunti hii maalum ni mchakato wa muda mrefu unaotumia muda; lakini vilevile unahusisha hatua mbalimbali ikiwemo suala zima la ukusanyaji na

uchambuzi wa takwimu na tumejaribu pia kuangalia uzoefu wa wenzetu ikiwemo Afrika Kusini, ikiwemo nchi ya Thailand ambayo tayari tumeshaitembelea.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi mchakato huu wa kukamilisha uandaaji wa akaunti ya *DESA* inachukua kama takribani miaka mitatu. Ninapenda tu kuarifu Bunge lako tayari tumeshaanza hatua ya kukusanya takwimu za upili au *secondary data* ambazo zimetokana na tafiti na *studies* mbalimbali kwa ajili ya maandalizi ya *digital supply* ya *news table*, ambayo tunaamini *table* hii itaweza kutumika katika kuandaa *DESA* akaunti.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu kwa umma, Wizara kupitia mamlaka yetu ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* na kwa kushirikiana na watoa huduma wetu wa mawasiliano ya simu tumeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na matumizi sahihi na salama ya huduma za mawasiliano ikiwemo kuhakikisha kwamba namba 100 ndiyo namba pekee inayotumika kwa mawasiliano kati ya mtoa huduma na wateja, lakini namba nyingine ya *106# itumike kuangalia na kuhakiki namba zilizosajiliwa katika kitambulisho cha Taifa cha mteja na namba 15040 ndiyo itumike kutoa taarifa za namba zilizotumika kufanya ulaghai ili ziweze kuchukuliwa hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niirudie namba hiyo, 15040, wewe ikitokea umepata ujumbe ambao una mashaka nao, weka tu namba ya huyo aliyekutumia katika namba 15040 na hatua stahiki zitaweza kuchukuliwa ikiwemo pia kuweza kufunga namba hiyo na hatimaye hatua nyingine za kiuchunguzi na za kisheria kuweza kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, *TCRA* pia imeendelea kutoa elimu kuhusiana na matumizi sahihi na salama ya mtandao kupitia redio, televisheni, kupitia mitandao ya kijamii, mashuleni pamoja na vyuoni.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza hoja ya vifurushi na Waheshimiwa Wabunge wengi wameweza kulizungumzia hili kwa kina kabisa na vizuri sana, tunawashukuru na hasa akiwemo pia Mheshimiwa Eric Shigongo, ambaye suala hili amekuwa

akilizungumza mara kwa mara hata wakiwemo wakati wa watangulizi wangu amekuwa akilielezea.

Mheshimiwa Spika, nipende kusema kwa wengine wote waliyozungumza tumepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na tunaahidi kuufanyia kazi, ambapo kwa sasa mtumiaji ambaye muda wake upo katika bando la mwezi husika endapo anaona kabla halijakwisha anadhani hatafikisha ule muda kulitumia anatakiwa auhishe bando lake alilonunua kabla ya kwisha muda wake ili asipoteze bando lake la awali baada ya kwisha muda.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo tunaendelea kufanyia kazi suala hili, tunalipokea na tunaamini ni hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi kama walivyoeleza, wameeleza kwa uzito mkubwa ili kuweza kuona ni namna gani mtu basi hatapoteza bando lake la awali kabla ya kwisha muda.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hili pia ukiangalia katika hoja hii Mheshimiwa Shigongo, ametolea mfano wa *ICASA* ya Afrika Kusini na bahati nzuri tunayo mahusiano mazuri sana na *ICASA* na walikuja pia kututembelea kupitia *TCRA* na baadhi ya kanuni ambazo Mheshimiwa Mbunge, pia anazitaja ukiangalia na sisi kwa kanuni zetu za mwaka 2018 kwa kiasi kikubwa maeneo kama saba ambayo Mheshimiwa Mbunge aliyasema pia yapo. Hata hivyo, tunaendelea kupokea ushauri kuweza kuona ni kwa namna gani tutaweza kuliangalia suala hili kwa ujumla wake la vifurushi ili kuweza kuleta nafuu kwa ajili ya wateja wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utoaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha wa 2025/2026, Wizara imepokea shilingi bilioni 139.8 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo shilingi bilioni 55.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 84.4 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, ninapenda vilevile kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na haswa Wajumbe pia wa Kamati kwa namna ambavyo wameonesha umuhimu wa Serikali kuendelea kutoa fedha kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi ile ya maendeleo na tuwashukuru kwa namna ambavyo wamelisemea.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tuwashukuru pia Wizara ya Fedha kwa mwezi huu tumeweza kupokea takribani shilingi bilioni 13.7. Kwa hiyo tunaendelea kuamini kama Wizara na kwa namna maoni ambavyo ya Kamati wameendelea kuweka msisitizo, basi tunaamini fedha hizi kwa kuwa bado mwaka wa fedha haujakwisha, tunaamini tutaweza kuzipata ili kuhakikisha kwamba fedha zote zilizoidhinishwa zinatolewa kwa wakati ili kuweza kutekeleza miradi yetu na kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, kikubwa nipende kusema tu kwamba, tunaendelea kupokea maoni na ushauri kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wameyatoa na tunaamini tutaweza kuendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja ya Wajumbe wa Kamati kuhusiana na Serikali kuongeza jitihada za kupambana na uhalifu wa kimtandao kama nilivyosema. Nipende tu kusema kwamba, tumeendelea kulifanyia kazi suala hili na hadi sasa tuliweza kufungia laini takribani 62,879; lakini vilevile tumeweza kuchukua hatua za kuzuia kufanya usajili wa laini mpya za simu kwa vitambulisho vya Taifa takribani laini 60,177 ambazo zilikuwa na viashiria, lakini na nyingine zilihusika katika matukio ya utapeli.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia *TCRA* imeendelea kushirikiana na watoa huduma wetu wa mawasiliano ya simu kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na matumizi sahihi na salama ya huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna hoja pia ya Kamati yetu kuhusiana na namna ya kuliokoa shirika letu la Posta na hasa kugeuza deni la shirika kuwa mtaji ili Posta iweze kujiendesha kwa faida na hatimaye kuweza kuongeza ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tu kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Shirika la Posta limekuwa na madeni ya kodi na riba kiasi cha takribani shilingi bilioni 54.7 ambazo kwa kiasi kikubwa zilitokana na huko mwanzo shirika kutokupewa mtaji wa uendeshaji au *working capital* tangu lilipoanzishwa.

Mheshimiwa Spika, la pili, Shirika la Posta lilitakiwa kulipa kwa niaba ya Serikali, wastaafu waliokuwa wafanyakazi wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu wakati huo la Afrika Mashariki, bila kurejeshewa fedha hizo kwa wakati. Hizi ndizo fedha ambazo Kamati imekuwa ikizizungumzia mara kwa mara, kwamba deni la shilingi bilioni 54.7 likifutwa, basi litasaidia kuongeza mtaji wa Shirika letu la Posta ili liweze kufanya vizuri katika huduma usafirishaji wa vifurushi na vipeto, kuweza kuboresha ofisi zake ziwe za kisasa na kuweza kushindana na washindani wao.

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua hiyo itasaidia kuboresha mfumo wetu wa usafirishaji wa *SwiftPack. V*ilevile tunazo *Bureau de Change* za Posta, *Posta Bureau* na yenyewe pia wanayo *potential* kubwa sana tunaamini mtaji huu ukipatikana utaweza kuwa wa msaada mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru tumeanza mashauriano na Wizara ya Fedha kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* na tayari Wizara ya Fedha imeielekeza *TRA* kujaza na kuwasilisha *loss report* ya kufuta deni tajwa ili kuwezesha Wizara ya Fedha kuweza kuendelea na taratibu zingine kwa ajili ya kulileta Bungeni kufuta madeni hayo kwa mujibu wa kifungu cha sheria, kifungu cha 34(1) cha Sheria ya Fedha ya Umma, Sura ya 348 pamoja na kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, aidha, tumeendelea kuchukua hatua hatujakaa kusubiri kuendelea kukarabati takribani Ofisi za Posta 65 za wilaya, lakini tumeendelea kuwaboreshea kwa kuwanunulia vitendea kazi ikiwemo *computer* 102, bajaji za umeme 50, thamani za ofisi, lakini vilevile tumeweza kuwawezesha Shirika la Posta kwa kuwapatia magari 12 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.2 ili waweze kuimarisha zaidi huduma za usafirishaji ambazo kimsingi ndiyo kazi ya msingi wa Shirika la Posta Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hatujawasahau vilevile watumishi wetu wa Posta, tunaendelea kuangalia uboreshaji wa masilahi yao. Kwa sasa tumeanza zoezi la uchambuzi wa awali wa mapendekezo ya kuboresha mishahara na tumeshawasilisha katika mamlaka ya Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Utumishi kwa ajili ya uchambuzi wa kitaalam ili tuweze kuona ni namna gani

watatupatia kibali kuridhia ili tuweze kufanya maboresho sasa ya masilahi ya watumishi wa Shirika letu la Posta Tanzania, tukiendea katika safari ya kuligeuza shirika hili ili liweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ya kuangalia ni namna gani vilevile, tutaweka mkakati wa kuzisimamia taasisi ambazo ziko chini ya Wizara yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na hususan Mheshimiwa Wabunge na Kamati walijikita katika ukusanyaji wa mapato ili taasisi zetu ziweze kujiendesha kwa faida na kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija bila kutegemea Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge tunaendelea kuzisimamia taasisi hizi zilizoko ziko chini ya Wizara kwa kuziwezesha kimtaji ili ziweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija. Kwa mfano, kwa mwaka huu wa fedha ambao tunaumalizia, tumeweza kama Wizara kuzipatia taasisi zetu takriban shilingi bilioni 31.5 na hasa Shirika la *TTCL*, Shirika la Posta pamoja na Tume yetu ya Taifa ya TEHAMA.

Mheshimiwa Spika, kupitia utoaji wa fedha hizo shilingi bilioni 31.5, imeziwezesha taasisi zetu hizi tatu kuimarika zaidi katika utekelezaji wa majukumu yao. Ikiwemo mfano, kwa *TTCL*, kuanza kutengeneza faida sasa. Jamani habari njema, *TTCL* sasa nyumbani kumenoga zaidi! Tumeanza kutengeneza faida na tunaamini sasa Serikali yetu itaendelea kupata gawio kupitia Shirika letu la *TTCL* na Posta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ambavyo tumeendelea kuongeza huduma za bidhaa ikiwemo *Fiber* Mlangoni pamoja na huduma nyingine, lakini pia kuendelea kuboresha masuala ya *mobile money* ikiwemo *T-Pesa*. Pia, tumeanza utaratibu wa kuhakikisha *TTCL* sasa tunakuja na maduka ya *franchise* kama ambavyo tunaona katika *Airtel Shop,* kama ambavyo tunaona katika *Voda Shop, Halotel Shop* na wenyewe sasa tutakuja pia na *TTCL Shops* nyingi kabisa kwa kushirikiana na sekta binafsi ili na sisi tuweze kushindana kibiashara.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia tu kwa mujibu wa taarifa ya *CAG*, kwa namna ambavyo imewasilishwa, kwa taarifa ya

Mwaka wa Fedha 2024/2025, *TTCL* sasa imetengeneza faida ya shilingi 22,000,000,000, wakati huko nyuma ilikuwa ni hasara kwa kiwango cha takriban shilingi bilioni 24. Kwa hiyo, tunaamini hatua hii itasaidia sana kuendelea kuliboresha Shirika letu la *TTCL* na tunaamini ndani ya muda mfupi sana na kwa kuwa tumeshaandaa mkakati wa miaka 10 wa kulifanya Shirika letu la *TTCL* liweze kujiendesha kibiashara, tunaamini basi tutaweza kuongeza mapato ya *TTCL*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwa *TPC* na wenyewe wakiweza kufutiwa deni la shilingi bilioni 54.7 nako wataweza kupiga hatua na bila kuwasahau wenzetu wa Tume ya TEHAMA na wenyewe pia tutaendelea kuwaangalia kwa ajili ya kuwaimarisha zaidi ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia ya kukamilisha Muswada wa Sheria ya TEHAMA wa Mwaka 2026 na kwenye eneo hili nimshukuru sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna ambavyo ameendelea kutupa ushirikiano kama Wizara, kuhakikisha mchakato huu wa kutunga Sheria ya TEHAMA unaharakishwa. Ninapenda tu kusema kwamba tayari kama Wizara tulishandaa andiko la kuwezeshwa kutungwa kwa Sheria hii na kwa sasa uchambuzi wa maoni ya wadau unaendelea.

Mheshimiwa Spika, tunaamini utakapofika mwisho basi tutaweza kuwasilisha katika hatua nyingine za utungaji na tutaomba Waheshimiwa Wabunge, tutakapoiwasilisha katika Bunge lako Tukufu basi waweze kutuunga mkono na hatimaye kupata sheria ya kisasa kabisa inayoendana na wakati tulionao. Kama ambavyo tumeeleza, itakayozingatia masuala mazima ya akili unde; itakayozingatia masuala mazima ya *blockchain technology*; pamoja na teknolojia nyingine zinazoibukia.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia ya kuendelea kujipanga kutekeleza mkakati wa kuzuia uhalifu wa mitandao na wizi wa mitandaoni, hasa katika ile mikoa minne vinara. Tukianza na Mkoa wa Morogoro ambapo Mheshimiwa Asenga amekuwa

akiizungumzia sana na hasa katika Wilaya yake ya Ifakara; Mkoa wa Dar es Salaam; Mkoa wa Mbeya pamoja na Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusema tu kwa Waheshimiwa Wabunge, kupitia *TCRA* tumekuwa tukiendelea kuainisha maeneo ambayo tunaona yanaongoza katika utapeli uliokithiri. Tumekuwa tukitoa ripoti zetu za kila robo mwaka za *TCRA* na maeneo haya yamekuwa yakijitokeza. Tutaendelea kutumia ripoti hizi kuona ni namna gani pia tutashirikiana na jeshi letu la polisi kuchukua hatua stahiki katika maeneo hayo manne niliyoweza kuyataja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, pamoja na mambo mengine yote, ninaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kutuunga mkono na tuendelee kuwahakikishia kwamba yote yaliyoelezwa hapa tunayachukulia kwa uzito mkubwa tukiamini ninyi ndiyo wawakilishi wa wananchi, mnayoyasema ndiyo matamanio ya wananchi wanayotaka kuyaona. Tutayafanyia kazi wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama walivyosema, tunachotaka ni kuleta tabasamu la Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wananchi wake wa Tanzania kupitia Sekta yetu ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mkubwa, kwa usikivu wao na umakini wao mkubwa, lakini sisi kama Wizara na taasisi zetu tumefaidika sana na michango yao madhubuti na makini kabisa na tunajionea fahari kuwa na wawakilishi wa aina yao na tunaamini tutaweza kupiga hatua kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*……………..................Sh. 2,546,382,600

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa hapa kuna mshahara wa Waziri na nilipata jina moja la Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Ningependa kupata ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri. Ninawapongeza kwanza kwa kazi nzuri, dada yangu Angellah Kairuki unafanya vizuri, anafikika pamoja na Naibu wake. Mungu awabariki sana na sisi tutawapa ushirikiano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Taifa tulikuwa tunapenda tuone Shirika letu la *TTCL* linajiendesha kibiashara, linashindana na *Vodacom*, *Tigo*, na *Airtel,* lakini kumekuwa pia na changamoto sana na mkakati madhubuti wa Serikali wa kuhakikisha shirika hili linajiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, *promotion* (matangazo) ya shirika hili bado ipo chini, kule kwenye wilaya hivi hata tukijiuliza

taasisi ngapi za Serikali zinatumia mtandao wa *TTCL*, kwenye wilaya, kwenye halmashauri zetu bado halijafahamika vya kutosha. Ni lazima sasa kama Wizara tuwe na mkakati madhubuti wa kulitangaza na kuhakikisha linaweza kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kwenye Mkongo wa Taifa hela nyingi zinaenda Serikali Kuu, lakini ni asilimia ngapi inarudi kwa ajili ya uendeshaji? Haya yote tukiyaunganisha tunaamini Shirika letu linaweza likasimama. Waziri amesema hapo wakati ana-*wind up* kwamba sasa hivi wanatengeneza shilingi 22,000,000,000. Sasa *imagine* tukilitangaza Watanzania wakajua, tukaliwekea mikakati kama maeneo mengine ambayo tumefanya, kwenye Mfuko wa Bima ya Afya na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kujua ni mkakati gani ili Shirika letu liweze kufanya vizuri na kuleta ushindani na Watanzania waweze kunufaika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia nafasi na kipekee, nimshukuru Mheshimiwa Ester Bulaya kwa swali lake zuri au hoja yake nzuri ya kuona ni namna gani tunaendelea kupambana ili *TTCL*, Shirika letu la muda mrefu la kihistoria la Taifa letu kuona ni namna gani linashindana na watoa huduma wengine, lakini vilevile, kuona ni namna gani tunaendelea kuboresha matangazo, lakini pia kuweka mkazo kuhakikisha taasisi nyingi zaidi zinatumia shirika letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kumthibitishia Mheshimiwa Ester Bulaya kwamba tayari tunao mkakati wa miaka 10 wa kuliendesha Shirika letu hili la *TTCL* kibiashara kuanzia mwaka 2025 - 2035 na tunaamini kupitia utekelezaji wa mkakati huu Shirika letu litaweza kujiendesha kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejipanga vilevile katika mkakati huu, kuendelea kuboresha zaidi aina ya huduma na bidhaa ambazo tunazitoa kwa wateja wetu, lakini vilevile kuona ni

vifurushi vya aina gani watu wanavipenda ili kuona ni kwa namna gani tutaweza kupata wateja wengi zaidi, siyo kupata tu wateja ambao watakaa mwezi mmoja, halafu baada ya hapo hawatumii tena, wateja ambao watakuwa ni endelevu na watakaodumu kwa muda mrefu. Pia bidhaa ambazo zitakuwa ni rahisi zaidi kwa wateja wengi na kuona ni namna gani tunaboresha utendaji wa kazi utakaokuwa na tija kwa wafanyakazi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tutalisimamia kuendesha mkakati wetu huu wa kuliendesha Shirika letu kibiashara ni pamoja na usimamizi thabiti wa mali za Shirika. Tunazo mali nyingi sana, tuna viwanja vingi sana kama Shirika la *TTCL*, kwa hiyo na lenyewe tumeanza kulifanyia tathmini na kuandaa mpango kabambe kwa ajili ya kutumia rasilimali zile za ardhi ambazo tunazo tayari ili kuona maeneo gani ya kimkakati. Kwa mfano, tumeshabaini maeneo ya kimkakati takriban zaidi ya 300 katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kupambana, tukishakamilisha taratibu tutakaribisha wawekezaji ambao wataweza kuja kuwekeza *wether* itakuwa kwa ubia au kwa mfumo ambao tutakuwa tumekubaliana kwa mujibu wa uchambuzi wa wataalam wetu ili kuhakikisha tunaendelea kuongeza mtaji kwa Shirika letu hili la *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo vilevile tutaendelea kupambana kuona katika mahesabu ya awali yaliyokaguliwa kuhakikisha kwamba haturudi katika historia ile ya nyuma. Tumeshaanza kupata faida, tuendelee kutengeneza faida kubwa zaidi ili kuhakikisha Shirika letu linaendelea kupiga hatua na kama nilivyosema kwa upande wa *franchising,* lakini vilevile kuboresha *T-Pesa*. Ukiangalia kampuni nyingine za watoa huduma wanapata fedha nyingi sana kupitia *mobile money*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunadhani sasa ni wakati na *TTCL* na yenyewe iweze kunufaika na keki hii, tukitambua kwamba kupitia faida tutakayoipata, kupitia gawio litakalorudi Serikalini basi

litasaidia pia kuweka uwekezaji mkubwa katika huduma za kijamii na mahitaji mengine kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…………....Sh. 647,241,940
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…………….Sh. 4,282,698,560
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……………………….Sh.358,354,680
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*……………………..Sh. 376,432,680
Kifungu 1006 –*Government Communication Unit*…...Sh.339,460,680
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*…….Sh. 514,525,100
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*………Sh. 514,915,100
Kifungu 2001 – *Communication Division*…………….Sh.1,289,297,840
Kifungu 2002 – *Information, communication and Technology*……………………………………..Sh. 0
Kifungu 4001 – *Information Services Department*…....................Sh.0
Kifungu 4002 – *ICT Systems Development and Services Division*…………….........…Sh. 1,153,850,867
Kifungu 4003 – *Communication Safety and Security Unit Division*……..……………………Sh. 402,019,013
Kifungu 4004 – *ICT Infrastructure Unit*…………………..Sh. 720,992,940

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 68 – Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……………Sh. 34,500,000,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*………………..........Sh. 530,480,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*…..……..…..Sh. 0
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*……..……..….Sh. 0

Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*……Sh. 2,166,560,000
Kifungu 2001 – *Communication Division*…………Sh. 57,076,233,000
Kifungu 2002 – *Information, Communication and* Technology……………………………………..Sh.0
Kifungu 4001 – *Information Services Department*…...................Sh. 0
Kifungu 4002 – *ICT Systems Development and Services Division*…..…………….…..…Sh. 40,395,381,000
Kifungu 4003 – *Communication Safety and Security Unit Division*………………….……………..……Sh. 1,824,200,000
Kifungu 4004 – *ICT Infrastructure Unit*…………..…Sh. 72,950,425,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 126 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Agosti, 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake, hivyo ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi*

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji kuhusu Hoja Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana Mheshimiwa Waziri wewe na timu yako na wataalam, kazi inaonekana, mnafanya kazi vizuri sana, hongereni. Ninawapongeza Wabunge, hoja za msingi zimesemwa na hasa pale mliposema kwenye ku-*carry forward bundles* ambazo mnasema nyinyi zitumike zote. Nchi nyingi wameweka *regulation bundle* likibaki unai-*carry forward* kwenye *credit* nyingine na ukitazama kwa hesabu ndogo tu, kwa wateja milioni 20 kwa uchache wa shilingi 50 ya kila *bundle* ya mtu ambayo inaliwa *is almost one bilion*.

Kwa hiyo, unaweza kuweka kwa wateja milioni 60, kwa wiki au kwa mwezi ni pesa ngapi zinapotea, zinabaki kwenye kampuni za simu? Ni jambo muhimu sana mkiweza kulinda. Mheshimiwa Waziri, *mobile penetration* Tanzania ni kubwa zaidi ya nchi za jirani, lakini mpaka leo kampuni hizi za simu hazioneshi faida. Wenye hisa zao, hakuna *dividend* ambayo kampuni hizo inatoa kwa watu wenye hisa. Jaribuni kukaa nao, tatizo ni kitu gani, watu waliowekeza walipwe na Serikali iweze kupata mapato mengi ya kutosha. *(Makofi)*

Kuna nchi zimepiga marufuku mitandao hii kwa watoto chini ya miaka 16, lakini wameona ni kosa, ni bora kutokupiga marufuku kwa sababu mitandao ina kazi yake vilevile. Ni bora *contents* zile ambazo hazina maadili zizuiwe na sheria ya *regulation* ya *AI,* Wabunge wengi wamesema ni muhimu sana. Ikitumika vibaya inaweza ikadhalilisha watu na watu wengi wameshadhalilika kwa taarifa za upotofu na picha za kubuniwa ambazo si za kwao, lakini zinawekwa katika mazingira mabaya na

familia nyingi zinaharibikiwa kutokana na hisia na matumizi mabaya ya mitandao.

Ninawapongeza sana na wataalamu wenu pamoja na Wabunge kwa kazi nzuri ambayo mmefanya.

Sasa ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka tarehe 4 Mei, 2026, siku ya Jumatatu.

*(Saa 1.19 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 4 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*